

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Thelathini na Moja – Tarehe 22 Julai, 2011

(Mkutano Ulianza Saa Tatuh Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. George B. Simbachawene) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:-

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka 2011/2012.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:-

Taarifa ya Mwaka na Hesabu Zilizokaguliwa za Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha kwa Mwaka 2009/2010 (*The Annual Report and Audited Accounts of Arusha International Conference Centre (AICC) for the year 2009/2010*).

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha, 2011/2012.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):-

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje. Ulinzi na Usalama Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka 2010/2011 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

MHE. EZEKIA D. WENJE - MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:-

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kabla ya Maswali naomba nitambue uwepo wa Mheshimiwa Spika, akiwa amekalia kitie chake cha Ubunge wa Jimbo la Njombe Kusini, nafurahi na mimi leo najisikia raha kukuona upo unaniangalia nikifanya kazi kwa niaba yako nakushukuru sana. Lakini pia nitambue uwepo wa Mheshimiwa Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Sumaye. Karibu sana tunafuraji kuwa na wewe siku ya leo. (Makofii)

Tuendelee na Maswali na Swali la kwanza linaulizwa na Mheshimiwa Modestus Kilufi.

Na. 283

Umuhimu wa Barabara ya Mlangali –Uturo –Ukwavila

MHE. MODESTUS D. KILUFI aliuliza:-

Barabara ya Mlangali –Uturo –Ukwavila ni muhimu sana kwa usafirishaji wa zao la mpunga unaolimwa maeneo hayo.

Je, Serikali ipo tayari kuimarisha barabara hiyo ili iweze kipitika mwaka mzima?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Modestus D. Kilufi, Mbunge wa Mbarali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Mlangali –Uturo-Ukwavila yenyе urefu wa Km. 18.9 ni ya changarawe na inahudumiwa na Halmashauri kipitia fedha za Mfuko wa Barabara. Kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, Halmashauri imekuwa ikitenga fedha kila mwaka ili kuwezesha utengenezaji wa barabara ili iweze kipitika kipindi chote cha mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011 Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ilitengewa shilingi milioni 44 kwa ajili ya matengenezo ya muda maalum km. 2, matengenezo ya kawaida km 10 na matengenezo ya sehemu korofii km 5. Tayari

mkandarasi amekwishapatikana na yupo kwenye hatua ya kukusanya mitambo sehemu za kazi kwa ajili ya kuanza kazi rasmi (*mobilization*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Halmashauri hii imetengewa shilingi milioni 401 kutoka Mfuko wa Barabara. Kati ya fedha hizo shilingi milioni 73.5 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya muda maalum km 5, matengenezo ya kawaida kilomita 6 ni matengenezo ya sehemu korofii moja katika barabara ya Mlangali –Uturo – Ukwavila.

Aidha, naishauri Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kuzingatia katika vipaumbele vyake, kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo.

MHE. MODESTUS D. KILIFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiw Naibu Waziri, lakini pamoja na maeleo mazuri barabara hiyo imekuwa ikitengenezwa vipande vipande bila kuikamilisha na hivyo kuleta usumbufu wakati wa kusarisha mazao pindi wakulima wanapotoka mashambani.

Je, Mheshimiwa Waziri atanihakikishia kwamba sasa hiyo barabara itatengenezwa yote ili kusudi iweze kumudu kusafirisha mazao kutoka mashambani?

Pili ni wazi kwamba Mbarali ni sehemu ya uzalishaji wa mazao mengi ya chakula na barabara zake nyingi za maeneo ya uzalishaji ni mbovu.

Je, Mheshimiwa Waziri atawahakikishia wananchi wa Mbarali kwamba sasa litachukuliwa jukumu maalum kuhakikisha barabara hizo zinaimarishwa ili kusudi mazao yale yasafirishwe kupelekwa maeneo ambayo hayana chakula nchini?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kilifi anasema fedha hizi zinakuja kidogo kidogo kwa hiyo zinatengeza vipande vipande. Ni kwa sababu fedha nazo zinakuja kwa utaratibu huo huo. Nimesema hapa fedha za barabara zilizotengwa ni milioni 401/- na sisi huko nyuma tulikuwa tunapokea hela kwa mwezi mmoja mmoja. Kwa hiyo barabara inatengenezwa kipande kipande kwa sababu na fedha zinakuja kipande kipande ndicho kinasababishwa hiyo. Ninyi mkiruhusu hapa mkasema milioni 4.1 zitatolewa zote kwa mpigo sisi Mheshimiwa Kilifi tunakupelekea hela zote kama zinavyozungumzwa hapa. Nimesikia Serikali ikitisema hapa kuititia kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba sasa tunategemea miezi mitatu mitatu huenda ita-improve hiki kipande kipande ili tuwe na hela nyingi zaidi. Otherwise hakuna tatizo lolote hela za barabara zikija tunapeleka moja kwa moja kwenye Halmashauri.

Swali lake la pili hili la uzalishaji wa mazao. Mimi nimefika Mbarali na Mheshimiwa Kilifi anajua kwamba nimewahi kufika Mbarali. Mbunge anayezungumza hapa ana-make a very valued point, ni eneo ambalo tunajua kabisa kwa mpunga linasaidia kulisha taifa zima kwa hiyo mapato ya Halmashauri yanaongezeka na mapato ya taifa pia yanaongezeka pale.

Hakuna mtu anaweza akabisha hapa kwamba hakuna umuhimu wa kuziangalia barabara zile kwa sababu *economics* zake ndizo zinazo-determine na politics za kwetu tulizonazo. Nataka niseme hapa kwamba tunaahidi tutashirikiana na yeze na kama tulivyosema hapa tunadhani kuna haja ya kukaa kuangalia vipaumbele vyetu ili tuweze kuelekeza nguvu kubwa zaidi katika barabara za Mbarali.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, aHsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Matatizo hayo yaliyojitekeza Mbarali yanafanana sana na yanayojitekeza katika eneo la Lwika katika eneo la Lundo Wilaya mpya ya Ziwa Nyasa. Sehemu zile kuna mradi mkubwa wa zao la mpunga na kuna mifereji iliyotengenezwa kiasi kwamba kupeleka maji kwenye barabara.

Kwa kweli ni tatizo kubwa sana ikizingatia kwamba eneo la Ziwa Nyasa ile ndiyo barabara kuu na pesa zinazotengwa kwenye Halmashauri ni kidogo nadhani ingefaa ziongezwe kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali Kuu. Je, Waziri ana majibu gani kuhusiana na tatizo hilo ambalo linawatesa sana wananchi wa eneo hilo hasa akina mama wanapohitaji kwenda kwenye hospitali kubwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme kwa kifupi tu kwamba eneo analolizungumzia Mheshimiwa Manyanya mimi nalifahamu na nimefika. Hii Wilaya inayozungumzwa hapa ni Wilaya mpya ambayo hatujaijengea miundombinu na vitu vingine na kuhakikisha kwamba tunakuwa na utawala na mpaka sasa hivi wanategemea Halmashauri ya Wilaya ya Mbanga.

Nataka niseme hapa, Mheshimiwa Magufuli Waziri wa Ujenzi alipokuwa anazungumza hapa kuhusu Mfuko wa Barabara alichosema Halmashauri zihakikishe kwamba zinaomba. Ukitegemea hela hizi tunazozitungumza hapa ni kweli kabisa kama anavyosema Mheshimiwa Manyanya hela hizi ni kidogo zinatumika kwa ajili ya *periodic maintenance* maeneo korofu na maeneo mengine, huwezi kuzungumza masuala ya construction kwa maana ya kujenga barabara mpya.

Kwa hiyo ninachowezwa kusema hapa kwa maana ya kujibu swali hili tunamwomba Mheshimiwa Manyanya pamoja na Halmashauri yake acha hii mpya ya Nyasa kwa sababu haijaanza, wakae waone jinsi ambavyo wanaweza wakaweka katika *special request*, maombi maalum ili tuweze kuangalia wote kwa pamoja tumsaidie. Mheshimiwa Manyanya ni Mbunge ambaye amejitekeza waziwazi mnawona wote kwamba anapigania maendeleo ya Ruvuma na sisi tunataka tukuthibitishie kwamba tutakusaidia katika kuhakikisha kwamba barabara hizi zinapitika.

Matatizo ya Maji – Vijiji vya Dodoma

MHE. FELISTER A. BURA (K.n.y. MHE. DAVID M. MALOLE) aliuliza:-

Dodoma ni Mji wa ukame na hupata mvua kidogo sana kila mwaka, hivyo vijiji vya Dodoma Mjini vinakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji safi na salama kwa matumizi ya nyumbani na kilimo cha umwagiliaji.

(a) Je, Serikali ina mpango ganiwa kupeleka maji safi na salama kwanza kwenye vijiji vya Mkonze, Ng'ong'hona, Michese, Mkoyo, Mchemwa, Chigongwe, Chihanga, Gawaye, Chididimo na Ntyuka ambavyo viko kwenye ukame uliokithiri?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka kuta za kukinga maji kwenye mito ya Ihumwa, Matumbulu na Mpunguzi ambayo hutumika kwa kilimo cha mbogamboga?

(c) Je, Serikali ina mpango gan iwa kupanua mabwawa ya Hombolo, Vikonhe, Makutupora, Mbalawala, Zuzu, Mbabala, Nkulabi na Mkalama kwa lengo la kupanua shughuli za kilimo cha umwagiliaji?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Mchiwa Malole, Mbunge wa Dodoma Mjini, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia na Jamii ipo katika mchakato wa utekelezaji wa miradi katika vijiji vya Mkonze, Ng'ong'hona, Michese, Mkoyo, Mchemwa, Chigongwe, Chihanga, Gawaye, Chididimo na Ntyuka ambapo kazi zilizokwishafanyika ni utafiti wa maji ardhini, uchimbaji visima na upimaji wa wingi wa maji.

Fedha zilizotumika kwa kazi hizi zilitengwa katika Bajeti ya mwaka 2010/2011 sawa na shilingi milioni 398.73. Visima vyote vilivyochimbwa vimeonyesha matokeo mazuri ya upatikanaji wa maji. Aidha, katika Bajeti ya mwaka 2011/2012 zimetengwa shilingi milioni 538.19 kuititia Mpango wa Maji na Usafi wa Mazingira kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu na usimamizi wa miradi ya maji inayoendelea kutekelezwa.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012 Serikali kuititia Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma imeweka kipaumbele katika kuboresha kilimo cha mbogamboga katika Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma kwa kujenga kuta za kukinga maji (makinga maji) kwenye mito ya msimu inapota katika vijiji vya Chigongwe, Mpunguzi, Chwahwa, Mbalawala na Mbabala 'B' ambapo shilingi milioni 175 zimetengwa chini ya TASAF.

Kutokana na ufinyu wa Bajeti vijiji vingine vikiwemo Ihumwa na Matumbulu vitaingizwa kwenye mpango kulingana na upatikanaji wa fedha.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia programu za kuendeleza Sekta ya Kilimo (*ASDP*) na Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*) na Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Umwagilija (*DIDF*) inao mpango wa kuongeza maeneo ya umwagiliaji katika Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma ambao kwa mwaka 2011/2012 Vijiji vya Zepisa na Vikonje vilitengewa shilingi milioni 767 kwa ajili ujenzi wa mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi/upanuzi wa mabwawa katika vijiji vingine vikiwemo vya Zuzu, Mbabala, Nkulabi, Makutupora, Hombolo na Mkalama utafanyika kulingana na upatikanaji wa fedha na vipaumbele vilivyowekwa na jamii katika kilimo. (*Makofi*)

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kazi ya kujenga kuta ya makinga maji yameonyesha mafanikio makubwa katika Kijiji cha Mkonze na Vijiji vingine ambavyo vimeweza kupata huduma hii ya makinga maji.

Kwa kuwa kuna Wahisani kama Kanisa la *Menonite* walikubali kutoa fedha kwa ajili ujenzi wa makinga maji na kwa kuwa wananchi kutokana na umaskini walionao wameshindwa kuendeleza mradi ambao ni wa makinga maji kwa vijiji vingine je, Serikali iko tayari kuwashawishi wahisani ambao wako tayari kushirikiana na Serikali yetu na wananchi wetu kwa ajili ya kujenga makinga maji na maeneo kame ya vijiji vingine katika Wilaya ya Dodoma Mjini?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana. Naomba niongezee majibu ya maswali ya nyongeza yaliyoulizwa na Mheshimiwa Bura kama ifuatavyo:-

Kwanza niseme kulingana na Sera ya Maji ya mwaka 2002 kipaumbele ni maji ya kunywa halafu ndiyo maji mengine yanafuata. Kwa hiyo, tunachokifanya sasa hivi tunajaribu kuzihamasisha Halmashauri zote na waibuaji wa miradi wanapoibua miradi wasifikirie kitengo kimoja tu. Tukiamua kufanya mradi huo unaweza ukahudumia maji ya kunywa, maji ya kilimo na maji ya mifugo na kufanya hivi tutakuwa tunaipunguzia hata Serikali isiwe inakuja kila sekta inakuja na mradi wake. Kwa hiyo nakubaliana kabisa kwamba kuna upungufu wa maji lakini tunhitaji kuangalia mtizamo katika kuibua miradi hii.

Lakini kuhusu suala la makinga maji, mimi nimhakikishie Mheshimiwa Bura kwamba Serikali imeshalionna na nakumbuka nimekwenda na Mheshimiwa Waziri Mkuu tumetembelea lile Kanisa la Menonite tumetembelea ile miradi na Mheshimiwa Waziri Mkuu alishaonyesha njia kwa kuchangia shilingi milioni 60 na akatuagiza. Kwa hiyo Wizara yangu inalishughulikia hili suala la kuvuna maji kwa kutumia makinga maji.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwulize Naibu Waziri kuhusu suala hili la maji. Vijiji vyangu vingi vya Jimbo la Mbanga Magharibi viko kandokando ya Ziwa Nyasa na maji yako karibu kabisa. Lakini, tangu uhuru havinamaji. Hivi Serikali itaona umuhimu wa kuweka *pump* ya maji kila kijiji ambayo itakuwa ni rahisi kupata maji wakati wote wakati maji wanayaona kila siku? Ni lini kazi hiyo itafanyika?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, Serikali ingependa kwamba wananchi pale panapowezekana waweze kupata maji mahala ambapo chanzo ni maji mengi kama kwenye Ziwa Nyasa na kwingineko.

Lakini, tatizo ni kwamba kwenye sera yetu tumesema kwamba wananchi wahusishwe katika kuamua chanzo kwa maana kwamba waweze kuwa na uwezo wa kuendesha miradi ile. Na chanzo cha maji ukichukua kwenye Ziwa, inamaana kwamba utahitaji kuweka *investment* kubwa ya gharama kubwa ambayo wananchi hawataweza kuendesha mradi wa aina ile.

Katika mradi wa vijiji 10, sehemu kubwa ya hii nchi wameamua kuchagua chanzo ambacho ni visima ambavyo wanaweza wakaendesha. Kwa hiyo, ili kusudi miradi hii iwe endelevu, tumeanza na hatua hiyo. Lakini, jinsi tunavyojenga uwezo baadaye tuaanza kuingia kwenye awamu ya pili ya kuchukua maji kwenye Ziwa Nyasa. (*Makofii*)

Na. 285

Bei ya Upasuaji Mbao

MHE. MENRAD L. KIGOLA aliuliza:-

Vijana wengi katika Wilaya ya Mufindi wameajiajiri katika shughuli za upasuaji mbao na kusafirisha sehemu mbalimbali nje na ndani ya nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha vijana hao kwa kupata vibali vya upasuaji mbao kwa masharti na bei nafuu?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Menrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa Serikali imekuwa ikitekeleza Sera ya Taifa ya Misitu ya Mwaka 1998 na Sheria ya Misitu Na.14 ya Mwaka 2002. Kwa mujibu wa sheria hiyo pamoja na Mwongozo wa Uvunaji Endelevu wa Mazao ya Misitu ambao unaweka utaratibu madhubuti wa kufuatwa katika uvunaji na biashara ya mazao ya misitu ya mwaka 2007 sambamba na Tangazo la

Serikali Na.231 la mwaka 2007, imeainisha bei za miti ya aina mbalimbali. Hivyo, haitakuwa sahihi kwa Serikali kutoza bei tofauti kwa watumiaji tofauti na miongozo niliyoitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugawaji wa miti ya kuvuna pia unategemea uwezo wa shamba kutokana na malighafi iliyoko kwa mwaka (*allowable cut*). Kutokana na kuongezeka kwa mahitaji, malighafi iliyopo haitoshi kugawia waombaji wote. Kipaumbele hotolewa kwa wenyewe viwanda vyenye mikataba ya Kitaifa na ambayo hutoa ajira kwa Watanzania walio wengi. Viwanda vya misitu (*Saw Mills*), halafu hufuatia wananchi wanaozunguka mashamba na hatimaye Watanzania wengine.

Hata hivyo, kwa kuzingatia uhaba wa malighafi, mwaka 2010 Wizara yangu ilianzisha mpango maalum ambao unawawezesha wananchi katika Mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya na Morogoro kuunda vikundi vya wakulima wa miti (*tree growers associations*) ambapo mpaka sasa vikundi 18 vyenye washiriki takriban 500 vimeanzishwa Wilaya za Mufindi, Kilolo, Rungwe, Kilombero, Njombe Mjini na Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inatoa ushauri kwa vijana kuungana pamoa na kuunda ushirika ambao utawezesha kuingizwa kwenye mpango huu wa upandaji miti ili wawe na miti yao. Aidha, Wizara yangu itawapa ushirikiano katika kutafuta mikopo kutoka katika taasisi za fedha na hatimaye kujenga uwezo wa kununua mashine za kuchakata miti ili waweze kuomba na kuvuna kama wavunaji wengine.

MHE. MENRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Waziri. Lakini, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa umesema kuwa kipaumbele wanapewa wenyewe viwanda vikubwa na wenyewe mikataba ya Kitaifa, sasa Je, Serikali haioni kwamba inawanyima haki wafanyabiashara wenyewe vipato vidogo ili wasiweze kupasua msitu huo?

Katika Wilaya ya Mufindi wazee wengi sana walitoa ardhi wakitegemea kwamba baadaye wangeweza kupata faida kutokana na msitu huu. Je, Serikali itaweza kutoa fidia kwa wale ambao walitoa ardhi kwa ajili ya upandaji wa misitu? (*Makofii*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Menrad Kigola kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utaratibu wetu wa ugawaji, ukiachilia mbali wale wawekezaji wakubwa ambao wana mikataba kama nilivyosema, sehemu kubwa ya malighafi huwa inakwenda kwa wavunaji wadogo wadogo wanaotoka kwenye vijiji vinavyozunguka mashamba. Kwa mfano, kwa shamba loa Sao Hill, mwaka 2008/2009 wavunaji wadogo wadogo wa vijiji vinavyozunguka shamba hilo walikuwa ni asilimia 66 ya wale wote waliogawiwa mgao wa kuvuna. Mwaka 2009 tulitoa asilimia 66 na mwaka jana 2010/2011 tulitoa kwa asilimia 51 kati ya wote walioomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kiasi kikubwa tunajitahidi sana kuhakikisha kwamba tunatoa kipaumbele kwa wananchi wanaozunguka maeneo hayo na hata kwenye maeneo mengine tutafanya hivyo na tunafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ardhi ambayo imetwaliwa, hili ni suala la kisheria, ukikumbuka sheria zetu za zamani kabla ya sheria ya mwaka 1999, ardhi iliyokuwa ikichukuliwa kwa ajili ya matumizi ya umma kama ambavyo mashamba haya yalivyochukuliwa miaka ile, kulikuwa hakuna fidia. Sheria imekuja inayozungumzia fidia kwa *land* ambayo haijawa *developed* mwaka 1999. Kwa hiyo, kwa mazingira ya sasa tunachokifanya ni kujaribu tu kujenga uhusiano mzuri na kuwafanya wananchi watambue kwamba ardhi ile iko kwao na malighafi iliyoko pale inapaswa iwanufaishe na ndiyo maana tunaweka msisitizo katika kuwapa malighafi zaidi kuliko wengine.

MHE. CHIKU A. ABWAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa inaonekana kwamba bei ya miti ya kupasua mbao ni gharama sana, na wawekezaji sasa hivi waliowekeza kwa ajili ya kutengeneza *furniture* hapa nchini wanalamika kwamba bei ya mbao ni kubwa kiasi kwamba wamekiri wazi na kutamkia Kamati ya Viwanda na Biashara tulipokuwa kwenye ziara kwamba wameshindwa kununua mbao Tanzania. Matokeo yake wanaamua kununua mbao kutoka Kongo na tena Kongo kwenyewe haziji kwa njia halali, zinakuja kwa njia ya panya. Je, Serikali ina mpango gani wa kusahihisha suala hili ili tusiendelee kupata hasara?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya mazao ya misitu kwa bahati mbaya sana kule kwenye soko hairatibiwi na Serikali, inaratibiwa na nguvu za soko lenyewe. Kwa upande wa bei ambazo tunatoza kwenye mashamba ni kidogo sana, na niseme tu ukweli kwamba si kweli kwamba bei kwenye soko ni kubwa kwa sababu ya bei tunazotoza sisi.

Ukitaka kujua kwa nini ni hivyo au ukitaka kujua kwa nini mnasema hivyo, waangalie waombaji na hesabu tulizozifanya. Mtu akigawiwa *cubic meter 100* za *softwood*, gharama jumla anayoitumia kwa kulipa Serikalini haizidi shilingi 300,000/=.

Lakini ukiweka na gharama za kuvuna, anaweza akatumia shilingi 1,500,000/=. Anachokwenda kuuza, akiuza mwenyewe anafika zaidi ya shilingi milioni 9. Kwa hiyo, kama sisi tunatoza *not more than 1.5 million*, anakwenda kuuza *over 9 million* na ndiyo maana *pressure* ya watu kuomba kuvuna ni kubwa sana. Kwa hiyo, bei ni ndogo sana kwenye shamba, na sasa hivi tunanza mchakato wa kuongeza bei.

Mwaka 2007 ndiyo mara ya kwanza bei ilipandishwa, baadaye mwaka 2009 tukapunguza kwa asilimia 30, jambo ambalo limeleta *crisis* ya maombi. Sasa hivi tunazungumzia kupandisha tena ili kuongeza fedha za Serikali tuweze kuhudumia jamii yetu. Kwa hiyo, si kweli kwamba bei ni kubwa kwa sababu ya mashamba au kwa sababu ya gharama za Serikali, ni kwa sababu ya soko lenyewe kwamba pengine *supply* ni ndogo kuliko *demand*.

**Kituo Kidogo cha Polisi Kupandishwa
Hadhi Kuwa Kituo Kamili**

MHE. WILLIAM A. MGIMWA (K.n.y. MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA)
aliuliza:-

Jimbo la Mwibara lina vituo vidogo vitatu ambavyo kwa mujibu wa sheria hufungwa saa 12.00 jioni na kufunguliwa saa 12.00 asubuhi kesho yake na nyakati za usiku wakati vituo hivyo vimefungwa kumekuwepo na matukio kadhaa ya uhalifu ya ujambazi wa kutumia silaha hata kuua watu kadhaa na kusababisha wananchi kukosa mahali pa kutoa taarifa ya matukio hayo kwa sababu vituo hivyo vinakuwa vimefungwa kwa nyakati hizo:-

- (a) Je, ni lini kituo cha Polisi cha Mwibara ambapo ni Makao Makuu ya Jimbo la Mwibara kitapandishwa hadhi kuwa kituo kamili ili kiweze kufanya kazi saa 24?
- (b) Kama tatizo la kutopandishwa hadhi kituo hicho ni jengo la kituo na nyumba za askari. Je, ni lini Serikali itatatua tatizo hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola, Mbunge wa Mwibara, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango wa kujenga kituo chenye hadhi ya daraja C pamoja na nyumba za askari wasiopungua tisa (9) katika Tarafa ya Kibara. Mpaka sasa eneo la kujenga kituo limeishapatikana na tayari ramani ya kituo imeishatumwa kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo cha sasa cha Polisi Kibara kipo katika jengo dogo ambalo limetolewa na mwananchi. Hata hivyo mmiliki wa nyumba hiyo ametutaka tuondoke kwani kwa sasa anahitaji kwa matumizi yake. Kwa mazingira hayo, ipo haja ya kuhakikisha kituo kipyä kinajengwa haraka iwezekanavyo. Jitihada za kupata fedha kwa shabaha hiyo zinafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo cha Polisi Kibara kinatarajiwa kujengwa kwa ushirikiano kati ya Jeshi la Polisi, wananchi, Halmashauri ya Wilaya ya Bunda na wadau wengine. Tunamwomba Mheshimiwa Mbunge atusaidie kuhakikisha wananchi pamoja na Halmashauri kuchangia ujenzi wa kituo hicho.

MHE. WILLIAM A. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Mwibara linafanana kabisa na tatizo la kituo cha Ifunda katika Jimbo la Kalenga. Kituo kile

kinahudumia Kata tatu; Ifunda, Kiponselo mpaka Wasa, lakini kituo kile hakina gari na ofisi imepangwa kwa mtu binafsi. Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kuwa na jibu gani kwa ajili ya utatuzi wa kituo hiki?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sahihi taarifa aliyoitoa hapa Bungeni kwa njia ya swali. Ni jambo ambalo tunalifahamu katika Wizara. Lakini, mara kadhaa nimekuwa nikija hapa nikieleza uhaba wa rasilimali fedha ambao tunao. Hakika shabaha na nia ya kujenga vituo mahala ambapo vinastahili kujengwa tunayo kama Wizara, na maombi kweli yapo, lakini tatizo kubwa tulilonalo ni uhaba wa rasilimali fedha, na jinsi tunavyopata uwezo na ndivyo hivyo tunavyokwenda kwa utaratibu wa kutengeneza vituo katika maeneo mbalimbali nchini, na izingatiwe kwamba nchi yetu ni kubwa kulingana na rasilimali fedha tulizonazo.

MHE. REGIA E. MTEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Vituo vya Polisi Wilayani Kilombero vipo katika hali mbaya kwa maana ya majengo ni chakavu na mengine yamejengwa kwa mabati. Je, Mheshimiwa Waziri ana mpango gani wa kuhakikisha vituo hivi vya Polisi vinakarabatiwa na kuwa na hadhi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu langu la msingi katika swali la msingi, ingawaje eneo lilikuwa ni tofauti, lakini tunaelewa kwamba hii ni hali ambayo ipo katika Taifa letu kwa ujumla.

Lakini, nitasema tu kwamba ukarabati ama uanzishaji wa vituo ama upanuaji wa vituo hufuatana na hali kama ni daraja A, daraja B, daraja C, nasema kwamba utaendana kwa kadri tutakavyokuwa tunapata rasilimali fedha. Lakini, nia tunayo.

Lakini pia nimwombe Mheshimiwa Mbunge atusaidie katika Halmashauri na kwa wananchi pia kuweza kuchangia katika jambo kubwa kama hili. Lakini, kubwa mimi nafikiri tusishikilie vituo, tujaribu kuelimisha wananchi tupunguze uhalifu katika nchi.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyoni geza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tatizo lililosemwa na Mheshimiwa Lugola la kufungwa vituo saa 12.00 jioni linafanana sana na tatizo linaloikumba vituo vya Polisi Madaba, jimbo la Peramiho na Kituo cha Polisi Muukuru.

Jimbo la Peramiho; na tatizo la kufungwa kwa vituo hivyo mapema kunasababishwa na ukosefu wa magari ukizingatia kwamba Muukuru ni mpakani mwa Tanzania na Msumbiji, Peramiho tunajenga sasa Makao Makuu ya Halmashauri, Madaba ni Mji Mdogo unaotarajiwa kwa sasa, na Mheshimiwa Waziri alishaahidi kutekeleza ahadi hiyo ya kupeleka magari kwenye vituo hivyo.

Je, Mheshimiwa Waziri ataniambia kwenye Bajeti yake ya mwaka huu vituo hivyo vitapata magari ili kuondoa tatizo hilo la wananchi kutopatiwa huduma ya Polisi inapohitajika?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala limeanzia Mwibara na limekwenda, sasa tumefika mpaka....

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba tatizo la vituo, uimarishaji wa vituo vya Polisi ni tatizo katika nchi yetu nzima. Na kila Mbunge hapa kila eneo analotoka analo tatizo hilo. Lakini, hiyo ni sehemu moja tu ya maeneo mbalimbali ambayo Jeshi la Polisi linawajibika kuyatazama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu, kulihakikisha Bunge lako Tukufu kwamba jitihada zitafanyika kwa kiwango ambacho kitakuwepo katika Bajeti ambayo ataisoma Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi wiki ijayo, na tutajitahidi kuona mgao wetu katika kuimarisha maeneo mbalimbali.

Lakini kuhusu suala la gari, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, tulifanya ile ahadi na ilikuwa bado haijatimizwa. Kwa hiyo jitihada zitafanyika kuhakikisha kwamba hiyo ahadi tuliyoitoa ya kutoa gari inatimilika, na aliwahi kuniuliza swalii hilo siyo ndani ya Bunge, nikamwambia kwamba jitihada zinafanyika kuhakikisha kwamba ahadi hiyo tunaitimiza. (*Makofî*)

Na. 287

Watumishi wa Uhamiaji

MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS (K.n.y. MHE. ABDALLAH HAJI ALI) aliuliza:-

- (a) Je, watumishi wa Idara ya Uhamiaji kisheria ni raia wa kawaida au askari Polisi?
- (b) Je, kwa nini watumishi wa Uhamiaji hawapewi posho ya chakula na makazi kama ilivyo kwa Askari Polisi ambaao nao wako ndani ya Wizara hiyo?
- (c) Je, ni kwa nini watumishi wa Uhamiaji hawaangaliwi kimaslahi hata baada ya kusoma?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Aballah Haji Ali, Mbunge wa Kiwani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo wa Idara ya Uhamiaji uliopitishwa tarehe 17 Septemba, 2010 na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania umeifanya Idara kuingia katika mfumo wa kiaskari.

Hata hivyo, ili muundo huo uweze kutekelezwa inapaswa kusimamiwa na sheria ya uhamiaji ambayo inaanndaliwa hivi sasa. Sheria hiyo itakapokamilika, Idara ya Uhamiaji itajumuishwa katika Kamisheni ya Polisi na Magereza ambayo husimamia maslahi ya askari (*The Police Force and Prison Service Commission Act, Cap. 241, 2002*) katika kipindi hiki.

Hadi hapo sheria hiyo itakapokamilika, watumishi wa Idara ya Uhamiaji wanaendelea kusimamiwa na Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 (*The Public Service Act, 2002*).

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa wa Uhamiaji wanapewa posho ya chakula (*ration allowance*). Aidha posho nyingine kama vile posho ya weledi na posho ya makazi (*professional and house allowance*) zitalipwa mara mchakato wa sheria ya Uhamiaji utakapokamilika kama nilivyosema hapo awali.

(c) Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba watumishi wa Idara ya Uhamiaji hawaangaliwi kimaslahi hata baada ya kusoma. Maafisa Uhamiaji wenye cheo cha chini ya Mkaguzi Msaidizi wa Uhamiaji hupandishwa cheo kuwa Wakaguzi Wasaidizi wa Uhamiaji wanapojiedeleza kielimu na kupata shahada au stashahada.

MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa, sheria ya Idara ya Uhamiaji iliyopitishwa na Rais tarehe 17 Septemba, 2010 imeifanya idara hiyo sasa iwe chini ya Jeshi la Polisi:-

- (a) Je, sasa Wafanyakazi wa Idara ya Uhamiaji watapatiwa mafunzo ya uaskari?
- (b) Je, hapo kabla ambapo walikuwa ni Watumishi wa Utumishi wa Umma kwa nini Vyeo vyao vilikuwa ni kama vya kiaskari?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, Uhamiaji kwa utaratibu mpaka sasa wanakwenda kwa sheria ambayo ni tofauti na sheria ya kiaskari.

Uamuzi ulichukuliwa mwaka 2010 kama nilivytaja katika jibu langu la msingi na tukishatengeneza sheria yao baada ya uamuzi huo na ikapitishwa na Bunge, basi hawa watapata mafunzo ya uaskari kama askari wengine. Taratibu zingine zote ambazo zinaendana na Kiaskari zitaendana pia na Idara hii ya Uhamiaji.

Gharama kwa Wakulima wa Tumbaku

MHE. SAID J. NKUMBA aliuliza:-

Wakulima wa tumbaku hulipia gharama za magunia ya kufungia tumbaku lakini ununuzi ukishafanyika huwa mali ya mnunuzi:-

Je, ni lini utaratibu wa kuwaongezea wakulima gharama utaondolewa?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magunia ya vitambaa (*Hessian Cloth*) ni moja ya vifungashio vinavyotumika katika kufunga tumbaku. Vifungashio vinginevinavyoambatana na magunia hayo ni kama *jute* au *cotton twine*. Majadiliano na makubaliano ya bei ya tumbaku kati ya wakulima na wanunuzi hufafanyika katika kikao cha Halmashauri ya Tumbaku ambapo gharama za uzalishaji huzingatiwa katika mfumo mzima wa bei. Gharama hizo zinajumuisha pembejeo na vifungashio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu unaotumika ni kwamba baada ya kusindika tumbaku iliyonunuliwa, wanunuzi wanarudisha baadhi ya magunia yaliyotumika kufungia tumbaku kwa wakulima, kuitia vyama vyao vya ushirika vya msingi kwa gharama za wanunuzi ili kuwapunguzia wakulima gharama za kununua magunia mapya kwa msimu unaofuata.

Tatizo linalojitokeza hapa ni kwamba magunia yaliyotumika yanayorudishwa huwa hayatoshi mahitaji ya wakulima na hivyo kulazimisha ununuzi wa magunia mengine mapya ya kuchanganya jambo ambalo linamjengea mkulima hisia ya kuongezewa makato ya magunia mapya katika msimu unaofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba mkulima anapata mapato halali kwa mazao yake. Ili kuondoka utata unaoendelea kujitokeza na kuongeza imani ya wakulima kwa vyama vyao vya ushirika na wanunuzi, nimeingiza Bodi ya Tumbaku kuhakiisha kwamba suala la bei ya magunia na vifungashio, linapelekwa katika kikao cha Halmashauri ya Tumbaku kitakachofanyika tarehe 4 Agosti, 2011, ili lijadiliwe kwa uwazi zaidi na wadau wote. Aidha, nashauri bei halisi ya magunia iwekwe wazi kwa wakulima na Bodi ya Tumbaku ihakikishe kwamba wakulima wanaelewa vizuri mchakato wa bei na makato yote yanayofanywa kwao ili kuondoa manung'uniko.

MHE. SAID J. NKUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana, lakini nina swali dogo la nyongeza:-

Kwa kuwa, magunia yanayofungiwa tumbaku ni vifungashio kama ambayo vifungashio vingine vya biashara yeote hata ukienda dukani, kwamba unaweza ukafika dukani ile bidhaa unaponunua yule anayenunua bidhaa ndiye anayenunua kifungashio, kinyume cha sasa ambapo kwenye tumbaku yule anayeuzza tumbaku anamlazimisha anayeuzza tumbaku atoe tena fedha za kununulia kifungashio;

Je Serikali sasa itakubaliana nami kwamba haya mapendekezo ambayo inayapeleka katika vikao hivyo vya wadau kuondoa kabisa suala la wakulima sasa kuchangia kwa namna yeote ile magunia ambayo ni jambo ambalo haliwahusu wakulima hawa?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO,CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, utata huu mimi ninauona, lakini tatizo hili lipo kwa sababu nadhani wakati wanapofanya mchakato huo wa kupanga na kujenga makato kwa mkulima suala hili haliwi wazi. Ndiyo maana kwenye majibu nimeagiza kwamba Bodi ya Tumbaku iende ikae na wadau wote jambo hili linalohusu makato ya wakulima lijadiliwe na liwekwe wazi. Kwa sababu wakati mwingine Mkulima anakatwa in kind hatoi fedha anaambiwa utakatwa kwenye kilo, sasa mkulima kila wakati anapata hisia kwamba hapa ninanyanyasika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo majibu yangu ni yale yale kwamba maombi yake ni ya msingi, nataka yajadiliwe katika Baraza la Tumbaku katika Halmashauri ya Tumbaku tarehe 4 Agosti na wakulima wawekewe wazi mchakato mzima.

MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona ni historia katika eneo hili la kijiji cha *Maisha plus* kupata nafasi finyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliruhusu Wilaya ya Serengeti kuwa katika majoribio ya kilimo cha Tumbaku, lakini muda huo uliisha mwezi wa tatu, Kwa utaratibu msimu ulikuwa uanze mwezi wa saba.

Wananchi wa Wilaya ya Serengeti wakulima wa Tumbaku wapo gizani hawajui wafanye nini, Serikali inasemaje, kama tathmini ilifanyika majibu hayo ni yapi, na wafanye nini?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO,CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikwishazungumza kuhusu suala hili, nilichomwahidi Mheshimiwa Kebwe ni kwamba kwanza bado tuna matatizo ya tumbaku ambayo ipo mpaka leo hii haijanunuliwa. Tumezalisha tumbaku nyingi sana tani 130,000 mpaka leo hii bado wakulima wanayo, na tunahaha kutafuta masoko mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimwahidi Mheshimiwa Kebwe kwamba tutakaa pamoja tuangalie mustakabali wa wakulima wa tumbaku wa Serengeti kwa sababu nao tayari wamekwishaitikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado namwalika Mheshimiwa Kebwe karibu sana tukae tulijadili tulipatie ufumbuzi. (*Makofi*)

Na. 289

Mashamba ya Mkonge

MHE. SALUM KHALFAN BARWANY aliuliza:-

Wamiliki wa mashamba ya Mkonge Manispaa ya Lindi hawayaendelezi na hutumia Hatimiliki za mashamba hayo kupata mikopo wakati wananchi hawana ardhi kwa ajili ya kilimo:-

- (a) Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka wa kufuta hati hizo na sehemu ya ardhi wapewe wananchi kutumia kwa kilimo?
- (b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kutafuta wawekezaji wengine kuendeleza maeneo hayo?
- (c) Je, Serikali itawasaidiaje wafanyakazi wa shamba la mkonge kikwetu ambao hawajalipwa kiinua mgongo chao kwa zaidi ya miaka ishirini sasa na wengine tayari ni marehemu?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany Mbunge wa Lindi Mjini naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Manispaa ya Lindi kuna mashamba 12 ambayo zamani yalikuwa yanamilikiwa kwa miliki zisizo na kikomo ambazo zilifutwa mwaka 1963 na mwaka 1969 miliki zilibadilishwa kuwa za miaka 33.

Tathmini iliyofanywa na bodi ya Mkonge kati ya Tarehe 29 Oktoba, 2006 na 3 Novemba 2006 inaonesha kwamba karibu mashamba yote yamegeuka kuwa mapori isipokuwa shamba la Kikwetu ambalo mmiliki wake ni *TASCO*. Baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swalii la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kubaini mashamba ambayo ni mapori, Mkoa wa Lindi unashauriwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, kuandaa mapendekezo kwa

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili hati miliki zifutwe kuruhusu mashamba yagawiwe kwa watakaoweza kuyaendeleza.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya hatimiliki kufutwa kisheria, ni muhimu sasa kutafakari na kuangalia ni nani aweza kuyaendeleza mashamba hayo.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mmiliki wa shamba la Kikwetu anajulikana, Serikali kuptit Bodi ya Mkonge Tanzania na Uongozi wa Mkoa wa Lindi itawasaidia waliokuwa wafanyakazi wa shamba la Mkonge la Kikwetu au familia zao hasa wale amba ni marehemu kutumia sheria za kazi zilizopo ili waweze kupata mafao yao wanayostahili.

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Kwa kuwa, kilio hiki ni cha muda mrefu, na siyo katika Mkoa wa Lindi tu, ni katika maeneo yote ya nchi yetu.

(a) Je, Serikali kwa sasa haijaona umuhimu wa kuleta Muswada huo Bungeni ili ujadiliwe na kutafuta ufumbuzi wa sheria?

(b) Wafanyakazi hawa amba kwa muda mrefu wamekuwa katika mashamba haya ya Mkonge ambayo walikuwa wanarithiwa kutoka katika kampuni moja kwenda katika kampuni nyingine, na haki zao huwa zinahamishwa bila malipo yeoyote. Je, Serikali kwa sasa haioni umuhimu wa kuwasaidia watu hawa wakapata haki zao hata kama wengine hawapo duniani?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Barwany kwa sababu suala hili amelifuatilia sana. Kama nilivyosema mashamba 12 katika Manispaa ile, ukisoma historia yake kabla ya uhuru yamekuwa yanahamishwa miliki kutoka mtu mmoja kwenda mwingine na hatimaye wengine na kama ye ye mwenyewe anavyojua wamekuwa wakitungia hati hizi kwa ajili ya kupatia mikopo, jambo ambalo kwa kweli ukilitazama linakiuka taratibu zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Barwany kwamba hili tumeliona na haiwezekani mashamba yale yakaendelea kuwa mapori wakati watu hawalimi na waendelezaji hawaendelezi. Tutachukua hatua kama nilivyosema.

Lakini ni lazima tuishirikishe Halmashauri yenye kwa sababu pale kwenye Manispaa ni wadau wa kwanza. Mimi nimesema Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa sababu kuna *element* ya hati miliki Wizara yangu tutashirikiana ili tujue mustakabali wa watu wote hawa, lakini pia tutashirikisha Wizara ya Kazi kwa sababu iko haja ya kuangalia mambo ya kisheria kuhusu hao watu amba wanadai haki zao na wengine tayari ni marehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na maombi ya Mbunge. (*Makofi*)

MHE. YUSUPH ABDALLAH NASSIR: Mheshimiwa Mwenyekiti asante, kwa kuwa, kumekuwa na upotoshaji wa kauli iliyotolewa na Waziri wa Kilimo tarehe 14 wakati akitoa majibu ya msingi ya maswali matatu ambayo nimekuwa nikuliza. Ningependa kumwuuliza Naibu Waziri wa Kilimo maswali yafuatayo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa ni swali moja tu.

MHE. YUSUPH ABDALLAH NASSIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, Je, ni vema sasa nikawashauri waathirika wa Mkonge kwenye mashamba ya Mgombezi, Hale, Mruazi pamoja na Mwelya waelekee kwa Msajili Hazina kwa ajili ya kupata mafao yao?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO,CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina uhakika ya upotoshaji uliofanywa na Waziri, sijui kama kuna upotoshwaji ambao umefanywa. Sidhani kama Waziri anaweza kuja hapa kupotosha Bunge na Wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama naweza nikakumbuka sikuwepo lakini najua kabisa hoja iliyopo kwenye mashamba hayo, tulicho sema ni kwamba mashamba yale ambayo tayari yamekwishashughulikiwa, madai yamekwishapelekwa Hazina ili tuangalie wale ambao wanastahili kulipwa walipwe. Lakini kama si hilo naomba niseme kwamba naamini Waziri wa Kilimo hakupotosha na wala hakusema sasa nendeni Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri alisema tunalishughulikia kama Serikali kwa sababu mwisho wa siku maombi ya fedha yanapelekwa Hazina ili yaweze kulipwa. Lakini sisi pia hatuwezi kuchukua tu tukaanza kulipia watu waliokuwa na mashamba wamewadhulumu wakulima tukaanza kuwalipa bila sababu, ni mpaka tujiridhishe kwamba kuna sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi yetu kubwa ni kuhakikisha kwamba wale waliodhulumu kwanza wanalipa na pale inapobidi ndipo Serikali itaingilia. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Mbunge hili tuliweke vizuri, Hakuna upotoshaji uliofanywa na Waziri wa Kilimo.

Na. 290

Vyanzo vya Maji Kukidhi Jiji la Dar es Salaam

MHE. AMINA N. MAKILAGI aliuliza:-

Serikali imefanya kazi nzuri ya kutafiti na kupata vyanzo vya kukidhi mahitaji ya maji katika Jiji la Dar es Salaam ili kuondokana na tatizo sugu la maji kwenye Jiji hilo.

Je, Serikali katika mwaka wa fedha 2011/2012 imekusudia kutenga fedha kiasi gani ili kuendeleza mradi wa chanzo cha Mpiji, Mpera na Kidunda ili wananchi wa Mikoa ya Pwani, Morogoro na Dar es Salaam wapate maji safi na salama na ya uhakika.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeandaa mpango maalum wa miaka mitatu 2011-2013 kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji safi na uondoaji wa majitaka Jijini Dar es Salaam. Mpango huo unalenga kuongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 300 kwa siku zinazozalishwa sasa, hadi lita milioni 710 kwa siku ifikapo mwaka 2014.

Kazi zitakazotekelawa katika mpango huo ni pamoja na ujenzi wa bwawa la Kidunda; uchimbaji wa visima vya Kimbiji na Mpera; upanuzi wa chujio la maji kutoka chanzo cha Ruvu chini, upanuzi wa mitambo ya Ruvu Juu na ujenzi wa bomba kuu la maji kutoka chanzo cha Ruvu chini hadi Dar es Salaam, na kutoka Kibaha hadi Kimara. Baada ya kazi hizo kukamilika huduma ya majisafi kwa wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam na Wilaya za Bagamoyo na Kibaha Mkoani Pwani itaongezeka kutoka asilimia 55 ya sasa hadi asilimi 75.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mpango wa majisafi na uondoaji wa majitaka Dar es Salaam utagharimu jumla ya shilingi bilioni 654. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 Serikali imetenga shilingi bilioni 171.3. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 38.6 ni kwa ajili ya kuendeleza chanzo cha Kimbiji na Mpera na shilingi bilioni 6.5 ni kwa ajili ya mradi wa bwawa la Kidunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mkoa wa Morogoro watapata huduma ya maji kupitia miradi mimgine inayoendelea kutekelezwa nchini kote kupitia programu ya maendeleo ya sekta ya Maji. (*Makofî*)

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Naomba nimshukuru sana Waziri kwa majibu mazuri sana aliyoyatoa ambayo yanaleta matumaini kwa wananchi wa Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, chanzo cha maji ya Mpera Wilaya ya Mkuranga na chanzo cha maji cha Mpiji karibu sana na Wilaya ya Kisarawe. Kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Kisarawe na wananchi wa Wilaya ya Mkuranga wana shida sana ya maji katika Miji yao hasa miji mikuu?

(a)Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu mradi wa maji utakapokamilika wa kusambaza maji Dar es Salaam uweze kuwafikia pia wananchi wa Kisarawe na M kuranga.

(b)Je, Serikali inatoa tamko gani kuwafikishia maji wananchi waishio vijiji na wanaozungukwa na mito na maziwa yakiwemo maeneo ya ziwa Nyasa, ziwa Victoria, ziwa Manyara na ziwa Tanganyika?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Makilagi kwa namna anavyowatetea wananchi wa mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro ili waweze kupata huduma ya maji safi. Amekuja mara nyingi ofisini tumezungumza na nimemweleza na nikamshukuru sana kwa mawazo yake mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mpango wa kuchimba visima vya Mpela na Kimbiji lengo kubwa lilikuwa ni kupeleka Dar es Salaam lakini hutawezi kupeleka Dar es Salaam lazima upitie kwenye vijiji ambavyo bomba lile linapita. Kwa hiyo, tutahakikisha kwamba vijiji vile ambavyo viko karibu na lile bomba vitapata maji kwanza wawe na majukumu kuona kwamba ule mradi ni wao na waweze kuulinda. Kwa hiyo, tutawapatia maji wananchi wote wa Mpera, Kimbiji katika Wilaya za M kuranga na Kisarawe.

Katika sehemu ya pili lake Serikali itahakikisha vipi wananchi kama watapata maji kutoka kwenye mito na maziwa wanayoishi karibu nayo. Kama nilivyojibu katika swali la nyongeza la Mheshimiwa Komba, nimesema kwamba nimesema sera inasema kwamba wananchi watashirikiana na Serikali kuweza kuona chanzo ambacho ni nafuu kukiendesha.

Lakini kuna maeneo mengine kwamba hakuna namna nyingine yoyote ya kupata njia ambayo ni nafuu zaidi. Tutatoa maji kwenye mito hiyo. Serikali inaweza kuweka *investment* lakini wananchi ndio wataweza kuendesha miradi ile kusudi iwe endelevu. Kuna maeneo mengi sana Serikali imeweza kuweka miradi hii na miradi hii imekufa kwa sababu haikuwa labda ni mfadhili amejenga ukakabidhi kwa wanakijiji, lakini kwa sababu wanajua maji yanatoka ni bure walishindwa kuiendesha ndio maana tukaja na sera mwaka 2002 kwamba wananchi waichukue hiyo miradi ni mali yao waweze kusaidia na kuitunza ili iwe endelevu.

MWENYEKIDI: Swali hili lina watu wengi kweli kweli. Sasa Dar es Salaam, maji nimpe nani? Nampa Mheshimiwa John John Mnyika, Mbunge wa Ubungo.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Katika jibu lake la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema kwamba Bwawa la Kidunda lililopo Morogoro litatengewa shilingi bilioni 6 peke yake kwenye mwaka huu wa fedha. Nina fahamu kwamba kwa mujibu wa maazimio ya Baraza la Mawaziri huu mradi unatakiwa utekelezwe kwa kasi zaidi kwa shilingi bilioni 6 ni ndogo sana.

Sasa niulize tu swali la nyongeza ukiondoa hiyo kasoro ya kiwango kidogo cha fedha kwa Bwawa la Kidunda. Je, ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa upande wa upanuzi wa bomba la Ruvu Juu kwa maana ya kutoka Kibaha mpaka Kimara?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba uelewe kwamba mradi mzima tumesema utagharimu bilioni 654. Sasa hivi bilioni 654 zimechanaganuliwa katika maeneo mbalimbali ikiwemo Bwawa la Kidunda kuna kupanua chanzo cha Ruvu Juu, kupanua chanzo cha Ruvu Chini, kujenga mabomba ya Ruvu Chini kwenda mpaka Dar es Salaam na Ruvu Juu kwenda mpaka Kimara.

Sasa michanganuo ya kila sehemu ni kiasi gani cha fedha kimepangwa hilo nitakupatia Mheshimiwa Mbunge. Lakini kwa sasa hizi bilioni 6 za bwawa la Kidunda ni za usanifu na kulipa fidia. Maana lazima uende hatua kwa hatua huwezi kuanza tu ukaweka bilioni 200 zikakaa miaka miwili hujaanza kujenga lile bwawa.

Kwa hiyo, nikuhakikishie kwamba mpaka mwaka 2013 bwawa lile litakuwa limejengwa na mradi wa maji Dar es Salaam Desemba 2013 tayari utaanza kutoa maji na huduma ya maji kwa wananchi wa Dar es Salaam.

MWENYEKITU: Ahsante swali hili lina waulizaji wengi Mheshimiwa Naibu Waziri tafuteni namna nzuri ya kuwasiliana na wadau hawa wote ili waeleweshwe mipango ya Serikali.

Na. 291

Kupunguza Muda wa Masomo ya Uuguzi

MHE. SUZAN J. LYIMO aliuliza:-

- Je, ni sababu gani za kuamua kupunguza muda wa masomo ya uuguzi toka miaka minne hadi miaka miwili na nini athari zake?
- Kwa sababu uuguzi ni taaluma iliyojulikana kimataifa kwa msingi huo ina *standards* zake. Je, kimataifa uuguzi kwa ngazi ya cheti inapaswa kusomewa muda gani?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kubwa ya kupunguza muda wa mafunzo ya uuguzi kutoka miaka 3 hadi 2 ilitokana na kuanzishwa kwa mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi ambaa unalenga kuwa na zahanati katika kila Kijiji na Kituo cha Afya, katika kila Kata. Hivyo, ililazimu kuwa na mkakati wa kuongeza idadi ya Wauguzi katika soko la ajira ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa watalaam hawa nchini. Pamoja na mikakati mingine ilikubalika kupunguza muda wa mafunzo ya uuguzi kutoka miaka

mitatu iliyokuwa inatolewa awali hadi miwili bila kuathiri kiwango cha ubora wa mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutayarisha mtaala ngazi ya cheti kwa mafunzo ya uuguzi, Wizara ilifanya upembezi yakinifu kulingana na mahitaji ya nchi yetu. Matokeo ya upembusi huu yalionyesha kwamba kuna sehemu nyingi katika mtaala zilizokuwa zinajirudia na hivyo kuzipunguza katika mtaala hakujaleta madhara yoyote ya kiwango cha ubora wa mafunzo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kila nchi Ulimwenguni inatoa taaluma ya uuguzi kwa *standards* zake kulingana na mahitaji ya nchi husika.

Katika nchi yetu tuna chombo cha *International Confederation of Nurses* ambacho kimetoa ngazi mbili za mafunzo ya uuguzi ambazo ni *Enrolled Nurses* kwa ngazi ya cheti na *Registered Nurses* kwa ngazi ya stashahada na shahada ya uuguzi kulingana na mahitaji ya nchi yetu. Hivyo kupunguza muda wa mafunzo hadi kufikia miaka miwili imekubalika na hiki chombo muhimu kinachoangalia viwango vya uuguzi. (*Makofi*)

MHE. SUZAN J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kweli niko *disappointed* na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vyovypote vile ni lazima kutakuwa na athari hasa za kiutendaji kutokana na kupunguza muda huo. Kwa mfano, siku za nyuma ukunga ilikuwa ni mwaka mmoja lakini sasa hivi imepunguzwa mpaka mwezi mmoja. Kwa hiyo, lazima kutakuwa na athari hasa ukizingatia kwamba sasa hivi Tanzania tuna mpango maalum wa kupunguza vifo vya watoto wanaozaliwa. (*Makofi*)

(a)Je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoini kwamba kupunguza huku kwa watalaam wetu kutoka mwaka mmoja hadi mwezi mmoja kutapelekeea akina mama wajawazito sasa kutokwenda Hospitalini na kwenda kwa wakunga wa jadi hasa ikizingatia kwamba watu hawa hawatakuwa na utalaam?

(b)Kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi sana kwa wale ambao wamemaliza *nursing* kwa kutumia miaka miwili kutokupata ajira kwa vigezo kwamba hawana utalaam wa kutosha. Je, Naibu Waziri haoni kwamba hii ni *contradiction* kwa Serikali yenyewe? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Suzan amezungumza kwamba kulikuwa na kipindi cha *practical* kwa mwaka mmoja, tumeponguzwa mpaka mwezi mmoja.

Mimi naomba niseme hivi kwamba vyuo vyetu vyote vya unesi hata ambao wanafungua vyuo vya *private* sasa hivi *condition* ni kwamba viwepo mahali ambapo kuna hospitali. Kwa hiyo, sambamba na kutoa na mafunzo ya nadharia wanakuwa

wanaendelea wanafundishwa pia mafunzo ya *practical*, wanafanya *practical* ikiwa ni sambamba *parallel* na mafunzo wanayofundishwa.

Maana yake kama unafundishwa kwa mfano wanapoingia kwenye *obstetrics* inapokuja kwamba wanafundishwa *obstetrical problems and how to handle the cases*, wakimaliza darasani jioni wanakwenda kufanya *practical* katika *maternity* wodi na hii imeonekana kwamba inawapa wanafunzi mafunzo mazuri zaidi kuliko ambapo walikuwa wanasesibiri zamani wakimaliza mafunzo ya nadhari wanakwenda kukaa kule kwa mwaka mmoja. Sasa kule kulikuwa hakuna *supervision* wanafanya kazi ya unesi kama Nesi aliyemaliza chuo.

Kwa hiyo, ile *quality* ya *practical* ikawa haipo. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Lyimo kwamba sasa hivi Manesi wote ambao ni *enrolled* na *registered* wanapata kazi tena katika *system* ya Serikali ambayo inawapa motisha kuliko kwenye *private sector*.

Swali la pili, anasema kwamba hatuoni kama kupunguza kutaongeza vifo vya akina mama zaidi na vya watoto. Naomba nikuhakikishie kwamba mahali popote ambapo tumewapeleka hawa Manesi na ndio sababu kwamba sasa wameongezeka kwenye vituo vyetu vya afya na kwenye *dispensary* hivyo vifo vinaanza kupungua na akina mama wanaanza kwenda kuzalishiwa Hospitali kwa sababu ziko karibu nao na hawa vijana wetu wanafanyakazi nzuri na kwa ari kubwa sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sina muda kwa swali hilo, hata hivyo sijakiuka kanuni ninatumia muda tuliotumia kuwasilisha Hati Mezani.

Na. 292

Ujenzi wa Bandari ya Kipili

MHE. DEUSDERIUS J. MIPATA (K.n.y. MHE. ALLY KEISSY MOHMAED) aliuliza:-

Serikali imejenga Bandari ya Kipili, lakini hakuna barabara inayofikia Bandarini:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara hiyo ya kilomita 7?

WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Katongoro – Kipili lenye urefu wa kilometra 7.27 ni barabara ya Mkoa inayoishia katika bandari ya zamani ya Kipili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mamlaka ya bandari kujenga bandari mpya ya Kipili mbali na bandari ya zamani ilikokuwa inaishia barabara ya Katongoro – Kipili na kwa kutambua umuhimu wa Bandari ya Kipili, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Uchukuzi itaangalia uwezekano wa kujenga barabara kutoka Bandari ya zamani hadi Bandari mpya ya Kipili.

MHE. DEUSDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ujenzi wa kukamilika kwa Bandari ya Kipili kutasababisha uwepo wa mizigo mingi na wafanyabiashara wengi wa nje na ndani kutumia bandari hiyo na kwa sababu uzito huo itahitaji kuwa na barabara ya lami kutoka Namanyere mpaka Kilando.

(a)Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuunganisha barabara hiyo iwe ya lami kutoka Namanyere mpaka Kilando?

(b)Changamoto hii inafanana na changamoto iliyopo kwenye Jimbo langu la Nkasi Kusini, barabara ya Kitosi wa Mpemba na barabara ya Nkanakala zote zinakwenda Ziwa Tanganyika. Barabara hizi zimekuwa na changamoto kubwa na ni barabara ambazo Mheshimiwa Rais, alizotolea ahadi katika Uchaguzi wa Mwaka 2010.

Mkoa katika kutekeleza ahadi ya Rais ilipendekeza kuzipandisha hadhi jambo ambalo lilithibitishwa kwenye swalii langu la msingi tarehe 21 Juni, 2011 kwamba Wizara imeshapata maombi hayo. Kwa huruma namwomba Mheshimiwa Waziri apunguze vifo vya akina mama na watoto kupitia kwenye Bajeti hii kwa kuzishughulikia na kupunguza changamoto ambazo zimebainishwa wakati huo? Ahsante sana. (*Makofii*)

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mipata kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ombi lake la kutengeneza barabara ya Namanyele hadi Kilando kwenye kiwango cha lami nataka niseme kwa dhati kabisa kwamba uwezekano wa kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami haupo na hasa ni kwa kuzingatia kwamba Mkoa wa Rukwa kwa sasa hivi kuna barabara nydingi sana ambazo zinatengenezwa kwa kiwango cha lami. Kuna barabara ya kutoka Tunduma hadi Sumbawanga zaidi ya kilometra 231 ambapo gharama yake ni bilioni 304 kuna barabara ya kutoka Sumbawanga hadi Kasanga kilometra 112 bilioni 133, kuna barabara ya kutoka Sumbawanga hadi Kibaoni bilioni 161.

Kwa hiyo, katika miradi tu inayotengenezwa kwa kiwango cha lami katika Mkoa wa Rukwa kwa sasa hivi ni bilioni 600.

Lakini katika barabara hii aliyoitaja ya Namanyere- Kilando inatengenezwa kwa mpango *PMMR* ambapo unahusisha barabara zingine nydingi kama Ntendo – Munze, Namanyere Kilando, Kitangoro – Kipili jumla ya kilometra 112 na nydingine ya Chara – Paramawe, Kize - Stalike, Stalike – Mpanda na kadhalika ambako kuna bilioni 9 zinatumika katika kutengeneza kwa kiwango cha changarawe na mradi huo utatumika katika kipindi cha miaka mitano.

Kwa hiyo, nataka kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Namanyere – Kilando kwamba barabara hii hatutaitengeneza kwa sasa hivi kwa kiwango cha lami kwa sababu msema ukweli ni mpenzi wa Mungu tumalize kwanza hizi barabara zingine. Katika mipango mingine inayokuja ndipo tunaweza tukaangalia hizi barabara nazo katika kuziweka katika mpango unaotakiwa.

Kuhusu barabara ya Ziwa Tanganyika ambazo ni Halmashauri za Wilaya nimekwishazungumza na Mheshimiwa Mipata tunaangalia ni kwa namna gani hizo barabara zinaweza zikatengenezwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Ningependa niwaombe Mkurugenzi na wahusika wote wa Wilaya hiyo, watoe maombi maalum kupitia fedha za mfuko wa barabara ili barabara hii iweze kutengenezwa kulingana na ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Wabunge, nashukuru sana kwa kipindi cha maswali, tumemaliza maswali yetu yote. Sasa ninayo matangazo ya wageni. Wageni tulionao hapa kwa kweli ni wengi sana, sijui kama tutapata muda wa kuwataja wote.

Lakini nitambulische wageni wa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Mheshimiwa Bernard K. Membe amba ni Balozi Juma Alfa Mpango, Balozi wa Congo ambaye ni kiongozi wa Mabalozi wanaoziwakilishi nchi hapa nchini. *Can you please raise up nso that the house can acknowledge your presence. Yes* namwomba Balozi Alfa Mpango halafu anayefuatia ni Balozi Japheth Isaack. Balozi wa Namibia Nchini Tanzania. (*Makofi*)

Halafu anafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Timothy Clerk Mkuu wa Ujumbe wa Umoja wa Ulaya hapa nchini, *you are welcome in this house.* Tunaye pia Ndugu Ali Rashid Alsheh, mwakilishi na Kiongozi wa Mabalozi wa nchi za Kiarabu kutoka Ubalozi wa Uarabuni. (*Makofi*)

Lakini pia wako wageni wengine Ndugu Criss Gipson, Mkurugenzi Mtendaji wa *Gear Capital of Canada. Yes you are welcome.* Tunaye pia Delft Duvall anatoka *TRX Consultant* ya Canada. Karibuni. (*Makofi*)

Tunaye pia Joseph Kahama, *Chief Operation Officer* wa *Tanzania Royalty Cooperation.* Karibuni sasna. Tunaye Eric Arson, Mkurugenzi Mtendaji wa *Kassim Capital* *you are welcome.* Tunaye Kennedy Changu, Meneja kutoka *Tanzania American International Development. Karibuni sana.*

Tunaye pia Miriam Kizito kutoka *TRX* ya *Canada. You are welcome.* Wageni wengine tunaye Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Ndugu John Haule, karibu sana. Lakini pia yuko Balozi Rajab Gamaha karibu, Balozi Mohamed Mahundi, Mkurugenzi wa Chuo cha Diplomasia karibu sana. (*Makofi*)

Wageni wengine ni kutoka *Department of International Development (DIFD)* ambao ni Piety B., mshauri mwandamizi. Tunaye R. Bidet na mwingine ni Athuman Mbena, Meneja wa *Program*. (*Makofî*)

Wageni tunao wanafunzi 65 na walimu watatu (3) kutoka shule ya sekondari Hazina Dodoma, Karibuni sana, tunawatachia kila la kheri katika masomo yenu. Tunao wanafunzi wengine 60 na walimu watatu (3) kutoka *Hijra Secondary School* Dodoma hawa nadhani hawakupata nafasi. Tunao walimu wa Skuli kutoka Zanzibar karibuni sana Dodoma. (*Makofî*)

Tunao pia wanafunzi 46 kutoka shule ya msingi Kisangaji iliyoko Babati Vijiji Kata ya Mwada wakiongozwa na Diwani wao, mwalimu wao na mfadhili wao kutoka Marekani. Karibuni sana wageni wetu kutoka Babati. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa... (*Makofî*)

Mbona bado sijasema lolote, lakini kabla ya kusema lolote, salamu hizo ziwafikie Mheshimiwa William Ngeleja, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Mheshimiwa Mussa Zungu, lakini Rais wa Simba, Mheshimiwa Aden Rage. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, na hawa ni wachezaji 41 wa timu ya mpita ya Yanga ambao ni Klabu Bingwa ya Tanzania na washindi wa Kombe la Kagame wakiongozwa na Mwenyekiti wa timu hiyo, Ndugu Llyody Nchunga. Karibu sana, simuoni Mheshimiwa Samuel Sitta hapa, lakini najua huko aliko salamu zitamfikia. Mlifanya kazi nzuri na kwa kuwa...Naomba mkae na kwa kuwa kwa mujibu wa Kanuni na mimi nafungwa kusema kitu ambacho sina maslahi nacho, nataka ni-*declare* kwamba na mimi ni mpenzi wa Yanga na mwanachama wa Yanga. (*Makofî*)

Karibuni sana, mmeefanya kazi nzuri, mmetupa heshima na hasa sisi Wanayanga, tutaendelea kuwasifia situ zote na endelezeni wembe uleule kwa Simba, kila mara mtakapokutana. (*Makofî*)

MWONGOZI WA SPIKA

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Mwenyekiti, Kanuni ya 68 (8) naomba Mwongozo.

MWENYEKITI: Sikuoni.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi Lusinde niko hapa, Lusinde.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lusinde Mwongozo.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(8), naomba Mwongozo wako. Timu ya Simba imekuwa bingwa mara saba kwa kombe

hili la Kagame na haijawahi kualikwa hapa Bungeni, timu ya Yanga imekuwa bingwa mara nne tu, imekuwa nongwa kwa nchi hii, naomba Mwongozo wako juu ya ubaguzi huu. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Kweli kwa kweli.

MWENYEKITI: *Order in the house please*, naomba tusikilizane. Mheshimiwa Mbunge ameomba Mwongozo, Mwongozo wangu ni kwamba Yanga ndiyo mabingwa wa ligi ya Tanzania Bara ndiyo mabingwa, lakini pia ni Mabingwa wa Kombe la Kagame na mwisho wa Mwongozo wangu ni kwamba siku ya fainali waliwafunga Simba bao moja bila, bao lililofungwa kwa *cross nzuri* sana, hebu aliepiga ile *cross yupo* hapa? Asimame.

(*Hapa mchezaji aliyetajwa alisimama katika gallery*)

MWENYEKITI: Eh! Safi sana na likapigwa kwa kichwa na mchezaji anaitwa Asamoah, yuko wapi yuko hapo? Safi sana. Huo ndiyo Mwongozo wangu Waheshimiwa Wabunge tuendelee.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia Taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama (*NUU*), naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha 2011/2012. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nachukua fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa tena kuongoza kwa muhula wa pili wa Serikali ya Awamu ya Nne.

Pili, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa imani kubwa aliyonayo kwangu kwa kunichagua kwa mara nyingine tena kuongoza Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Aidha, ninampongeza Dkt. Mohammed Gharib Bilal kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile, ninampongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kwa kuchaguliwa bila kupingwa kuwa Mbunge na kuteuliwa tena na Mheshimiwa Rais na hatimaye kuthibitishwa na Waheshimiwa Wabunge kuwa Waziri Mkuu kwa muhula wa pili wa Serikali ya Awamu ya Nne. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kwa kishindo kushika nafasi ya Spika wa Bunge letu Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivyo kuwa mwanamke wa kwanza kushika nafasi hiyo tangu kupatikana kwa Uhuru wa nchi yetu miaka 50 iliyopita. Uteuzi wake ni kielelezo cha ukomavu wa demokrasia ya nchi yetu na imani kubwa tuliyonayo sisi Waheshimiwa Wabunge juu ya utendaji wake uliotukuka. (*Makofi*)

Kadhalika, nampongeza Naibu Spika, Mheshimiwa Job Ndugai pamoja na Wenyeviti kwa kuchaguliwa katika kusaidia uendeshaji wa Bunge hili Tukufu. Napenda pia kuwapongeza Mawaziri wenzangu pamoja na Naibu Mawaziri wote kwa kuteuliwa kwao na Mheshimiwa Rais kushika nyadhifa hizo. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kupata heshima na dhamana kubwa ya kuwawakilisha wananchi wa Majimbo pamoja na makundi mbalimbali ya jamii katika Bunge hili. (*Makofi*)

Naomba kwa namna ya pekee niwashukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda na Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo kwa hotuba zao ambazo zimetoa mwelekeo wa Taifa letu katika mwaka huu wa fedha. Hotuba zao zimegusia mambo ya kimsingi yanayohusu Wizara yangu. (*Makofi*)

Naomba pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Mawaziri wenzangu wote walionitangulia katika kuwasilisha hotuba zao kwa kuzungumzia kwa ufasaha baadhi ya masuala ya Ushirikiano wa Kimataifa wanayoyashughulikia katika Wizara zao. Wizara yangu imekuwa ikishirikiana vyema na kwa karibu sana na Wizara hizi na mara zote imekuwa ikizingatia ushauri wao kwa umakini mkubwa, ningependa kwa nafasi hii pia kumshukuru sana Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa John Chiligati nimewaona leo asubuhi kwenye *television* wamesema mambo mazito na mmenipunguzia kazi yangu ya leo mchana huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama (*NUU*) chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa kwa ushauri wao ambao umekuwa wa msaada mkubwa katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu kwa mafanikio. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mheshimiwa Mahadhi Juma Maalim, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ambaye ameendelea kuwa wa msaada mkubwa kwangu katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu, Bwana John Haule, Naibu Katibu Mkuu, Balozi Rajabu Gamaha, Wakurugenzi wote, Mabalozi wetu pamoja na wafanyakazi wenzangu wote Wizarani na katika Balozi zetu kwa bidii na kujituma kwao ipasavyo katika kutetea na kulinda maslahi ya nchi yetu ndani na nje na pia kwa kufanikisha kwa wakati hotuba hii ya Bajeti. Ningependa kusisitiza kuwashukuru na kuwasifu sana viongozi na watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Nje wanafanya kazi kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru wapiga kura wangu na wananchi wa Jimbo la Mtama, kwa upendo wao na imani yao kwangu na kunichangua mwaka jana kwa asilimia 86. Napenda pia niwashukuru viongozi wote wa Chama cha Mapinduzi na Serikali ya Mkoa wa Lindi kwa uongozi thabiti na kwa ushirikiano wao mkubwa ambao wamekuwa wakinipatia. Kwa upande wa familia yangu, ningependa kumshukuru sana mke wangu, Dorcas Membe, pamoja na watoto wetu kwa kunitia moyo na nguvu katika shughuli zangu za kila siku. Kwa bahati mbaya Mama Membe hayupo pale juu leo kuangalia na mimi katika Bajeti hii kwa sababu yupo nje ya nchi akimuuguza kijana wetu Denis ambaye amefanyiwa upasuaji mkubwa na namtakia afya njema, nimezungumza nae leo asubuhi na amenipa nguvu sana ya kuitoa hotuba hii bila kinyongo na bila wasiwasi. (*Makofi*)

Lakini nimalizie pia kama ulivyofanya Mwenyekiti kuipongeza kwa dhati sana timu ya Yanga ambao ni mabingwa wa Tanzania na washindi wa Kombe la Kagame. Nifichue siri leo kwamba na mimi ni mpenzi sana wa Yanga ingawa muda mwingi sipo pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijaribu kuileta dunia ndani ya Bunge. Hali ya uchumi na usalama duniani kwa ujumla ni shwari isipokuwa katika maeneo machache ambayo yanahitaji uangalizi wa makini wa Jumuia ya Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya uchumi katika nchi nyingi duniani ikiwemo Tanzania, imeendelea kuimarika baada ya kipindi kigumu cha m dororo wa uchumi ulioikumba dunia mwaka 2008 licha ya baadhi ya nchi kama Ugiriki, Uhispania na Ureno kuendelea kususua katika kuimarisha uchumi wao. Kwa ujumla, hali ya usalama duniani inatia moyo ingawa kuna maeneo machache ambayo yamegubikwa na migogoro ya ndani iliyo sababishwa na shinikizo la kutaka mabadiliko ya kisiasa, kupanda kwa gharama za maisha na ukosefu wa ajira. (*Makofi*)

Hali hiyo imeleta madhara makubwa katika nchi ambazo hazikuingia katika mageuzi ya kisiasa na kiuchumi yaliyoanza katika miaka ya 1980 hadi miaka ya 1990. Madhara hayo ni pamoja na vifo vya raia, ongezeko la wakimbizi, uharibifu wa miundombinu, kuzorota kwa shughuli za uzalishaji na hivyo kuongezeka kwa umaskini na hatari ya kuibuka kwa vitendo vipyta vya kigaidi. Wizara yangu imeendelea kufuatilia na kushiriki kikamilifu katika michakato ya kutafuta suluhuishi ya kudumu ya migogoro hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, hali ya kisiasa na kiusalama Barani Afrika katika kipindi cha mwaka mmoja sasa, ni nzuri isipokuwa katika nchi za Somalia, Sudan, Côte d'Ivoire, Tunisia, Misri na Libya ambako hali ya usalama siyo ya kuridhisha na hali ya kisiasa bado haijaka sawa. Hali hiyo imesababishwa na matukio mbalimbali ambayo kwa sasa nitapenda kuyapitia kwa ufupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Ukanda wa Mashariki ya Kati na Afrika ya Kaskazini limekumbwa na machafuko makubwa yaliyobatizwa jina la Mapinduzi ya Yasmini (*Jasmine Revolution*) kwa upande wa Tunisia au kwingineko kama Chemichemi

ya Uarabuni (*Arab Spring*). Nchi za Misri, Libya, Oman, Jordan, Syria, Yemen na Bahrain zimekumbwa na vuguvugu hili ambalo limekuwa na madhara na matokeo tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimewahi kueleza huko nyuma, sababu zilizochangia machafuko hayo ni nyingi na hakuna majawabu mepesi na wala hakuna jawabu moja linalokidhi hoja ya matukio yote. Lililo dhahiri ni kuwa baada ya nchi kama Tunisia na Misri kufanikiwa kuziondoa Serikali zao zilizokuwa madarakani kwa njia ya amani, bado nchi hizo hazijawa na hali ya utulivu wa kisiasa na kiusalama kwa sababu ya kugombania madaraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, machafuko hayo yameleta athari mbalimbali kwa Bara la Afrika na dunia kwa ujumla. Athari hizo zinatokana na ukweli kuwa nchi za Afrika ya Kaskazini hususan Libya ni wawekezaji Barani Afrika na wachangiaji wakubwa katika Bajeti ya Umoja wa Afrika. Kuingia kwa nchi hizo katika machafuko kunaweza kuathiri Bajeti ya Umoja wa Afrika (*UA*) na uwekezaji katika baadhi ya nchi za Afrika. Pamoja na hayo, hali ya usalama katika eneo la Kaskazini mwa Afrika itaendelea kuwa ya wasiwası kutokana na hali ya usalama nchini Libya kutotengamaa hadi sasa. Hali hii inaweza kuleta machafuko katika nchi nyingine za Kaskazini mwa Afrika. Kwa upande wa uchumi, machafuko haya yatachangia katika kuongezeka kwa bei ya mafuta kutokana na kupungua kwa uzalishaji wake na hivyo kuathiri uchumi wa nchi zinazoagiza mafuta kama Tanzania. Tanzania, inaungana na wadau wote kuunga mkono jitihada za kuhakikisha kuwa nchi hizi zinavuka katika mtihani huu kwa njia ya amani. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti na maandamano ya raia wa Tunisia na Misri yaliyoendeshwa kwa njia ya amani na kutwaa madaraka, hali haikuwa hivyo nchini Libya. Maandamano nchini Libya yalichukua sura ya uasi na ghasia kwa waandamanaji kutumia silaha za kivita na hivyo kusababisha mapigano kati yao na majeshi ya Serikali. Hali hiyo imesababisha madhara makubwa nchini Libya ikiwa ni pamoja na raia kupoteza maisha, kuikimbia nchi yao, kuharibu miundombinu na mali nyingi pamoja na vingine kadhaa kuharibiwa vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hatua zilizochukuliwa na majeshi ya Serikali dhidi ya waasi, Jumuiya ya Kimataifa ilianza kuingwa na hofu na hivyo kuamua kuingilia kati mgogoro huo. Jumuiya ya Nchi za Kiarabu ilisimamisha uanachama wa Libya na baadaye Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lilipitisha Azimio Na. 1973 la tarehe 16 Februari, 2011 Azimio lililopiga marufuku ndege kuruka katika anga ya Libya (*imposition of no fly zone*). Aidha, Azimio hilo liliitaka Jumuiya ya Kimataifa kuchukua hatua za kulinda mali na raia wa Libya dhidi ya mashambulizi ya vikosi vya Serikali ya Libya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia njema ya Azimio Na. 1973, ambalo Tanzania na Umoja wetu wa Afrika uliliunga mkono, utekelezaji wake umevuka mipaka ya madhumuni ya Azimio hilo hata hatima yake ilikuwa nayo haieleweki. Mashambulizi yanayofanywa na majeshi ya Umoja wa Kujihami wa Nchi za Magharibi (*NATO*) na waasi wa Libya pamoja na majibu ya mapigo yanayotolewa na Majeshi ya Serikali

yanaua watu, yanaharibu miundombinu na mali za raia kinyume na Azimio Na. 1973. Kutokana na hali hiyo, Tanzania, Umoja wa Afrika, Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote na baadhi ya nchi za Kiarabu, zililaani na kupinga utekelezaji wa Azimio hilo la Baraza la Umoja wa Mataifa na kutoa wito wa kusitisha mashambulizi ili kutoa fursa ya mazungumzo kufanyika kwa pande zote zinazohusika na kumaliza mgogoro huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu pia nzungumzie suala la maradhi yanayoikumba Afrika yetu. Afrika bado inaendelea kukumbwa na maradhi sugu ya Malaria na UKIMWI. Ugonjwa wa Malaria unaua watu 700,000 kwa mwaka Barani Afrika na kati ya hao vifo 595,000 ni vya watoto chini ya umri wa miaka mitano. Kila mwaka, Afrika ina wastani wa wagonjwa wa malaria milioni 176 wanaopatiwa matibabu. Aidha, Bara la Afrika linapoteza dola za Kimarekani bilioni 12 kwa ajili ya kununua dawa na vyandarua pamoja na matibabu ya Malaria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua uzito na ukubwa wa tatizo hili, Umoja wa Afrika umeamua kwenda vitani kupambana na ugonjwa huu. Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete ambaye sasa ni Mwenyekiti wa viongozi 39 wa Umoja wa Afrika waliopania kutokomeza ugonjwa wa Malaria Barani Afrika, yeye na wenzake wanafanya kazi kubwa ya kuunganisha nguvu za Mashirika mbalimbali duniani yanayojihuisha na utokomezaji wa Malaria, kuelekeza nguvu zao Afrika kwa lengo la kutokomeza na siyo kutibu tu ugonjwa wa Malaria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na ugonjwa wa Malaria, yapo maradhi sugu ya UKIMWI Barani Afrika. Hadi sasa, UKIMWI umeua watu milioni 22.4 Barani Afrika tangu ugonjwa huo uanze mwaka 1984. Kati ya hao watoto na akinamama wapatao milioni 11.2 wamepoteza maisha yao. Tuna wagonjwa milioni tano Barani Afrika wanaopatiwa matibabu na idadi ya watu wanaoambukizwa na UKIMWI kwa siku Barani Afrika sasa wanakaribia 5,000 kwa siku, kwa dunia nzima ni 7,600 kwa siku watu wanaoambukizwa ugonjwa wa UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wote mnavyojuu, ugonjwa huu hauna dawa. Dawa ni sisi wenye. Tuendelee kuelimishana na hasa kuelimisha kina Fataki ili wabadili tabia na tabia zetu ili kukwepa ugonjwa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti na maoni ya baadhi ya watu kuwa mgogoro wa Libya ulipoibuka Umoja wa Afrika ulikaa kimya, siyo ya kweli hata kidogo. Umoja wa Afrika ulichukua hatua mbalimbali ikiwemo ya kuunda Kamati Maalum ya Usuluhihi inayojumuisha viongozi wa nchi tano za Mauritania, Afrika Kusini, Uganda, Mali na Kongo ili kutathmini hali ya kisiasa nchini Libya na kukutana na pande zote zinazohusika kwenye mgogoro huo kwa lengo la kutafuta ufumbuzi kwa njia ya amani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hiyo ilitengeneza na kuwasilisha Mpango wa Amani wa kusuluhiha mgogoro wa Libya (*AU Peace Roadmap*) na ulikuwa na vipengele vitano ambavyo ni kuwalinda raia na kusitisha mapigano; utoaji wa misaada ya kibinadamu kwa raia na wafanyakazi wa kigeni; kuanzisha majadiliano ya kisiasa na pande zinazohusika ili kufikia makubaliano ya kumaliza mgogoro; kuanzisha kipindi cha

mpito ambacho kitahusisha pande zote; na kuridhia mageuzi ya kisiasa ambayo yatakidhi matakwa ya Walibya wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika walifanya mkutano maalum tarehe 25 Mei, 2011 mjini Addis Ababa, Ethiopia na kusisitiza mshikamano kwa nchi za Afrika katika kutetea na kulinda uhuru na umoja wa Libya. Aidha, viongozi hao walilaani mashambulizi ya *NATO* na kutaka yasitishwe mara moja ili kuipa nafasi zaidi Afrika kutekeleza mpango wa Amani (*Road map*) uliowasilishwa kwao na Kamati Maalum ya Umoja wa Afrika. Afrika inaamini kwa dhati kuwa amani ya kudumu nchini Libya haiwezi kupatikana kwa nguvu za kijeshi peke yake. Msimamo huo ulisitisizwa tena na Wakuu wa Nchi na Serikali za Afrika katika mkutano wao wa kumi na saba uliofanyika Malabo, *Equatorial Guinea* mwishoni mwa Juni, 2011.

Napenda kuchukua nafasi hii kusisitiza tena msimamo wa Tanzania kuwa pamoja na nia nzuri ya Azimio Na. 1973 la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, Tanzania kama ilivyo kwa nchi zote za Umoja wa Afrika hazikubaliani na utekelezaji wake na hatima yake. Tunazitaka pande zote zinazopigana yaani *NATO*, majeshi ya waasi na ya Serikali kusitisha mapigano hayo mara moja na kuipa Afrika nafasi ya kumaliza mgogoro huo kwa njia ya amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wa Côte d'Ivoire kama tunavyosema, ulihitimishwa baada ya Mheshimiwa Alassane Ouattara kuapishwa tarehe 9 Mei, 2011 kuwa Rais mpya wa nchi hiyo kufuatia ushindi katika uchaguzi uliofanyika tarehe 28 Novemba, 2010 na kupingwa na baadaye kuondolewa kijeshi kwa Rais aliyeng'ang'ania madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kuwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alitoa mchango mkubwa kama mmoja wa Wajumbe wa Kamati Maalum ya Umoja wa Afrika iliyoundwa kushughulikia mgogoro huo. Kutohakana na mafanikio hayo, Tanzania inaendelea kupata heshima kubwa katika masuala ya utatuza na usuluhishi wa migogoro Barani Afrika. Aidha, uzoefu wa kilichotokea Côte d'Ivoire unatufundisha kuwa Umoja wa Afrika unaweza kumaliza migogoro yake pale inapoachwa huru na bila kuingiliwa katika kushughulikia migogoro hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafurahi kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba kama mnavyofahamu wote, hatimaye Sudan ya Kusini imekuwa Taifa huru tarehe 9 Julai, 2011 na hivyo kuongeza idadi ya nchi huru za Afrika kufikia 54. Nachukua fursa hii kuwapongeza tena Rais Salva Kiir Mayardit na wananchi wote wa nchi mpya ya Sudan ya Kusini kwa kuvuna walichopanda; Uhuru uliotokana na jasho na damu yao. Aidha, Tanzania itaikaribisha kwa mikono miwili nchi ya Sudan ya Kusini itakapoamua kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tanzania itamkumbuka daima mwasisi na mwanamapinduzi marehemu John Garang kwa kuanzisha mapambano yaliyoleta Uhuru Sudan ya Kusini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Rais mstaafu wa Awamu ya Batu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kuongoza jopo la watu watatu mashuhuri walioteuliwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kusimamia mchakato wa kura ya maoni nchini humo. Ni matumaini yangu kwamba Uhuru uliopatikana utapanua nyanja za ushirikiano kati ya nchi yetu na Sudan ya Kusini. Hivyo natoa rai kwa Watanzania wenzangu wachangamkie bila kuchelewa, fursa zilizopo katika Taifa hilo jipya. Wizara yangu itatoa ushirikiano utakaohitajika ili kufanikisha azma hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya usalama nchini Somalia katika siku za hivi karibuni inaleta matumaini baada ya vikosi vya usalama vya Serikali ya Mpito ya Somalia na Umoja wa Afrika (*AMISOM*) kufanya mashambulizi makali dhidi ya wanamgambo wa Al-Shabaab. Kutokana na mashambulizi hayo, maeneo mengi yaliyokuwa ngome ya Al-Shabaab mjini Mogadishu yapo chini ya Serikali ya mpito na hivyo kusaidia kuimarisha hali ya usalama na usambazaji wa misaada ya kibinadamu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa hivi sasa kuhusiana na mgogoro wa Somalia ni uhaba wa askari wa kulinda amani. Tanzania inazisihi nchi zilizoahidi kuchangia vikosi vya kulinda amani zitekeleze ahadi hiyo. Aidha, tunatoa wito kwa Umoja wa Mataifa kuhakikisha kuwa Azimio lake la kuongeza vikosi vya *AMISOM* kutoka idadi ya majeshi 8,000 hadi kufikia 12,000 linatekelezwa haraka iwezekanavyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania itaendelea kushirikiana na Jumuia ya Kimataifa katika juhudzi za kutafuta suluhu ya mgogoro wa Somalia. Mwezi Aprili 2011, Rais wa Somalia Mheshimiwa Sheikh Sharif Sheikh Ahmed alifanya ziara hapa nchini na kuonana na mwenyeji wake Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo mchakato wa amani nchini Somalia ulijadiliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuzorota kwa amani ya usalama kwa muda mrefu nchini Somalia kumezusha baa la njaa nchini humo na kuwafanya baadhi ya vijana wa Kisomali kujihusisha na vitendo vya uharamia kwenye pwani ya Afrika Mashariki. Matukio ya uharamia yanazidi kuongezeka na hivyo kuathiri uchumi wa nchi yetu. Athari hizo ni pamoja na kupanda kwa bei za bidhaa kutokana na kuongezeka kwa gharama za usafirishaji. Gharama hizo zinatokana na mahitaji ya ulinzi kwa ajili ya kusindikiza meli za bidhaa na kufanya doria katika eneo hilo na kuongezeka kwa gharama za bima na meli kulazimika kuzunguka umbali mrefu ili kukwepa maharamia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania haiwezi kukwepa athari za uharamia kutokana na mahali ilipo kijiografia. Hivyo Wizara yangu inashirikiana na wadau wengine zikiwemo nchi kubwa na zenye uwezo, kuongeza nguvu ya kukabiliana na changamoto hiyo. Juhudi hizi ni endelevu na zinahitaji ushirikiano mpana.

Meshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imeendelea kushiriki katika shughuli za Umoja wa Mataifa hususan katika masuala ya amani na usalama, haki za binadamu na maendeleo. Ushiriki huu wa Tanzania umetuletea sifa nyingi pamoja na kuijenga taswira ya nchi yetu katika medani za Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la amani na usalama, Wizara yangu ikishirikiana na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, imeendelea kushiriki kikamilifu katika ulinzi wa amani chini ya mwavuli wa Umoja wa Mataifa. Hivi sasa nchi yetu ni moja ya wachangiaji muhimu wa maafisa na askari kwenye misheni za kulinda amani za Umoja wa Mataifa, wakiwemo wanajeshi, polisi na maafisa magereza. Wote hao wameonyesha uhodari, utii na umakini mkubwa katika kutekeleza majukumu yao na hivyo kuipatia nchi yetu sifa kubwa duniani. Kwa kutambua mchango wetu mkubwa hususan kule Darfur, Meja Jenerali Wynjones Mathew Kisamba, Mkuu wa Kamandi ya Majeshi ya Ardhini wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), ameteuliwa kuwa Naibu Kamanda wa Vikosi Mahuluti vya Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa huko Darfur (*UNAMID*). Naomba tuungane kumpongeza yeye, pamoja na maafisa na askari wetu wote wanaotumikia Umoja wa Mataifa kwa kazi nzuri wanayoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ilishiriki kikamilifu katika Mikutano mikubwa ya Kimataifa kama vile Jukwaa la Kimataifa la Uchumi (*World Economic Forum*) huko Davos, Switzerland, mwezi Januari, 2011 na Cape Town, Afrika Kusini mwezi Mei, 2011 ambapo nchi yetu ilipata fursa ya kunadi mkakati wake wa kuboresha kilimo nchini unaojulikana kama *The Southern Agriculture Growth Corridor of Tanzania – SAGCOT*. Aidha, mikutano mingine ambayo Tanzania ilishiriki kikamilifu ni pamoja na ule uliohusu Malengo ya Milenia uliofanyika jijini New York mwezi Septemba, 2010 na ule wa nchi maskini sana duniani uliofanyika Istanbul, Uturuki mwezi Mei 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imeendelea kupewa heshima kubwa na Umoja wa Mataifa baada ya Katibu Mkuu wa Umoja huo, kumteua Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa Mwenyekiti Mwenza wa Tume kuhusu afya ya akina mama na watoto (*Commission on Information and Accountability for Women's and Children's Health*). Tume hiyo ilipewa jukumu la kuunda mfumo wa kufuatilia ahadi na fedha zilizotolewa na Mataifa na vyombo mbalimbali vya Kimataifa na namna zitakavyotumika kuboresha afya ya akina mama na watoto. Tume hiyo imekamilisha kazi yake na itawasilisha taarifa rasmi katika Kikao kijacho cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mwezi Septemba mwaka huu 2011. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitishwa kwa Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Misaada na Maendeleo nchini (*United Nations Development Assistance Plan*) utakaoteklezwa kuanzia Julai, 2011 hadi Juni, 2015 katika kugharamia miradi mbalimbali ni kielelezo kingine cha mafanikio ya Mradi wa Majaribio unaoteklezwa nchini na Umoja wa Mataifa ujulikanao kama *One UN*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika tunajivunia heshima kubwa ambayo tumepewa na Umoja wa Mataifa kupitia kwa Bwana Ban Ki-moon, Katibu Mkuu wa Umoja huo. Tunampongeza kwa dhati kwa kuchaguliwa tena kwa kishindo kuongoza Sekretarieti ya Umoja wa Mataifa kwa muhula mwingine wa miaka mitano. Tunaahidi kumpa ushirikiano wa kutosha katika kutekeleza majukumu yake hayo. (*Makofi*)

Mheshimwia Mwenyekiti, nizungumzie kundi la nchi zisizofungamana na upande wowote (*NAM*). Ninayo furaha kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa kundi la nchi zisizofungamana na upande wowote (*NAM*) linatimiza miaka 50 tangu kuanzishwa kwake. Kundi hili limeendelea kuwa sauti ya nchi zilizo katika Ukanda wa Kusini mwa dunia katika kukabiliana na ubabe wa Mataifa makubwa. Mikutano ya *NAM* inaendelea kutoa fursa nzuri kwa nchi wanachama kukutana na kuendeleza ushirikiano wa kiuchumi na kijamii. Sherehe za miaka 50 ya *NAM* zitahitimishwa mjini Belgrade, Serbia zamani ikijulikana kama Yugoslavia mwezi Septemba 2011. Kama historia inavyotukumbusha, *NAM* ilizaliwa jijini Belgrade mwaka 1961.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Jumuiya ya Madola, hivi sasa Wizara yangu ipo katika mchakato wa maandalizi ya ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa Wakuu wa nchi na Serikali wa nchi za Jumuiya ya Madola (*CHOGM*) utakaofanyika Perth, Australia kuanzia tarehe 28 hadi 30 Oktoba 2011. Kauli mbiu rasmi ya mkutano huo ni *Building National Resilience, Building Global Resilience*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kaulimbiu hii inalenga zaidi katika kutekeleza shabaha mbalimbali za Jumuiya hiyo ambazo ni kuimarisha demokrasia, utawala wa sheria na utawala bora mionganoni mwa nchi wanachama. Aidha, changamoto mbalimbali zinazoikibili dunia, mathalan, hali ya chakula, kusimamia maliasili, maendeleo endelevu, mabadiliko ya hali ya hewa pamoja na namna ya kujinasua kutoka katika m dororo wa kiuchumi ulioikumba dunia mwaka 2008 zitajadiliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umoja wa Afrika unaendelea na mchakato wa kubadili Kamisheni yake kuwa mamlaka kufuatia maagizo yaliyotolewa na Wakuu wa Nchi na Serikali za Umoja huo kwenye kikao chao kilichofanyika Sirte, Libya mwezi Julia, 2009. Hatua inayoendelea hivi sasa ni kukamilisha Itifaki ya Bunge la Afrika na Mahakama ya Afrika. Kwa ujumla Umoja wa Afrika unaendelea kuimarika licha ya changamoto mbalimbali zinazolikobili Bara la Afrika hususan migogoro, umaskini na maradhi. Umoja huo unafanya kila linalowezekana kwa kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa na wadau wengine, kukabiliana na changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inaendelea kushiriki kikamilifu katika shughuli za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ushiriki huu umeleta manufaa mbalimbali katika nyanja za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Katika kupanua wigo wa ushirikiano, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wamepitisha Itifaki ya Uratibu wa Sera za Mambo ya Nje kwa Nchi wanachama wa jumuiya. Itifaki hiyo itazipa nchi wanachama fursa ya kuendeleza ushirikiano katika masuala ya kidiplomasia na kikonseli kupitia Balozi zetu zilizopo nje ya eneo la Jumuiya hiyo. Wizara yangu itaendelea kushiriki na

kushauri vilivyo hususan jinsi ya kutengeneza mfumo bora wa kuhakikisha Itifaki hii inatekelezwa bila kuathiri maslahi muhimu ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) Tanzania imeendelea kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha demokrasia inashamiri katika eneo la *SADC*. Ustawi wa demokrasia umesaidia kudumisha mazingira mazuri ya biashara, uwekezaji, amani na utulivu katika nchi za *SADC*. Ukomavu wa demokrasia nchini, uliojidhihirisha kupitia Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 ambao ulishuhudiwa na waangalizi zaidi ya 100 kutoka nchi za *SADC* na kuthibitishwa kuwa ulikuwa huru na wa haki, umezidi kujengea heshima kubwa nchi yetu, ndani na nje ya Bara letu la Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka 50 ya Uhuru, nchi yetu imejijengea heshima ya pekee katika harakati za ukombozi duniani hususan Kusini mwa Afrika. Tumeendelea kuwa wasimamizi wa haki na usawa na hatujawahi kusita kuidai haki hiyo kwa niaba ya wale walionyanyaswa, kubaguliwa, kukandamizwa na kutawaliwa. Vilevile, nchi yetu imekuwa tegemeo la wengi katika usuluhishi na utatuzi wa migogoro iliyopo katika baadhi ya nchi za *SADC*. Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine imeendelea kuhakikisha heshima hiyo inadumishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua mchango wetu, *SADC* ilimtunuku Mtanzania mwenzetu Brigedia Jenerali Mstaafu, Balozi Hashim Iddi Mbita nishani ya *SADC* ya Sir. Seretse Khama (*Sir. Seretse Khama SADC Award*) kwa mchango wake katika harakati za ukombozi wa Mwafrika. Tukio hili la kihistoria lilifanyika sanjari na maadhishimo ya miaka 30 ya *SADC* pamoja na ufunguzi wa jengo la Makao Makuu ya *SADC* lililopo mjini Gaborone, Botswana mwezi Novemba 2010. Kiongozi mwingine aliywahidi kutunukiwa tuzo hiyo ni Mheshimiwa Kenneth Kaunda, Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Zambia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudzi za kuziunganisha Jumuiya za *SADC*, *EAC* na *COMESA* ili kuwa na eneo moja huru la kibashara zinaendelea. Mkutano Mkuu wa Pili wa Wakuu wa Nchi na Serikali kutoka nchi zilizo katika eneo linalokusudiwa kuanzhishwa ushirikiano, waliweka saini mkataba wa kuanzisha Soko Huru la Pamoja mjini Sandton, Afrika Kusini tarehe 12 Juni, 2011 na wakazindua rasmi majadiliano kuhusu soko hilo. Soko hili litajumuisha nchi 27 kati ya 54 za Afrika ikiwemo Sudan ya Kusini zenye wakazi wasiopungua milioni 700 na Pato la Taifa la jumla la takriban dola za Kimarekani trilioni 1.6. Changamoto iliyopo mbele yetu ni kujipanga vyema ili tuweze kunufaika na matunda ya ushirikiano huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ufinyu wa Bajeti, Wizara yangu imeendelea kuyapa uzito stahiki masuala ya diplomasia ya uchumi ambayo kimsingi yanahitaji fedha nyingi kuyatekeleza. Katika kufanikisha hilo, Wizara imejishughulisha katika maeneo ya kutafuta wawekezaji, kuhamasisha watalii na kutafuta masoko ya bidhaa zetu. Aidha, Wizara imeendelea kuratibu ziara za viongozi wetu nje ya nchi na ushiriki wa Tanzania katika Tume za Kudumu za Pamoja za Ushirikiano (*JPCs*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011 viongozi wakuu wa Kitaifa walifanya ziara na kuhudhuria mikutano katika nchi mbalimbali duniani zenyelengo la kukuza diplomasia ya uchumi, kukuza ushirikiano na kuimarisha ujirani mwema baina ya Tanzania na nchi nyingine pamoja na taasisi na Mashirika ya Kimataifa. Aidha, katika kipindi hiki viongozi kutoka nchi mbalimbali pamoja na taasisi za kikanda na Kimataifa waliitembelea Tanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya ziara hizi za viongozi wetu na viongozi kutoka nje ni pamoja na kusainiwa kwa mikataba ya ushirikiano, kutangaza fursa za uwekezaji na vivutio vya utalii nchini. Kwa mfano, ziara ya Mheshimiwa Lula Da Silva, Rais wa Jamhuri ya Brazil aliyoifanya mwezi Julai, 2010 ilifanikisha kusainiwa kwa mkataba wa makubaliano kati ya Shirika la Petroli la Brazil (*Petrobras*) na Shirika la Maendeleo ya Petroli la Tanzania (*TPDC*); mkataba wa makubaliano kati ya Ofisi ya Makamu wa Rais (*Mazingira*) ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Mazingira ya Jamhuri ya Brazil kuhusu kupunguza hewa chafu itokanayo na ukataji miti na uharibifu wa mazingira na makubaliano ya ushirikiano katika masomo ya diplomasia baina ya Chuo cha Diplomasia cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Taasisi ya Ruo Branco ya Jamhuri ya Brazil na mwisho, mazungumzo ya Tanzania kufutiwa deni lake na Brazil yalifanyika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwengine ni ziara ya mwezi Aprili, 2011 ya Mheshimiwa Dkt. Manmohan Singh, Waziri Mkuu wa India, iliyopelekea makubaliano ya awali ya ushirikiano wa pamoja baina ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Bodi ya Udhramini ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) na Hospitali ya Apollo ya India kuhusu kuanzisha hospitali kubwa ya kisasa itakayokuwa inatoa huduma za magonjwa ya moyo, ubongo na mifupa na mpangokazi wa pamoja baina ya Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo la Tanzania (*SIDO*) na Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo la India. Aidha, katika ziara hiyo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya India zilifikia makubaliano ya mikataba ya kutolipisha kodi mara mbili na kuzuia ukwepaji wa kodi ya mapato. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mikataba mbalimbali baina ya Tanzania na nchi nyingine duniani, Mikataba ya Kikanda na Mikataba ya Uenyeji. Katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Wizara yangu imesimamia majadiliano yaliyofanikisha kusainiwa kwa mikataba ishirini katika nyanja za biashara, mazingira, sayansi na teknolojia, utamaduni, usafirishaji na haki za binadamu. Tunatarajia mikataba yote iliyosainiwa na mingine itakuwa ni chachu ya maendeleo kwa Tanzania, natoa rai kwa taasisi za Serikali na nyinginezaji zijipange vizuri kufanikisha utekelezaji wa mikataba hii kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushirikishwaji wa Watanzania wanaoishi Ughaibuni (*Diaspora*), Wizara yangu tayari imeunda Idara ya *Diaspora* na tumefanikiwa kuwafikia kwa wingi Watanzania walioko nje kupitia mikutano na majukwaa mbalimbali na kupata maoni yao. Kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar ameunda Kitengo cha *Diaspora* kinachoongozwa na Naibu Katibu

Mkuu ambacho kipo chini ya ofisi yake na tunashirikiana nacho kwa karibu sana. (*Makofi*)

Aidha, yapo maelewano na wadau mbalimbali ikiwemo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Benki Kuu, Kituo cha Uwekezaji, Mamlaka ya Mapato, Shirika la Nyumba la Taifa, Mfuko wa Uwekezaji (*UTT*), Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii na wadau nje ya Serikali kama Benki za *CRDB*, Benki ya *Exim* (Tanzania), *Commercial Bank of Africa* na Mawakala Binafsi wa Ajira (*Recruitment Agencies*). Maelewano haya yanasaidia katika mkakati mzima wa kujenga mazingira ya kisheria na kisera ya kuwezesha *Diaspora* kushiriki kikamilifu katika kuleta maendeleo ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muda uliobaki ili ni-determine speed. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Zilizobaki Mheshimiwa Waziri ni dakika 25.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Nakushukuru, zitanitosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua iliyo mbele yetu ni kwa Wizara yangu kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Mwanasheria Mkuu, kujenga mazingira mazuri kwa *Wana-diaspora* na kuondoa kero ambazo zinaathiri jitihada zao za uchangiaji katika maendeleo ya nchi yetu. Hivi sasa Wizara zetu zinajandaa kuwasilisha Waraka kwenye Baraza la Mawaziri, ili ujadiliwe na kisha kwa wakati muafaka, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kutakiwa kuwasilisha rasmi mbele ya Bunge lako Tukufu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Uraia kwa majadiliano. Kwa kuwa mchakato wa suala hili unagusa Katiba, ni azma yetu kuona kwamba suala hili linakwenda pamoja na mchakato wa Katiba mpya. Ni dhamira ya Wizara yangu kuona suala la uraia wa nchi mbili linazinduliwa sanjari na Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa *APRM* nchini Tanzania sasa unaelekea ukingoni baada ya kusimama mwaka jana kutokana na Uchaguzi Mkuu. Tunatarajia kupokea timu ya wataalamu kutoka Makao Makuu ya *APRM* mwezi ujao mwaka, 2011 yaani Agosti, kwa ajili ya maandalizi ya tathmini itakayofanyika mwezi Septemba, 2011. Inatarajia kuwa taarifa kamili ya Tanzania itawasilishwa katika Mkutano Mkuu wa nchi wanachama wa *APRM* mwezi Julai 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma ya kikonseli, Wizara yangu ndiyo yenye dhamana ya kulinda maslahi ya Watanzania wanaoishi nje ya nchi. Kufuatia machafuko yaliyotokea hivi karibuni katika nchi za Mashariki ya Kati na Kaskazini mwa Afrika, hatua za makusudi na za haraka zilichukuliwa ili kuhakikisha kuwa Watanzania wanaoishi katika nchi hizo hawapatwi na madhara yoyote. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuwarudisha nyumbani Watanzania 83 kutoka Misri na nane kutoka Libya; kuufunga kwa muda Ubalozi wa Tanzania nchini Misri, kukusanya taarifa zote muhimu na kuziwasilisha Wizarani; kuwaita na kuzungumza na wawakilishi wa nchi husika hapa Tanzania ili kufahamu kwa kina mustakabali na hatua ambazo Serikali zao zinachukua

katika kukabiliana na machafuko hayo. Aidha, Wizara imetua taarifa kwenye vyombo vya habari juu ya maendeleo ya hali ya Watanzania na hali ya usalama katika nchi hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inatoa changamoto kwa Serikali kuchukua hatua za haraka katika kuwaokoa raia wake kila inapobidi. Hivyo, ninatoa wito kwa Watanzania wanaoishi nchi za nje kujirodhesha kupitia jumuiya zao katika Ofisi za Balozi zetu ili kuwafikia kwa urahisi kila inapohitajika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoleza awali nchi yetu imeendelea kuwijengea heshima kubwa Kimataifa kama Taifa lililokomaa katika nyanja za utawala bora, usuluhishi wa migogoro, demokrasia, utawala wa sheria, utawala unaojali haki za binadamu na utawala unaowekeza kwa watu wake. Hali hii imefanya nchi yetu kuzidi kuaminiwa na Mataifa mengine, Taasisi na Mashirika ya Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hayo, Umoja wa Mataifa umemteua Rais wetu kuwa Mwenyekiti Mwenza wa Kamisheni ya kupunguza vifo vya watoto na akinamama na pia imemteua Meja Jeneralis Kisamba kuwa Naibu Kamanda wa Majeshi ya Umoja wa Mataifa ya kulinda amani Darfur, Sudan. Aidha, viongozi wa Umoja wa Afrika wamepitisha jina la Mtanzania Ludovick Utouh, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa mgombea pekee wa Bara la Afrika atakayewania nafasi ya ujumbe wa Bodi ya Ukaguzi ya Umoja wa Mataifa kwenye uchaguzi utakaofanyika mwezi Septemba mwaka huu New York, tuna hakika kabisa ya kushinda. Naye Mtanzania Profesa Chris Peter Maina amepitishwa na viongozi hao hao wa Umoja wa Afrika kugombea nafasi ya ujumbe wa Kamati ya Sheria ya Umoja wa Mataifa. Vile vile Umoja wa Afrika kwa kauli moja umepitisha jina la Tanzania kugombea nafasi ya ujumbe kwenye Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (*International Atomic Energy Agency*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya yote ili kuwaeleza Watanzania kuwa nchi yetu inaheshimika sana duniani na tuwapuuze wale wachache wanaobeza kuwa nchi hii haiheshimiki duniani! Tunaheshimika sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Taasisi ya Kitaalamu ya *Fund for Peace* ilitoa tathmini yake ambayo huitoa kila mwaka kuonyesha hali ya usalama duniani. Tathmini hiyo huzingatia vigezo 12 vikiwemo idadi ya watu, watu wanaolazimika kuwa wakimbizi katika nchi; uhasama na visasi baina ya makundi, hali ya haki za binadamu na utawala wa sheria, kukubalika kwa Serikali, mwenendo wa vyombo vya usalama, taswira ya utumishi wa umma, tofauti za mgawanyo wa keki ya Taifa, tofauti za matabaka ya umangimeza (*factionalized elites*) na uwezo wa kuhimili shinikizo kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ripoti yao ya mwaka 2011, Tanzania ni moja kati ya nchi zilizoonekana kuwa salama zaidi dhidi ya hatari za kiusalama. Tanzania ni nchi ya 65 kati ya nchi 193 duniani na inaongoza nchi zote za Afrika Mashariki na za SADC kwa amani na usalama. Tuna kila sababu ya kuienzi amani yetu tunapoadhimisha

miaka 50 ya Uhuru wetu na tusikubali kuruhusu mtu au watu wachache kuvuruga amani nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina jumla ya watumishi 440, kati ya watumishi hao 249 wapo Makao Makuu, 19 wapo Ofisi ya Mambo ya Nje Zanzibar na 172 wapo katika Balozi zetu nje. Katika mwaka wa fedha 2010/2011 Wizara iliajiri jumla ya watumishi wapya 49 kati ya 53 waliodhinishwa. Watumishi wanne ambao walifaulu usaili hawakuweza kujiunga na Wizara kutokana sababu mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya watumishi 29 walipelekwa mafunzoni kati ya hao 20 walipelekwa mafunzo ya muda mrefu na tisa mafunzo ya muda mfupi ili kuongeza ujuzi katika taaluma zao. Aidha, jumla ya watumishi 59 walipandishwa vyeo na wengine 12 walithibitishwa kazini katika mwaka wa fedha 2010/2011. Wizara itaendelea kusimamia maendeleo ya watumishi na kuboresha maslahi yao kadri hali itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yaliyoelezwa hapo juu, changamoto kubwa inayoikabili Wizara yangu ni ufinyu wa Bajeti. Hali hiyo imesababisha Wizara kutofikia ipasavyo malengo ya utekelezaji wa sera ya mambo ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara yangu imeongeza ufanisi katika masuala ya usimamizi wa Bajeti na fedha kwa ujumla ambapo kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Balozi nane zilipata Hati Safi za Ukaguzi wa Hesabu ikilinganishwa na Balozi tano zilizopata hati kama hiyo kwa mwaka 2008/2009. Balozi 21 zilipata Hati Safi zenye masuala ya msisitizo ikilinganishwa na Balozi 23 mwaka 2008/2009. Aidha, Balozi mbili zilipata Hati zenye Shaka ikilinganishwa na Balozi tatu zilizopata hati kama hiyo mwaka 2008/2009. Kwa mwaka 2009/2010, hakuna Ubalozi uliopata hati isiyoridhisha ikilinganishwa na Ubalozi mmoja kwa mwaka wa fedha 2008/2009. Wizara yangu itaendelea kusimamia ipasavyo matumizi ya fedha za Serikali Wizarani na katika Balozi zake 32 kwa misingi ya sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kudhibiti matumizi ya fedha Balozini, tayari Balozi saba zimewekewa mtandao wa malipo ya Serikali (*Integrated Financial Management System - IFMS*). Wizara yangu kwa kushirikiana na Hazina itaendelea kusimamia utekelezaji wa mpango huo katika Balozi zilizosalia. Vile vile, Wizara imeweka saini mikataba na Mabalozi wa Heshima 14, ili kudhibiti taratibu za kukusanya maduhuli kwenye Balozi hizo. Wizara itaendelea kutekeleza zoezi hilo kwenye Balozi za Heshima zilizosalia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inaendelea na hatua za kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa kituo kipyaa cha mikutano mjini Arusha kitakacho julikana kama *Mt. Kilimanjaro International Convention Centre (MK-ICC)*. Mradi huo ni moja ya nguzo muhimu utakaokiwezesha kituo kupanua wigo wa huduma zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa mara nyingine tena, Kituo kimepata Hati Safi ya hesabu zake zilizoandaliwa na kukaguliwa kwa wakati kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni, 2010. Kituo kilipata faida ghafi ya shilingi 988,890,266.00 na kinaendelea kufanya shughuli zake kwa ufanisi na bila kuwa tegemezi kwa Serikali. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012 Kituo kimepanga kuingiza mapato ya shilingi 7,769,743,737.00 kutokana na vyanzo vyake mbalimbali vya mapato na kinategemea kupata ziada ghafi ya shilingi 1,405,841,931.00. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa Chuo cha Diplomasia sasa kimepata usajili wa Baraza la Ithibati ya Elimu ya Ufundı (*National Council of Technical Education - NACTE*). Hatua hii itafanya mafunzo yanayotolewa na Chuo kutambulika Kitaifa na Kimataifa, hivyo kufanya idadi ya wanafunzi kuongezeka kuliko ilivyokuwa awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo kinaendelea kuishauri Wizara yangu katika masuala mbalimbali ya Kidiplomasia. Aidha, Chuo kimekuwa kikijishughulisha na utoaji wa taaluma ya utatuza wa migogoro, tafiti na ushauri wa kitaalamu katika masuala ya itifaki, diplomasia ya uchumi, stratejia, menejimenti ya mahusiano ya nje na kutoa mafunzo kwa watumishi wa Wizara na wanafunzi wengine kutoka ndani na nje ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 Wizara yangu ilipangia kutumia kiasi cha shillingi 112,336,928,000.00 kati ya fedha hizo shilingi 64,040,792,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (*OC*); shilingi 3,796,136,000.00 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi 44,500,000,000.00 ni kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2011 Wizara ilikuwa imepokea kutoka Hazina kiasi cha shilingi 93,959,549,620.00; kiasi hiki cha fedha ni sawa na asilimia 83.4 ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kuititia Balozi zake ilitegemea kukusanya kiasi cha shilingi 12,732,300,000.00. Hadi kufikia tarehe 31 Juni, 2011 kiasi cha shilingi 15,756,949,932.00 kilikusanya kikiwa ni makusanyo ya maduhuli Balozini na Makao Makuu. Kiasi hiki cha fedha ni sawa na asilimia 123.76 ya makusanyo ya fedha zote za maduhuli zilizokadiriwa kukusanya Balozini na Makao Makuu kwa mwaka wa fedha 2010/2011. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, pamoja na mambo mengine, Wizara yangu imepanga kutekeleza malengo makuu muhimu kulingana na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 kama ifuatavyo:-

Kwanza kuitangaza nchi yetu kama moja ya nchi duniani zenyе mazingira muafaka kwa ajili ya uwekezaji hasa kutokana na historia yake ya miaka mingi ya amani,

umoja, utulivu na mshikamano wa Kitaifa. Pili, kutangaza utajiri mkubwa wa vivutio vya utalii tulivyonyavyo na kuvutia watalii wengi kutoka mabara yote ya dunia waje kuviona. Tatu, kuzitafutia masoko bidhaa zetu zenye ubora unaotakiwa katika nchi za nje kwa kushauriana na wazalishaji wa ndani wa bidhaa hizo. Nne, kudai mageuzi ya Umoja wa Mataifa hususan katika Baraza la Usalama la Umoja huo, kwa kuzingatia hoja ya wingi wa *agenda* zinazojadiliwa na kuamuliwa na Baraza hilo bila ya uwakilishi wetu na tano, kushiriki katika utatuizi na usuluhihi wa migogoro inayotokea barani Afrika na nchi nyingine duniani, kama vile mgogoro wa Libya.

Sita, kuendelea kutekeleza mpango wa ujenzi, ununuzi na ukarabati wa majengo ya ofisi na makazi balozini na saba, kukamilisha mchakato wa kuitambua na kushirikisha Jumuiya ya Watanzania wanaoishi ughaibuni na kuweka utaratibu utakaowawezesha kuchangia maendeleo ya taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kutekeleza kikamilifu kazi zilizotajwa hapo juu, Wizara yangu imepangiwa kiasi cha shilingi 125,102,875,000.00 kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Kati ya fedha hizo shilingi 76,387,187,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (*OC*), shilingi 4,215,688,000.00 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 44,500,000,000.00 ni kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara (*OC*) shilingi 2,049,475,000.00 ni kwa ajili ya mchakato wa *APRM*, shilingi 1,504,574,478.00 ni kwa ajili ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na shilingi 1,400,436,227.00 ni kwa ajili ya fedha za mishahara na Matumizi ya Kawaida ya Chuo cha Diplomasia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara yangu inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 14,872,492,000.00 kama maduhuli ya Serikali. Kwa maana ya utekelezaji wa Bajeti, kiasi hiki cha maduhuli tayari kimehesabiwa kama sehemu ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):
Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa Iamuliwe*)

MHE. AUGUSTINO M. MASELE (K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2007, Kanuni ya 99 (7) na Kanuni ya 114(11), naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha 2010/2011; na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya

Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2011/2012, na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kujadili Taarifa hii na hatimaye kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake ya kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, tarehe 23 Machi, 2011, Kamati ilikutana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na kupata maelezo kuhusu muundo wake na utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2010/2011. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufuatilia kwa karibu na kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii, tarehe 24 Machi, 2011, Kamati ilipokea maelezo ya Wizara kuhusu hali ya ushirikiano baina ya nchi yetu na Jumuiya ya Kimataifa pamoja na matukio mbalimbali kuhusu diplomasia duniani na uhusiano wa Mataifa ulivyo. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Tanzania ni nchi inayoheshimu misingi ya uhusiano na ushirikiano wa Kimataifa pamoja na diplomasia duniani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuheshimu kanuni na taratibu za Kidiplomasia bila kuathiri maslahi na mustakabali wa Taifa letu.

Aidha, Kamati imeguswa na hali inayoendelea nchini Libya ambapo nchi za Magharibi na *NATO* wanatumia nguvu kubwa za kijeshi kuishambulia Serikali ya Kanali Muammar Gaddafi wa Libya inayotambuliwa na Umoja wa Afrika kuwa halali. Ni maoni ya Kamati kuwa kitendo hicho ni uonevu mkubwa na ni uvunjifu wa heshima kwa utawala wa Libya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaamini kuwa kuivamia nchi yenyewe mamlaka kamili na moja ya wanachama wa Umoja wa Afrika ni dharau na ni kuudhalilisha Umoja wa Afrika. Inasikitisha kuwa Umoja wa Afrika ulikaa kimya kwa muda mrefu bila ya kuchukua hatua yoyote dhidi ya hali inayoendelea nchini Libya. Aidha, hakuna kauli yoyote iliyotolewa na Umoja huu angalau kuonyesha kutoridhishwa na tukio hilo la kibabe. Hali hii si njema kwa Umoja wa Afrika na inaathiri hadhi ya Umoja huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, tarehe 01 Juni, 2011, Kamati ilikutana mjini Dar es Salaam ili kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2010/2011, iliyowasilishwa na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Bernard K. Membe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati, maelezo yalihu utekelezaji wa malengo ya Wizara kwa kipindi cha mwaka 2010/2011 na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa malengo hayo sambamba na hatua zilizochukuliwa kukabiliana na changamoto hizo. Aidha, Mheshimiwa Waziri alifafanua kuhusu Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Napenda

kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa taarifa ya Waziri ilionyesha kwamba hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2011 ambayo ni robo ya tatu ya kipindi cha Bajeti, Wizara ilipokea kutoka Hazina kiasi cha shillingi 65,669,935,227.00.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi hiki kilichotolewa ni sawa na asilimia 58.4 ya Bajeti ya Fungu 34 iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Taarifa ilionyesha kuwa hadi mwisho wa robo ya tatu ya kipindi cha Bajeti, asilimia 41.6 ya Bajeti ya Fungu hili haikutoka Hazina. Kwa maelezo hayo tatizo kubwa la mtiririko wa fedha kutoka Hazina lilidhihirika. Hali hii iliathiri utekelezaji wa majukumu na diplomasia ya uchumi. Vilevile hali za Balozi zetu nchi za nje imeendelea kuathiriwa na ufinyu wa Bajeti pamoja na mtiririko wa Bajeti usioridhisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kupitia na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ya Bunge la Tisa ilitoa maoni na ushauri kwa ajili ya utekelezaji. Maoni hayo yalihusu utaratibu wa kidiplomasia, ununuzi wa majengo nje ya nchi na kuhamishwa kwa kifungu cha gharama ya safari za viongozi wa Kitaifa kwenda nje ya nchi.

Naomba kutoa taarifa kuwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri yanaonyesha kwamba sehemu kubwa ya ushauri inaendelea kufanyiwa kazi. Kwa mfano, kuhusu utaratibu wa kidiplomasia, taarifa ilionyesha kuwa Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na kuendelea kutumia njia mbalimbali za kidiplomasia katika kukuza na kudumisha mahusiano na Mataifa mengine kisiasa na kiuchumi. Utaratibu huu umelisaidia Taifa letu kuwa katika usalama, amani na utulivu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwengine ni kuhusu ushauri wa kununua, kujenga na kukarabati majengo ya Balozi zetu. Taarifa ilionyesha kuwa Wizara inaendelea kufanya majadiliano na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama vile *NSSF* ili kuishirikisha katika utekelezaji wa miradi iliyopo katika mpango wa miaka 15 wa ununuzi, ujenzi na ukarabati wa majengo ya ofisi na makazi Balozini. Kamati ilibaini kuwa ni mwaka mmoja sasa tangu ushauri huo utolewa na Wizara kufanya majadiliano na *NSSF*. Ni maoni ya Kamati kuwa kasi ya kutekeleza azma inayokusudiwa ni ndogo kiasi cha kuathiri tija. Ni vema Serikali ikaongeza kasi ili matokeo ya mpango huo yawe na faida inayotakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2011/2012, kuhusu Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Kamati ilielezwa kuwa ili kutekeleza kikamilifu kazi zilizopangwa kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 Wizara hii imepangiwa kiasi cha shilingi 125,102,875,000.00. Kati ya Fedha hizo, shilingi 80,602,875,000.00 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 44,500,000,000 ni kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Mheshimiwa Waziri yalionyesha kuwa kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida (*Recurrent Expenditure*) shilingi 76,387,700,187 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (*Other Charges*) na 4,215,688,000 ni kwa ajili ya

mishahara. Kamati ilipitia na kuchambua kwa kina vifungu vyote vya Fungu 34 Bajeti ya Maendeleo na ile ya Matumizi ya Kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba asilimia 64.4 ya Bajeti ya Wizara hii imetengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na asilimia 35.6 ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo. Katika fedha zilizopangwa kwa Matumizi ya Kawaida asilimia 94.8 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (*Other Charges*) na asilimia 5.2 imetengwa kwa ajili ya mishahara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ililinganisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 na mwaka 2010/2011 na kubaini kuwa kwa ujumla kuna ongezeko la asilimia 11.4 katika Bajeti yote vya Fungu 34. Lakini kwa upande wa Bajeti ya kugharamia Miradi ya Maendeleo (*Development Expenditure*) kiasi kilichopangwa ni sawa na Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Ni dhahiri kuwa ongezeko hilo la jumla linatokana na kuongezeka kwa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Ongezeko kwenye Bajeti ya Kawaida ni matokeo ya kuongezeka kwa fedha inayotengwa kwa ajili ya mishahara kwa kiasi cha asilimia 11 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2010/2011. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kujadili kwa kina taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa mwaka 2010/2011 na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi yake kifungu kwa kifungu, napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati inaunga mkono hoja na kutoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Chuo cha Diplomasia ni kituo muhimu kwa utaalamu utakaosaidia utekelezaji wa azma ya Serikali ya kuboresha diplomasia ya uchumi kwa manufaa ya nchi yetu, ni vema chuo hiki kikawezeshwa zaidi kifedha na rasilimali nyinginezo. Aidha, mpango wa kuinua chuo hicho kitaaluma utekelezwe sambamba na kikitengea fedha za kutosha kwa ajili ya uendeshaji wake. Serikali ikiweshe Chuo hicho kutatua tatizo kubwa la ukosefu wa gari imara na fedha za kutosha kwa uendeshaji wa shughuli zake.

Tatizo la umiliki wa ardhi kwa Chuo cha Diplomasia kilichopo eneo la Kurasini lipatiwe ufumbuzi ili chuo hicho kiweze kupanuliwa na kutoa elimu bora na stadi muhimu kwa watu wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwatendea haki watumishi wa Serikali wanaohamishwa kutoka Ofisi za Balozi zetu au wanaomaliza muda wao wa utumishi, suala la fedha kwa ajili ya uhamisho lipewe umuhimu kwa namna inayofaa. Aidha, kwa kuwa kumbukumbu za kiutumishi zinahifadhiwa ni wazi kuwa Bajeti inayopangwa kwa kila mwaka inapaswa kuzingatia mahitaji hayo ya watumishi.

Katika kutekeleza nia ya Serikali kuendelea kutoa mchango katika masuala ya amani kwenye Ukanda wetu na Barani Afrika, diplomasia itumike kuzishawishi nchi zinazoshughulikia tatizo la uharamia, kujikita kwenye kiini cha tatizo.

Utaratibu wa kuwatumia Mabalozi wa Heshima utumike katika maeneo ambayo Tanzania hajafungua Ubalozi. Aidha, ni vema Tanzania ifungue Ubalozi mdogo mjini Lubumbashi – Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Kamati inasisitiza ushauri uliotolewa katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 kuwa ili utekelezaji wa Bajeti na malengo katika Fungu 34 ufanyike vizuri, pesa kwa ajili ya safari za viongozi wa Kitaifa kwenda nje ya nchi zitengwe nje ya Fungu 34 na kulipwa moja kwa moja na Hazina. (*Makofi*)

Kwa kuzingatia umuhimu wa mchakato wa kujitathimini wenyewe kwa vigezo vya utawala bora (*APRM*), Kamati inashauri kuwa kuna umuhimu mkubwa kwa Serikali kutenga pesa kwa ajili ya mchakato huo sanjari na kulipia michango na ada ya uanachama kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Balozi zetu nje ya nchi ziweze kutekeleza vema majukumu yake pamoja na kuziwezesha kuheshimika, Serikali iongeze juhudhi ya kuboresha makazi ya watumishi ubalozini na kuziwezesha ofisi za Balozi zetu kuwa na magari yanayofaa kwa shughuli za Kibalozi. Aidha, kuna umuhimu mkubwa wa kuhakikisha kuwa malipo ya stahili za watumishi wa Serikali katika Balozi zetu yanakwenda kwa wakati na kwa kiwango kinachostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, naomba kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii adhimu ili niweze kutoa taarifa hii pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Nawashukuru pia Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Mheshimiwa Bernard K. Membe, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Mahadhi Juma Maalim na watumishi wote chini ya uongozi wa Ndugu John Haule, Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wa kuchambua Bajeti hii.

Aidha, nawashukuru wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa umakini mkubwa na ushirikiano wa kutosha waliokuwanao na hatimaye kufanikisha kazi hii. Kwa kuthamini mchango wao naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Edward Lowassa, Mwenyekiti, Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan, Makamu Mwenyekiti na wajumbe ambao ni Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Capt. Mst. John Chiligati, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Mheshimiwa Betty Machangu, Mheshimiwa Augustino Masele, Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa, Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, Mheshimiwa Mch. Israel Natse, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Brig. Jen. Mst. Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Rachel Mashishanga Robert, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mheshimiwa John Magalle, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo na Mheshimiwa Anastazia Wambura. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kumalizia, namshukuru Ndugu Athuman Hussein, Katibu wa Kamati hii kwa kuratibu vema shughuli za Kamati. Nawashukuru pia watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Dkt. Thomas Kashililah, Katibu wa Bunge kwa huduma iliyowezesha Kamati kutekeleza wajibu wake ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa hii na maoni ya Kamati na hatimaye liidhinishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kamataifa kama alivyowasilisha mtoa hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, kwa kusoma hotuba hiyo kwa niaba ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Sasa nitamuita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kuhusu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Ezekia Wenje. (*Makofi*)

MHE. EZEKIA D. WENJE - MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2007. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na uzima na leo nipo hapa na ninaamini aishivyo Mungu mimi nitaendelea kuwepo na hakuna silaha itakayopandikizwa dhidi yangu itakayoniangamiza maana hii ni ahadi ya Mungu kwangu. (*Makofi*)

Aidha napenda kwa upekee kabisa kutoa pole kwa wananchi wa Jiji la Mwanza kwa vurugu zilizotokea hivi karibuni kati ya wafanyabiashara wadogo wadogo yaani Wamachinga, polisi na askari wa Jiji iliyopelekea uchumi wa Mwanza kusimama takriban siku nzima. Naamini Mwenyezi Mungu ataleta heri kwa Jiji letu la Mwanza na hayo yaliyotokea hayatatokea tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nipende kutoa shukrani za dhati kwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mboge, Naibu wake Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto pamoja na Wabunge wenzangu wote wa Kambi kwa maoni na miongozo yao hadi kukamilika kwa hotuba hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha nimkushukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wenzako wa Bunge wote kwa namna mnavyotuongoza katika shughuli zetu za kila siku humu Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kipekee napenda kutoa ponezi kwa Rais Salva Kiir pamoja wananchi wa Taifa jipya la Sudani ya Kusini kwa kujipatia Uhuru wake Julai

9, 2011. Uhuru huu ni changamoto kwetu sote kwani tunatambua jinsi ambavyo wananchi wa Sudani ya Kusini walivyopambana kudai Uhuru wao kwa muda mrefu na hatimaye sasa wameweza kuupata. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani tunaitaka Serikali ileze Watanzania juu ya ni fursa gani ambazo kama Taifa tunaweza kuzitumia kwenye Taifa hili jipya kwa maslahi ya wananchi wa nchi zetu hizi mbili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, itifaki na taratibu za mawasiliano kati ya viongozi na Mabalozi, kwa mujibu wa Waraka wa Rais Na. 2 wa mwaka 1964 (*Presidential Circular No.2 of 1964*) unaohusu itifaki na taratibu za mawasiliano kati ya viongozi wa Serikali na Mabalozi, umeainisha mambo makubwa matatu katika mawasiliano kama ifuatavyo:-

Kwanza mawasiliano yote ni lazima yaratibiwe na Wizara ya Mambo ya Nje na mawasiliano ya Balozi zetu nje ni lazima yanakiliwe Wizara ya Mambo ya Nje. Pili, miadi yoyote kati ya Waziri na Balozi wa nje nchini lazima ifanyike kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na afisa wa Wizara atahudhuria kwa lengo la kuchukua kumbukumbu na tatu, hairuhusiwi kwa Waziri kutembelea ofisi au nyumbani kwa Balozi isipokuwa kwa madhumuni ya kuhudhuria sherehe za Kitaifa za balozi husika. (*Makofii*)

Kambi ya Upinzani tunaitaka kujua hivi bado waraka huu ambao unatumika pamoja na masharti yake una malengo gani kwa ulimwengu wa sasa na hasa ikizingatiwa kuwa masharti haya yaliwekwa wakati wa vita baridi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Nje kwenye mada ilioandaliwa na kuwasilishwa Mei, 2011 kwenye Baraza la Mawaziri, wanakiri kuwa mnamo tarehe 23 Machi, 2011 Waziri Mkuu aliiandikia Wizara ya Mambo ya Nje barua akiwataka wadhibiti mienendo isiyoridhisha ya baadhi ya Mabalozi na viongozi wa Jumuia za Kimataifa waliopo nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mada hiyo Wizara inakiri kuwa kuna baadhi ya Mabalozi, ofisi zao, nyumba zao na kumbi zao za mikutano hutumika na Vyama vya Upinzani kupanga mikakati dhidi ya Serikali na Chama Tawala kwa kuwa kimekaa muda mrefu madarakani hivyo kupanga kuwaondoa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara katika andiko lake iliongeza shutuma lukuki kama vile baadhi ya Mabalozi kukutana na wahariri wa vyombo vya habari na kuvipongeza kwa kuikashifu Serikali, kushabikia waziwazi vitendo vya uvunjifu wa amani kama maandamano na kuonyesha kusikitishwa kwao kwa ushindi wa Chama Tawala na nyuso zao kusomeka, nanukuu.... “*Inshallah, kuvunjika kwa koleo sio mwisho wa uhunzi.*” (*Makofii*)

Kambi ya Upinzani, tunataka kupata majibu juu ya shutuma hizi kwani zinaonyesha kuwa Mabalozi wengi hasa ambao ni kutoka nchi wafadhili/wahisani wapo nchini kwa ajili ya kuiangusha Serikali, hii ni shutuma nzito sana kutolewa na Waziri wa Mambo ya Nje. Ni hatua gani Serikali imechukua kwani hili ni sawa na kosa la uhaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shutuma nyingine na ambayo imetustua ni hii iliyosomeka; “Baadhi ya Mabalozi kujitembelea kiholela kwenda kwenye majimbo yaliyo chini ya upinzani au Bungeni kwa nia ya kushawishi Wabunge kupinga Miswada” wakati huo huo kwenye hitimisho la andiko lake Waziri anasema ; “Nimeulizwa na Mawaziri juu ya utaratibu wa kufuata wakihitaji kukutana na Mabalozi kwa ajili ya masuala ya majimboni mwao. Waraka wa Rais Na.2 wa mwaka 1964 haukuzingatia suala hili kwa kuwa mahitaji na mazingira ya namna hiyo hayakuwapo Waheshimiwa Mawaziri, kama walivyo Wabunge na viongozi wengine tuko huru kukutana na Mabalozi hao.” (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ni ya kusikitisha sana na hasa inapotokea kuwa Waziri anaandika mada na kuiwasilisha mbele ya Baraza la Mawaziri kuwa mabalozi wanajitembelea kiholela kwenye majimbo yanayoongozwa na upinzani, wakati huo huo akikiri kuwa hakuna kosa wanaloofanya kwa mujibu wa Waraka Na.2 wa mwaka 1964. Kumbe kosa ni kutembelea majimbo yanayoongozwa na Wabunge wa Kambi ya Upinzani na kukutana nao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya upinzani tunaona kuwa hii ni kuwadhalilisha Wabunge wa Kambi ya Upinzani na wananchi waliowachagua na pia tunamtaka Waziri awaombe radhi kwa kitendo hiki Wabunge wa Kambi ya Upinzani, wananchi waliowachagua pamoja na Mabalozi wote kwa kitendo cha udhalilishaji huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kupata majibu ni hatua gani zimechukuliwa na Serikali na haswa ikizingatiwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje aliwahi kutoa kauli hadharani na kusema kuwa Serikali ilikuwa inachunguza baadhi ya Mabalozi kwa kitendo cha wao kutoa fedha kwa Vyama vyta Upinzani hapa nchini. Je, uchunguzi ule umefikia wapi? Na ni nini matokeo ya uchunguzi ule? Ripoti ya uchunguzi huo haina budi sasa kuwekwa hadharani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya mambo ya nje na uchumi wetu, katika hotuba yetu mbadala ya Ofisi ya Rais Mahusiano na Uratibu tuligusia na kuishauri Serikali juu ya kufanya ujasusi wa kiuchumi (*Economic Espionage*) wa Kimataifa ili kufanya nchi yetu kunufaika na fursa mbalimbali ambazo zinaweza kupatikana katika nchi zingine duniani hasa zile ambazo uchumi wake unakua kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa sera yoyote inayotungwa kwa nchi ni kulinda maslahi ya nchi. Maslahi ya nchi ni neno lenye tafsiri pana sana katika matumizi yake. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani pamoja na mambo mengine inaamini kabisa Tanzania kama nchi yenye rasilimali nyingi inawajibika kuhakikisha rasilimali hizo zinatumika kwa maslahi ya kizazi kilicho sasa na kizazi kijacho kijacho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndipo msingi mkuu wa sera wa maslahi ya Taifa, yaani *National Interest* unapoingia na kushika hatamu katika kila jambo linalohusisha matumizi ya rasilimali zetu. Ujasusi wa kiuchumi ni mwendelezo wa kulinda maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kufanya hivyo kwa kulinda na kutafuta fursa kwa raslimali zetu na bidhaa zetu nje, tunaweza pia kupata taarifa mbalimbali za wawekezaji kutoka nje na lengo lao kwetu ili hatimaye kunufaika na shughuli zao humu nchini kuliko kuanza kuingia nao katika mikataba ambayo haina manufaa halafu baadaye nchi kuingia hasara ya kuvunja mkataba kama iliyotokea katika wawekezaji wa *RITES* kutoka India, *City water, Dowans* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatia mashaka kuwa hata Balozi zetu zinashindwa kufanya hivyo wakati moja ya majukumu yao huko nje ni pamoja na kuhakikisha maslahi ya nchi yetu yanazingatiwa kikamilifu huko nje. Inashangaza kuona makampuni yanayotutia hasara yanafanya hivyo bila sisi kuyajua mapema wakati wanapoonyesha tu nia ya kuingia nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali kutueleza mkakati au mipango yake juu ya suala hili na sio kupiga siasa za kudai chenji ya fedha za rada wakati Serikali hii ndiyo ilioingia kwenye mkataba huo wa kifisadi wa chombo hicho hata baada ya wadau mbalimbali kuwaonya wasifanye hivyo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa lugha nyepesi, Kambi ya Upinzani inasema kuwa, wawakilishi wetu nje ya nchi hawaelewi maana halisi ya masilahi ya Taifa, jambo ambalo kama halitapatiwa ufumbuzi, nchi itaendelea kupoteza raslimali zake kuititia uwekezaji uchwara, kama ambavyo makampuni yaliyosajiliwa *offshore* ndiyo yanayokuja kuwekeza katika miradi mikubwa ya gesi na raslimali kadhaa tulizonazo. Huu ni udhaifu mkubwa wa nchi yetu katika sura ya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani hatuwezi kuendelea kupata aibu ya kizembe namna hii. Kabla ya kufanya uteuzi wa uwakilishi nje ya nchi, vigezo maalum viandaliwe na watu wasiende kutuwakilisha kwa lengo la kumalizia siku zao za utumishi wa umma, au urafiki na umwenzetu. Kambi ya Upinzani, tunaitaka Serikali iwasilishe hapa Bungeni vigezo mahususi ambavyo hutumika katika kumteua Balozi ili kuweza kuiwakilisha nchi yetu na hasa kwenye nchi *strategic* kama vile China, India, Marekani, Uingereza na nyinginezo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa China ni nchi ambayo inafanya biashara nyingi na Tanzania, na Watanzania wengi sana wanafanya biashara mbalimbali na nchi ya China na biashara hizo zinafanyika katika miji mbalimbali ya China. Hivyo basi, ni muhimu kwa Tanzania kuwa na mkakati maalum wa kuanzisha Balozi ndogo katika mji ya Guangzhou badala ya kuwa na Ofisi moja tu ya Beijing, hii itasaidia kutatua matatizo wanayokutana nayo wafanyabiashara wengi wa Tanzania wanaokwenda China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Wizara nyeti kama hii utendaji wa Wizara unatakiwa uwe na umakini na wenye kwenda na wakati kwa kuwa ni kioo kwa Mataifa mengine. Inashangaza kuona kuwa bado mambo mengi ndani ya Wizara hayaendani na jina lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma nyingi zitolewazo na Wizara bado haziendani na maendeleo ya sayansi na teknolojia mathalani matumizi ya TEKNOHAMA. Kwa mfano ulio thabiti ni kuwa hata wanafunzi wa vyuo wanaoomba fursa ya kufanya tafiti Wizarani inachukua wiki mbili mpaka tatu kujibiwa kama wanaruhusiwa au la. Hata masjala ya Wizara bado inatoa huduma kizamani na kushindwa kutumia njia za kielektroniki kuhifadhi nyaraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuboresha utendaji wa Wizara na Balozi zetu ni vizuri sasa Wizara kuzingatia ushauri wa Kambi ya Upinzani tuliusiwa mwaka jana kuwa inabidi Wizara izingatie sifa binafsi za kiutendaji, yaani *Personal Integrity* katika suala la kuajiri Watendaji pamoja na wanadiplomasia na siyo kupeana wadhifa kwa sababu ya kujuana na sio kuzingatia uwezo wa mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, hata Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa fedha za Serikali ametoa mapendekezo kuhusu hili na kuishauri Serikali kufanya marekebisho ya kanuni za mwaka 1979 za Balozi zetu ili ziendane na wakati uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado utendaji kwa Balozi zetu una matatizo mbalimbali kama ambavyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali amethibitisha. Pamoja na mambo mengine, bado kuna usimamizi mbaya wa mali za Serikali, na mfano mzuri ni kuwa Serikali ilinunua mashine za kuchapisha *visa* kwa ajili ya Balozi zetu nje ya nchi. Mashine hizi hazikutumika na Serikali haikupata thamani halisi ya fedha kutokana na ununuza wa mashine hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Serikali imepuuza ushauri uliokuwa ukitolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali kuhusu Balozi zetu kuwa wanapokusanya maduhuli yalipwe katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Hii itatoa mwanya kwa Mdhibiti kukagua usahihi wa matumizi katika Balozi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inatoa rai kwa Wizara kuzingatia ushauri huo uliotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali ili kuboresha matumizi bora ya fedha za walipa kodi. Pia Serikali itoe kauli kama tayari majengo ya Balozi zetu katika miji ya London, Nairobi na Maputo yameshapatiwa hati miliki kwa kuwa iligunduliwa kuwa majengo hayo hayakuwa na hati jambo ambalo linatia shaka juu ya uhalali wa umiliki huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kila haja ya kuanza kuboresha utendaji wa watumishi wetu Wizarani na katika Balozi zetu ili kuendana na kasi ya ushindani katika masuala ya kiuchumi duniani. Kwa kuwa bado Wizara ina upungufu wa watumishi wenye uelewa mkubwa wa kidiplomasia na wenye uwezo wa kuendana na ushindani na hata taarifa zao, wengine ni siri na hivyo kuwa vigumu kwa wananchi kuhoji utendaji wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera yetu ya mambo ya nje hivi sasa ilibadilika na kuwa sasa tupo kwenye diplomasia ya uchumi, yaani *Economic Diplomacy*, ila tangu tuwe na sera hiyo hakuna dalili zinazoonyesha kwa uwazi kuwa tunaishi maneno yetu,

kwani katika hali ya kawaida tulitegemea kuona Serikali ikifungua Ofisi za Balozi kwenye nchi ambazo uchumi wake unakua kwa kasi kubwa na hasa zinazojulikana kama *Asian Tigers*.

Kambi ya upinzani, tunaishauri Serikali ili kuweza kuendana na sera hii waige mfano wa nchi ya Kenya kwani wao wameshafungua Balozi zao na kutuma watu makini kwenye eneo hilo kwa ajili ya kuhakikisha kuwa wanawavutia wawekezaji na mitaji mikubwa, pamoja na teknolojia kuweza kufikishwa nchini mwao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inasikitika kuona kuwa nchi yetu inadhalilika pale Mabalozi wetu nje wanafikia hatua ya kupewa *notice* ya kuhama kutokana na kutokulipa kodi ya pango. Ubalozi wetu Malaysia ni mfano mzuri kwani sasa ni miezi sita Serikali haijalipia kodi ya pango. Hii ni aibu kubwa kwa nchi yetu, tunaitaka Serikali kulitolea kauli suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uraia wa nchi mbili, yaani *Dual Citizenship*. Suala hili tumelizungumza sana katika hotuba zetu kwa Wizara hii kwa miaka mingi sasa, na tuliainisha mafanikio mbalimbali ambayo tunaweza kuyapata kutokana na kuhalalisha suala hili. Hata majumuisho ya Waziri katika Mkutano wa Bajeti uliopita katika suala hili alisema utaratibu ulikuwa unafanyika kuliwasilisha kwenye Baraza la Mawaziri na baadaye kuwasiliana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kulipitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani ilisikitishwa baada ya kupishana kwa kauli za Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Waziri wa Mambo ya Ndani (aliyekuwepo wakati huo, Mheshimiwa Lawrence Masha) kuhusu suala hili. Pamoja na Waziri wa Wizara kukubali suala hili, mwenzake alitokea hadharani kupinga suala hili na kusema kuwa Serikali ina mkakati mwengine wa kuanzisha mpango wa makazi ya kudumu, yaani *permanent residency*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani tunataka maelezo na kauli ya Waziri juu ya mpango huu, kwa kuwa umechukua muda mrefu kukamilika huku kukiwa na haja ya kufanya hivyo ili kupata mafanikio ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika suala hilo tunazidi kuweka msukumo kuwe na mpango mbadala kwa Watanzania ambao tayari wameshakuwa na uraia wa nchi nyingine kuruhusiwa kushiriki katika maendeleo ya Tanzania. Hii inajulikana kama *Diaspora Bond*. Je, Serikali ilizingatia kwa namna gani ushauri ambao tuliutoa mwaka wa fedha uliopita kuhusu suala hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli ulio wazi kuwa kuna Watanzania wengi sana wako nje ya nchi ambao miaka yote hawapati nafasi ya kupiga kura kuwachagua viongozi wao. Kambi ya Upinzani, inaitaka Tume ya Uchaguzi ishirikiane na Wizara ya Mambo ya Nje kuweka utaratibu kwa Watanzania waishio nje ya nchi ili washiriki Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 kwanza kwa kujiandikisha kwenye Daftari la Kudumu la Wapigakura na hatimaye kuweza kushiriki kupiga kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Kambi ya Upinzani inataka maelezo kwa mtoto ambaye amezaliwa na wazazi wake wakiwa wote Watanzania, lakini wanaishi Canada au nchi nyingine za Ulaya ambapo mtoto aliyezaliwa katika nchi hizo anapewa uraia, yaani *citizenship by birth* katika hizo nchi. Wazazi wao wakirejea, kwa nini mtoto huyu anatakiwa kuwa na *Visa* ya kuingia Tanzania wakati hajatimiza miaka 18 na analipa *Visa* ya mtu mzima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Watanzania kuoa/kuolewa na watu ambao sio watanzania na suala la uraia limekuwa na ubaguzi mkubwa sana na hasa kwa upande wa wanawake ambao ni Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa zaidi kwenye suala hili ni kwa upande wa wanawake, kwani utaratibu wa kukosekana uraia wa nchi mbili kunawadhalilisha sana dada zetu na hasa wanapoolerwa na raia wa nchi nyingine, kwani inapotokea raia wa kigeni ambaye ni mwanamke, akiolewa na mwanaume wa kitanzania ye ye anapata uraia moja kwa moja (kwa tendo la kuolewa), ila hali ni tofauti kwa mwanamke wa kitanzania akiolewa na mwanaume ambaye sio raia wa Tanzania, huwa mumewe hawezi kupata uraia wa moja kwa moja.

Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali kuondoa utaratibu huu kwani ni kandamizi kwa wanawake na unaonyesha jinsi ambayo mfumo dume umekomaa kwa watunga sera na hasa wanaume dhidi ya wanawake. Tunaitaka Serikali kuweka usawa baina ya wanawake na wanaume kwani kama mwanamke akiolewa anakuwa raia, basi na mwanaume akioa Mtanzania naye aweze kupata uraia kwa utaratibu huo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha ushirikiano wa kimataifa, nafasi ya Tanzania katika Umoja wa Afrika pamoja na mambo mengine inatakiwa iwe ni kukomesha uonevu na ukandamizaji na kuchochea utawala bora na ukuaji wa demokrasia, hasa katika nchi zetu hizi ambazo hukabiliwa na changamoto nyingi katika masuala hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika siku za hivi karibuni, zimeibuka aina nyingine za kidemokrasia katika Bara la Afrika mathalan baadhi ya Vyama Tawala vimekuwa vikishindwa kwenye masanduku ya kura na kung'ang'ania madarakani na kulazimisha ushirikiano. Hili husababisha machafuko ambayo mwisho wake ni wananchi walio wengi kupata shida kwa sababu ya migogoro baina ya makundi hayo hasimu. Hii inadhihirika baada ya chaguzi za nchi za Kenya, Zimbabwe na hata *Ivory Coast*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani tunaungana na Wizara kupinga nia ya kampuni ya *BAE Systems* ya kutaka kulipa fedha za rada kuitia Asasi Zisizo za Kiserikali za Uingereza, kwani hatua hiyo itakuwa ni udhalilishaji mkubwa kwa Watanzania wote. Ni sawa na kutuambia kwamba sote hatuna uwezo wa kuamua na kusimamia mambo yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inatambua kuwa Bunge lako Tukufu litatenga muda maalum kwa ajili ya kujadili suala la madai ya fedha za rada kiasi

cha takribani pauni za Kiingereza milioni 12 takribani shilingi bilioni 28.9 za Kitanzania, ambazo kampuni ya uuzaji wa zana za kivita ya *BAE Systems* ya nchini Uingereza imeamriwa kutulipa baada ya kubainika kuwepo ukiukwaji mkubwa wa sheria na taratibu katika ununuzi wa rada hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kwa kuwa suala hili linagusa misingi ya utawala bora, Kambi ya Upinzani kwa niaba ya mamilioni ya Watanzania tunaowawakilisha, tunachukua fursa hii kutoa msimamo na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunataka wahusika wote waliohusika na kashfa ya rada (akiwemo aliyejewa Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa wakati huo), wachukuliwe hatua zote za kinidhamu na kisheria kwa kufikishwa Mahakamani haraka iwezekanavyo, kwani uchunguzi uliofanywa na Idara ya Upelelezi wa Ufisadi (*SFO*) ya nchini Uingereza, umeonyesha kuwapo kwa hongo na ukiukwaji mkubwa wa sheria na taratibu katika mchakato mzima wa ununuzi wa rada hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani tunaona kuwa, bila watuhumiwa hawa kuchukuliwa hatua, ni dhahiri kuwa Taifa haliwezi kuwa na uhakika wa kuzilinda vizuri fedha hizo za rada pindi zikilipwa, pamoja na fedha nyine za umma ambazo zinaweza kuendelea kupotea kwa sababu umekuwa ni utamaduni wa Serikali yetu kutochukua hatua kwa wahusika wa rushwa kubwa kubwa yaani *high voltage corruption* za namna mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala yake, tunataka Bunge lako Tukufu lijadili na kuazimia pamoja na mambo mengine lizingatie ushauri wetu tulioutoa katika hotuba yetu mbadala ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuwa fedha hizo zisirudishwe Serikalini moja kwa moja na badala yake kuwe na akaunti maalum itakayoratibiwa na wadau ambao tuliwaainisha. Pia kampuni ya *BAE* ilipe fedha hizo mapema iwezekanavyo kupitia akaunti hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukuza Diplomasia kimataifa. Kambi ya Upinzani inatambua kuwa ili tuendelee, tunahitaji kushirikiana na nchi nyine ili kujenga mahusiano ya kidiplomasia pamoja na kiuchumi. Katika kufanikisha azma hii, kuna wakati viongozi wetu wa kitaifa hulazimika kusafiri nje ya nchi na kutembelea nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mingi sasa Kambi ya Upinzani tumekuwa tukiitaka Serikali kupunguza safari za nje kwa viongozi wetu, kwa sababu safari hizo za viongozi wetu wa juu zinatakiwa ziendane na hali ya uchumi tuliyonayo pamoja na changamoto mbalimbali ambazo zinatukabili kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika dhana ya kupunguza matumizi, tuna kila sababu ya baadhi ya safari za nje ambazo siyo lazima mkuu wa nchi kwenda kuwaachia viongozi wengine washiriki kwa kuwa ni wazi kuwa msafara wa Rais nje ya nchi una gharama kubwa sana ukilinganisha na Mawaziri au Maafisa wengine wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Wizara ikishirikiana na Ofisi ya Rais kuweka utaratibu wa safari za viongozi nje ya nchi, ili kupunguza matumizi makubwa ya Serikali na hatimaye fedha hizo zielekezwe katika miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo humgusa mwananchi wa hali ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupanua wigo wa diplomasia ya Tanzania na nchi nyingine tumekuwa tukipewa majibu ya ahadi ya misaada mbalimbali ambayo Tanzania kama nchi inapata kutokana na safari hizo za nje. Aidha, dhana hii inaweka mashaka kuwa Serikali hii inaendekeza tabia ya kuwa ombaomba badala ya kujenga urafiki wenye tija kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongo kadhaa iliyopita Tanzania ilikuwa inajulikana duniani kwa misimamo ya kimantiki na katika kuendesha na kuunga mkono harakati za ukombozi wa wanyonge popote duniani. Aidha, Tanzania ilitia mkazo kwenye sera ya kujitegemea isiwe Taifa ombaomba. Ni kutokana na misimamo ya kimantiki, Tanzania iliweza kujulikana na kuheshimika kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, katika miaka ya karibuni, Serikali hii imeharibu misingi ya mahusiano ya kimataifa iliyojijengea nchi yetu sifa za kuwa huru katika mshusiano yake na nchi za nje. Badala yake, sera ya Serikali hii kuhusu ushirikiano wa kimataifa imelenga katika kuiwezesha Tanzania kuomba misaada kutoka nchi zilizoendelea na hata zile ambazo siyo muda mrefu zilikuwa zikiongozwa na Tanzania katika harakati za kudai mfumo mpya wa kiuchumi ulimwenguni. Matokeo yake kwa sasa nchi yetu inajulikana zaidi jinsi inavyoombaomba na kuwa moja ya nchi maskini zaidi duniani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii imekuwa ikidhihirika mara kwa mara katika majibu ya Waziri mara kadhaa akijibu suala hili akionyesha namna nchi hii inavyopata misaada kutokana na safari za nje za viongozi wetu. Pamoja na kuwa hatubezi misaada ya nje yenye lengo zuri kwa nchi yetu na siyo kwa ile yenye matakwa ya kunufaika kiuchumi kutokana na raslimali zetu, kuna haja ya kuwa na mipango thabiti ya kuratibu mahusiano yetu na nchi nyingine ili yatujenge kiuchumi na siyo kutembeza bakuli kila kukicha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kukuza diplomasia yetu kwenye Nyanja za kimataifa, ni lazima tuhakikishe kuwa jina la Tanzania huko nje halichafuliwi kwa namna yoyote ile kwani hiyo inajenga heshima kwa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Nje na hususan Mheshimiwa Waziri, analifahamu kikamilifu suala la shamba lililopo eneo la Oldean Arusha llijulikanalo kama *Ndamakai Estates Ltd* na sasa linajulikana kama *Acacia Hills Ltd* kwani alimteua mwanansheria mwandamizi wa Wizara hiyo ndugu Irene Kasyanju kulifuatilia suala hilo ambalo linamhusisha raia wa *Trinidad & Tobago* aliyekuwa analimiliki hapo awali kwenye miaka ya 1970.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili limekuwa likiwasumbua viongozi wakuu wanapokuwa wanahudhuria mikutano ya Umoja wa Mataifa kama Rais wetu alivyowahi kukumbana nalo mwaka 2007 kwani mmiliki wa shamba hili ajulikanaye kama Sohooba alikutana na msafara wa Rais akiwemo Mheshimiwa Waziri, Balozi wa Tanzania Umoja

wa Mataifa - Augustino Mahiga tarehe 30 Septemba, 2007, pia Waziri Mkuu wa *Trinidad & Tobago* aliweza kuwasiliana na Serikali kuhusu suala hilo bila mafanikio. Lalamiko kuhusu umiliki wa shamba hili ni kutokana na shamba husika kubadilishwa mmiliki wakati Wizara ya Mambo ya Nje ilikuwa inalishughulikia na kulifuatailia suala husika.

Kambi ya Upinzani tunataka kupata majibu kuhusu ni jambo gani hasa linaendelea kuhusiana na shamba hili kiasi cha kuweza kulichafua jina la nchi yetu kimataifa. Tunamtaka Waziri alieleze Bunge juu ya ushiriki wa Wizara ya Mambo ya Nje kwenye suala hili, kwani mnamo tarehe 23 Julai, 2010 Waziri Membe aliandikiwa barua akilalamikiwa kuhusiana na ushiriki wake katika kubadilisha umiliki wa shamba hili na kumilikiwa na raia wa Ugiriki ajulikane kama *Leon Christianakis*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika kukuza diplomasia ya kimataifa ni kuhusiana na nidhamu ya utendaji kazi ya maafisa mbalimbali wa Balozi zetu ambao ndio kioo cha Watanzania kwenye nchi ambazo wanawakilisha Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 4 Februari, 2011 Balozi wa Tanzania nchini Marekani aliandika barua kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje yenye Kumb, Na. WEPC.179/53 kuhusiana na suala la Afisa Mwambata wa Ubalizi Dkt. Allan Mzengi, na kampeni iliyokuwa inafanywa na Mawakili wa Bi. Zipora Mazengo kwa *Congress* ili kuichafua Tanzania kuhusiana na deni linalomkabili ambalo ni kutokana na hukumu ya Mahakama kutokana na kubainika kuhusika katika biashara haramu ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ilimuamuru afisa huyu kulipa dola milioni moja za kmarekani, yaani zaidi ya shilingi bilioni moja na nusu za kitanzania, ila kwa mujibu wa barua ya Balozi inasema kuwa mara baada ya majadiliano na Mawakili husika walikubali kupunguza deni hilo mpaka kiasi cha dola 170,000, takribani shilingi milioni 200 za kitanzania.

Kambi ya Upinzani, tunataka kupata majibu, ni hatua gani zimechukuliwa na Wizara mpaka sasa kuhusiana na suala hili na je, deni husika limelipwa? Kwani kwa mujibu wa barua ya Balozi ni kuwa deni hilo linaweza kuathiri upatikanaji wa misaada kutoka Marekani na hasa ule wa *MCC Compact*. Mtumishi huyu wa Serikali alichukuliwa hatua gani za kinidhamu kutokana na kuhusika kwake katika suala ambalo limeichafua sura ya nchi katika ulingo wa kimataifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni moja ya nchi za Kiafrika zinazoshiriki katika mchakato wa kuimarisha utawala bora kwa kujifanyia tathmini yenyewe. Kwa taarifa za Serikali, hatua iliyofikiwa hivi sasa ni kusubiri kupokea ujumbe kutoka Sekretarieti ya Mpango wa Kujitathimini (*APRM*) iliyoko Afrika Kusini ili kuja kuhakiki taarifa za Tanzania kuhusu utekelezaji wa misingi ya utawala bora na haki za binadamu nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kuwa Bunge hili liliridhia nchi yetu iingie kwenye mpango wa *APRM* tangu tarehe 1 Februari, 2005. Hatua ya Bunge letu Tukufu kuitisha mpango huo ilimaanisha na kuashiria jambo moja kubwa kuanzia wakati huo, mpango huo ulikuwa upo kwa nguvu ya sheria na jambo moja tu lililobaki lilikuwa ni

kwa Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kuanza utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hatua ya utekelezaji ambayo nchi yetu imefikia hivi sasa, ni dhahiri kuwa nchi yetu imechelewa sana. Ni dhahiri kuwa Serikali haikutimiza wajibu wake kuhakikisha mchakato huu wa kujitathmini unatekelezwa kwa wakati, kwani takribani miaka sita imepita tangu Bunge hili lipitishe uamuzi wa kuingia kwenye mchakato wa *APRM*, lakini hadi leo hatujaweza kupata ripoti ya mwisho ya *APRM* kuhusu nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida, zoezi la kujitathmini linapaswa kufanyika mara moja ndani ya kila miaka mitano. Wakati nchi yetu imechukua miaka sita bila hata kupata ripoti ya mwisho ya *APRM*, nchi nyingine za Afrika kama Ghana, Uganda, Rwanda na nyinginezo zimeshajitathimini na kupata ripoti nzuri. Huu ni uzembe. Kambi ya Upinzani inahoji, ni sababu gani za msingi zilizoifanya Serikali ishindwe kutekeleza mchakato wa *APRM* kwa wakati kama nchi nyingine za Afrika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ripoti ya awali ya kujitathmini wenyewe ipo tayari na kwa kuwa taarifa tulizonazo ni kwamba timu ya Wakagazi wa *APRM* kutoka Afrika Kusini, itafika nchini mwezi Septemba kwa ajili ya kuihakiki, Kambi rasmi ya Upinzani inalitaka Bunge lako Tukufu kutenga muda kwa Bunge hili kujadili ripoti hiyo ili kupitia mjadala huo Bungeni, tupate fursa ya kuiboresha kabla ya kuwasili kwa Wakagazi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani ina taarifa kuwa ndani ya kipindi chote cha miaka sita Serikali haikulipa ada ya uanachama wa *APRM* pamoja na deni la nchi yetu katika Sekretarieti ya *APRM* ngazi ya Bara la Afrika na malimbikizo kufikia jumla ni shilingi bilioni 1.07. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuthibitisha taarifa hizi na kujieleza ni kwanini kwa kipindi chote hicho haikulipa ada ya uanachama *APRM* na lini italipa fedha hizo, kwani hii ni aibu kubwa kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mojawapo ya malengo ya Wizara katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 imeelezwa kuwa ni kuongeza uwakilishi wetu nje kwa kufungua Balozi mpya na kuongeza umiliki wa nyumba za makazi na ofisi za Ubalozi katika Balozi zetu nje kwa kadri hali itakavyoruhusu. Pamoja na lengo hili kuwa zuri la kuwa na majengo yetu wenyewe hasa, kungesaidia kupunguza fedha nyingi inayotengwa kwa ajili ya Balozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la utekelezaji wa kuwa na majengo yetu wenyewe, utekelezaji wake hauko kivitendo. Hii ni kutokana na kutenga bajeti ndogo kwa shughuli za maendeleo kwani mwaka huu wamepanga fedha kununua jengo la ofisi ya Ubalozi wa Paris tu kati ya zaidi ya Balozi 22. Kwa kasi hii ya kununua jengo moja kati ya 22 huwezi kusema kuna dhamira ya dhati ya kuwa na majengo tunayoyamiliki wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa spidi hii, itatuchukua zaidi ya miaka 20 kuwa na majengo ya Balozi kwenye nchi ambazo tuna ofisi. Hii itatimia tu kama hatutaongeza kufungua Balozi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutakuwa na dhamira ya dhati ya kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya maendeleo kwa kununua majengo mengi zaidi, kutaokoa zaidi ya shilingi bilioni 9.9 kwa mwaka kiasi ambacho ni kikubwa mno kulipia pango la ofisi na nyumba za watumishi wa Balozi. Hii ni sawa na asilimia 12 ya fedha yote ya matumizi ya kawaida ya Wizara hii ya shilingi bilioni 80.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika malipo yanayogubikwa na rushwa na asilimia 10, ni malipo na mikataba inayofanyika nje ya nchi. Balozi hizi kama zisipokuwa na wafanyakazi waadilifu ni rahisi sana Balozi hizi kuwa na wizi kwenye malipo haya ya pango na ununuzi wa majengo. Kambi ya Upinzani inashauri Serikali kuweka uwazi mkubwa katika malipo haya ya Balozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaamini kwamba wakati umefika ambao maslahi ya nchi yawekwe mbele kuliko maslahi ya mtu mmoja mmoja au kundi la watu, kwani nchi hii na maliasili zote ni kwa ajili yetu na vizazi vijavyo. Hivyo basi, lazima wote tupaze sauti zetu kwa umoja ndani ya hili Bunge Tukufu katika kulinda maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ezekia Wenje - Waziri Kivuli wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Waheshimiwa Wabunge sasa nitawataja tu wale ambao wataanza kuchangia asubuhi ya leo na waendelee kuijandaa nitakapokuwa nasoma matangazo ya kazi. Mchangiaji wa kwanza atakuwa Mheshimiwa John Shibuda, wa pili atakuwa Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, na wa tatu atakuwa Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya. Waendelee kuijandaa lakini kwa sasa nifanye kazi ya kutangaza matangazo ya kazi ambayo nilikuwa sijayatangaza kwa sababu yalichelewa kufika.

Waheshimiwa Wabunge, kesho tarehe 23 Julai, 2011, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira itakutana na asasi isiyo ya Kiserikali ya Haki Ardhi, kwa ajili ya kujadili masuala yanayohusu wafugaji na wakulima. Hii siyo kwa Kamati tu, hata wale wadau wa wafugaji ambao ni Waheshimiwa Wabunge wanaotoka maeneo ya ufugaji, basi na wao wanawenza wakahuduria kikao hiki.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine, leo tarehe 22 Julai, 2011 jioni kutakuwa na tafrija ya Wabunge kwenye viwanja wa Bunge. Tafrija hii imedhaminiwa na Kampuni ya Simu ya *VODACOM*. Kabla ya tafrija hiyo kutakuwa na maonesho yanaendelea, ambayo yalianza toka jana na yanafanyika katika viwanja vyetu vya maonesho. Wote

mnakaribishwa na kadi zimekwishagaiwa. Kwa hiyo, jioni wakati tunaipongeza Yanga kwa ubingwa, tutaendelea kusherehekeea na *VODACOM*. (*Makofi*)

Kesho pia tarehe 23 Julai, 2011 kuanzia saa mbili jioni kutakuwa na *cocktail party* iliyoandalila na *NMB* kwa nia ya kuwapongeza Wanamichezo wa timu ya Bunge na *NMB* watakaoshiriki mchezo kesho. Kwa hiyo, kesho kutakuwa na mchezo na baadaye kutakuwa na hiyo tafrija katika viwanja vya Bunge. Waheshimiwa wote mnakaribishwa.

Tangazo lingine ni kwamba, leo mchana katika Chumba Na. 133, Ghorofa ya Kwanza, watacutana wachezaji wa timu ya *Pool Table* ya Bunge kwa nia ya kuweka mkakati kwa ajili ya mechi ya kesho dhidi ya Viongozi wa Taifa wa Mchezo wa *Pool Table*. Wale Wachezaji najua tunafahamiana, tukutane kwenye Chumba Na. 133 ili tuweke mikakati hiyo. Lakini leo tutakwenda hoteli ya *Tiger Motel Area C*, kwa ajili ya mazoezi, pale kuna meza nzuri ambayo itatufaa kwa mazoezi. Kwa hiyo, wachezaji wote wa *Pool Table* tunaombwa tufike pale saa 2.00 baada ya kuahirisha Bunge.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, leo tarehe 22 Julai, 2011 itakuwa na kikao cha Kamati katika Ukumbi Na. 231 kuanzia Saa 7.00 mchana. Pia kuna tangazo lingine la *Club* ya kulenga Shabaha. Waheshimiwa Wabunge wanataarifiwa mashindano ya kulenga shabaha yatakayofanyika katika Kambi ya Makutupora kesho siku ya Jumamosi tarehe 23 Julai, 2011 kuanzia saa 4.00 asubuhi. Mabasi ya kuwapeleka Waheshimiwa Wabunge kambini Makutupora yatakuwa tayari katika viwanja vya Bunge kuanzia saa 1.00 asubuhi.

Tangazo la mwisho, Wabunge wote wa CHADEMA wanatakiwa kukutana katika kikao saa 7.00 mchana. Mahali ni katika Ofisi za Kambi ya Upinzani. Tangazo limetolewa na Mheshimiwa Raya Ibrahim, Naibu Mnadhimu.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo ya kazi. Sasa tunaanza na wachangiaji, na mchangiaji wetu wa kwanza kwa siku ya leo katika Wizara hii ni Mheshimiwa John Shibuda.

MHE. JOHN SHIBUDA MAGALLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kushukuru kupata nafasi ya kwanza kuchangia hoja ya hotuba ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Kwanza kabisa napenda kujitambulisha kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati hiyo, na vivyo hivyo napenda kuunga mkono hoja iliyotolewa na Kamati na naomba kuunga mkono msisitizo wa kwamba Waziri na Wizara yake, pamoja na Serikali Kuu sasa wakati umefika watambue kwamba kuwapeleka Mabalozi nchi za nje na wakawa hawana nyenzo za kulitumikia Taifa letu ni sawasawa na kumpeleka askari vitani bila kumpa silaha. Kwa hiyo, nashauri kwamba, wakati umefika Serikali iwe na ujasiri wa maamuzi magumu ya kuangalia kwamba faida ya kumpeleka Balozi katika Nchi za Nje, inakuwa na tija kwa ustawi na maendeleo ya nchi, kuliko kwenda kujaza nafasi za Ubalozi, lakini wajibu ni mtupu. Kwa hiyo, naomba hilo lifahamike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kutambulisha kwamba Mheshimiwa Bernard Membe, ni rafiki, ndugu wa muda mrefu. Haya haya nitakayosema kama yatakuwa yanamgusa hisia binafsi, atambue kwamba tuko hapa kujenga mustakabali wa umoja wa fikra endelevu kwa maslahi ya Taifa. Kwa hiyo, hayo nitakayoyasema naomba tu aeewe kwamba udugu wetu uko pale pale, na namtakia kila la kheri pamoja na Mama Alpha Omega.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Taifa letu linazungumzia mustakabali wa Ushirikiano wa Kimataifa, Wananchi wa Maswa, Shinyanga, Mwanza na maeneo yote yanayolimwa Pamba wanasema ya kwamba, hivi faida ya ushirikiano wa kimataifa ni nini kwa Wakulima wa Pamba wakati bei ya Pamba imeteremka? Ushirikiano huu wa kimataifa unaleta faida gani katika nchi yetu? Ikiwa tuna raslimali zetu lakini hatuoni faida yake ili Serikali iweze kufidia bei nzuri, huu ushirikiano wa kimataifa una faida gani kwa Watanzania, hususan tunapozungumza kuhusu ushirikiano wa uwekezaji wa kimataifa?

Wao wakiona ya kwamba wamedhulumika kidogo, wanatushitaki kimataifa, tunatuhumiwa: Je, Serikali yetu inatazama vipi? Napenda kulisema hilo kwa sababu madai ya mkulima kuhusu uchumi wa kaya, afya bora, maisha bora, wajasiriamali, madai yao ya kupata mitaji ni kutokana na kutambua ya kwamba nchi hii inaweza kujitegemea kutokana na raslimali zake na maliasili tulizonazo. Hivyo, ushirikiano wa kimataifa ambaou umefikia hatima ya kuzaliwa mikataba mibovu: Je, Wizara yetu inajituma vipi kuona ya kwamba matatizo hayo yanaondolewa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia imeshuhudia kuperomoka kwa uchumi, inashuhudia nchi ambazo zinasaidiwa na Umoja wa Ulaya kuhakikisha kwamba zinakuwa *bailed out* ili ziweze kuendelea. Lakini je, sisi tunakuwa *bailed out*? Tunapata unafuu gani kwa kubebwa ili hatma ya bei ya mazao yetu kutokana na bei ya raslimali dhahabu, almasi na madini mbalimbali, utalii; unajenga bei imara dhidi ya kuperomoka kwa bei ya pamba na mazao mengine? Ushirikiano gani huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na ujenzi wa hali hiyo naomba kumtambulisha Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwamba Mau Mau wa Kenya jana kupitia BBC wamekubaliwa kuishitaki Serikali ya Uingereza dhidi ya dhulumati walizopipata wakati wa Ukoloni. Je, Serikali yetu na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, wanajituma kwa tabia ya desturi ya vitendo gani vya ujasiri kufungua kesi Umoja wa Mataifa, kuhusu Makampuni ya Kimataifa ambayo mikataba yake ni ya unyonyaji? (*Makofi*)

Mnafanya nini? Kwanini Mheshimiwa Bernard Membe asishitakiwe kwenye Mahakama ya Kimataifa kwa kuacha kuwa na ujasiri na uzalendo wa kujituma, kutumia ujuzi wa Wataalam mbalimbali wa kwenda kufungua madai dhidi ya bei dhulamati ya raslimali zetu? Nimesema hayo kwa sababu gani? Mahakama ya Kimataifa imezidi kushika watu wanaoitwa Viongozi wa Bara la Afrika kwa utawala mbovu: Je, hao watu

ambao wanatunyonya kwa mikataba mibovu kwanini wasipelekwe kwenye Mahakama ya Kimataifa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, upole na ustaarabu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kukaa kimya dhidi ya dhulumati hizi, tunaogopa nini? Tunaogopa nini ikiwa Baba wa Taifa alikuwa na ujasiri, na ikiwa Serikali inatekeleza uasilia wa siasa na sera za TANU na Afro - Shirazi zinazoitwa sera za CCM? Ikiwa matakwa ya Katiba ya nchi na katiba ya CCM yanahimiza raslimali zitumike kwa maslahi ya Tanzania: Je, Serikali inatekeleza hii? Mnatekeleza siasa na sera ya CCM asilia au mmeishajivua? Je, ninyi ni chama gani ambao hamheshimu hata matakwa ya Katiba yenu na matakwa ya Katiba ya nchi? Je, wakati umefika wa kwamba korokoroni kamaliza masaa yake ya kulinda lindo, sasa aondoke Chama cha CHADEMA kishike lindo? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli humeza na utamu wa uhondo wa maneno ya uongo ya kufanana na ukweli. Nasikitika sana kuna maneno ambayo yanasemwaa kila siku, Serikali sikivu imeyapokea, tutayafanyia kazi, tutawajulisha. Hivyo, hayo maneno ya uhondo wa uongo mtamu na kufanana na ukweli ni lini mtaayacha? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umma wa Watanzania unashangazwa na ukimya kuhusu ujasiri wa kutotetewa maslahi ya Taifa letu. Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba nchi iambiwe, Baba wa Taifa na TANU ilipokuwa inadai uhuru tulisema, raslimali za Tanzania haziwezi kuwa malighafi ya maisha bora ya Ulaya. Leo mikataba hii kinyemelea ukoloni mambo leo, naomba mtuambie Watanzania kelele iko wapi? Mbona hatujaisikia hata Umoja wa Mataifa? Hatujasikia Umoja wa Mataifa mkikataa Tanzania tusiwe malighafi kupitia mikataba mibovu.

Je, ninyi kweli ni CCM asilia? Je, huo ndiyo ushirikiano wa kimataifa? Je, ukimya wa Wizara hii ndiyo mbinu ya kulinda Ujamaa na Kujitegemea? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema hayo kwa sababu wahenga husema, "Lisilopendwa kusemwa ama kwa kuandikwa, basi liimbiwe wimbo." Kwa hiyo, Uhuru ni Kujitegemea, Uhuru ni Ujamaa, naona ya kwamba wimbo wake ni maandamano ya kuwahimiza Watanzania wazinduke, wadai haki na watoe ujumbe kwa hao Mabalozi waliopo Tanzania, kwamba Watanzania wana machukizo, wanadhulumika.

Tunapozungumza hayo na ninyi Wabunge wa CCM muunge mkono kwa sababu ni matakwa tu ya katiba ya CCM na pia matakwa ya Katiba ya nchi, anayekataa kuunga mkono hayo na Mheshimiwa Bernard Membe usipounga mkono hayo wewe lazima ushitakiwe Mahakama ya Kimataifa kwa kuhifadhi dhulumati kwa kukataa kutumia ujasiri na maarifa yako kwenda kudai haki za Watanzania. Mimi nitashangaa. Ni kweli, ukumbuke nilikuwa mgombea wa Urais. Ningekutoa kama ningekuwa Rais. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, CCM ilikuwa na utaratibu wa kujisahihisha, na kujikosoa ni kujiimarisha. Afrika imeanzisha *African Peer Review Mechanism (APRM)*

nashukuru Wabunge mlinichagua kwenda kuwakilisha katika *APRM*, lakini vii *APRM* inayotekeleza mwegemeo wa siasa ya kujisahihisha na kujikosoa na kujiimarisha hadi leo pana kulegalega kufanikisha bajeti ya mahitaji yake? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ni hodari wa maneno matamu, rafiki yangu namjua huyu. Wewe hata kama unataka kupeleka posa kwa Mfalme, mtume Mheshimiwa Bernard Membe, hata kama una chongo ataita kengeza. Lakini naomba kumwambia aache maneno matamu, *APRM we need money*, tunataka pesa ili muweze kuhakikiwa kama mnatekeleza majukumu yenu. Serikali lazima itazamwe, *APRM* ni darubini ya kutaka kutambua ukweli uko namna gani. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeridhia Itifaki nyingi sana, lakini napenda kusema kwamba Wizara hii ni nyenzo ya kutunza imani ya Ushirikiano wa Kimataifa. Wizara hii ni nyenzo ya kuwafanya Watanzania wapende Ushirikiano wa Kimataifa. Wizara hii itambue historia ni kwanini *ANC*, *FRELIMO*, *SWAPO*, *MPLA*, na vyama mbalimbali vildai uhuru? Ni kwa sababu ya dhulumati ya ushirikiano wa Kimataifa baina ya nchi hizo. Kwa hiyo, naomba Taifa hilo uliondoe katika hali hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufedhuli wa mikataba mibovu ya makampuni mabovu, NI ukificha ukweli wake, maana yake unaandaa kuzaliwa mivumo. Naomba sasa kusema tu majumuisho ya nasaha na ushauri kwa sababu uzee ni dawa. Ukificha ukweli, unaomba mivumo ya hisia ya kusaliti ukweli. Kuishi kwangu kwingi, nimeona mambo mengi. Baadhi ya viongozi ni giza, wanaogopa mwanga. Viongozi wanaoogopa mwanga, wana tabia ya kuzusha, mtu asingiziwe hoja kwa maslahi ya kulinda na kusitiri upungufu wa huyo kiongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwaambia, Wanamaswa wanasesma kwamba, “raha ya maharusi ni kutomasana.” Maswa wanasesma na kuwaambia Watanzania kinagaubaga, “tulieni, ukichoma kuni moto, hutoa majivu.” Lakini wananchi wa Maswa wanawaambia kuwa, “Shibuda ni gogo la udi, likichomwa moto ndiyo linavutia zaidi.”

Kwa hiyo, napenda kuwaambia, “anayeuzza mkufu bandia hulipwa pesa bandia”, na maana yake ni nini? Fikra bandia ni tofauti na fikra asilia. “Aliyepewa na Mungu hapokonyeki.” (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, umma una kiu ya ustawi na maendeleo ya Jamii. Cheo cha dhamana kisiwe ukiziwi wa kusikiliza wasio na vyeo, kwani mtu maskini siyo fukara wa busara na hekima. Uongozi wa kujenga na kuzua mema utajengwa hivi sasa. Viongozi wetu acheni mambo ya kufikirika na mkahamisha upungufu wenu kwa kubambika kesi bandia kwa watu ambao ni wanyonge eti hawawezi kuwa na haki kwa sababu siyo viongozi. Wosia wa Baba wa Taifa ulikuwepo, umeonya, ni kweli vyeo vina vishawishi vya ulevi. Hivyo, naomba kusema kama mazalia ya mbu hakuna, na malaria hakuna. Lakini kama hakuna mazalia ya dhulumati, hakuna manung’unico ya kusigana. Ukweli una tabia ya kuudhi masikio ya mtu dhulumati, ndiyo maana Manabii waliudhi sana Wafalme dhulumati. Inshallah Mwenyezi Mungu tuokoe Tanzania tusiwe na Wafalme dhulumati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa John Shibuda. Nadhani vijana wanaosoma sasa wanawenza kuona uwezo wa tenzi ulionao ni mkubwa na tumefurahi na hotuba yako. Ahsante sana. Anayefuatia sasa ni Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia Wizara hii ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nishukuru Shirika la Umoja wa Mataifa kwa kuiheshimu nchi yetu ya Tanzania na kumchagua Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete aweze kuwa ni Mwenyekiti wa Afya ya Mama na Mtoto. Hii ni heshima kwa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuipongeza Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa suala moja kubwa la msingi ambalo pia ni la muhimu ambalo limetokea hivi karibuni nalo ni la kuhusu suala la rada. Ukweli ni kwamba wametambua umuhimu wa wawakilishi wa wananchi. Kwa sababu wanajua fedha hizi ni za wananchi ndiyo maana wakawenza kutuma wawakilishi wa wananchi kwenda Uingereza kwa ajili ya *ku-negotiate* masuala ya fedha kutoka *BAE*. Mimi nawapongeza kwa hili, hii ni *purely shuttle diplomacy*. Nawapongeza sana. (*Makofi*)

Nakumbuka hata Mchungaji Jassey Jackson wa kule Marekani kulikuwa na *crisis* kule Kosovo alitumwa yeye kwenda *ku-negotiate*. Vile vile kule *Eastern Congo* kulikuwa na *crisis*, alipelekwa Olesegun Obasanjo, aliyekuwa Rais wa Nigeria, kwenda *ku-negotiate* lakini baadaye pia kwa heshima ya Tanzania akatumwa Mzee wetu Mheshimiwa Benjamin Mkapa kwenda kule, na hii yote ni *shuttle diplomacy* ambayo mimi nasema Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa inafanya kazi yake vizuri. Naipongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tuko kwenye sera ya *economic diplomacy*. Ni kweli mambo yetu yanahusiana na mambo ya Kitaifa, ushirikiano na kadhalika. Lakini tunapozungumza *economic diplomacy*, tuna maana gani? Mimi naweza nikasema kwamba pamoja na pongezi zote ambazo nimezitoa, lakini nchi kama nchi bado Balozi zetu hazifanyi kazi hasa katika masuala ya *economic diplomacy*. Mabalizi wetu nchi za nje wawe wanatoa *opportunities* kwa wafanyabiashara wetu wa Tanzania ili wawe wanajua kule nchi za nje kuna *opportunities* za aina gani? Lakini hilo halifanyiki, na kama linafanyika, basi ni kwa nadra sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunapozungumzia *economic diplomacy*, hii *economic diplomacy* unakuta kwamba nchi yetu ina Balozi nchi za nje, lakini hizi Balozi nchi yetu inafaidika nini? Kuna masuala ya *political integration* ni sawa, lakini sasa hivi tuko kwenye hii *economic diplomacy*, tujaribu kuangalia zile *Asian tigers countries* zote kama siyo Balozi, basi tuwe na *Consulate* ili nchi yetu na yenewe iweze kunufaika.

Kwa mfano, China tuna ubalozi kule Beijing. Sasa ukiangalia Beijing na Gwan Zou ni mbali sana. Nchi yetu wafanyabiashara waweze kunufaika angalau pale Gwan Zou kuwe na *Consulate*, wananchi hawa wa Tanzania wanaoishi kule ama wanaokwenda kufanya biashara kule waweze kunufaika na mambo yao yaweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia tena masuala haya ya *economic diplomacy*, Balozi zetu kule nje kwa kweli zimechoka sana, tuna *commercial attaché*. Mimi sielewi kazi wanayoifanya ni kazi gani. Kwa sababu hawa *commercial attaché* wanasubiri vitu viwafuate. Wanatakiwa ifike mahali sasa hivi waweze kuwa *pro-active*, wasiwe *Just in active*. Wawe *pro-active* wao waende nje wakatafute *opportunities* waweze kuwasiliana na huku nyumbani kwa sababu wamepelekwa huko kwa sababu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine, hata Mabalozi wetu imefika wakati sasa pamoja na kwamba kuna *political appointees* na vile vile kuna *career appointees*, ifike mahali twende na wakati kwamba tuko kwenye *economic diplomacy*, mtu kama anapelekwa ni *political appointees*, basi ijulikane hiyo nchi anayopelekwa ni nchi ya aina gani na sifa za huyo Balozi zinaendana na hiyo nchi? Vinginevyo tutabaki kuzungumzia masuala ya ushirikiano wa Kimataifa lakini kwenye suala la uchumi tunaliweka kando na sasa hivi tuko katika masuala ya uchumi kuangalia nchi yetu inapiga hatua kiasi gani kwa mambo ya uchumi. Kwa hiyo, zile kazi nyingine zinazofanywa na Balozi ni kweli zipo, ziendelee, lakini tutilie mkazo zaidi kwenye masuala haya ya uchumi kama sera yetu inavyosema *economic diplomacy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Balozi zetu kama nilivyokwisha kuzungumza ni kwamba zimechoka sana, wafanyakazi ni wachache na mishahara yao inachelewa. Majengo yanunuliwe, siyo kukodi, maana wata-*sublett*, itaongeza kipato cha kujiendesha kiofisi/kiuchumi. Kwa mfano, hata hapo Balozi wetu wa Rwanda, wafanyakazi ni wachache Balozi hata gari hana, inasikitisha sana na sielewi ni kwa nini. Kitu kingine unakuta nchi kama ya Hungary hakuna Balozi kabisa. Lakini *Tanzanian Community* inayoishi kule inajikuta haina msaada wowotehakuna *Councilor/Consulate* ambayo anaweza akawasiliana nao pale wale Watanzania wanaoishi huko au nchi yoyote ile ambayo Watanzania wapo.

Kwa hiyo, ningeshauri Wizara husika kwenye hizi nchi zetu zote ambazo tunawakilisha wakati mwingine hatuna Balozi, sawa, inawezekana bajeti ikawa ni ndogo ama finyu. Lakini tujaribu kuwa na *Councilor* mahali pale ambaye atafanya *admisistrative work*. Kwa mfano, Mtanzania amefariki au anaumwa, ni rahisi sana kujua jinsi gani ya kufanya na huyu *Councilor* awe ni Mtanzania asiwe mtu wa pale, maana yake anapokuwa mtu wa pale, hiyo tunazungumzia sasa ni *goodwill ambassador*, sio *Councilor*. Sasa kama *goodwill ambassador* ni kweli unaweza ukachagua *celebrity* yoyote katika ile nchi au mfanyabiashara yejote kwa ajili ya *ku-raise flag* ya Tanzania kutokana na masuala ya uchumi na kadhalika. Lakini linapokuja suala la Utanzania, mila na desturi, huyu Mtanzania *Councilor* anakuwa anazijua. Kwa hiyo, ni vizuri kuwe na *Councilor* ambaye anakuwa ni Mtanzania *obviously* atakuwa ameshawekewa vigezo vya

aina gani ili aweze kufaa kwa ajili ya hiyo kazi na hiyo vile vile itasaidia sana katika kupunguza bajeti kwa sababu tunaelewa tuna tatizo la ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho ningependa kukizungumzia ni kuhusu masuala ya *currency* kwa hawa Maafisa Balozi zetu ambao wako nchi za nje. Naomba nitoe mfano mmoja kwenye nchi hizi za *European Union*. Tuna Balozi zetu kule, kwa mfano, pale Brussels tuna Ubalozi, ni kweli, lakini hawa *foreign officers* wanatumia *euro* na unakuta kuna nchi nyingi tu ambazo zinatumia *euro* katika *European Union*. Lakini naona hapa haki haitendeki kwa sababu hizi nchi unakuta uchumi wao unatofautiana, lakini *rates currency* wanayopewa ya *euro* ni ile ile. Sasa hawa Maafisa wa Ubalozi wetu wanakuwa hawatendewi haki pamoja na pia kwamba pesa hizi zinachelewa. Lakini hebu Wizara ijaribu ku-*differentiate* kwamba hawa Maafisa Ubalozi wa nchi Fulani, uchumi wa hiyo nchi upo hivi na hivi, kwa hiyo, hata *rate* iendane kulingana na uchumi wa hiyo nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia pia suala la Balozi zetu ambazo kwa kweli hazitendewi haki. Lakini vile vile tuangalie kwenye masuala ya *economic diplomacy* kwamba hapa Kenya, Kenya wana Balozi nyingi karibu kila nchi, sawa inawezekana uchumi wao ni mkubwa. Lakini tukumbuke tena kwamba sisi kama nchi ya Tanzania ni nchi isiyofunganama na upande wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu kingine ambacho kinachonishangaza, kwa nini tuwe na mahusiano mazuri na nchi kama Palestina halafu tusiwe na mahusiano mazuri na nchi kama Israel? Ningombwa Mheshimiwa Waziri hili ajaribu kutufafanulia, ni kwa nini kwa sababu sisi hatufungamani na upande wowote, tungekuwa hata na *Councilor* pale Israel kama siyo Ubalozi kamili.

Ni vizuri siku zote kama nchi, tukajitahidi pamoja na kwamba tunaendeleza ushirikiano wa Kimataifa na nchi zote, lakini vile vile tuhakikishe kwamba tunainua hii sera yetu ya uchumi. Sasa kama nilivyozungumza, kama tunainua sera yetu ya uchumi, basi tujitahidi kuwa na Balozi, kama sio Balozi kutookana na ufinyu wa bajeti, tuwe na *Consulate* kwenye nchi zote zile ambazo tunafanya nazo biashara, kuliko kuhangaika na kusisitiza kwamba *Political integration*, sijui Mashirikiano. Tukumbuke tuko kwenye *economic diplomacy*. Kwa hiyo, hebu tujaribu kuwa *creative* katika hilo, tuwe *strategic*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu ni hayo kwa leo. Nashukuru sana. (*Makofi*)

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia. Lakini pia nikiwa kama Mbunge katika Bunge la *SADC* ambalo halijawa kamili kama Bunge, niseme kwamba nakushukuru sana.

Nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Mambo ya Nje - Mheshimiwa Bernard Membe pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Mahadhi Juma Maalim kwa kazi nzuri waliyoifanya. Niwatie tu moyo kwamba juhudzi zao zimeonekana na changamoto zote zinazotolewa.

Kimsingi ni kwamba binadamu tumeumbwa kupenda kusikia yale ambayo tunayapenda sisi wenyewe, yanapotolewa na watu wengine tunaona ni machungu, ni changamoto na kwa siku ya leo nimefurahishwa pia kuona kijana wetu kutoka Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Wenje kwa kweli amechangia mambo ya msingi ambayo sisi pia tunatakiwa kuyachukua yale ambayo tunaamini kabisa yatatusaidia ukiacha yale ambayo ya kuchomekea kidogo kunogeshea Kambi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba katika siku hii ya leo, nikimshukuru Mwenyezi Mungu nitoe shukrani zangu za dhati katika nchi ya Uholanzi, hususan Ubalozi wa Uholanzi ambao walituwezesha kupata *visa* kwa ajili ya matibabu ya mtoto wangu, Hope na kwa kweli kwa juhudhi kubwa ambazo zimefanyika na wananchi wa Uholanzi kupitia Kibo *Trust Fund* chini ya uongozi wa Bwana Betty pamoja na wengine wote, Laura na Janduurt, Winnie na Gerald, Madaktari wa Hospitali ya Rijnstate, Dr. Defeezer na Dr. Simon kuhakikisha kwamba mtoto wangu ambaye alikuwa ni mlemavu akitembea kwa magoti, sasa anaweza kutembea kama sisi. Nashukuru sana. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi katika suala la amani, umelizungumzia vizuri sana kuhusu amani, kuhusu matatizo yaliyopo kwa wenzetu huko Afrika ya Kaskazini, hususan Libya, niseme tu kwamba mimi nikiwa kama mwanamke, nasimama nikiwaomba Mataifa yote, nikiziomba nchi zote zinazosimamia usalama wa Kimataifa wafahamu kwamba vita ni vita, hakuna vita tamu, kombora ni kombora na lina maumivu na halina upenzi wowote ule hasa linapotua sehemu ambayo kuna mwanamke mwenye watoto na asiye na hatia. Inabidi walitazame upya na kuangalia jinsi gani tunaweza tukasuluhisha migogoro yetu kwa njia ya amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea pia taarifa ya suala la mapambano dhidi ya malaria ambalo pia liko katika changamoto za malengo ya *millenium*. Tanzania tukiwa wapambanaji wa kwanza katika eneo hili kupitia *NDC* Tanzania, tunajenga kiwanda cha kutengeneza dawa za kutokomeza malaria ambayo pia tunasaidiwa na wenzetu wa Cuba. Tanzania ina majukumu yake ya kutoa pesa kwa ajili ya maji na umeme. Ningeomba sana Serikali isiweke kigugumizi katika hilo, itoe pesa kwa wakati kuhakikisha kwamba kiwanda hicho kinakamilika mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi katika taarifa za Bunge la *SADC* mlionituma, safari hii *theme* yetu ilikuwa ni Kuelekea Bunge la *SADC* au *Towards SADC Parliament*. Katika Mkutano wetu tulizungumzia umuhimu wa kuwa na Bunge kamili la *SADC* kwa sababu ili tuweze kuwa na usimamizi wa wananchi wenyewe katika maendeleo ya kiuchumi na maendeleo ya maisha ya kawaida ya wananchi waliopo katika eneo la Kusini mwa Afrika, ni vyema sasa tukawa na Bunge kamili ambalo litaweza kusimamia na kuratibu shughuli zote zinazoendelea. Ndio maana hata sisi Tanzania leo tunajivunia kuwa na Bunge hili kutokana na umahiri wake katika kusimamia mipango isiyo na usimamizi, mipango isiyo na uwajibikaji kutokana na kutokuwa na Bunge ambalo lipo kamili. Sasa hivi watu wanazungumza lakini kwa sababu Bunge lile halijawa ni Bunge kamili, haliwezi kutoa maamuzi ambayo yanaweza kumwajibisha au yanaweza kutoa kauli iliyosimama katika nchi zinazohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hivyo tu, ni shukrani za pekee kwa nchi yetu ya Tanzania ambayo imekuwa kama daraja kati ya nchi za Afrika Mashariki na nchi za Afrika ya Kusini na hivi kutaka pengine Mungu akibariki huko mbele, hili liwe ni *block* moja na hatimaye kuwe na Afrika moja. Tunaona kwamba ni muhimu sana kuwa na Bunge hilo na lugha ya Kiswahili iwe ni mojawapo ya lugha zitakazotumika. Jinsia ziweze kuzingatiwa kama ambavyo *SADC Protocol on Gender and Development* inavyozungumza na mambo mengine yote ambayo ni mazuri yaliyokuwemo katika Mabunge haya mengine yaweze pia kuambukizwa katika Bunge lile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi katika pongezi kwa suala ambalo lilikuwa linanigusa sana kuhusu vibali vyta ukaaji nchini au *Resident Permits*, ni jambo la kuhuzunisha sana hasa kwa sisi wanawake. Unapoolewa na mwanamume wa nchi nyingine au unapooa mwanamke wa nchi nyingine ni sehemu mojawapo ya kuvutia uwekezaji. Kwa sababu unaweza kuwa umeolewa na mtu ambaye ana uwezo mkubwa sana wa kuwekeza nchini au mwanamke mwenye uwezo mkubwa sana wa kuwekeza nchini, lakini kutokana na kukosa uraia, kutokana na kukosa kibali cha muda mrefu cha kukaa nchini, mtu huyo anajikuta ni mtu wa kupita, anakuwa hana mapenzi na nchi ile na hakika inapunguza hata mapenzi ya hao waliooana. Ninayo mifano ambayo inanigusa sana. Mfano wa kwanza ni wa huyu jirani yangu Dr. Mahenge, yeche kwa bahati nzuri alisoma Urusi na akaoa mama wa Kirusi, ana watoto naye. Lakini eti kila baada ya miaka miwili aende akamlipie kodi mke wake kwa ajili ya kibali dola 500 maana yake mwanzo ilikuwa dola 200 sasa hivi ni dola 500. Huu ni mfano halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaye Mwalimu mwengine yuko pale *Saint John's* hivyo hivyo, mke wake hawezi hata kuruhusiwa kufanya kazi, ni mtaalamu na wengine wanaoa Madaktari, wengine wanaolewa na watu muhimu tu wenyewe ujuzi mbalimbali, eti kwa sababu hawana hivyo vibali vyta uraia hawawezi kufanya kazi nchini. Jamani mbona tunaondoa fursa za muhimu? Mbona tunawatesa wenzetu? Kila wakati anaishi na mke wake au mume wake wakionana kwamba wewe mwenzangu ni raia wa nchi fulani na mimi ni raia wa nchi fulani, jamani tunakwenda wapi? Mimi nadhani hili ni tatizo kubwa sana na ni unyanyasaji mkubwa sana. Kwa kweli lifanyike kwa haraka hata kama sio kutoa uraia wa nchi mbili, basi vitolewe vibali vyta kudumu vitakavyomfanya mtu huyo aweze kuishi kwa amani katika kipindi chote anapokuwa katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anakuwa amemaliza tu masomo, anarudi na mke wake, anaambiwa lipa dola 500. Maskini pengine ndiyo alikuwa hana hizo hela! Kwa hiyo, inabidi aachane na mke wake, *simply* kwa sababu ametakiwa kulipa hiyo dola, na zilikuwa dola 200 tu, sasa hivi dola 500. Hivi nacho kibali cha kumwingiza mke wa mtu ni biashara? Kwa nini tumeongeza kodi katika eneo hilo? Kwa nini tumeongeza kiwango?

Mimi naiomba Serikali ifute mara moja au ibakize zile zile zilizozoeleka dola 200. Hii ni kunyanyasa mtu, sio sahihi. Matokeo yake mwanamume anaishi nchi nyingine, mwanamke anaishi nchi nyingine na sasa hivi tuna tatizo la UKIMWI, akijipitisha mtu maeneo mengine tutamfanya nini? Watu wanazidi kufa. Naomba suala hilo lishughulikiwe mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la mpaka wa Tanzania na Malawi. Tumeshalizungumzia sana hili suala. Huu mpaka ambao wengine wanasema uko katikati ya maji, wengine wanasema upo pembezoni. Mheshimiwa Membe kwa bahati nzuri ni mwekezaji kwenye eneo letu, ameoa kwetu, mbona hilo suala haliishi? Sisi tunashindwa kupata wawekezaji, tumeshakaa katika hali ya unyonge muda mrefu, tuna *beach* nzuri sana na sasa hivi tuna Wilaya ya Ziwa Nyasa, mpya, Serikali tunaishukuru imetupatia Wilaya ambayo kwa kweli inategemea sana maji kuwa ndiyo chanzo chake kikuu cha uchumi. Lakini pia ule ni mpaka ambao unaheshimika, kwa nini hili suala haliishi? Jamani sijui tufanyeje! Mpaka tulie, tufanyeje jamani? Watu wananyanyasika, matokeo yake kule kunakuwa ni kama tu chaka la kupita watu bila sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii mipaka tuiangalie vizuri jamani, kwa sababu haturuhusiwi kuchangia kila Wizara kutokana na wingi wetu. Lakini hebu tuseme, juzi wameshikwa Wasomali 70, boti lao likiwa linataka kuzama, wapo Ziwa Nyasa wanaelekea sijui Msumbiji kama wanavyosema wenyewe. Hebu niambieni mpaka wametoka huko Somalia mpaka wamefika huku wanashikwa baada ya kutaka kuzama. Kweli sisi hatuna ulinzi wa kutosha mpaka tunafikia kupata watu waliofika mpaka Ziwa Nyasa wametokea huku huku jamani! Hebu tuelezane ukweli, hapo hali hii ya kukosekana kwa ulinzi inatokea vipi? Hali ikoje?

Lakini pia tumeomba mara nyingi, tufungulieni mpaka sisi ndugu zetu wengine wako Malawi, tusifungwe sisi kuwasiliana na kupata fursa za kiuchumi za nchi jirani. Mbona maeneo mengine mnafungua, kama Kenya na wapi? Kwanini sisi hamtufungulii? Kikwazo eti ni meli. Juzi watu wamezama na boti na watu sita wamekufa na kwa taarifa yenu hata mkituzuia sisi maboti yetu yanaendelea kwenda, hata msipotaka kutoa vibali halali, boti zetu zitaendelea kwenda na watu wanachukua sukari wanatuuzia kwa sababu sukari ya huku ni ghali, kilo moja Sh. 2,500/=, kwa kule tunaipata kwa Sh. 1900/=. Watu wataendelea kufa, kwanini tusiweke haya mambo yakawa vizuri ili watu watumie fursa kwa uwazi na walipe kodi inayotakiwa?

Tunamshukuru Mheshimiwa Rais, ameliona hilo na akatuahidi meli, kwa kweli tunaingojea kwa hamu na tunaogopa, kama Chama cha Mapinduzi hakitatekeleza hilo, nina wasiwasi mwaka 2015 wale watu wanaweza kutunyima kura sisi. Maana wameshaanza tayari, Kata yangu mimi wamechukua CHADEMA. Tafadhalini, hiyo meli ipatikane, watu wafanye shughuli zao vizuri na kwa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo, nadhani muda wangu umekwisha. Ahsante sana, naunga mkono hoja na nizidi kuomba utekelezaji wa masuala hayo. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi nitoe mchango wangu. Ingawa Waziri wetu Mheshimiwa Membe ni rafiki yangu, lakini leo kidogo bora nikisema nisikuangalie, nimwangalie Mheshimiwa Mwenyekiti. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imebahatika sana kuwa na watu wengi wanaoishi nje ya Tanzania ambapo kwa lugha nyingine tunawaita *Diaspora*. Ila tu kilichokosekana ni kutokuwatuma raia hawa ama wa nchi hizo wanazoishi au Watanzania kuitumia nafasi yao kujenga uchumi wa nchi yetu. A very good example nitakayoitoa leo ni nchi mbili za kiafrika ambazo nimezifanyia *research* nikaona ni kiasi gani nchi hizo zinavyofaidika na *Diaspora* yao inayoishi nje ya nchi hizo. Nigeria leo inaingiza karibu dola bilioni sita mpaka nane kwa mwaka. Inasemekana kwamba Amerika peke yao wako milioni 15 na milioni tano wako Chicago. Sikwambii walioko Uingereza, walioko Scandinavia; na fedha hizi zinaingizwa nchini Nigeria kwa njia halali kupitia Benki. Hii ripoti niliyonayo ni ripoti ambayo imetolewa na *Western Union Bank* pamoja na *World Bank*. Tanzania tumejiandaaje *Diaspora* yetu ikatumika kusaidia uchumi wa nchi yetu? (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya wao, Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje alikabidhiwa barua rasmi na Wakenya wanaoishi nje wakitaka *open petition* na barua hiyo ikapelekwa kwa Rais kwa Mwai Kibaki, Raila Odinga kama Waziri Mkuu, akaipeleka kwa Spika na Mawaziri kutaka Wakenya hao waisaidie Kenya kwamba wao wanaishi nje ya Kenya, lakini Kenya ifaidike na Wakenya hao kiuchumi, kiteknolojia na kiutamaduni. Leo mwaka huu kuanzia Januari mpaka Mei Wakenya wameiingizia nchi yao Dola milioni 334.7. Only five months period. Chukulia miezi mitano mingine kabla hujatimiza mwaka mmoja, ina maana kwa hesabu za haraka uki-multiply by two utakuta mwaka huu Dola milioni 669.4. Tanzania tunaingiza nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakenya hawa wanapitisha kwa njia halali za kibenki. Sikwambii wale wanaowapa jamaa zao kupitisha kwa njia nyingine wanazoelewa wenyewe kupitia nchi za jirani kama kwetu Zanzibar au Tanzania. Kwa hiyo, utakuta Kenya imejidhatiti *Diaspora* yake iweze kufanya kazi vizuri. Sasa Tanzania tunaliweza hili, lakini mnakijua kilichokosekana? Kilichokosekana, hii Wizara Bajeti wanayotengewa ni ndogo mno. Kwa sababu watayarishaji wa mambo haya ni mabalozi wetu walioko nchi za nje. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda kamwulize Balozi Kallaghe aliye London, kamwulize Balozi Sefue, kamwulize Balozi Sisco aliye Malaysia, ana fedha gani za kuwaunganisha Watanzania wanaoishi pale wakaweba kuwa na *remittance* ikasaidia nchi yetu? Ni jambo la kusikitisha sana na kama hatutakuwa makini wakatengewa fedha za kutosha, Balozi akatumia hii nafasi, basi tutatengeneza mambo mengi ya ajabu. Mimi nilikuwepo *Diaspora III* mwaka huu London, tulikutana na Watanzania na Wazanzibar. Cha kusikitisha wale Watanzania walioko upande wa pili wa Muungano kutoka Bara hawajijui hata idadi yao ni ngapi. Lakini Wazanzibar wanajielewe idadi yao.

MWENYEKITI: Samahani Mheshimiwa Sanya umesema Watanzania na Wazanzibar? Weka vizuri.

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sorry nimeteleza ulimi. Nakusudia Watanzania wako sehemu mbili za Muungano. Wazanzibar na Watanzania Bara na zile *Diaspora* zimegawanyika hivyo pale London kwa sababu

kama alivyozungumza Mheshimiwa Waziri kwa upande wa Zanzibar Ofisi ya Rais ina Katibu wake anayeshughulikia mambo hayo. Kwa hiyo, Zanzibar wanajielewa wako wangapi.

Sasa hivi wale wa upande wa pili kwa maana ya Tanzania Bara hawajaanza kufanya hiyo kazi, sasa mimi nasema fedha zitolewe, bila ya fedha ni fedheha. Hii Wizara hata kama haizalishi, itakuja kuzalisha baadaye. Lakini watengewe fedha za kufanya hii kazi. Kinachotakiwa hapa kuwa na *coordination* nzuri. Leo la kusikitisha unakwenda Ubalozi kama Malaysia, Balozi wa Malaysia amepangishiwa nyumba, wanalipwa mwezi kwa mwezi. Ni aibu. Balozi ni *reflection* ya nchi. Bora usifungue Balozi kabla hujajiandaa. Kwa sababu unapofungua Balozi unaujulisha ulimwengu na nchi ile kwamba mimi nipo, bendera yangu ipo hata zile sherehe za uhuru wa nchi yetu wanashindwa kuwaalika Mabalozi wenzao kwa kukosa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Balozi wa Malaysia anawakilisha *Thailand, Laos, Vietnam, Brunei, Philippines* anatakiwa angalau kwa mwaka mara mbili azitembelee zile nchi. Leo Balozi anakaa katika nyumba amepangishwa, matokeo yake anadaiwa kodi sasa mwenye nyumba anakuja hana ustahimilivu anachukua wateja wengine kwenda kumwonyesha nyumba ambayo Mheshimiwa Balozi anaishi ndani ya nyumba ile, anamtembeza kwenye vyumba. Nyumba ina vyumba sita, hapa ukumbi, Balozi yuko ndani, si hasha kesho bahati mbaya Rais wetu akatembelea nchi ile, akawa yuko ndani ya Ubalozi wakagongewa mlango akaambiwa tupishane kidogo, tumekuja na mteja mpya. Tutafanya nini? (*Makofi*)

Lazima kuwe na *reputation* ya nchi, wale ni watu *Diplomats*. tumia ujenge ili upate uchumi wako kuinuka. Hali za Mabalozi wetu ndivyo zilivyo na Mabalozi hawa hasa huyu Mheshimiwa Kallaghe, Sefue, Sisco, Balozi wa Zambia na wa Kenya wanafanya kazi katika hali ngumu sana ya kimaisha. Wakati mwingine wanashindwa hata kupokea mishahara yao. Wanakuwa na wagonjwa ambao ni Maafisa Ubalozi wao wanashindwa hata kuwalipia gharama za hospitali. *Why this?* Lazima tuwe tayari kujenga heshima yetu kuitia Mabalozi wetu. Was wahili tunasema, “*kata pua, unga wajih*”. Tuchuke kasma ya fedha mafungu mengine, lakini hizi Balozi zifanye kazi. Balozi awe na gari ya Kibalozi, Balozi awe na dereva, Balozi awe na hospitali, awe na *insurance* apate tiketi ya kutembelea maeneo ambayo amepangiwa. Ndipo Balozi anaweza akafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho nataka nizungumzie hapa ni kuhusu hawa Mabalozi wanapofanya kazi katika hizo nchi. Desturi ya Balozi akifanya kazi katika ile nchi anaangalia mazingira ya nchi yake na nchi anayokwenda kufanya kazi. Unampompangia Balozi kuwa Malaysia, basi Balozi huyo *definitely* awe na *concept* ya nini kinazalishwa Malaysia, nini tutaweza tukauza na nini tutaweza tuka-*gain*. Kwa hiyo, Malaysia wako *advanced* kwenye *IT* na ajikite kwenye *IT, Agriculture* wanazalisha mpira na michikichi, ajikite huko ili na sisi tujifunze tuweze kujua namna gani wao wanazalisha, namna gani wanatengeneza bidhaa, namna gani wanasa firisha nchi za nje ili sisi mabalozi wetu wafanye kazi za kiuchumi zaidi kuliko za kisiasa kama ilivyokuwa wakati wa miaka ya 1960. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ardhi zetu zinavyotumika. Tunakuwa na *bogus investors* kutokana na matatizo yetu wenyewe. Tukishamkatia mtu kitalu au ardhi ya madini, ma-*geologist* hawafanyi kazi yao wakaainisha madini gani yaliyoko kwenye ardhi. Ukishaainisha ukampa kibali, kwa hiyo, mwenye kumiliki ardhi hatakuja *investor* akambabaisha, akamwambia uongo, akaingia kwenye mikataba ambayo inatuletea hatari katika nchi yetu. Lakini akijua kama kuna almasi, hutamwambia kama kuna shaba, anajua na *geologist* wameshampa ripoti ya kwamba kuna almasi chini. Sasa Mabalozi wetu wafanye kazi za ziada kutafuta *investors* ambao wana uchungu na wanakuja kuvuna, lakini iwe ni *win-win situation*. Isiwe yeye anakuja ku-*grab* raia anapata matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda Angola, hufanyi biashara bila kuwa na leseni ambayo ina jina la mzaliwa wa Angola kama ilivyo Dubai. Lakini sisi leo mtu anauza *beach* yake ili ijengwe hotel, baada ya miaka mitano kauza kwa dola 50,000/= hazipo pesa, hotel inaendelea. Kwanini Serikali isimsimamie ikamwambia kweli unauza, lakini utapata pesa kiasi fulani na kiasi fulani uta-*invest* katika hii hoteli na wewe utakuwa *unAGAIN 10 - 15 percent for your life time*. Atapata yeye, watapata wanawe na wajukuu zake na ndivyo ilivyo leo Karikoo watu wanaiza majumba watu wana-*invest buildings* mwenye nyumba anakwenda sehemu nyingine baadaye anashindwa kuwa na fedha, anashindwa kuyamiliki maisha yake. *Information is power, but what is more powerful is the use of information*. Kwa hiyo, lazima tuwape *information* wa kile wanachokimiliki wananchi wetu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Dual citizenship* ni muhimu. Leo ninavyozungumza, mwanamke akiolewa hana haki, mwanaume akioa ana haki. Kuna tofauti gani? Si Watanzania? Tena mimi nampa haki zaidi mwanamke anayeolewa. Niulizeni, kwa nini? Akiolewa akizaa mtoto wa kitanzania, yule mtoto atapata utamaduni wa kitanzania kwa sababu atafunzwa na mama yake ambaye ana utamaduni wa Tanzania. Lakini kama mimi Sanya nikienda nikioa London, mtoto wangu atafuata makole ya London kwa sababu mke wangu ndiye atakayemlea mwanangu. Hatuangalii hapo sisi. Sheria za *Migration* ziharakishwe kufanyiwa marekebisho ili wanawake wapate haki sawa na wanaume. La sivyo, hapo patakuwa hapakaliki. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kuna ripoti hapa ambayo kidogo ndiyo ilinitia wasiwasili kwamba Bajeti ya maendeleo ya mwaka jana na mwaka huu ni sawasawa. Why? Sisi nafikiri tungekuwa *gradually* tunapanda. Mwaka jana ilikuwa shilingi bilioni 44.5 mwaka huu shilingi bilioni 44.5 kuna maendeleo gani? Lazima bajeti hizi ziongezwe katika Wizara muhimu ili kujenga uchumi wa nchi yetu. Halafu hapa kuna watumishi 440 kati ya watumishi hao 249 wako Makao Makuu, kati ya hawa Wazanzibar wangapi? Chombo cha Muungano hiki. Hata kama ni Bara watakuja kufanya kazi huku, ni chombo chao, watafanya nini? Tungojee mpaka tukae na Rais tuje turekebishe! Hapana! Ifanye kazi sasa ili Katiba ikifika turahishe mambo ambayo ni kero za Muungano, ni haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako watumishi wetu 172 walioko nje. Watumishi wa kutoka Zanzibar ni wangapi? Unajua kuna mambo, sisi wenyewe tukijipanga tukaweka

katika hadhi ya kimuungano, *there is no problem*. Kitu muhimu ni kuaminiana, kupendana, kugawana madaraka na kugawana kazi. Kwani Mzanzibar hawezi kuwa Balozi? Hawezi kufanya kazi Makao Makuu Dar es Saalam, kwanini wa Dar es Salaam wasiende Zanzibar? *These are union matters*. Tukianza hapa, huko tunakokwenda kutakuwa rahisi. Lakini kama hatukuanza hapa tunakokwenda kutakuwa na mvutano na ugumu wake. Mimi nasema Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje naipongeza. Lakini fedha waongezewa wafanye kazi kuinua uchumi wetu na vilevile tuwe tayari kuonyesha dira ya kimuungano katika sekta zote na vyombo vyote nya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sanya ahsante sana kwa mchango mzuri. Hata mimi nimeguswa. Nilikuwa Uganda wakati juzi Rais Museveni anaapishwa tukatembeزوا na Kaimu Balozi pale, tukaangalia jengo lile la Tanzania zuri na kubwa ambalo linachakaa. Pale mkitumia hata ile *PPP* mnaweza mkafanya uwekezaji mkubwa, zile pesa zikawalipa watumishi na bado wakarudisha na nyumba kwa sababu lile jengo ni kubwa sana. Mheshimiwa Waziri na mimi ndiyo mchango wangu. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, huyu ndiye alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho na kwa sababu sina tangazo lingine lolote nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(*Saa 6.55 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11. 00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

MWENYEKITI: Nitamwita sasa mchangiaji anayeanza jioni hii naye ni Mheshimiwa John Paul Lwanji na baadaye atafuatia Mheshimiwa Leticia Nyerere.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, napenda kusema kwamba siungi mkono hoja. Sababu ya kusema hivyo, mtoa hoja anajua. Wala sisemi uongo, nasema ukweli na yeye anajua kabisa kwamba kwa nini nasema hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimboni kwangu tunachimba *gypsum*. Ni *ingredient* muhimu sana katika kutengeneza saruji. Wazo *Hill*, Kiwanda cha Mbeya na Tanga *Cement* na Viwanda nya Nje - Rwanda na Burundi, hata Uganda wamekuwa wakitegemea kwa sehemu kubwa malighafi hii kutoka Itigi. Sasa sijui kwa sababu Itigi ni sehemu isiyojulikana, ndogo, basi labda kwa sababu hiyo nadharauliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hoja, ni muda mrefu kampuni moja ambayo inachimba hapo na inawapa ajira sana vijana wetu pale, inaitwa *General Business and Equipment Supplies*, kampuni hii ilikuwa inasafirisha pia hii malighafi kwenda Rwanda na Burundi. Wakati huo ilikuwa inasafirisha kwenda kwenye kiwanda cha Serikali cha kutengeneza saruji kule Rwanda. Sasa yalipotokea machafuko, magari yao yakawa *impounded* na Wanajeshi lakini baada ya vita nya wenyewe kwa wenyewe kupita, nchi hii na nchi ya Burundi walisaini *protocol* ya kukubaliana kwamba mali zilizokuja upande

huu, kulikuwa kuna ndege, wale wenzetu walikuwa wanakimbia, walikuja na ndege zao wengine, wamekuja na...

MWENYERKITI: Mheshimiwa Lwanji, sogeza *mic* yako vizuri!

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa hiyo, wakasaini *protocol* mwaka 1995 kukubaliana kwamba mali za pande zote mbili kama iko huku basi irudi, zikiwepo na mali za watu binafsi na hii *protocol* ipo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa bahati mbaya sana, katika kudai *trucks* zao mbili pamoja na *trailer*, lakini hawakuwezwa kusikilizwa mpaka hawa watu ikabidi waende Mahakamani. Wakaenda Rwanda kule, Mahakama za Rwanda wakashinda, wakaja hapa Tanzania, wakashinda lakini mpaka leo hawa watu hawajapewa haki yao kwa kile kinachosingiziwa kwamba haya masuala ni ya kidiplomasia, lakini ukweli kwa muda wa miaka mitano (5) hawa wanadai haki na haki wamepewa na Mahakama zetu, lakini kwa bahati mbaya sana, hawa watu hawajaweza kupewa hii haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wanataja vipengele kadhaa, lakini mimi kwa mara ya mwisho wakati nimemwona Mheshimiwa Waziri mtoha hoja, alinipa matumaini kwamba hili suala lingewezekana kulimaliza kidiplomasia kati ya Balozi wa Rwanda pamoja na yeye mwenyewe. Kwa bahati mbaya sana, ni muda mrefu umepita toka mwaka jana, mwaka juzi hili suala linafuatiliwa. Mwaka juzi lilikwenda kwa Mheshimiwa Rose Migiro na akamkabidhi Mheshimiwa Chami, aliahidi kabisa kwamba hili suala angelimaliza lakini nasikitika sana kwamba suala hili mpaka leo lipo. Huyu mtu anadai pesa nyingi, ilikuwa 1.5 *million dollars*, sasa hivi imepanda, nafikiri zinaweza kufika hata dola milioni 10 kwa sababu ya kusubiri kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hili suala limenikera na mara ya mwisho hata Wizara ya Sheria ilikuwa imeiomba Wizara ya *Foreign Affairs* na huyo mlalamikaji au wenyewe hao wanaohusika kuititia Mwasheria wao walishauriwa kwamba wasubiri hili suala litatekelezwa na waliandikiwa barua kabisa ya mwaka 2007, inasema, “*The Protocol you have sided in enforcement to, we have also learnt that this matter is being handed by the Ministry of Foreign Affairs and International Corporation Legal Department. Since the said Ministry is the proper authority to deal with the matter, we argue you to contact the same for feedback*”. Hii barua ni ya *Attorney General* na ndivyo ilivyokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumekuwa tukifuatilia toka muda huo. Mimi mwenyewe nimeandika barua na nimekwenda mara kadhaa, huyu mhusika amekwenda mara kadhaa lakini ukiwaliza wanasema bwana, huyu mtu ni mgumu. Sasa mgumu vipi! Kwa sababu tunachotaka ni jibu, siyo kuzungushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi napenda leo hii nipate jibu, ni nini hasa? Wizara hii inashindwa nini? Balozi wa Kigali anafanya nini? Kama inashindikana, Waziri hana muda, basi wanafanya nini? Je, hawa Wanasheria wa hii Wizara wanafanya nini? Maana nimekwenda mara mbili pale wananiambia kwamba bwana huyu mtu ni

mgumu. Sasa mgumu kwa sababu hajasema labda pengine atatoa kiasi gani au ni nini? Maana kuna ka-element kakuonyesha kwamba labda kuna kitu anataka. Maana, unaposema mgumu au mgumu kwa sababu huyu mtu ni Mhaya, maana ni Mr. Kibila yupo hapa. Wahaya mimi nawafahamu ni watu *very enterprising* na wamekuja kwetu wanafanya kazi nzuri sana kuweza kutupatia ajira na ni watu wasomi. Sasa anaposema kwamba ni wagumu, nashindwa kuelewa ugumu huu uko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba sana suala hili lipatiwe ufumbuzi leo au labda kesho baada ya kupita hii bajeti, aondoke naye akampe, kweli nimezungushwa sana Wizara hiyo. Ukifika Wizara hiyo, unawenza ukafikiri kwamba mara nyingine ni watu ambao hawajali Watanzania wenzao. Ukiangalia sana ile Wizara utakuta kama inataka kufanana na *State Department*. Sasa, nadhani msitusahau wenzetu mnapovaa suti hizo, ninaomba mtukumbuke na mkumbuke tulikotoka. Unapokwenda pale, Mbunge ninawakilisha watu 150,000, nakwenda nazungushwa mimi, je, mtu wa kawaida atazungushwa kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili suala waliangalie. Sitaki kugombana na mtu, mimi sina ugomvi. Wajaribu kuondoa huo urasimu walionao pale ofisini, waweze kumjibu huyu mtu. Sheria zote zinam-favour huyu bwana. *Wana-site Geneva Convention* ooh sijui, *Geneva Convention* wala haihusiani na suala hili. Mimi *I'm a layman*, lakini watu tumeuliza, afadhali hata wange-site *Lome Convention* inayohusiana na masuala ya biashara maana alitibuliwa biashara yake. Naomba Wizara hii, inanikumbusha sana ninapoona picha za wale Mawaziri waliopita, *they were humble men*, walikuwa wanasaidia watu, basi wafanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ukienda katika hiyo Wizara unakuta *vision and mission*. Sasa unashindwa kuelewa hiyo Wizara ni ya nani maana *mission and vision* imewekwa pale na kwenye *reception* pale unakuta picha ya Waziri wala siyo ya Mheshimiwa Rais, wala siyo ya Mheshimiwa Baba wa Taifa. Zile picha za Mheshimiwa Rais na Baba wa Taifa zimekuwa *relegated* kwenye vyumba kule, lakini pale mbele unapofika kuna *mission and vision* na picha ya Waziri. Ndiyo maana tunasema kwamba labda inataka kufanana na *State Department* na magari yao meusi. Sasa, tunaomba tujue ni kwa nini, maana hali ndivyo inavyoashiria kwamba mmewasahau watu hawa. Mimi nadhani hii Wizara inajali zaidi mambo ya watu wa nje lakini watu wa ndani humu, sidhani kama inawashughulikia. Naomba sana turudi nyuma, tujue tulikotoka ni wapi. Hizi mbwembwe zinazoonekana hizi, nadhani si muda wake. Matatizo yako mengi, sasa hivi tulikuwa tunazungumza hapa *the Arab Spring* kule na wapi, ndiyo mambo madogomadogo yanaanza hivihivi, watu wanaeleza shida zao lakini hawasikilizwi. *Details* zote zipo na amepanga vizuri kabisa. Kama watamhitaji bwana Kibila wakamsikilize upya, walimalize hili tatizo, vinginevyo mimi sitaunga mkono hoja hii mpaka nitakapokuwa nimepata maelezo kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika, mimi ni kati ya ile *generation* ambayo tumeona *OAU*, tumesoma vizuri jinsi UN ilivyoanza lakini vyombo hivi sasa hivi ni kweli ni tofauti kabisa. Haiwezekani Libya leo inateswa bila sababu yoyote, sisi tumenyamaza! Inashangaza sana! *We are laymen*, lakini kuna utu. Juzi tumeona

tumedhurumiwa hapa zile hela za rada wanataka kupewa *NGOs* na mambo mengine, tulikuja hapa tukapiga kelele haraka sana lakini, masuala ya utu wa binadamu wenzetu wanavyoteseka kule Libya, sababu ni tatu, ni mafuta na ile ndege ya Lockerbie pamoja na ye ye ku-*advocate African Unity*. Wakubwa hawa hawapendi kuona kwamba tunaungana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni tatizo kubwa sana. Sidhani kama hizi nchi za Magharibi au nchi hizi kubwa zinapenda kuona Afrika inaungana. Juzi nilikuwa namwangalia Balozi wa Marekani, alikuwa anafurahi sana katika *ceremony* ile ya pale Juba – *South* Sudan, wanataka kuona *patches, patches, patches, patches* za nchi,, hawataki kuona kitu kinachoungana. Wizara hii ilikuwa inaweza ikazungumza na ikasikika. Hivi kweli Mwenyekiti, Gaddafi wanam-*ditch* hivihivi huyu mtu ambaye ametusaidia sana! Leo hapa Dodoma tunaona hata Msikihi Mkuu hapa ni wa Gaddafi, upo hapa! Mafuta ametusaidia mara ngapi? Sasa, nisiwe mwanadiplomasia kwenye masuala hayo, lakini kibinadamu, hivi kweli hiyo sijui wanasema nini, chombo kile cha Ulinzi na Usalama cha *African Unity* kinafanya kazi gani? Maana *one of the objectives* wanasema ni kulinda mipaka na usalama wa nchi husika mionganoni mwa wanachama. Hivi kweli wanashindwa kupata ka-*contingent* kila nchi ika-*contribute* Askari wakaenda kumsaidia huyu bwana? Hivi tukifanya hivyo sasa ndiyo hawa wakubwa wata-*declare* vita kwa Afrika nzima? *I don't think so!* *NATO* ndiyo itaanza kuja kupiga mabomu Dar es Salaam, wapiwapi kama wanavyofanya? *It is not true at all.* Ile ni Serikali halali. Mimi naona hatutendi haki kwa suala hili, *since* tumekwishakuwa wakala tu, *African Union* imekuwa wakala tu wa UN, hatuna meno hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashukuru kwa kunipa nafasi, niliona *ni-raise concern* yangu hiyo. Huyu bwana atambuliwe kwamba, yanayotokea Misri si lazima yawe yanayotokea Libya, yaliyotokea Tunisia si lazima yatokee Syria lakini *of all the places*, Libya *a member of the African Unity* na huyu bwana ame-*champion* sana tuungane, lakini *we have betrayed him*. Nataka kuuliza swali moja, *suppose* anashinda hii vita, tutapeleka wapi nyuso zetu sisi? Anaweza kushinda! Wamejaribu *relentlessly* mpaka leo wameshindwa, sasa wanatafuta roho yake tu. Hawakunituma watu wa Manyoni kuzungumza haya, lakini mimi nalizungumza *on humanitarian ground*. Mimi natetea kama ninavyotetea bwana Kibila au hiyo kampuni inayodhulumiwa, ndivyo ninavyotetea, yanaweza kutukuta hapa, *why are we silent?* Ukiuliza, wanasema *African Unity, it is not true!* Kuna mambo mengine inabidi tuonyeshe ukweli, uhalsia wetu kwamba tunasimama wapi lakini hata kuonyesha uhalsia tunasimama wapi tumeshindwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ya kwangu ni hayo, lakini lile la kwanza, siungi hoja mkono mpaka nitakapopata maelezo. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba niwashukuru watoto wangu wapenzi, Hellena Nyerere, Julia Nyerere na Julius Nyerere, kwa ushirikiano wao

mkubwa walionipa hatimaye wakaniruhusu kuja kugombea Ubunge. Vilevile, nitakuwa mtovu wa fadhila endapo nitamsahau Mume wangu mpenzi, baba yao Madaraka Nyerere, kwa ushirikiano wake mkubwa na uvumilivu wake mkubwa aliouonyesha kwangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mama Mkwe wangu mpendwa, Mama Maria Nyerere kwa msaada wake mkubwa wa hali na mali alionipa wakati wa kampeni. Siwezi kumsahau baba yangu mpendwa bwana Msobi Mageni kwa msaada wake wa fedha, wa hali na mali alionipatia wakati nagombea kuingia Bungeni. Naomba niwashukuru ndugu zangu wote kwa msaada wao mkubwa walionipatia, hatimaye nikaweza kuingia hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuwasahau viongozi wa CHADEMA, Mheshimiwa Freeman Mbewe, Mheshimiwa Dkt. Slaa, nawashukuru sana kwa kuniamini na kudhani kwamba nitakuwa mwakilishi mzuri hatimaye wakasaidia kuhakikisha kwamba naingia Bungeni. Vilevile siwezi kuwasahau wanachama wote wa CHADEMA, wanachama wote wa BAVICHA, wanachama wote wa BAWACHA na wapenzi wote wa CHADEMA, Nawashukuru sana kwa msaada wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa naenda kuzungumzia mambo ya *Dual Citizenship*, naomba kwanza nimshukuru, pamoja na kwamba si kawaida yetu watu wa Upinzani kumshukuru Kiongozi wa Serikali, lakini leo, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa imani yake kwangu, akanituma kwenda kuwakilisha kwenye Mkutano wa *Diaspora* huko Arusha. Namshukuru sana kwa imani yake kwangu. Vilevile naomba kumshukuru Mheshimiwa Spika wa Bunge, Mheshimiwa Mama Anne Makinda kwa kutoa ridhaa hiyo, hatimaye nikaenda kuwakilisha Wabunge kuzungumzia masuala nyeti ya *Diaspora* hasa suala la Uraia wa Nchi Mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kwenye mada moja kwa moja. Suala la *Diaspora* si suala la mchezo, si suala la mzaha. Kuna Watanzania wameondoka nchini wakaenda kuishi nchi za nje, haimanishi kwamba wanaichukia Tanzania, wameenda kule kama *economic refugees* (wakimbizi wa kiuchumi). (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapoenda nchi ya ng'ambo ni lazima utaishi kama wananchi wengine wanavyoishi, utafanya kazi, utasoma na ikibidi utazaa. Kuna watoto waliozaliwa nje ya nchi hii, wamezaliwa na Watanzania, lakini cha kusikitisha Watanzania wanapokuja Tanzania na watoto wao wanalazimika kuwalipia Visa. Naomba Serikali sasa tuanje kujiuliza, hivi hii ni haki? Hivi tunawatendea haki watoto wetu ambao pia ni raia, wewe ukizaliwa na Mtanzania *definately* wewe ni Mtanzania, sasa tunawabagua watoto wa Watanzania, hii ni haki? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sioni tatizo la mivutano kuhusu suala la *Dual Citizenship*, kuna watu wanavutana kwa sababu zao wanazozijua wenywewe. Kuna watu wanavutana kuhusu swalii la uraia wa nchi mbili, wengine wanahofia kunyang'anywa nafasi zao za kisiasa na kuna wengine wanahofia hao watu watakuja kuchukua nafasi zao

za kazi. Sasa ultaka wachukue nafasi ya nani, hawa ni Watanzania, kama wewe hutaki wachukue nafasi yako ya kazi, *you have to be competent*, uingie kwenye ushindani ili uhakikishe hawachukui nafasi yako ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati sasa umefika nchi yetu tuwe *realistic*, tuache mambo ya kuvutavuta vitu ambavyo vinaeleweka. *It is a matter of common sense*, mtoto amezaliwa na mzazi Mtanzania, wakati mwininge wazazi wake wote wawili ni Watanzania unamnyima uraia, unasema hawezi kuwa raia kwa sababu amezaliwa Marekani na akapata uraia wa Marekani, unafikiri anayepoteza ni nani? Hivi kuna mtu ambaye ana uraia wa Marekani atakuja ku-*give up* uraia wake wa Marekani kwa ajili ya kupata uraia wa Tanzania? Naomba tuwe *realistic*. Suala la *dual citizenship* linatunufaisha sisi wenyewe, hawa watu walioko nje ya nchi, waliopo kwenye *Diaspora*, watakapokuja Tanzania sisi ndiyo tutanufaika, watatuletea ujuzi na uzoefu wao wa kazi walioupara kule na tutanufaika. Tunapowaleta nchini hawa Watanzania amba wana mapenzi makubwa kabisa na nchi yao, wanakuja kuwekeza, kwa hiyo tutakuwa tunakuza uchumi wetu. Mimi nashangaa ni kitu gani kinawafanya mcheleweshe suala hili Mheshimiwa Membe! Sielewi, kwa sababu katika hali ya kawaida *you don't lose anything*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwape mfano wa Mtanzania mmoja ambaye aliulizwa na Mwenyezi Mungu, chagua kitu kimoja nikupatie lakini kitu hicho nikikupatia jirani yako atapata mara mbili. Mtanzania akaanza kujiburuzaburuza kwa sababu anahofia akisema anataka ghorofa, jirani yake atapata mawili, tuache tabia ya ubinafsi. Suala la *Dual Citizenship* linatunufaisha wenyewe na matokeo yake sisi ndiyo tuna *lose*. Unaona shida gani ukimpa yule na wewe ukufaika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia kuna mambo mengine yanajitokeza kwenye hili suala ambayo ni ya kisiasa, naomba kutoa ushauri. Endapo tutaamua watoto wetu amba wazazi wao ni Watanzania, warudi Tanzania, tuwape uraia kwa masharti, tuwaambie msigombee Urais, msigombee Uwaziri Mkuu, Msigombee Umakamu wa Rais maana hivyo ndivyo vinatutoa roho. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Serikali yetu itoe maamuzi haraka ili watoto wetu na Watanzania wote amba wapo nje na wangependa kuja kuwekeza ndani ya nchi yao warudi nyumbani na kwa kufanya hivyo uchumi wetu utakua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashangaa sana, mimi ni Mtanzania lakini nikiangalia nashangaa mambo yanayoendelea katika nchi yetu. Unashindwa kumrudisha Mtanzania mwenzio kwa kuhofia kwamba atakupokonya cheo, unashindwa kumrudisha Mtanzania asaidie na kuchangia kwenye maendeleo ya kiuchumi kwa kuogopa kwamba anaweza akaja akagombea Ubunge? Ninamtaja tena Mheshimiwa Membe, naomba ukaze buti, hatukubali nchi yetu iwe ni ya kubagua Watanzania amba wana haki ya kupata uraia wa nchi hii kwa wazazi wao pia ni raia wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia suala ambalo linatudhalilisha Watanzania, suala la kuwa na sheria ambazo zinatudhalilisha. Nchi yetu bado inapiga

watoto mashuleni kama adhabu, hivi tupo dunia ya ngapi? Hivi mnajisikiaje Waziri akienda kwenye Mikutano ya Kimataifa anaulizwa kwa nini ninyi mnapiga watoto mashuleni anasema tuna Sheria inayoturuhusu kuwapiga watoto, *that is child abuse*, tuachane na tabia inayopigwa vita dunia nzima. Hamjui tunaweza kuwa *sanctioned* kwa sababu ya kuwa *abusive* kwa watoto? Kwa nini tunaendeleza sheria zilizopitwa na wakati? Kwa nini tunaishi katika *old stone age*?

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. YUSSUPH A. NASSIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo!

MWENYEKITI: Anayeomba Mwongozo asubiri kwanza Mbunge amalize ndipo utaomba Mwongozo. Mheshimiwa endelea!

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante, maana Mbunge angenifanya nipoteze *point*, nakushukuru.

Mhehsimiwa Mwenyekiti, kuna suala la wanawake wanakwenda nje ya nchi, kama nilivyowaambia sababu ni za kiuchumi, watu wanaipenda nchi yao, lakini kwa sababu uchumi wetu unalegalega na ninyi ni mashahidi wanaamua kwenda kutafuta maisha nje ya nchi. Ukiwa kule utafanya kila kitu kama nilivyowaambia pamoja na kuzaa. Sasa mtoto anazaliwa anakuwa *victim*, mama anaamua kupata mwenzi wake, anaamua kumleta Tanzania anabaguliwa, hapati uraia, hapati kazi, huyu mama angekuwa mwanaume akaleta mwanamke ndiyo ingekuwa kinyume chake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kukuambia kwamba wakati sasa umefika tuachane na zama za *Old Stone Age*, wakati sasa umefika tuanze kwenda na wenzetu sambamba, hamuoni aibu mnapoenda kwenye Mikutano ya Kimataifa, hamuwadhalilishi Mawaziri wanapoulizwa *why are you still abusive to the children*, mnataka watoe majibu gani? Watasema tuna Sheria inayoturuhusu *ku-abuse* watoto. Hivi ukimwambia mtu hivyo atakuelewaje? Atakudharau na hata ukienda pale unatembeza bakuli unaomba msaada atakudharau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani haya yote yanatosha, naomba Serikali yetu iweke mkazo zaidi katika jambo hili, ahsante, naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. YUSSUPH A. NASSIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 144(2), inasema kwa kadri itakavyowezekana Mbunge ajitahidi kutokuchanganya lugha zote mbili wakati anasema Bungeni isipokuwa tu pale anaponukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikikerwa sana na tabia hii, baadhi ya Wabunge wamekuwa wakichanganya lugha na kutupunguzia ile hamu ya kusikiliza na hata kuchanganya lugha za jamii zetu kule tunapotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ni kweli Wabunge wengi tunalo tazito hilo, siyo tu msemaji huyo aliyemaliza, pengine huyu mimi leo naweza nikasema tumsamehe kwa sababu anazungumzia mambo ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na huko ndiko wanazungumza kimombo na lugha yetu bado haijapata nafasi kubwa sana.

Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo wangu ni kwamba tujitahidi sana wakati mwininge tusichanganye lugha mbili, ama uzungumze Kiingereza tupu, sasa sijui kama wapigakura wako watakuelewa, kama utaona hiyo inafaa unaweza kufanya hivyo au Kiswahili kitupu, kuchanganya vyote viwili ndiyo Kanuni inakataza, kwa hiyo, tujitahidi.

Mchangiaji wetu anayefuatia sasa ni Mheshimiwa Moses Machali atafuatiwa na Mheshimiwa Yahya Kassim Issa.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki taarifa yake.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge wala hajakupa taarifa, ye ye aliomba Mwongozo. Mheshimiwa Machali endelea!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa nami niweze...

MWENYEKITI: Samahani Mheshimiwa Machali, naomba ukae. Waheshimiwa Wabunge, kumekuwa na utaratibu wa mtu kukataa tu, ndiyo maana sasa hata hajatolewa taarifa mtu anakataa tu. Kwa mujibu wa Kanuni hapa huwezi ukakataa kitu ambacho ni cha ukweli na cha uwazi. Kama mtu amekutolea taarifa ni lazima uikubali hata kama imesemwa kinyume na matakwa yako, kama ni cha ukweli ni lazima uikubali useme nimepokea taarifa wala haiharibu chochote na wala haikuharibii hotuba yako. Kwa hiyo, naomba sana, kama mtu atapewa taarifa ya ukweli halafu akaikataa ni kosa na Kiti kinawenza kikachukua hatua yoyote ile. Tuendelee na Mheshimiwa Machali.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ili nami niweze kuchangia Wizara hii ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanafalsafa mmoja nitaomba nimnukuu tena kwa lugha yake aliwahi kusema kwamba:-

“You are not supposed to be so blind with patriotism that you can’t face reality, wrong is wrong no matter who does or said it”.

Samahani kwa yule ambaye anasema kwamba tunachanganya lugha lakini tukirejea kwenye Sera ya Taifa ya Luga, nafikiri lugha zote hizi mbili ni *appropriate*

kabisa. Lugha ya Kiingereza na lugha ya Kiswahili ni sahihi kuzitumia kwa sababu tunategemea kuweza ku-*compete* kwenye *standards* za Kimataifa. Kwa hiyo, niombe tu kwamba tu-*officiate* na tuendelee kutumia lugha hizi mbili vizuri ili kusudi tuweze kuzungumza vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijielekeza moja kwa moja kwenye hotuba iliyotolewa hapa na Waziri wa Mambo ya Nje, Mheshimiwa Bernard Membe kwa niaba ya Serikali. Leo naomba nianze kuzungumzia kidogo juu ya suala la Mabalozi wetu ambao wanaiwakilisha nchi yetu katika nchi mbalimbali hapa Duniani. Naungana na Mbunge rafiki yangu Mheshimiwa Sanya aliyeleza kilio na matatizo ambayo yanawakabili Mabalozi wetu juu ya ukata wa fedha na hatimaye wanaishi kama vile ni watu ambao siyo muhimu katika Balozi zetu ambazo ziko nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Sanya anazungumzia kuhusiana na Ubalozi wa Malyasia kwa sababu ndiyo inaonekana ndiyo *case study* na hotuba ya Kambi ya Upinzani kupitia kwa Waziri Kivuli wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa imeweza kueleza suala hilo, nitoe tu ushauri kwa Waziri wa Mambo ya Nje, uangalie ni namna gani ambavyo unaweza ukawasaidia Mabalozi wetu ili kuhakikisha hawafanyi kazi katika mazingira walijonayo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendelea kuwaacha Mabalozi wetu kufanya kazi bila ya kuwa na uhakika wa fedha, hakika ni kuwaonea, hata umakini wao hauwezi ukaonekana. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba kuanzia mwaka huu baada ya Bunge hili katika mwaka wa fedha ambao umeanza kuanzia tarehe Mosi Julai, ni imani yangu kwamba Mabalozi matatizo yao yatapungua. Niombe Ubalozi hasa wa Malaysia muwasaidie. Kweli ni aibu wanakaguliwa na mwenye nyumba kama vile ananadi nyumba yake, anamwingiza mteja mwingine, nyumba hii hapa napangisha, nyumba ya Balozi, ni fedheha kwa Serikali ya Tanzania. Chondechonde, fumba macho Balozi zingine, naomba uanze na Ubalozi wa Malaysia kwa sababu kwa kweli inatia aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni umri wa Mabalozi wetu ambao wanafanyakazi kama Mabalozi katika nchi mbalimbali. Tunajua kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, umri wa kustaafu ni miaka sitini, lakini inazidi ku-*develop culture* mtu amestaafu mahali fulani labda alikuwa ni Katibu Mkuu au alikuwa ni kiongozi wa masuala ya kisiasa au ni Afisa mahali fulani amestaafu miaka sitini imetimia, kesho unasikia ameteuliwa kwenda kuwa Balozi Japan, kesho kutwa unasikia mwingine ameteuliwa kwenda kuwa Balozi nchini China, umri wa miaka sitini ulishatimia. Naomba Waziri wakati unafanya majumuisho yake, kwa niaba ya Serikali atusaidie kutueleza ni kigezo gani kinachotumika kuwateua Mabalozi ambao walishatimiza umri wa kustaafu kama Watumishi wa Umma, ni imani yangu kwamba Mabalozi nao pia ni sehemu ya Watumishi wa Umma, sasa sijui mnatumia vigezo gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili lipo pia hata kwa uteuzi wa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, wamestaafu katika Majeshi, kesho unasikia wanateuliwa kuwa ni Wakuu wa Mikoa, ni Wakuu wa Wilaya, hizi ajira ambazo tumekuwa tunapiga kelele kwamba vijana hawana ajira, vijana wamesoma, wameelimika wanawenza

wakafanya kazi, tunaacha kuwaajiri kwa kigezo gani tunaenda kuwaajiri watu ambao walilitumikia Taifa na wametimiza umri wao wa kustaafu, unamteua tena kwenda kuwa Balozi, hii ni kuwaonea Watanzania wengine ambao hawajaajiriwa na kuweza kukamata nafasi nzuri, hususani vijana ambao wanahitimu katika taasisi mbalimbali za elimu hapa nchini na nje ya nchi. Nitaomba Waziri atoe ufanuzi kwamba mnatumia Sheria gani kwa sababu naona kama mnakiuka Sheria ya Utumishi wa Umma ambayo inataka umri wa miaka sitini watu waweze kustaafu au pengine nao ni wanasiasa sijui, Waziri utatuambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze kwenye *issue* ya *Rada*, mimi binafsi na nina imani na Watanzania wengine, wanamheshimu sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Bernard Membe. Kwanza, imani yangu niliyonayo kwa Mheshimiwa Membe, najua ni mmoja wa watu waliopita Seminari, Waseminari siku zote huwa ni wa kweli na huwa ni wacha Mungu. Watanzania wengine huwa wanaamini kabisa watu wa namna hiyo huwa hawawezi wakalidanganya Taifa. Kwa hiyo, Waziri Membe kwanza naomba ku-*declare interest* kwamba binafsi mimi ninakuamini na ninakuaheshimu sana, naomba utusaidie jambo moja kwa niaba ya Watanzania ambao tunaipenda nchi yetu, leo wakati unafanya majumuisho yako ututajie majina ya watu waliosababisha ile *rada* ikanunuliwa na hatimaye kulisababishia Taifa hasara ya mabilioni ya shilingi. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo Watanzania ambao wanaimani kwamba unaweza ukawa hata Rais wa Nchi hii, wapo Watanzania tumepata kusikia wakizungumza hayo, sasa kama Waziri Membe leo huwezi ukatuambia, imani yangu hata mimi kwa kweli itatoweke. Watanzania wanakuaheshimu na wanakutegemea sana wewe na ndiyo maana leo ni Waziri, sasa kama huwezi ukalithibitishia Taifa kwamba ni watu gani ambao waliosababisha hasara ya mabilioni ya shilingi katika ununuzi wa rada, samahani ninakuaheshimu sana lakini naomba niseme katika hilo kwa kiasi fulani naomba niseme utakuwa umesababisha imani yangu niliyonayo kwako ipungue, itashuka! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ule mchakato wa ununuzi wa rada haukuibuka tu wenye kama wenye *just from no where*, ni kwamba kuna watu ambao waliweza kuratibu hiyo *process* mpaka leo Serikali ya Uingereza ina-*realize* kwamba Tanzania tulichezewa mchezo wa kuigiza, mchezo mchafu katika ununuzi wa rada. Sasa tunakuwa tunapigana chenga na danadana tunajadili jambo moja kwa muda mrefu bila kuweza kupa majibu, tatizo ni nini? Naomba leo kitendawili hicho ambacho hakijaweza kupata jibu lake, utueleze hapo na Watanzania watakuaheshimu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli kama ndugu yangu na kiongozi wangu ambaye ni Waziri wa Mambo ya Nje, kama hataweza kutuambia, kwa hili naomba niahidi kwamba nitatoa shilingi katika Wizara hii, naomba leo utusaidie katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nijielekeze kwenye suala zima la uraia wa nchi mbili, Serikali yetu imekuwa inasita sana katika suala zima la kuruhusu wananchi wetu kuweza kuwa na uraia wa nchi mbili. Mimi binafsi ukija kuniuliza sioni tatizo la wananchi kuweza kuwa na uraia wa nchi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge waliotangulia wamejaribu kuchangia hapa suala la *Diaspora* ina faida gani, siwezi nikaendelea kurudia, naomba Waziri wa Mambo ya Nje pia atusaidie wakati anakuja kuhitimisha hoja yake atueleze kigugumizi kinatoka wapi kwa Serikali yetu kutokuruhusu uraia wa nchi mbili. Hii kuendelea kusema kwamba mtu kama pengine atapata uraia wa nchi nyingine basi moja kwa moja asitambuliwe kama raia wa Tanzania ni uonevu. Nafikiri tungeweza kuenzi Lengo la Nane la Millennia kama sijasahau ambalo ni suala la *global partnership*. Hatuwezi kusema kwamba sisi tunashirikiana na mataifa mengine na kama sehemu ya kuweza kuenzi *Millennium Development Goals* wakati tunaweka *restrictions* kwa watu wetu kutoweza kuwa na uraia wa nchi mbili. Mimi nafikiri tutoe uhuru kwa wananchi wetu, kila raia aamue ambaye anapenda kuwa na uraia wa nchi mbili, hii itaweza kutusaidia hata katika masuala ya kiuchumi kutoka hapa nchini na kwenda katika Mataifa ya wenzenetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuendelea kuwa na mtazamo wa kusema kwamba hili suala lina matatizo, tuombe tuainishe matatizo hayo. Kama basi kuna matatizo ambayo labda pengine Serikali inayaona ndio maana inakuwa na kigugumizi basi ipo haja ya kuweza kuwa na *forum* ya kujadili suala hili kwa kina na pengine *t-change* utaratibu isijekuwa kwamba siku moja moja tunamuona Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa yupo kwenye *television* anajaribu yeye kuweza kufanya *sensitization* kadri ya mtazamo wake. Hebu tupite katika maeneo mbalimbali kwenye Taasisi za wasomi kwenye Vyuo Vikuu tujadili hili suala kwa kina, tuangalie kiuchumi lina faida gani na hasara zake ni zipi. Kama itathibitika kweli kwamba hasara ni nyingi, tukubaliane na mtazamo ambao pengine Serikali imekuwa inaona kwamba suala hilo liwe hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho, kuna tatizo katika Wilaya ya Ngara, inasemekana ardhi ya Tanzania imemegwa katika Wilaya ya Ngara na zaidi ya kaya 36 zimeweza kuondolewa katika eneo lile na matokeo yake ni nini wale watu wameweza kupokonywa na ardhi yao na eneo lile limeweza kuchukuliwa na raia wa Burundi kwa mujibu wa taarifa tulizo nazo na mgogoro huu umeanza mwaka 2007. Mkuu wa Mkoa wa Kagera aliwahi kushirikiana wakati fulani na pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Burundi, iliamuliwa ardhi ile isitumike mpaka suluhisho litakapokuwa limepatikana lakini dakika hii tunapozungumza wananchi wa Ngara hawa ambao waliweza kuondolewa katika ardhi ile ambayo walikuwa wanaitumia katika shughuli mbalimbali ikiwemo kilimo kama uti wa mgongo wa uchumi wao hawajui hatima ya eneo lile ambalo walikuwa wanakalia kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba Mheshimiwa Waziri kwa maslahi ya Watanzania wanaoishi Ngara na kwa maslahi ya Tanzania, suala hilo liweze kupatiwa ufumbuzi. Kama haliwezi kupatiwa ufumbuzi basi Ramani ya Tanzania ibadilishwe moja kwa moja kama wamekubali Burundi waweze kuchukua ardhi ile. Sioni sababu ya Tanzania kuendelea kuiogopa Serikali ya Burundi kwa sababu naona kama vile kuna uwoga katika suala hili. Kama kweli taarifa hizi na kwa mujibu wa nyaraka nilizonazo limefanyika, naomba Serikali leo itoe tamko juu ya kauli hiyo kwa sababu waliohusika

katika kugawa ile ardhi ni viongozi wa Tanzania, ni watu ambao wameajiriwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao wamesababisha tatizo hilo. Ikiwezekana hatua za kinidhamu ziweze kuchukuliwa dhidi ya watumishi hao kwa sababu wameridhia na Bendera ya Burundi inapeperushwa katika maeneo yale, nini hatima yake? Niombe kama tumeridhia Ramani ya Tanzania basi ibadilishwe na tujue kwamba lile eneo tumeamua kuwaachia Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani wananchi wa Ngara, wa Kata ya Kirusha wakaendelea kutaabika toka miaka ya 2007 ilihali kuna watu wachache ambao tena wanajulikana wameweza kuuza ardhi hiyo wao bado wanaendelea *ku-survive* halafu wananchi wanataabika. Hali hii ikiendelea ndio matokeo yake sasa watu wengine huwa wanaandamana na wakiandamana inaonekana kwamba ni wahuni, maandamano ni sumu, maandamano siyo sumu, kwa nini watu wasiandamane kama wanapokonywa rasilimali zao za ardhi na wakati Serikali ambayo inasema kwamba iko makini, umakini wa Serikali utaweza kuonekana tu pale ambapo itakuwa haraka katika kutatua kero za wananchi la sivyo tutazidi kuwapinga na kuwaambia kwamba Serikali hii sio makini. Kwa hiyo, niombe kwa sababu suala hili pengine hata Wizara yako inahusika ukishirikiana na Waziri wa Ardhi, mtusaidie tujue na nitaomba kauli ya Serikali katika hili, vinginevyo pia katika suala hili nakusudia kutoa shilingi, nitakamata mshahara wako Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nikushukuru na niwaacie wachangiaji wengine waweze kuendelea, ahsante. (*Makofit*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Machali ingawa umesema Mheshimiwa Memba anastahili, kwa hiyo, ninyi CHADEMA hamuweki mgombea, tuendelee. (*Kicheko*)

MHE. MOSES J. MACHALI: Mimi siyo CHADEMA, mimi ni *NCCR Mageuzi*.

T A A R I F A

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama kwa kifungu hicho na kusema Taarifa. Wakati Mheshimiwa Machali anachangia alionekana kama anamfanyia kampeni Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, Mheshimiwa Bernard Membe, inaweza ikawa sawa kwamba Mheshimiwa Membe anaweza akawa Rais kwa kupitia kura yake lakini siyo kwa wananchi wa Tanzania. Nilikuwa naomba kumpa hiyo taarifa. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Wala hamna taarifa hapo, hapo na wewe umeingiza tu mambo yako, tuendelee. (*Kicheko*)

MHE. REGIA E. MTEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi. Kwanza kabisa, napenda kutoa pongezi kwa Wizara hii kwa kuwa kwenye hotuba yao wametuletea na orodha ya waliowahi kuwa Mawaziri wa Mambo ya Nje kuanzia

Uhuru mpaka sasa. Wale ambao tulikuwa hatujui historia vizuri leo tumeifahamu, nawapongeza kwa hilo na naomba Wizara zingine ziige mtindo huu, wameweka Mawaziri wote wa Mambo ya Nje kuanzia uhuru mpaka sasa kitu ambacho ni kizuri kwa mustakabali wa Taifa letu la Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mimi nitachangia mambo machache, la kwanza ni suala zima la upatikanaji wa *visa* hasa nchi za USA pamoja na Uingereza. Kwa kweli masharti ambayo nchi hizi zimeweka yamekuwa ni kero kwa Watanzania ambao wana kipato cha kati. Mtu ukitaka kusafiri kwenda kwenye nchi hizi, unaanza kuulizwa una kipato kiasi gani kwa mwezi, unatakiwa ujaze fomu hasa zile za *online* mwananchi wa kawaida ambaye anatoka kijijini au anaishi mjini lakini yupo kwenye kipato cha kati, hana *access* vizuri, hafahamu masuala ya mitandao imekuwa ni tabu kwao matokeo yake wameibuka watu ambao wanafanya biashara kuwajazia watu hawa. Bado kwenye *interview* kuna kero kubwa, maswali ni mengi na wengi Watanzania wa kipato cha kati ambao wamekuwa wakiomba na wale wa chini wamekuwa hawapati *visa* kwenda kwenye nchi hizi. Huu ni ubaguzi kwa kuwa wao wanakuja bila masharti mazito na wanaingia wakati wowote wakijisikia. Kwa hiyo, naishauri Wizara ya Mambo ya Nje ikaongee na Balozi hizi kwamba tunapozungumzia *free movement of people* iwe ni *free* kweli siyo kwa kiwango hiki. Tunataka Mtanzania yejote ambaye ame-*apply* kwenda Uingereza, ame-*apply* kwenda USA, basi aende bila masharti mazito. Hilo ni la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ambalo napenda kuzungumzia siku ya leo pamoja na kwamba wachangiaji wengi wametetea Balozi zetu lakini nitakwenda kinyume na wengi walivoyzungumza. Nilikuwa napitia Ripoti ya *CAG* ya mwaka 2010, nimepitia Balozi 21, Balozi za New Dell, Harare, Lusaka, Abu Dhabi, Washington, Addis Ababa, Saudi Arabia, Muscat, Lilongwe, Abuja, Kinshasa, London, Moscow, Stockholm, Kigali, Nairobi, Paris, Roma, Beijing pamoja na Tokyo. *CAG* amegundua mambo ya msingi ambayo tungependa kupata ufanuzi kutoka kwa Waziri husika. Kuna baadhi ya Balozi kwa mfano Balozi za Harare na Lusaka zenyewe zimeonekana zimepewa fedha kinyume na bajeti walizoomba kutokana na gharama za kibenki. Ameeleza kabisa kwamba kutokana na hali hii kwamba Balozi hizi zitafanya kazi vibaya kwa sababu fedha hazitoshi. Kwa hiyo, naomba Wizara husika itupe maelezo ya kina kwa sababu wao wanajua masuala ya gharama za kibenki wanapofanya *transaction* inakuwaje wanawapelekea fedha pungufu tofauti na walivyoomba? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninazopenda kuzungumza ni hizi 12 kati ya hizi 21, zimeonekana kwamba zime-*overspend* tofauti na bajeti zilizopitishwa na Bunge bila kibali cha Katibu Mkuu wa Wizara husika. Balozi hizo zimeonekana zimetumia zaidi ya shilingi milioni 200 kinyume na taratibu, bila kibali cha Katibu Mkuu. Inawezekana kuna mambo matatu yamesababisha wao wafanye hivyo. Kwanza kabisa, yawezekana ni kweli kwamba labda wamepelekewa fedha kidogo kwa hiyo ikabidi wa-*overspend* kinyume na bajeti iliyopitishwa na Bunge au yawezekana Balozi hizi hazina watalaam wa masuala ya fedha ndio maana wanakwenda kinyume na Kanuni za Fedha na au yawezekana kuna harufu ya ufisadi kwenye balozi zetu *that is why* wamekwenda kinyume na Kanuni za Fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha atupe ufanuzi kwa nini Balozi hizi 12 kati ya 21 zime-*overspend* au zimetumia fedha za maduhuli bila kibali husika. Balozi zingine zimenunua vitu bila idhini ya Kamati ya Manunuzi, naomba maelezo ya kutosha ili tuweze kwenda sambamba, tuondokane na hisia ambazo wengine tumeanza kuwa nazo vichwani mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo napenda kuzungumza siku ya leo, Ripoti hii ya *CAG* ya mwaka jana ambako alipita kukagua Wizara ya Mambo ya Nje, *CAG* anasema kwamba Wizara iliingia mkataba na Kampuni ya *Fuja Engineering Group* ili kujenga Julius *Nyerere Convention Centre* ambako ilitumia jumla ya fedha za Kichina milioni 183,500,000 lakini anatuambia mkataba huu ulikwenda kinyume kwa kuwa Mwanasheria Mkuu alikuwa hana habari wala hakupitia. Kwa hiyo, umekiuka Kanuni ya Kifungu cha 55 cha Sheria ya *PPA*. Vilevile *CAG* ameelleza wazi kwamba hata Katibu Mkuu wa Wizara hakusaini mkataba huu. Maana yake mkataba huu ulifanyika kwa siri, kuna harufu ya ufisadi hapo. Nitamwomba wakati wa majumuisho Waziri husika atupe maelezo kutokana na mkataba huu, vinginevyo nitaondoa shilingi. Atuambie mkataba huu ulingiwa na nani, ni shilingi ngapi zilitumika na kwa nini Mwanasheria Mkuu ambaye amewekwa kwa ajili ya kazi hiyo, ambaye analipwa na kodi za Watanzania hakupewa kuupitia mkataba huu? Pia kwa nini ambaye anahuksika na mikataba yote ya Wizara, Katibu Mkuu, hajasaini ambapo ni kinyume na kanuni ambazo tumejiwekea? Asiponipa majibu ya kutosha leo ninaondoa shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo wenzangu wamezungumza, ningependa kuzungumzia Chuo cha Diplomasia. Chuo hiki ni kizuri, kinaandaa Watanzania katika kuja mambo ya Kimataifa lakini kiukweli Chuo hiki hakijulikani vyta kutosha na hasa wananchi wa Vijijini wanajua watu wa Mijini, wa Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma na kadhalika. Kwa hiyo, naiomba Wizara hii iandae mpango mahsus wa kuhakikisha Chuo hiki kinafahamika hasa kwa wanafunzi wanaomaliza Kidato cha Sita ili anapomaliza awe anajua kuna Chuo cha Diplomasia, kipo sehemu fulani kinatoa kozi hizi na hizi mtu anayetaka kusoma akasome. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. (*Makofî*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. DKT. LUCY S. NKYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na Watendaji wao wote kwa hotuba nzuri. Aidha, nawapongeza sana Mabalozi wetu wote walio katika Balozi zetu za nje. Hawa wanafanya kazi nzuri na kwa uzalendo wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia yafuatayo kwa nia njema sana. Kwanza, napenda kutoa rai ya uwakilishi wenye uwiano wa kijinsia. Naomba uteuzi wa Mabalozi uzingatia uwiano wa kijinsia kwani wanawake wanaweza na mifano hai ipo kwa kuona jinsi Mabalozi wanawake hata kama wanakaimu wanavyojituma kwa uzalendo mkubwa. Wanawake wanaweza, wapewe nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Balozi zetu ofisi zao nyingi zipo kwenye hali mbaya sana. Ikiwezekana, uwepo mpango (*road map*) ya kuziboresha aidha kwa ukarabati au kujenga upya. Mfano wa Balozi zilizo hoi ni *DRC*, Moscow pamoja na mwonekano wa ofisi yetu ya Umoja wa Mataifa. Ofisi hii ni kioo cha nchi yetu, tukijipanga, tunaweza ili mradi nia ya dhati iwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, naomba Wizara hii ishauri Balozi zetu ili pamoja na majukumu yao wawashauri Watanzania wanaosoma nje wajenge utamaduni wa kusoma kwa bidii ili wamalize masomo yao kwa mafanikio na hatimaye warudi nchini kwani tunawahitaji katika kuchangia uchumi wa nchi yetu. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa juhudzi zake za kuwashirikisha Watanzania waliopo ughaibuni kuchangia maendeleo ya nchi yetu, naomba kama inawezekana tujue ni nani anaratibu zoezi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nawatakia mafanikio ya utekelezaji mwema wa majukumu na malengo kama ilivyoainishwa katika hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ina umuhimu wa pekee sana wakati huu dunia iko kwenye mwelekeo wa ubeberu na ubepari, hivyo iongezwe fedha kwenye bajeti yake kwa ajili ya kulinda maslahi ya Taifa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza kazi yake, inahitajika kufanyike mabadiliko ya kisheria na kitaasisi ili kuweka mkazo katika diplomasia ya uchumi na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kitabu cha bajeti, *Volume II*, Fungu 34; Wizara ieleze sababu za kupanda kwa Kasma 220800 Kifungu 1002, hizi zimepanda kwa kiwango kikubwa ukilinganisha na mwaka 2010/2011 na 2011/2012. Kifungu 2006 ielezwe hatua zilizochukuliwa kurekebisha ongezeko la matumizi ya zaidi ya 832 milioni nje ya bajeti iliyopitishwa na Bunge (Ubalozi wetu London). Kifungu 2009- hatua za kumaliza masuala ya nyuma yaliyotolewa na CAG ya takribani 451 milioni kuhusu Ubalozi wetu Moscow. Hatua zilizochukuliwa kurekebisha kasoro za mawasiliano na sekta mbalimbali kuwezesha utekelezaji wa miradi inayodhaminiwa na Serikali ya China na Taasisi/Makampuni yake, hii ifanyike kwa kutumia vizuri rasilimali zilizotengwa kwenye Kifungu 2014. Kifungu 2027; hatua zilizochukuliwa kushughulikia kasoro ya milioni 865 kutumiwa bila idhini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Volume IV*, Fungu 34, Kifungu 1604, Kasma 6391, kwenye utekelezaji 2009/2010, 2010/2011 na malengo 2011/2012, napenda kujua hatua zilizochukuliwa kwa Ubalozi wetu Kigali kulipa nyumba miezi saba bila kutumika, ukarabati wa Ubalozi wetu Nairobi na ujenzi kwenye kiwanja *Upper Hill*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya kulinda maslahi ya kiuchumi ya nchi yetu, mkazo uwekwe kwenye Balozi za nchi ambazo tuna maslahi mengi ya kiuchumi kwa

kurejea Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano. Aidha, safari za nje za viongozi zipunguzwe ukubwa wa misafara na idadi ili kuweka mkazo kwenye safari zenyetija. Haiwezekani kwa safari zote kati ya 2005-2010 kwa kisingizio cha kutafuta wawekezaji halafu tumeshindwa kuweka mstari wa mbele kuondoa kero ya umeme na upatikanaji wa gesi asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ijikite katika kuepusha uongozi wetu kutumiwa na makuwadi wa kiuchumi bila maslahi ya Taifa na rasilimali zake kulindwa kwa kiwango cha kutosha hususani kwenye ardhi, madini, gesi n.k Kampuni kama *Good Works International* zichunguzwe kwa ajili ya maslahi ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ishirikiane na Wizara ya Afya, NSSF na Ubalozi wa India kuharakisha ujenzi wa Hospitali ya Apollo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza ushiriki wa Watanzania wanaoishi ughaibuni (Diaspora) kwenye maendeleo; Wizara ishirikiane na mamlaka nyingine kuhakikisha inafanyika sensa rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya kiusalama yapewe kipaumbele katika kazi za Wizara. Serikali itoe kauli kuhusu malalamiko ya Askari wa Tanzania katika vikosi vya kuleta amani vya UN hususani nchini Lebanon na Sudan (Darfur). Malalamiko hayo yanahuisha kuchelewa kwa mishahara na kupelekewa malipo pungufu ya mikataba. Malalamiko hayo yameshaandikwa kwa Rais na Waziri wa Ulinzi badala ya haki zao kulindwa, wameandikiwa Waraka toka Makao Makuu ya Jeshi wa kuwatishia kuwa watarudishwa na kufukuzwa kazi. Ni muhimu Wizara ya Mambo ya Nje ikaingilia kati ili kuhakikisha masharti yote na stahili zote zilizomo kwenye mikataba ya kulinda amani baina ya Tanzania na Umoja wa Mataifa UN yanatekelezwa. Aidha, kwa ajili ya kusafisha taswira ya Tanzania Kimataifa, ni vizuri Serikali ikatoa kauli ya hatua ambazo imechukua kuhusu tuhuma za baadhi ya Watanzania kuhusika na biashara ya silaha haramu. Mathalani Ripoti ya Timu ya Wataalamu wa Baraza la Usalama la UN ya tarehe 26 Januari 2006. Pia mkataba wa tarehe 17 Agosti 1997 kati ya Kampuni ya *Executive Outcomes Inc.* na Tanzania kwenye mradi wa madini kupitia mradi wa Meremeta, suala ambalo limehusishwa na usafirishwaji wa silaha haramu Congo (DRC) kati ya 1997 mpaka 2007.

MHE. LOLESTIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri kwa hotuba nzuri. Pia nashukuru sana kwa ushirikiano mkubwa ambao Wizara inafanya. Aidha, nampongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara na Watumishi wote kwa kazi nzuri inayofanyika. Ni kwa sababu hii ndiyo maana nchi yetu ya Tanzania inazidi kung'aa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba, nimefurahia sana juhudhi na mpango wa kuziunganisha Jumuiya za SADC, EAC na COMESA ili kuwa na eneo moja huru la kibiashara. Soko hili ambalo linategemea kujumuisha nchi 27 kati ya 54 za Afrika zenyetia wakazi milioni 700. Soko hili ni kubwa sana na kama tutaweza kujipanga vizuri, nina uhakika tutanufaika sana katika nyanja mbalimbali za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012, sijaweza kuona Mpango Mkakati wa Wizara wa namna nchi yetu itakavyoshiriki katika Umoja huu na mpango wa namna tutakavyonufaika. Hivyo basi, napenda kujua au kupata maelezo ya ziada kuhusiana na mkakati huu. Tunazo rasilimali nyingi sana ndani ya nchi yetu ambazo nadhani kupitia Umoja huu, tunaweza kunufaika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya hotuba nimeona jinsi ambavyo mpango wa *SAGCOT* uliweza kunadiwa katika Mkutano wa Kimataifa wa Jukwaa la Uchumi (*World Economic Forum*). Kutokana na fursa hizi muhimu, naomba pia katika maeneo ya Maziwa Makuu, ipo Mikoa mingi ya Tanzania inayozunguka Ziwa Victoria ambalo kihistoria ni Ziwa la pili duniani kwa ukubwa, kupitia fursa hii tutakuwa na nafasi nzuri ya kukuza uchumi wetu kwa kuwa na mpango mahsus wa kiuchumi katika maeneo haya. Kupitia Ushirikiano wa Kimataifa, naomba Wizara itafute namna ya kuinua uchumi katika Maziwa Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika malengo ya Wizara katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, mojawapo ni kuzitafutia masoko bidhaa zetu zenyenye ubora unaotakiwa katika nchi za nje kwa kushauriana na wazalishaji wa ndani wa bidhaa hizo. Katika Kanda ya Ziwa tunalo zao la Pamba ambalo limeshuka bei. Je, Wizara inajipanga vipi kulitafutia soko zao hili ili kuwanusuru wakulima wa pamba katika Mikoa 13, Wilaya 42 na wakulima wapatao 350,000 na 500,000?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Col. Muhammad Bacar alipopindua kule Comoro, nchi za AU ziliazimia kumuondoa Kijeshi na Tanzania ikachukua hatua za kutuma kikosi kule na kazi ikafanikiwa lakini nchi ya Libya ilipovamiwa na NATO, AU imemezea, kulikoni? Hakuna anayethubutu kuweka Azimio kali kama lile lililopelekea kumuondoa Col. Mohamed Bacar kule Comoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naikubali sana Sera nzuri ya “*Engagement of the Opponent rather than Isolating Him*”, kama alivyosema Naibu Waziri wa *Foreign Affairs* wakati akijibu swali kuhusu Libya wiki iliyopita. Nadhani ‘details’ za hiyo “engagement” zinapaswa kuangaliwa upya. Comoro tulifanya “*Military Engagement*” na leo Libya tunafanya mazungumzo, ni vigezo vipi tunatumia kupima “*Level of Engagement*”?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni kwa nini mpaka leo bado hatuna “*Diplomatic Relations*” na Israel wakati ya Palestine tunayo? Hapa naona tumechanganya “*Engagement na Isolation*”. Ndugu zangu, naomba niwashawishi kwamba tunahitaji kufanya *reforms* kwenye Sera yetu ya Mambo ya Nje ili Tanzania tuwe na sauti na heshima kubwa zaidi huko nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jinsi gani na kwa kiasi gani tumeitumia fursa ya “*quota*” yetu ya ajira kwenye Mashirika ya Kimataifa na je kuna utaratibu gani wa kuwapata wataalam wenye sifa za kuchukua fursa hizo za ajira? Pengine nishauri Serikali yetu iwe ‘*more proactive*’ katika ku-*claim quota* yake na nafasi hizi zitangazwe *widely* hadi Mikoani na Wilayani na siyo kwenye ofisi za Dar es Salaam tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukiibiwa sana rasilimali asilia na urithi wa Watanzania. Hivi tunayo “*International Competitive Intelligence*” ya kutosha kupambana na ushindani wa kiuchumi katika zama hizi za utandawazi za “*knowledge economy*”? Kama jibu ni ndiyo, kwa nini tumekuwa tukirubuniwa na kujikuta tukipata hasara na kuibwa kwenye mikataba mmingi na makampuni ya Kimataifa? Ni kwa nini tumekuwa tukiingiza nchi yetu kwenye “*Tax stability Clauses*” kwenye mikataba inayowafaidisha wabia wa kigeni? Ni kwa nini tusivunje mikataba hii na kujitoa kwenye mikataba kama ya “*International Commercial Court*” na “*International Cotton Association*” ili tuwe na uwezo wa kuivunja mikataba hii bila kwenda kwenye Mabaraza haya ya Mapatano ya Kimataifa, maana ni dhahiri ubia na urafiki na makampuni ya nje umekuwa siku zote ni wa kutuibia rasilimali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano ni ule mikataba wa ubia wa Kampuni ya *Pan African Energy (Tanzania) Ltd* ambayo inachimba na kusambaza gesi asilia ya Songosongo. Tuna taarifa za kampuni hii kukwepa kodi ya USD 65m! Je, tunazipata vipi pesa hizi? Kuna mfano wa *BAE Systems*! Mfano wa mikataba ya Dhahabu na jinsi wanavyokwepa kodi. Makampuni ya Simu na Mahoteli na ukwepaji wa kodi ya *Capital Gain* na ile ya *Corporate Tax. Issues* za kutumia *Tax Havens* na *Submiller* etc. Kwa nini tunaendeleza urafiki na wezi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri aliyoitoa kwa umakini na ufanuzi mzuri wa mambo ya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo ninayo machache ya kueleza. Mabalozi wa nchi za nje kucheleweshewa mishahara na kuishi katika majengo chakavu, jambo ambalo linapunguza heshima ya Taifa letu. Mabalozi wapewe fungu la kutosha ili kukabiliana na adha inayoweza kujitokeza, kwa Watanzania waliopo katika nchi hiyo au wanaokwenda katika nchi hiyo ili kuwasaidia pale linapotolea tatizo lolote ambalo linahitaji msaada wa Kibalozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uteuzi wa nafasi za Ubalozi, uteuzi uendane na uwezo alionao mtu katika masuala ya kidiplomasia yanayoweza kukuza mahusiano ya kisiasa, kiuchumi ili kuleta sifa katika nchi yetu na siyo kupeana tu kindugu, kiurafiki, kupeana fadhila ikiwa kama njia ya kupumzishana au kama huduma ya kiinua mgongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo machache, naunga mkono hoja.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ni muhimu sana hasa ikizingatiwa kuwa ulimwengu wa sasa unahitaji kuenzi Lengo la nane (8) la Milenia, yaani “*Global Partnership*”. Ni Wizara gani inayowajibika kuiunganisha nchi yetu na nchi nyingine? Ni wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu imekuwa ikitiwa na kuripotiwa matatizo ya Wizara hii yanayosababishwa na ufinyu wa bajeti uliopo kwa sababu ya ubadhirifu wa fedha za umma kama ilivyodhihirishwa humu Bungeni wakati wa kuchangia hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini. Ufinyu huu wa bajeti umepelekea Mabalozi wetu na Maofisa mbalimbali kufanya kazi katika mazingira magumu. Nashauri Wizara ipeleke fedha katika Balozi zetu tena kwa wakati na ziwe za kutosha ili wasidhalilike na udhibiti wa matumizi ya fedha hizo ufanyike ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue* ya pili, kumekuwa na tatizo la kuteua Mabalozi waliozidi umri wa miaka 60 ambao ni wa kustaafu Utumishi wa Umma. Swali la kujiuliza, hawa Mabalozi sio Watumishi wa Umma? Serikali inataka vijana wafanye kazi gani? Nashauri Sheria ya Utumishi wa Umma izingatiwe katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kesi ya Costalick Mahalu aliyekuwa Balozi wa Tanzania nchini Italia inasemekana kuwa gharama zake zimezidi kiasi cha fedha zinazomfanya Profesa Mahalu kutuhumiwa na kushtakiwa Mahakamani. Naomba kauli ya Serikali katika hili. Ni sababu gani zimepelekea matumizi kuwa makubwa na umma wa Watanzania utanufaika namna gani baada ya mabilioni ya shilingi kuangamia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka wa Tanzania Wilayani Ngara, Mkoani Kagera, umeporwa na wajanja wachache kupitia uongozi wa WILAYA ya Ngara na hivyo kupelekea uhitaji wa Ramani ya Tanzania kuchorwa upya. Familia 27 zimepoteza makazi na mashamba yao katika Kijiji cha Kasange, Kata ya Kirusha, Wilayani Ngara baada ya Serikali Wilayani humo kuwafukuza wampishe mtu mmoja raia wa Burundi na hivyo kupelekea bikoni za mpaka wetu kuhamishwa na hivyo kupunguza ardhi ya Tanzania. Naomba Serikali itoe kauli yake katika hili na itawachukulia hatua gani viongozi wote wa Wilaya ya Ngara wanaotajwa kuhusika katika suala hili hadi kuruhusu bendera ya Burundi kupandishwa katika eneo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue* ya Rada, wahusika wote wafikishwe Mahakamani haraka kwani suala hilo limeitia hasara Serikali yetu. Kuna shida gani kuwakamata na kuwafungulia mashtaka? Kuna mazingira ya kuogopana, Serikali inaogopa nini na kwa nini au nayo ni sehemu ya ufisadi huo? Naomba kauli ya Serikali, itawakamata na kuwfikisha lini Mahakamani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uraia wa nchi mbili hauna tatizo, Serikali inasita kuruhusu suala hili kwa nini huku ikijua kuwa haki ya mtu kuamua aishi wapi ni ya kwake? Si busara kumzuia raia wa Tanzania anapopata uraia wa nchi nyingine kutotambuliwa kuwa si raia tena wa Tanzania. Huu ni uonevu mkubwa, Serikali iridhie matakwa ya Watanzania wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, mambo hayo ni muhimu yakapata ufanuzi kwa maslahi ya Watanzania wote na itakuwa vema sana iwapo Serikali itakubaliana na ushauri huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha.

MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa hotuba nzuri na kazi kubwa anayofanya katika nyanja za Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, naomba nishauri haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, fedha zinazotengwa kwa ajili ya kuendeleza Wizara ya Mambo ya Nje na Uhusiano wa Kimataifa ni ndogo ukilinganisha na kazi zilizo mbele yake. Nashauri kwa siku za usoni bajeti ya Wizara hii iongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Ndugu Ludovick Utouh, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa Mgombea pekee wa Bara la Afrika atakayewania nafasi ya ujumbe wa Bodi ya Ukaguzi ya Umoja wa Mataifa kwenye uchaguzi utakaofanyika mwezi Septemba mwaka huu New York, nashauri Serikali ya Tanzania impe kila msaada aweze kushinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nchi za Somalia, Kenya na Sudan ya Kusini zina upungufu mkubwa wa chakula kwa sasa. Kwa kuwa Tanzania ina chakula, nashauri Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa aishauri Serikali ijenge Soko la Kimataifa katika Mji wa Himo, Vunjo ili kuziwezesha nchi za Somalia, Sudan ya Kusini na Kenya kuja Tanzania kununua chakula na wala si Tanzania kuzifuata nchi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, inavyoelekea fedha za Rada zimehodhiwa huko Uingereza mpaka sasa. Madai ya kutaka kutoa chenji yetu kwa *NGO* hayakubaliki. Nashauri Serikali iendelee kufuatilia fedha hizo ambazo ni haki yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, uraia wa nchi mbili ni muhimu sana kwetu na una maslahi kwetu, ingefaa suala hili litekelezwe sasa.

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na wataalam wake wote kwa hotuba nzuri inayolewaka na kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uajiri wa Ofisi ya Mambo ya Nchi za Nje kwa Zanzibar ziko chache na hata wanaopata nafasi ya kwenda kufanya kazi nchi za nje kwa Zanzibar ni chache. Wakati unapotembelea ofisi ya Zanzibar ukweli jengo ni tupu hata hao wanaohitajiika kuwepo ofisini huwakuti sababu hawana kazi, utawaona inapotokea shughuli za Serikali. Hata kama kutakuwa na sherehe ya kitaifa au mgeni anatoka nje wa

Kimataifa, mgeni huyo ataongozana na viongozi kutoka ofisi ya Bara, hii inaonesha kwamba kwa huku Zanzibar hakuna wataalam wa kuwa na mgeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri naomba muikuze ile Ofisi ya Mambo ya Nje iliyopo Zanzibar nayo iweze kufanya kazi zake. Hata kama kungekuwa na Naibu Waziri akawepo Zanzibar ili kuipa hadhi ofisi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mungu kwa ajili ya nafasi hii ili nichangie juu ya shughuli zinazofanywa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Nimshukuru Waziri na timu yake yote, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai kuwa Watanzania waishio nje ya Tanzania (*Diaspora*) waelimishwe, wahamasishwe ili waje kuwekeza hapa nyumbani, ili wasaidie kukuza uchumi wa nchi kwani hao wote ni wale waliosomeshwa na kodi ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na uhusiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), natoa rai yangu kuwa Tanzania iwe macho kusitokee tena uvunjaji wa Jumuiya hii. Ni rai yangu pia kwa elimu itolewayo Tanzania iwe na uwiano mzuri/bora na elimu katika nchi nyingine za Afrika Mashariki (Kenya, Uganda, Burundi na Rwanda) ili na Watanzania waweze ku-*compete* na wenzao wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai yangu pia kuwa Tanzania iwasiliane na Zambia ili wakubaliane maporomoko ya Kalambo (Kalambo Falls) ili Rukwa tuweze kwanza kupata umeme kutokana na Kalambo Falls lakini pia tuweze kupata watalii wa ndani na nje ili kuinua uchumi wa Rukwa na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuchangia Bajeti iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ameeleza kuwa Malaria ni maradhi sugu katika Afrika. Ugonjwa huu ambao unaua watu wengi, hasa watoto chini ya miaka mitano, watoto 595,000 hufa kila mwaka, hawa ni watoto wengi sana. Ni lazima sasa kubadili vita dhidi ya Malaria kwani kugawa vyandarua pekee siyo uvumbuzi wa kinga ya kutosha dhidi ya Malaria. Napenda Mheshimiwa Waziri afahamu, baadhi ya (neti) vyandarua vingi vinavyogawiwa hapa nchini havitoshi hata kitanda cha futi tatu hasa huko vijijini kama Sengerema na maeneo mengineyo. Vyandarua pia vinatumika wakati wa kulala, lakini kama hujaamua kulala ni lazima utaliwa na mbu tu. Ni vizuri sasa tukarudia mpango wa zamani wa kunyunyuzia dawa madimbwi, makaro hata maeneo ambayo yanakuwa na mbu, nyumba zao zinyunyiziwe dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Mheshimiwa Waziri aniambie ni vidi anapokuwa nje ya nchi, anajifunza jinsi gani ambavyo wenzetu wanaongeza mapato na ni namna gani anatuletea ujuzi huo? Pamoja na kuitangaza Tanzania nje pia ni vizuri nasi kusoma kitu ambacho kinaweza kutuletea faida. Mfano, nchi ya Seychelles ni wavuvi wa uvuvi wa kisasa na mapato yao hupatikana katika uvuvi na utalii tu. Ni jinsi gani Mheshimiwa Waziri anaweza kuishauri nchi nasi tukaweza kupiga hatua kwenye uvuvi na utalii? Naomba Wizara tujifunze kusoma mambo mazuri ya wenzetu na sio kuhudhuria mikutano na kuitangaza nchi yetu peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni masikitiko yangu kwa Ubalozi wa Zambia, ambapo nyumba iliyojengwa haijafikisha hata miaka 10 lakini upande mmoja umetitia na Balozi wetu ameamuliwa asiitumie, kwani Balozi huyo anaishi ndani ya nyumba ambayo ni hatari kwa maisha yake. Pia Ubalozi wa Zambia hawana hata gari, kwani gari ni mbovu, hata gari wanaazima. Ni kwa nini Ubalozi huu usipelekewe gari nyingine? Ahadi ambazo mnawaahidi bila utekelezaji ni kuwadanganya watu ambao mnatarajia wafanye kazi, kweli wataweza? Napenda kujua kama Mkandarasi aliyejenga nyumba ya Zambia alichukuliwa hatua gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupunguze safari zisizo za lazima nje ya nchi na misafara mikubwa ya Mheshimiwa Rais anaposafiri nje ya nchi ipunguzwe. Ni vizuri kutumia pesa zetu vizuri na nyingine ziweze kununua vifaa muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kama sijakosea Afrika Kusini, Malaria ni hadithi, ni vidi wao walifanya hadi wakaweza. Ni lazima tukubali kujifunza kutoka kwa wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kufahamu aliyejeka Balozi wetu Afrika Kusini pamoja na kustaafu hali yake inaendeleaje na kama baada ya kuvamiwa na kupigwa, kuna kesi yoyote iliyofunguliwa na kama ipo inaendeleaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayofanya katika kusimamia maslahi ya Tanzania nje ya nchi yetu. Naipongeza pia hotuba ya Waziri kwa kuwasilisha kwa umahiri mkubwa. Inaonyesha wazi kwamba yuko mbele katika masuala anayoyasimamia. Mchango wangu uko katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani na azma ya Wizara ya kujenga Kituo kipy Cha Kimataifa kingine Mjini Arusha ilihali kuna AICC tayari pale Arusha. Nashauri kituo hicho kijengwe sehemu nyingine ili kusambaza mtawanyo wa utalii na kuhamasisha uwekezaji wa utalii katika maeneo mengine nchini kama vile Mwanza au Mbeya. Kujenga kituo hicho Arusha kunaendeleza dhana potofu kwamba eneo pekee linalofaa kwa utalii ni Arusha tu. Leo hii utalii unadumaa kwa sababu ya gharama kubwa

wanazokutana nazo watalii kwa kuwa vivutio vikubwa viko mbali na Dar es Salaam na Arusha ambako kuna viwanja vya ndege vya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushiriki wetu katika harakati za kimataifa ziwe zimelenga kulinufaisha Taifa letu. Juhudi kubwa za kukomboa Kusini mwa Afrika na vita vya Uganda hazikutunufaisha kiuchumi kama Taifa. Enzi hizo tuziache na sasa tuweke mbele zaidi manufaa ya Taifa letu. Leo Angola hawana msaada wowote kwetu ingawa sisi tuliwahangaikia sana, mifano ni mingi. Tuogope sana mambo ya sifa yasiyo na manufaa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Serikali kuanza kununua “properties” nchi za nje na kuweka mitaji. Kuendelea kukodi nyumba za Balozi si jambo jema. Nashauri angalau kila mwaka tuwe tunanunua majengo kwa ajili ya Balozi zetu na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Mheshimiwa Waziri atoe ufanuzi atakapokuwa anafunga hoja juu ya suala la Uraia wa Nchi Mbili (*Dual Nationality*) na suala la Tanzania kuwa mwanachama wa SADC na wakati huohuo ni mwanachama wa COMESA.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Wizara kwa kufuatilia kwa karibu suala la fedha za rada na msimamo wa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje kwamba fedha hizo ni za Watanzania hivyo zirudishwe kwa Watanzania wenywewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swalí moja kuhusu soko la mboga za majani katika nchi moja ya Ulaya ambapo Mheshimiwa Rais katika hotuba yake ya mpango wa Taifa wa Miaka Mitano alisema kwamba yupo mteja Mzungu ambaye alizaliwa Tanzania anahitaji mboga kutoka Tanzania. Je, Ubalozi umeshaanza kufuatilia suala hilo au mteja huyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iwawezeshe Mabalozi wetu nchi za nje kifedha ili waweze kufuatilia fursa kama hizi hata katika maeneo mengine yasiyo ya kilimo. Pia wapewe miongozo nini cha kufanya kwa kuzingatia Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano ili tuweze kutekeleza vizuri sera ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja.

MHE. CHIKU A. ABWAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa Hotuba nzuri pia nampongeza Waziri Kivuli kwa Hotuba nzuri. Nimeona nichangie kwa maandishi ili nije nichangie hoja ya Waziri wa Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iangalie upya namna ya kutoa uraia nchini, naona kama wanawake hatutendewi haki. Iweje mwanamke akiolewa na mtu wa

nje akipata watoto hawapewi uraia na mwanaume akioa mtu wa nje watoto wanapewa uraia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo naomba Wizara yako ilipiganie ni suala la Watanzania kuwa na uraia wa nchi mbili. Cha kusikitisha wakati nchi yetu haijaruhusu kuwa na uraia wa nchi mbili, tayari wapo Watanzania wenyewe uraia wa nchi mbili, Watanzania wengi wenye asili ya Kiasia wanautaratibu huo. Wakiwa hapa nchini wanajiita Watanzania na wana *Passport* ya Tanzania lakini wakienda kwao wanapewa *Passport* za kwao. Mara nyingi wakati wa uchunguzi wanaondoka wakihofia hatma ya uchaguzi. Vilevile wanakwepa kulipa kodi ya kibali cha kuishi nchini na kulilettea hasara Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Wizara hii ni muhimu ikafuatilia kwa karibu hawa watu wageni wanaoingia nchini kama wawekezaji, ni kweli wanatekeleza azma hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupata majibu ya hoja hizo nilizochangia, nakutakia kila la kheri kwa kazi unayoifanya. Wako katika ujenzi wa Taifa.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja/mawazo katika Wizara hii hususani katika mahusiano kati ya Mabalozi wetu katika nchi husika na Watanzania wanaoishi huko, kwani nimeshuhudia kuwa hamna *link* yoyote ile na hii inapelekea kutojua Watanzania waishio huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelishuhudia hili mara kadhaa nilipokuwa natembelea nchi tofauti wakati nikiwa bado nipo kazini UDSM. Nikagundua kuwa hata Balozi zetu hazina *Statistics* za Watanzania wanaosoma katika nchi husika. Hii ni mbaya sana na imetokea pia wakati nahudhuria Mkutano wa 4th UN-LDC uliofanyika Instabul huko Ugiriki/Turkey mwaka huu May 2011. Ilisikitisha kuwa hatukupata fursa ya kukutana na wananchi wa Tanzania waishio Turkey. Nilidhani kuwa Ubalozi ungewaeleza uwepo wa mkutano ule Watanzania wote ili hata baada ya mkutano wangeweza kupata fursa ya kukutana na Tanzania *delegation* ili waweze kupata *brief* ya yaliyojiri katika mkutano ule na hivyo kuweza kupata michango ambayo kwa njia moja au nyingie ingeboresha na kuleta changamoto kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu utoaji wa visa. Nimekuwa nikishuhudia kuwa sisi tunapokuwa tunaenda kwenye nchi husika za nje tunahitaji kuomba visa toka huku Tanzania ndio tuondoke lakini kwa Mataifa mengine yanapata *visa airport on arrival*, kwa nini na wao wasipewe *visa* kwenye Balozi zetu na *Consular* za Tanzania katika nchi husika? Huu ni ubaguzi wa hali ya juu, yaani Watanzania wanapoteza muda mwingi. Pamoja na usumbufu mwingi kufuatilia *visa* ili waweze kusafiri lakini wapo wanaopata *freelancer* yaani *visa on arrival* hii iangaliwe na naomba majibu kwenye majumuisho ya Waziri kuhusu dhamira hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri sasa tuna Watanzania wengi wanakosa fursa yao ya misingi ya kupiga kura na kuchagua viongozi wao hasa wale Watanzania ambao

wameenda nje kusoma kwa kipindi cha miaka michache yaani chini ya mitano ambapo hulazimika kurudi nyumbani na kuwa sio haki kuongozwa na kiongozi asiyemchagua. Hivyo ni bora suala hili litazamwe kwa macho mawili na lifanyiwe kazi ASAP.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni kuhusu ukuzaji wa kidiplomasia ya kimataifa kuhusiana na nidhamu ya utendaji kazi wa Maafisa mbalimbali wa Balozi zetu ambao ndio *image* ya Taifa letu katika nchi wanazotuwakilisha. Mfano, kashfa ya Afisa Mwambata wa Ubalozi wetu nchini Marekani, Dkt. Allan Mzengi na kampeni iliyokuwa ikifanywa na Mawikili wa Bi. Zipora Mazengo kwa *compress* ili kuichafua Tanzania kufuatia tuhuma inayomhusisha na biashara haramu ya binadamu ambayo ilimtaka alipe gharama. Sasa sijui kama ilishalipwa au? Hii imeanishwa vizuri katika maoni ya Kambi ya Upinzani, *page number* 17 hadi *page* 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia kwa maandishi Wizara hii. Nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuweza kuandaa Bajeti hii na kuileta ndani ya Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Mabalozi wetu walio nje ya nchi, hawa ni watu muhimu sana kama watafanya kazi zao vizuri. Nchi yetu imekuwa ikiingia mikataba mibovu inayoigharimu nchi yetu na makampuni mengi yanatoka katika nchi ambazo tuna uwakilishi wa Mabalozi, hivi Mabalozi hawa tuliotumua huko wanafanya kazi gani? Mimi nilifikiri wao wangkuwa wa kwanza kutoa ushauri kwa nchi yetu juu ya makampuni hayo kabla nchi yetu haijajiingiza katika mikataba hii mibovu ambayo inatumiza sana. Nafikiri umefika wakati Mabalozi watusaidie kufanya kazi hii ya kuchunguza hayo makampuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Mabalozi wetu hawana bajeti za kutosha katika nchi walizopo lakini tunawaomba watusaidie kutafuta masoko kwenye mazao ya wananchi wetu. Najua wakiamua wanaweza kutafuta masoko haya na itasaidia kuinua uchumi wa Taifa letu. Pia niiombe Serikali kuongea bajeti ya kutosha ili Mabalozi wetu waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tatizo la utoaji holela wa pasi za kusafiria ambao umefanya watu ambao si Watanzania kupewa pasi hizo za kusafiria na matokeo yake wanaposafiri nchi za nje wanafanya uhalifu na hii imechafua sifa ya watu wa Tanzania nchi za nje na watu hawa wengi wako kwenye magereza ya nchi hizo wanaonekana ni Watanzania kumbe siyo mfano, Hong Kong. Tunaomba Wizara hii na Wizara ya Mambo ya Ndani ifuutilie jambo hili na tujue hatua zilizochukuliwa kwa watu hao wenyе pasi za kusafiria wakati wao si Watanzania. Watu hawa wanalitia aibu Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kutoa mchango wangu huu kwa uchache.

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naipongeza Wizara hii kwa Hotuba nzuri ya Bajeti na naunga mkono hoja hii. Pamoja na kuunga mkono, ninayo maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uraia wa nchi mbili hili limejadiliwa sana, sasa ni wakati tufanye uamuzi. Katika dunia ya utandawazi suala hili halikwepeki. Tahadhari ni kwamba tuanze kwa awamu sio *wholesale*, kwa maana tufungue milango ya uraia wa nchi mbili kwa watanzania waishio nje. Hii itakuwa hatua ya majaribio (*pilot measure*). Bidii ya kuona zoezi hilo litakavyoenda ndipo tufungue milango kwa raia wa nchi zingine lakini uwepo utaratibu madhubuti wa kuwa *scrutinize* kabla ya kuwakubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Diaspora*. Suala la kuwatambua Watanzania waishio nje kwamba wapo nchi gani, wanafanya shughuli gani na jinsi gani wanaweza kusaidia shughuli za nyumbani sasa kukamilishwe na tuweke utaratibu mahsusini wa kutumia ujuzi wao, taaluma zao na fedha zao (*remittances*) katika kujenga uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi zetu za Ubalozi ziwezeshwe kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na hasa katika kutekeleza sera ya Diplomasia ya uchumi. Matatizo ya Ofisi za Ubalozi kuhusu vitendea kazi na mtaalam, linafanya zikose uwezo wa kutekeleza sera hii muhimu katika enzi hizi za utandawazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja hii.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Waziri, Naibu wake na wataalam wote kwa kuandaa Hotuba hii na kuleta hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inatumia fedha nyingi sana kugharamia Balozi zetu zilizoko nchi mbalimbali pamoja na watumishi 172 wanafanya kazi huko na wanalipwa fedha au mishahara mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa hili linanufaikaje kikamilifu kutokana na uwepo wa Balozi hizo? Watanzania wengi wanaishi nje kwa baadhi ya nchi ikiwepo Canada wanakuwa wanalamika kuwa Balozi yetu haiwajali wala kuwatambua hata wakiwa na shida. Waziri aeleze kuna utaratibu gani na mipango gani ya kuhakikisha watanzania wanaoishi ne wanatambuliwa na kuwa *registered* kwenye Balozi zetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Balozi zetu zinasaidiaje kupata wawekezaji wa ukweli, waaminifu na wenyre lengo la kusaidia nchi yetu? Kumekuwepo na tabia ya Serikali yetu kutotumia Balozi zetu kikamilifu kufanya utafiti na udadisi kwa masuala ya kiuchumi. Watendaji wa Serikali wamekuwa wanakwepa kutumia watumishi wa Balozi zetu na badala yake wanawasiliana moja kwa moja na nchi husika na matokeo yake tunakosa fursa muhimu za kufanikisha masuala muhimu ya kibiashara, kisiasa na hata kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iwe inafanya mawasiliano wakati Waheshimiwa Wabunge wanakwenda nje waweze kuwapokea na kuwasaidia pale wanapokwama. Mara nyingi Balozi zetu zinaonekana pale anapokwenda Rais au Waziri, lakini Mbunge ni kiongozi mkubwa na anapokuwa kwenye safari za mafunzo nje ya nchi angependa kupata kuonana na mwenyeji Mtanzania huko anapokuwa ili aweze kujua mambo mengi zaidi na hata kujua *opportunities* ambazo zitanufaisha Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri viongozi wanapotoa kauli kwenye vyombo vya habari wakawa makini sana sana na kauli zao. Kauli ikitolewa vibaya inaweza kuharibu mahusiano ya nchi na nchi na hata kuleta kutokuelewana. Mfano, kauli iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje wakati akizungumzia suala la Rada alisema “Uingereza waturudishie fedha zetu walizotuibia”. Hii kauli haikustahili kabisa kutolewa *open* kwenye media wakati Waziri unajua mazingira ya rushwa yaliyopelekea fedha zile kufika Uingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misafara ya Rais na viongozi waandamizi ndani na nje ya nchi inatumia fedha za walipa kodi na fedha za Taifa hili. Wizara ya Mambo ya Nje inapoandaa safari za viongozi inaangalia tija ya safari na watu wanaokwenda? Safari inakuwa na watu 15 hadi ishirini na tisa (29) kwa ajili ya nini? Hayo siyo matumizi mabaya ya fedha zetu? *We need to use our resources careful.* Tupeleke wataalam kwenye msafara wa Rais ili wakachote ujuzi, uelewa, maarifa na wakirudi waje watumie walichokipata kuinua uchumi wetu na siyo kupeleka watu matembezi.

MHE. JUMA SURURU JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi. Kuhusu suala la wawakilishi katika Mabalozi ya nchi mbalimbali nje ya Tanzania. Nimebaini kwamba Mabalozi au Maofisa Mabalozi walio nchi za nje wengi wao wametoka Tanzania Bara na idadi kidogo ndiyo wametoka Zanzibar. Hivyo, naishauri Serikali kupitia Wizara hii, iandae utaratibu maalum wa kuongeza idadi ya Wazanzibar katika kuliwakilisha Taifa letu huko nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la safari za Serikali nje ya nchi. Kwa kipindi kirefu nimekuwa nikiona safari nyingi za Serikali zikifanyika, lakini katika msafara huo ni viongozi kutoka Serikalini tu ndiyo wanaokwenda huko. Hivyo, naishauri Serikali kupitia Wizara hii ijaribu kuweka utaratibu wa kuwashirikisha Waheshimiwa Wabunge katika kila safari ili kuleta uwakilishi mzuri, kwa wananchi wa Tanzania na Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ofisi za Balozi ndogo huko Zanzibar. Hapo zamani kulikuwa na Ofisi nyingi za Balozi ndogo ndogo hapo Zanzibar, lakini kila siku zinavyokwenda mbele Ofisi hizo zimekuwa zikipunguka. Hivyo, naishauri Serikali kupitia Wizara hii kufungua Ofisi za Balozi ndogo ndogo huko Zanzibar na iwapo Serikali itaamua kulifanya suala hili, wananchi wa Zanzibar wataondolewa usumbufu na mzigo mkubwa wa kufuatilia huduma mbalimbali za *visa*, masomo, kazi na kadhalika kwani kwa utaratibu wa sasa hivi ni lazima Mzanzibar asafiri na kuja Dar es Salaam kwa kutafuta huduma hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Idara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa iliyopo Zanzibar, kimtazamo ukienda katika Ofisi hiyo utakuta iko katika hali ya kutofanya kazi kiofisi, Ofisi haina vitendea kazi, Ofisi haina Idara za kutosheleza za kuratibu mambo ya nje, kiutendaji Ofisi hiyo inakuwa na *activity* pale panapokuwa na ugeni kutoka nchi za nje na ugeni ukiondoka kazi zimeondoka. Hivyo, naishauri Wizara, Ofisi hii ipewe *facilities* zake kwa ukamilifu ili mwananchi akifika pale apate huduma zote na sio kusubiri, maamuzi kutoka Makao Makuu.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Mheshimiwa Benard Membe na Waziri mwenye dhamana, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote walioshiriki kuandaa Bajeti hii nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naipongeza Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti, Mheshimiwa Edward N. Lowasa kwa kazi nzuri iliyofanya kuijadili Bajeti hii na kuipitisha vema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kutoa mchango huu, napenda kutamka rasmi kuwa naunga mkono Bajeti hii mia kwa mia. Nawaombea Mwenyezi Mungu awape afya na mshikamano ili waweze kutekeleza malengo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upatikanaji wa uraia wa Tanzania. Naiomba Serikali ilegeze masharti ya kupata uraia, mgeni aliyeoa au kuolewa Tanzania kwani wengi wanapata taabu na inasababisha ndugu zetu walipoaa au kuolewa kupata uraia wa nje bila kupenda ili familia zao ziweze kukaa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la mahusiano ya nchi za Afrika Mashariki. Napongeza sana kwa mahusiano mazuri ya nchi zetu za Afrika ya Mashariki kwa masuala ya biashara, elimu na kadhalika. Napenda kutoa angalizo katika suala la kumiliki rasilimali hususan ardhi, naomba hili tulitazame kwa macho mawili kwani tusije tukauza rasilimali zetu bila kuweka taratibu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie majambazi wa kigeni. Bado ulinzi wa mipaka yetu siyo imara sana kwani majambazi wa kigeni bado wanaingia kama ilivyotokea Arusha. Naishauri Serikali kuweka ulinzi na mikakati ya pamoja vizuri ili nchi na nchi zisilaumiane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, narudia tena kuunga mkono hoja hii.

MHE. NAOMI A.M. KAIHULA: Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika masuala ya mikataba mibovu, Sheria ya Uraia wa Wanandoa na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, suala la mikataba mibovu linashangaza sana jinsi ambayo linashughulikiwa na Wizara hii, mikataba hii inafanywa na wananchi wa nchi zilizoendelea na zinajua fika namna gani makampuni yao yameingia kwa kuwadanganya

Watanzania, sasa inakuwaje pale inapotokea tatizo la wazi kabisa la hawa *Multinationals* kuwaumiza wananchi dhaifu na wasio na uwezo wa kujitetea, kwa nini hasa Wizara hii haichukui taratibu za kuomba ushauri kwa nchi zao kutusaidia. Mfano, ni migodi ya dhahabu, almasi na kadhalika. Ni muda muafaka kwa Wizara hii kuwa *more assertive* na kuwasemea wananchi wake wanaodhulumiwa na raia wao.

Mheshimiwa Spika, pili, ni suala hili la jinsia katika ndoa na Mataifa tofauti. Pamoja na nchi yetu kuridhia mikataba inayopinga unyanyasaji wa kijinsia lakini hadi sasa kuna suala ambalo Wizara yako haijaliona, nalo ni lile la kuwapendelea wanaume zaidi kuliko wanawake. Inakuwaje mwanaume anapooa mwanamke wa nje akija naye nchini mara moja anapatiwa haki za uraia. Lakini mwanamke akiolewa na mwanaume asiye Mtanzania, wa nje, ye ye hana haki kwa mumewe kupewa uraia bali anafanyiwa kadhia nyingi. Nashauri jambo hili Waziri alichukue katika anga zako alivalie njuga kwani suala hili ni kero.

Mheshimiwa Spika, naomba kushauri jinsi gani Wizara ya mahusiano na nchi za nje. Ni wakati wa nchi kuishi kwa akili sana kama kweli mnataka Taifa hili liendelee kuwepo duniani, jihadharini sana na Mataifa yaliyoendelea ambao ni rafiki zetu kwa mazingira yaani tulipata kuwa marafiki kwa vile tu au walitutawala au tuliwasaidia kwa njia moja au nyingine kuimarisha uchumi huko kwao. Sisi Watanzania tunashindwa nini kuwa wajanja wa kutambua na kuchuja nchi zipi zina nia ya dhati ya kuwa na uhusiano usio wa kijanja wa kututumia tu, mfano, Marekani inatupa vyandarua wakati Cuba inajenga kiwanda cha kuua mazalia ya mbu. Hapo yupi ni bora? Tuchangamke kama kweli tunataka kuinua uchumi wetu na tubadilishe mwelekeo, sasa tuangalie na nchi za America ya Kusini ambazo sasa zina nia ya kujikomboa.

MHE. REGIA E. MTEMA: Mheshimiwa Spika, masharti ya upatikanaji wa *visa* kwa wananchi wa kawaida, ni kero kubwa hasa *US* na *UK*. Habari za kuangalia mishahara au kipato cha waombaji sio sahihi. Wananchi wengi sana wamekosa *visa* kwa sababu ya kigezo hiki. Hivi ni Watanzania wangapi wenye kipato cha zaidi ya Sh. 500,000 kwa mwezi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, fomu za kujaza *online* zina usumbufu mkubwa. Waombaji wengi huhangaika sana mpaka wapatikane watu ambao wanafanyabishara ya kuwajazia. Napendekeza Wizara izungumze na Balozi hizi ili kulegeza masharti.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya *CAG* ya 2010 imeonyesha kuwa Balozi zetu za Harare na Lusaka zilipelekewa fedha pungufu kutokana na gharama za kibenki. Napendekeza suala hili liangaliwe vizuri ili kuongeza ufanisi wa utendaji wa Balozi zetu.

Mheshimiwa Spika, kuna Balozi takriban kumi na mbili zimefanya matumizi ya fedha kinyume na kanuni za fedha. Naomba ufanuzi, tatizo hasa ni nini. Hili haliwezekani litoke kwenye Balozi zetu, *there must something wrong somewhere*.

Mheshimiwa Spika, Wizara iharakishe zoezi la uraia wa nchi mbili. Ni muhimu kabla ya 2015 nchi ikawa imekwishaingia kwenye suala hili. Pia Tanzania iangalie upya suala la *Diaspora*.

Suala la ndoa yaani mtu kuolewa au kuoa mtu wa nchi nyingine basi aruhusiwe kuwa raia wa hiyo nchi.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu safari za viongozi. Niliwahi kuuliza swalii ndani ya Bunge la tisa kuwa kwa nini misafara ya viongozi hasa Rais isipunguzwe ili kupunguza gharama. Kwani anasafiri na watu wengi sana kutokana na wadhifa wake. Aende mialiko ya *state visit* na mikutano mingine inayolazimisha Rais kuhudhuria yeye mwenyewe. Lakini awakilishwe na Waziri Mkuu, mingine na Waziri wa Mambo ya Nje na Waziri wa kisekta. Tuige mfano, mzuri wa Rais wa Rwanda, amekuwa na tabia ya kutuma wawakilishi katika mikutano anayoona haina tija ya moja kwa moja kwa wananchi wake. Nilijibwa zitapunguzwa, zipunguzwe sasa kwa vitendo na si kwa maneno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi pia kuuliza faida gani inapatikana kwa safari za viongozi? Mbona hatuoni mabadiliko yanayotokana na safari hizo. Inashangaza kuwa baada ya safari hizo tunapewa vyandarua kama matokeo ya safari hizo. Hivi kweli Tanzania tunahitaji vyandarua vya misaada? Tuna rasilimali za kutosha, tunaweza bila kutegemea misaada ya vitu vidogo vidogo kama vyandarua. Kuna propaganda kuwa safari za nje za viongozi zinasaidia katika kusamehewa madeni, lakini kwa mujibu wa CAG, deni la Taifa limeongezeka mno. Hali inayotisha kwani vizazi na vizazi vitaendelea kulipa madeni hayo bila hata kujua zilikuwa za nini, naona umaskini Tanzania umekithiri na unaongezeka kwa mujibu wa *House Hold Survey* ya 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uraia wa nchi mbili. Suala hili limechukua muda mrefu sana. Inasikitisha kwa Mawaziri wawili kупingana kwa kauli juu ya hoja hii. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje alisema mchakato ulikuwa unafanyika ili kuliwasilisha kwenye Baraza la Mawaziri na baadaye Serikali ya Zanzibar ili kulipitisha, kauli hii ilitolewa katika Bunge la 2010. Wakati Waziri wa Mambo ya Ndani aliyejita alipinga hadharani suala hilo la *dual citizenship* na kusema nchi ina mpango wa kuanzisha makazi ya kudumu (*permanent residency*). Serikali ituambie suala la *dual citizenship* limefika wapi? Watanzania wanaoishi nje wanasubiri Serikali inawaambia nini? Maana tunawahitaji Watanzania wenye uraia wa nchi nyingine kupata uraia wa nchi yetu pia kwa ajili ya ushiriki wao wa kuleta maendeleo ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *report* ya APRM. Kwa kuwa lengo la APRM ni nchi kujitathmini juu ya uimarishaji wa utawala bora. Bunge hili liliridhia nchi yetu iingie katika mpango huu wa APRM tangu Februari, 2005. Hivyo, jambo hilo liko kisheria na linatambulika. Je, kwa nini Bunge lisipewe fursa ya kujadili *report* za APRM kuhusu nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nashauri Balozi zetu ziboreshw, pesa zinazotumwa ni kidogo na haziendani na hali halisi ya maisha ya nchi husika. Kwa kuwa

pesa yetu inashuka thamani kila kukicha, wanapopelekewa fedha kutokana na *exchange rate* wanapata pesa ndogo zisizokidhi mahitaji yao. Tukiboresha balozi zetu zitafanya kazi iliyokusudiwa hasa za kidiplomasia ya uchumi ambayo ndiyo sera ya dunia nzima.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii nitoe mchango wangu wa maandishi kuhusu Wizara hii ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Naomba nichangie eneo la utendaji wa Ofisi ya Balozi zetu nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na hali ya kiuchumi ya nchi yetu napendekeza ufanisi wa Balozi zetu usipimwe kwa jambo lingine lolote isipokuwa tu kiwango cha uwekezaji toka nchi husika kuja Tanzania ndiyo kiwe kipimo cha ufanisi wa Balozi zetu. Kwa maana hiyo, Ofisi za Balozi zetu ni lazima ziwe na taarifa kuhusu *economic potential or investment potential* zote zilizopo Tanzania, halafu kujua fursa na kuelewa uwekezaji uliopo katika nchi husika ambao unaweza kufanywa nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo Balozi zetu zinapaswa kuzingatia ni kuainisha ujuzi maalum (*special skill*) katika maeneo mbalimbali ambayo ubalozi utaona kuwa *skills* hizo zinahitajika Tanzania, *then* Balozi zifanye *facilitation* kuhakikisha *transfer of knowledge or skills* kutoka nchi hizo kuja Tanzania inafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo Balozi zetu zipimwe ni kiwango cha kutafuta *employment opportunity* kwa vijana wetu katika nchi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo Balozi zetu inabidi zizingatie ni kuhakikisha kuwa *aggressively* zinatafuta masoko kwa ajili ya bidhaa zinazotengenezwa Tanzania ili kuongeza *export*. Hili litawenza kutendeka iwapo tu, Balozi zetu ziwe na orodha ya biashara zote zinazozalishwa nchini na ubora wake na faida zake na Balozi zifanye juhudhi za makusudi kutafuta wanunuzi wa bidhaa hizo katika nchi hizo. Kwa hiyo, ni muhimu sana kuwa na *Exports Officers* katika Balozi zetu ambao *focus* yao ni kutafuta masoko kwa ajili ya bidhaa zinazotengenezwa nchini Tanzania.

MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nchi nyingi duniani zilikumbwa na m dororo wa kiuchumi uliosababisa na kufilisika kwa mabenki makubwa ya Marekani ambayo yaliyumbisha uchumi wa Taifa la Marekani na kwa sasa tunashuhudia nchi za Ugiriki, Ureno, Uhispasia na kadhalika bado ziko katika m dororo huo wa kiuchumi. Kwa vile Tanzania siyo kisiwa, je, Wizara ina mkakati gani kuhamasisha makampuni makubwa ili yawekeze mitaji hapa nchini na hivyo kuweza kuuhami uchumi wetu kutokana na m dororo wa kiuchumi unaoendelea kuiathiri dunia. Naiomba Wizara itupatia mikakati iliyonayo na hasa wakati huu ambapo nchi yetu inakabiliwa na tatizo sugu la umeme. Tatizo la ukosefu wa umeme hatima yake litadhoofisha uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta zote hapa nchini zinategemea uwepo wa umeme wa uhakika. Wizara ina mpango gani kuziomba nchi rafiki zipate kuisaidia nchi yetu iondokane na adha hii inayoleta aibu kubwa kwa Serikali na chama chetu cha CCM?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inafuata Sera ya Diplomasia ya Kiuchumi, je, ni Ofisi ngapi za Kibalozi zinazowakilisha nchi yetu, nchi za nje zimeweza kuitekeleza kwa vitendo sera hii? Ofisi hizo zimevutia wawekezaji kutoka nchi zipi na zimesaidia kwa kiwango gani uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Ofisi za Kibalozi zinazowakilisha nchi yetu huko nje ambazo hazisaidii kuvutia wawekezaji, Serikali kuititia Wizara hii ina kauli gani. Kwa wale Mabalozi ambao wameshindwa kuiwakilisha vizuri nchi yetu vizuri, Serikali haioni kwamba Mabalozi hao ni mzigo kwa Taifa na hivyo wanastahili kurejeshwa nyumbani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika siku za karibuni, tumeshuhudia Mataifa yenye nguvu ya kuingilia mambo ya ndani ya nchi changa, Serikali yetu inatoa kauli gani kuhusu suala hili ambalo nahofia likiachwa liendelee laweza kuja kutufika hata sisi hapa Tanzania kutokana na kasumba mbaya inayoenezwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA). CHADEMA inawahimiza wananchi wadai mambo yao kwa njia ya maandamano, lakini Serikali kuna wakati inazuia waandamanaji kwa nguvu za Polisi na wakati mwingine kwenye maandamano kuna uwezekano wa watu kujeruhiwa na hivyo nchi yetu kuonekana kana kwamba inakiuka haki za binadamu. Je, Wizara ina kauli gani kuhusu jambo hili ambalo linahamasisha wananchi wavunje taratibu na hata pia kuvunja sheria za nchi kwa kisingizio cha demokrasia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imeshuhudia mikataba mibovu inayoingiwa kati ya Serikali yetu na makampuni ya kigeni, mfano katika sekta ya Madini, Gesi, Umeme, Uchukuzi, na kadhalika. Ni nini hasa nafasi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa katika mambo haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. HAMOUD A. JUMAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwangi wa rehema kwa kuniwezesha kuchangia Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ya mwaka 2011/2012. Aidha, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuandaa Bajeti hii kwa umakini mkubwa na ambayo imeainisha mipango mizuri ya kuendeleza ushirikiano baina ya nchi yetu na Mataifa mengine katika mambo muhimu kama biashara, usalama, haki za binadam, mazingira, sheria na mahusiano katika nyanja mbalimbali. Yote haya yanahakikisha Tanzania inapata fursa mbalimbali zinazoweza kuiweka Tanzania katika ramani ya dunia kiuchumi. Bajeti hii inazingatia Ilani ya Chama cha Mapinduzi ilivyodhamiria kuimarisha amani na mshikamano wa binadamu wote duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imejitahidi sana kuwa na Ofisi za Ubalozi katika nchi nyingi ambazo tuna mahusiano mazuri. Balozi hizo kwa kweli kama tunataka

zitekeleze majukumu yake ipasavyo Serikali ina wajibu wa kuziwekea mazingira mazuri ya kufanya kazi. Mazingira haya ni pamoja na Ofisi nzuri zenyenye hadhi sawa na Balozi za nchi nyingine na pia ziwe na vitendea kazi stahili. Mabalozi na maofisa wanaofanya kazi katika Ofisi za Balozi zetu wapewe maslahi mazuri kwa maana ya mishahara mizuri, nyumba nzuri zenyenye hadhi na usafiri. Kwa kufanya hivi Maofisa wa Ubalozi na familia zao hawatajiingiza katika shughuli za biashara na kudhalilisha Taifa letu. Ili kuwa na ufanisi nzuri katika Balozi hizo, nashauri pia maofisa wanaoteuliwa kufanya kazi katika Balozi zetu, wapewe mikataba ya miaka mitano tu na baada ya hapo wateuliwe wengine, hii itasaidia sana kuepuka maofisa watakaofanya kazi kwa mazoea na pia tutawajengea Watanzania wengi uwezo wa uelewa wa mambo ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mjadala wa kuwapa haki Watanzania kuwa na uraia wa nchi mbili. Hili ni jambo zuri na litasaidia sana kuwapa fursa Watanzania walioko nchi za nje kuchangia mawazo na hata ufanisi katika uchumi wetu, kuna nchi nyingi ambazo zinaruhusu wananchi wake kuwa raia wa nchi mbili, kwa kawaida uzalendo wa nchi aliyozaliwa mtu ni mkubwa kuliko nchi ya pili, hivyo, wamekuwa wakitumia mwanya huo kuangalia fursa za biashara na uwekezaji katika nchi zao. Kuna raia wa Tanzania walioolewa au kuoa raia wa nchi nyingine, katika suala hili kuna haki anayonyimwa mwanamke aliyeolewa na raia wa nchi za nje endapo mume wake ameamua kuishi hapa Tanzania na kuomba uraia hapewi au inachukua muda mrefu sana. Hivyo, mume huyu anatakiwa aingie hapa nchini na kuishi kwa kutumia *visa*. Tofauti yake, mwanamme aliyeoa raia wa nchi za nje anamleta mke wake anaishi naye na mwanamke huyu anapatiwa uraia kwa urahisi zaidi. Jambo hili liangaliwe vizuri na kuwapa wananchi wote fursa sawa kwa watakaooa na watakaolewa na raia wa nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi za Balozi zetu pamoja na kwamba zina majukumu ya kuhakikisha ushirikiano wa Kimataifa, lakini kuna jukumu moja ambalo kwa enzi hizi za utandawazi ni lazima waweze kulifanya na kutunza kumbukumbu za Watanzania wote wanaoingia katika nchi husika kwa sababu mbalimbali kama kusoma, kufanya kazi, wameolewa au wameoa wenyeji wa nchi hiyo. Kwa kuwa na kumbukumbu za raia hawa itasaidia sana si kujua idadi tu bali kuwatambua raia na kushirikiana nao katika mambo mengi ya ushauri, kuangalia jinsi watakavyosaidia kukuza uchumi wa nchi yetu kwa kuchangia mawazo mapato au kwa kutumia nafasi na nyadhifa zao kusaidia katika maendeleo ya jamii. Pamoja na hayo kwa kutambua raia na sehemu wanayoishi katika nchi hizo, inarahisisha Serikali kusaidia kuwaokoa endapo kwa bahati mbaya itatokea kutokuelewana kwa Mataifa haya mawili, majanga na hata vita katika nchi ile na kusababisha raia warudi Tanzania. Kama Balozi zetu hazitakuwa na *data* hii basi, lolote baya likitokea wananchi wengi wanaweza kuathirika kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Wizara hii kuwa na majukumu ya ushirikiano wa Kimataifa lakini Maofisa wa Balozi zetu wengi au hawana elimu ya mahusiano au wanafanya kazi kwa mazoea. Mara nyingi wananchi waliopata nafasi ya kutembelea nchi za nje, wamekuwa hawazungumzii vizuri ushirikiano wa maofisa hawa. Kwa mfano, mtu aliyepata nafasi ya kwenda nchi ya nje kama pamoja na shughuli iliyompeleka, atakuwa na nafasi kidogo na akatamani kwenda kutembelea Ofisi ya

Ubalozi wetu katika nchi ile, basi wanapofika maofisa wale hawawakaribishi vizuri wanapewa (*cold shaulder*) kwani kinachotokea wanatazamwa kwa dhana ya pengine wana matatizo. Haya yamekuwepo na yapo kwani ukifika tu unayemkuta wa kwanza ukimsalimia anakuuliza una shida gani? Hii inavunja moyo sana kuzitembelea Ofisi za Balozi zetu. Kama mwananchi amekwenda kule kutibiwa au ni mwanafunzi ndio kabisa hawana muda. Wananchi waliopata kufanyiwa hivyo, wanauliza, je, kazi za maofisa hawa ni nini kama siyo kuwakilisha Watanzania na Ofisi zile ni mali ya Watanzania, hivyo, tunapokuwa nje ya nchi unapata faraja ukitembelea Ubalozini na wao wakajua upo na endapo litatokea janga au tatizo lolote basi waweze kuwa na taarifa na kuona jinsi ya kusaidia au kuwakilisha hali ile huku nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Balozi zetu nyingi ambazo maofisa wake wangetumika kikamilifu kuitangaza nchi yetu kwa mambo mazuri ya asili ambayo nchi yetu imejaaliwa kuwa nayo kama utalii, fursa katika uwekezaji na biashara, utamaduni wetu na mengineyo mengi. Napenda kumpongeza Balozi Mwanaidi Majaar aliyekuwa Balozi wa Tanzania, Uingereza na sasa ni Balozi wa Tanzania Marekani, kwa kweli amefanya kazi nzuri kuitangaza Tanzania katika nchi ya Uingereza na sasa hivi anajitahidi sana katika nchi ya Marekani. Kama Wizara inatoa tuzo kwa mfanyakazi bora basi huyu anastahili hiyo tuzo. Ila napenda kuishauri Wizara hii ijpange na kuweka Bajeti ya kila Balozi kutenga siku ya maonesho ya kuitangaza Tanzania na fursa zilizopo. Balozi hizo zialike wananchi na makampuni ya Tanzania kupeleka bidhaa zinazozalishwa hapa nchini, mazao yetu, utalii na utamaduni wetu ili kuweza kuwavutia wananchi wa nchi ile kuona na kushawishika kutembelea au kuwekeza katika nchi yetu. Hatua hizo zitaongeza kuchangia pato la Taifa na ushirikiano wa vitendo wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. DESDERIUS J.OHN MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Umoja wa Mataifa hausaidii sana katika migogoro inayotokea Afrika kama vile mauaji ya Kimbali ya Rwanda na Burundi. Umoja wa Mataifa haujasaidia kabisa kutengamaa kwa uongozi katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Leo ndugu zetu wa Libya wanaauawa kinyama tena kwa uchokozi wa wazi, Umoja wa Mataifa uko kimya na wanachokifanya ni ukoloni mamboleo tu. Migogoro ya Palestina, migogoro yote inayotokea katika nchi za kiarabu ni kutokana na mikono ya mabeberu hawa. Dunia tufanye nini sasa labda basi wanyonge wote duniani tuungane tupate Umoja wetu na tuunde chombo chenye nguvu cha kupigania haki zetu wanyonge duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Somalia kwa mfano, ni wao kwa namna moja au nyinigne wameweza kuhakikisha Somalia ina kuwa na matatizo yasiyokwisha. Afrika lazima tusimame na wanyonge wenzetu duniani kupanga kama Mandela na wenzake katika kupigania uhuru wetu wa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuamue tuungane. Tatizo la Libya na tatizo la Ethiopia ni matatizo yetu tuamue katika kulinda maslahi ya Afrika na wanyonge wote duniani.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa namna nzuri alivyowasilisha Hotuba yake kwa umahiri mkubwa. Kwa mantiki hiyo basi naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Kama ilivyo ada inaeleweka kwamba nguvu ya Taifa lolote kisiasa, kiuchumi na kiulinzi inategema sana sera ya nje ya Taifa husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwani maendeleo ya Taifa lolote duniani yanategemea sana jinsi na namna linavyoshirikiana na Mataifa mbalimbali kupitia mikataba ya Kimataifa na Jumuiya mbalimbali za Kikanda na zile za kiulmwengu. Tanzania kama Taifa huru na linaloinukia kiuchumi duniani linahitaji ushirikiano wa Kimataifa na ndiyo maana msisitizo mkubwa umewekwa katika Diplomasia ya kiuchumi. Kazi hii ndiyo kazi inayopaswa kutekelezwa na Balozi zetu ulimwenguni kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wake Serikali yetu tunaiomba iongeze Bajeti kila mwaka kuziwezesha Balozi zetu duniani kote. Nchi yetu inapiga hatua katika kushirikiana na Mataifa mengine yaliyopiga hatua mbalimbali na ndiyo maana tunashuhudia Mataifa mbalimbali ulimwenguni yaktaka kushirikiana nasi na ndiyo maana tumekuwa tukishuhudia wawekezaji na wafanyabishara wakubwa wakitiririka kuja kuwekeza nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza mambo mazuri ambayo yanatendwa na Serikali yetu tunauona umuhimu wa kuiunga mkono Bajeti ya Wizara hii kwa nguvu zetu zote. Ushiriki wa nchi yetu katika kusuluhisha migogoro mbalimbali na kuwatetea wale wote wanaoonewa duniani hauna kifani. Uungwaji mkono wa Watanzania wenzetu katika kuwania nafasi mbalimbali katika Taasisi za Kimataifa ni ishara nyingine ya kufanikiwa kwa sera ya mambo ya nje na ushirikiano wa Kimataifa kwa Taifa la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ushiriki wa Watanzania wenzetu walioko nje ya nchi ni jambo la muhimu sana tumeshuhudia ulimwenguni jinsi raia wa Mataifa mengi duniani wakitumia ujuzi na utaalam wanaopata kutoka Mataifa yaliyofanikiwa kiteknolojia na mifano ipo. Mfano, raia wa nchi ya China walivyoweza kupata teknolojia ya masuala ya anga kutoka nchini Marekani, kwa kifupi njia zinazotumika katika kupata teknolojia hapa duniani ni pamoja na kuinua au kuiiba kwa mtindo wa kijasusi *Espionage* na hii haiwezekani bila kutumia pesa, sasa Serikali ifikirie kuwekeza katika kutafuta teknolojia kwa kuipatia fedha zaidi Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa dunia hii inatawaliwa kwa ama maridhiano na mashirikiano au kwa vita hivyo ni vizuri Balozi zetu ziendelee kukusanya taarifa za kiusalama kuhusiana na mienendo mibaya inayoweza kuwa inaendeshwa na Mataifa jirani na ya mbali ili kuisadia Serikali kuwa tayari kivita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. SALEH A. PAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Napenda kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Balozi

zetu na watumishi wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya na hongereni kwa Hotuba nzuri. Hotuba hii imejaa maelezo ya kina kuhusu *overview* ya hali ya kisiasa duniani, Barani Afrika na nchini. Nasema Hotuba hii ni darasa kwetu (*lecture*) kuhusu mambo ya Kimataifa. Nchi yetu ina heshima kubwa Kimataifa kwa jitihada za Mheshimiwa Dokta Jakaya Kikwete katika *International Forum*. Mfano wa yeze kuwa Mwenyekiti Mwenza wa Tume kuhusu Afya ya Mama na Watoto. Jitihada za Mheshimiwa Rais katika masuala ya kiuchumi kwa kuleta *World Economic Forum* nchini mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ushiriki wetu katika kulinda amani Darfur. Mafanikio ya kuweza kupata misaada hasa toka Norway hasa baada ya *kupresent paper* kuhusu *The Southern Agriculture Growth Corridor of Tanzania (SAGCOT)*. Haya ni mafanikio makubwa katika kuendeleza Kilimo Kwanza. Tanzania tumekuwemo katika mchakato mzima wa kuleta amani *Southern Sudan*. Tatizo hili lilikuwa limedumu kwa zaidi ya miaka 50, *Great Achievement*. Tunaikaribisha *Southern* Sudani kama Taifa la 54 kwenye Africa Union na Jumuiya ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misaada ya Umoja wa Mataifa (*United Nation Development Assistance Plan*), tuweke mkakati wa kufaidika na *Programme* hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *COMESA, SADC* na *EAC Intergration*. Hili ni suala zuri litakalosaidia kufikia lengo la kuunganisha Afrika. Soko litapanuka kwa nchi 27. Balozi zetu zilizoko katika nchi hizo zitasaidia katika kukuza biashara baina ya nchi hizo. La msingi zaidi, ni kukuza uwekezaji ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *International Atomic Energy Agency*, nimefurahishwa na taarifa hii kwamba nchi yetu itagombea na *Inshallah* itaingia *IAEA*. Hii ni fursa nzuri kwa Tanzania kujifunza na kufaidika na chombo hiki, kwa vile Tanzania hivi karibuni itaanza kuchimba Urani huko Namtumbo (*Selous*). Wizara ijithadi katika Jumuiya za Kimataifa (*UNESCO*) ileze nia njema ya Tanzania katika kujikwamua kiuchumi, tusiachie Wizara ya Nishati na Madini na Maliasili pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *APRM Mechanism*. Hili ni suala jema kwa nchi yetu katika kujipima. Mchakato huu umeanza siku nyingi lakini tumechelewa sana. Tuharakishe ili *Rating* ifanyike ili kujijengea *confidence* ya Kimataifa. Wizara iwe karibu na *APRM* Tanzania ili yale yaliyotokea (ubadhirifu na kadhalika) yasitokee tena. *Have a watchful Eye on this* ili kazi ziende kwa mpango wa utekelezaji bila vikwazo. Ongezeni watumishi na vitendea kazi kwa timu ya *APRM* Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *AICC* inafanya kazi nzuri. Waungeni mkono katika jitihada zao za kujiimarisha kibiashara. Wapatieni *Joint Venture Partners* haraka ili kuweza ku-*capture* masoko ya mikutano duniani. Jumuiya ya Afrika Mashariki inakua na Arusha ndiyo makao Makuu. Hii miradi hii isichukue muda mrefu sana kukamilika. *All the Best* katika kutekeleza Bajeti yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Mabalozi wetu nchi za nje wapewe kitengo maalum cha kuitangaza Tanzania hasa utalii, fursa za kuwekeza na masoko huko nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Passport* za Tanzania zidhibitiwe kwa vile zinaheshimika sana duniani ndiyo sababu hata China imeanza kubaini watu wanaoghushi *Passport* za Tanzania na kuanza kutoa mashaka. Hii ni hatari kwa usalama na kulinda heshima ya nchi yetu. Wizara hii isaidie kwa karibu sana na Wizara ya mambo ya ndani kudhibiti uhamiaji haramu na uhamiaji holela ndani ya nchi yetu. Mfano, pia ni Mikoa na Wilaya zilizo mpakani kama ilivyo Wilaya ya Serengeti, kuna wahamiaji wengi toka Kenya ambao wamevamia Wilaya ya Serengeti tangu mwaka 1950's. Hadi leo hii uhamiaji holela na haramu unaendelea kwa kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvamiaji wa *NATO* kwa Libya utazamwe upya na umoja wa Afrika na kuweka msimamo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inayoruhusu mwanamke au mwanaume anayeolewa/oa na/au kuwa mtu asiye Mtanzania ni ya kibaguzi. Sheria hii inaruhusu mwanaume wa kitanzania anapooa mke ambaye sio raia, kupewa uraia *automatically* bila usumbufu wowote, lakini mwanamke wa Kitanzania anapoolewa na raia wa nje, anaporudi nchini, mume wake anatakiwa kuishi kwa kutumia *visa*. Kwanini sheria hii inabagua uraia wake hasa katika haki zao za msingi za kuchagua wenza wao wanaowapenda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida za mwanamke kuwa na mume asiye raia ni nyingi hasa anapopewa uraia wa Tanzania maana mama ndiye mlezi wa watoto na hivyo watoto wale watalelewa katika maadili ya Kitanzania na hivyo kutunza mila na desturi pamoja na utamaduni wetu. Lakini mume anapoona mwanamke ambaye sio Mtanzania, mama huyo atafundisha watoto wake *culture* ya huko alikotoka, na hii maana yake ni kuendelea kumomonyoka kwa maadili au kupoteza utamaduni wa Mtanzania. Suala hili nashauri litazamwe kwa umakini mkubwa ili kuweza kutoa haki sawa kwa raia wote wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wakimbizi ni suala nyeti, na sina nia ya kuwakataa wakimbizi nchini. Agizo lililotolewa na TAMISEMI kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani kwamba wakimbizi wote walipo wanatakiwa kusambazwa katika Mikoa yote ya Tanzania, linatia wasiwasi. Wakimbizi wengi wanaoingia nchini imethibitika kwamba wengi wao sio waadilifu, sasa kitendo cha kuwasambaza nchi nzima, maana yake ni kusambaza uhalifu nchi nzima. Pamoja na huruma ambayo nchi yetu imekuwa nayo kwa miaka mingi, lakini kwa jambo hili nachelea kusema kwamba huruma isizidi uwezo ili mwisho wa siku Taifa lisije kuanza kulia na kujiona wao ndio

wakimbizi katika nchi yao wenyewe. Wakimbizi hawa ni vizuri wakatengewa eneo lao maalum la peke yao ili waweze kuwa *monitored* kuliko wakisambazwa nchi nzima ambapo watajichanganya na raia na kueneza tamaduni zao ambazo nyingine hazina maadili mema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuishauri Serikali kuandaa utaratibu wa raia wote Tanzania waishio nje ya nchi kupiga kura. Hii itawapa Watanzania hawa kutumia haki yao ya kidemokrasia ya kuchangia viongozi hao (hasa Rais) wanaowapenda. Utaratibu huu uandaliwe kwa uchaguzi wa Rais peke yake ili kuondoa *complications* katika nafasi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na usumbufu na urasimu mkubwa sana katika utoaji wa visa za Uingereza na Marekani katika Balozi zao hapa nchini. Pamoja na *visa* hizo kutolewa kwa gharama kubwa, utaratibu wa kuzipata unakatisha tamaa. Unapotafuta *visa* hizi, ni lazima kwanza maombi yatumwe Nairobi – Kenya na baadaye majibu yarudi hapa Tanzania. Wakati huo mtu anakuwa ameshalipia. Je, kubwa ni majibu, maana yanaweza kurudi kwamba hupati *visa*, au maombi yamechelewa, na Ili upate *visa* hizo unahitaji uwe umeomba kwa muda usiopungua miezi mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati mwingine mtu anaweza kupata mwaliko wa muda mfupi na hivyo muda wa ku-*apply visa* wa miezi mitatu unaweza kuwa kikwazo kwake na kukosa *opportunity* ya mwaliko amba mara nyingi unaweza kuwa ni kwa faida ya nchi pia. Naishauri Serikali iangalie Balozi hizi, kwani zinanyanya Watanzania. Hata kama suala ni umaskini wetu, lakini hii isiwe sababu, maana wao wanapoomba *visa* za nchi yetu wanatetemekewa na kupewa upesi sana, nao wafanye hivyo kama taratibu za kidiplomasia zinavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Wizara iongeze jitihada za kiplomasia na kiuchumi (*economic diplomacy*) ili makundi yanayojihuisha na uharamia baharini (*piracy*) yapewe shughuli mbadala za kiuchumi ili waachane na kujihuisha na uharamia. Mataifa makubwa yaongeze misaada ya elimu ili wataalam Somalia wapatikane na kutuma raslimali za nchi hiyo kuwaletaa maendeleo ya nchi yao kwa kuimarisha Serikali ya mpito. Pia nchi ya *Puntland* ishirikishwe katika uongozi wa Serikali ya mpito Somalia. Hatimaye uongozi utakaochaguliwa kidemokrasia ulete maendeleo endelevu, amani na utulivu pia itapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, meli zinapotekwa na maharamia wa Kisomali kuna taarifa kuwa baadhi ya wapokeaji wa malipo (*ransom*) hulipwa Nairobi na baadhi ya makampuni yaliyosajiliwa Kenya ndiyo huwa ya kati (*facilitators*) baina ya walipaji na walipwaji. Hivi Serikali ya Kenya haiwezi kuwahoji hawa wahusika ili kujua wale wanaofadhili uharamia kuwakamata na kuwafikisha kwenye vyombo vyya sheria ili adhabu kali itolewe na iwe fundisho kwa wengine? Kupitia Wizara hii hili linaweza kujadiliwa, na jirani zetu wa Kenya au ni manufaa na faida kwa baadhi ya watu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za uharamia zinanunua na kuwekezwa katika ununuzi wa majumba ya fahari – Mombasa, Kenya ili kusafisha hizo fedha (*money laundering*). Je, Mheshimiwa Waziri, kuna taratibu zozote za kisheria zinazoweza kutumika ili kuwahoji wanunuzi hao ambao hawawezi kueleza jinsi walivyopata hizo fedha nyingi kununulia nyumba hizo? Bila kutumia sheria na taratibu za kidiplomasia, uharamia ni vigumu kuuangamiza. Uchumi wa nchi zetu utazidi kuathirika. Hatua za makusudi zichukuliwe.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia hoja ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Wizara hii ni nyeti, ndiyo kioo cha Tanzania nchi za nje, na ni Wizara muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naipongeza Serikali ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada yake kubwa na muhimu kuendeleza mahusiano na nchi mbalimbali na kuwapa imani kubwa nchi mbalimbali kuendelea kuweka mahusiano na Tanzania, kuendelea kutupa misaada mbalimbali na kuendeleza sifa nzuri ya nchi yetu. Pia kutokana na hiyo sifa, Watanzania mbalimbali wameendelea kupata nyadhifa mbalimbali muhimu katika nafasi za kimataifa, mfano mmoja ukiwa ni Mheshimiwa Asha-Rose Migiro - Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (*UN*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali yetu, ili kuinua uchumi wetu wa Tanzania, ni muhimu mabalozi wetu katika nchi zote pia wapate mafunzo mbalimbali kuhusu uchumi, elimu, utamaduni, utalii na afya. Kwanza wangepata elimu kuhusu nchi yetu, wajue vizuri katika nyanja mbalimbali, fursa zilizopo hapa nchini kwetu katika sekta ya utalii, kilimo, mifugo, afya, biashara mbalimbali; wakijua nchi yetu, wataweza kuiuza kibiashara, kuongeza utalii nchini, kutupatia masoko ya mazao yetu ya kilimo, mifugo na uvuvi. Pia Tanzania inaagiza takriban kila kitu kutoka nje, wangeweza kutupatia bei elekezi ya bidhaa mbalimbali ili wafanyabishara wa kitanzania wapate unaafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Ubalozi wetu katika nchi mbalimbali Wizara iangalie teknolojia mbalimbali ambazo tunaweza kutumia hapa nchini hasa katika nchi zinazoendelea kama Tanzania. Wakiona mambo mazuri wanapowakilisha nchi yetu, basi wajitahidi hayo mazuri tuyapate na sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Nje pia inaweza kuwa sehemu muhimu ya kutoa matangazo na kuisaidia kutafuta misaada mbalimbali ya kijamii kwa ajili ya nchi yetu. Misaada mingi hutolewa na taasisi mbalimbali na mara nyingi hawajui matatizo yaliyopo Tanzania. *NGO*'s zetu zingepata (*exposure*) mawasiliano na taasisi zinatoa misaada tungenufaika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba Serikali inapoteua mabalozi na wafanyakazi katika ubalozi zetu, wapate mafunzo maalum ya kiuchumi na namna ya

kuitangaza nchi yetu, namna ya kutafuta wawekezaji kutafuta misaada kutoka taasisi mbalimbali, kutafuta masoko kwa ajili ya mazao yetu ya kilimo, maliasili, uvuvi na kutangaza utalii mbalimbali wa ndani ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iangalie na kusaidia vyuo vyetu hapa nchini ambavyo wanafundisha masomo ya *International Relations*, Diplomasia na masomo ambayo wanafunzi hao wanategemea kufanya kazi Wizara ya Mambo ya Nje waboreshewe mitaala na nyenzo ya kupata mafunzo yawepo. Leo hii Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*), wanafunzi wa *International Relations* hawafundishwi lugha mbalimbali, hata Kiingereza kwa wanafunzi ni shida. Kifaransa kinafundishwa hatua ya digrii, wale ambao hawajapata kujifunza huko awali basi hawawezi kuendelea. Ni muhimu Watanzania waandaliwe vizuri katika *International Relations* na Diplomasia ili wapate ajira katika taasisi za kimataifa kwa wingi na huko mbele ya safari wataweza kuisaidia nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naendelea kuipongeza Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kazi nzuri wanayoendelea kufanya na kuiweka Tanzania katika ramani ya dunia.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwasilisha kwako mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya ofisi yake kwa mwaka 2011/2012 kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Bernard C. Membe – Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa uwasilishaji wake mzuri wenye weledi wa hali ya juu kabisa. Pili, nampongeza kwa imani, uvumilivu na moyo wa kujitolea sana kiutendaji. Huu ni mfano wa kuigwa kwa maana hachoki na amekuwa mstari wa mbele katika kulitetea Taifa letu ndani na nje ya nchi. Lakini siachi kumpongeza Naibu Waziri - Mheshimiwa Mahadhi kwa uwezo mkubwa aliuonyesha kwa kipindi kifupi tu ambacho ameingia katika Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sote tunavyofahamu, Wizara hii ni kioo na roho ya uchumi wa nchi yetu katika nyanja za kitaifa. Hivyo, majukumu yake ni mazito na yanahitaji umakini mkubwa sana katika utekelezaji. Ni kheri tuwaunge mkono na kusaidiana nao katika kuboresha na kuondoa mapungufu yanayojitokeza kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba nikushukuru kwa kunipokelea maoni yangu kwa kuamini kuwa yatafanyiwa kazi stahiki. Nakutakia kila la kheri. Namwomba Mungu atulinde sote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani za dhati zimfikie Mheshimiwa Bernard Kamilius Membe - Waziri wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Pia shukrani nyingine nazitoa kwa Mheshimiwa Mahadhi Juma Maalim - Naibu Waziri wa mambo ya Nje na Ushirikano wa

Kimataifa. Shukrani za dhati pia ziwaendee Watendaji Wakuu wa Wizara hii kwa kuandaa bajeti ya Wizara husika kwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia bajeti ya Wizara husika, mchango utakuwa kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, nataka kufahamu kama ile sera yetu ya nchi za nje ya siasa ya kutofungamana na upande wowote bado ina mantiki yoyote katika siasa za dunia ya sasa. Kama bado Tanzania ni mwanachama wa nchi zisizofungamana na upande wowote: Je, nchi yetu inanufaika vipi na siasa hizo? Je, sera hiyo bado inahitajika katika nchi yetu katika kipindi hiki ambacho hakuna vita baridi? Kama inahitajika, ni kwa nini? Kama haihitajiki, kwanini tuendelee kujitambulisha kuwa sera yetu ni ya Tanzania ya kutofungamana na upande wowote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vile vile kuhoji juu ya hadhi/heshima ya nchi yetu kimataifa. Enzi za Mwalimu J.K. Nyerere akiwa madarakani, nchi yetu ya Tanzania ilijijengea heshima na hadhi kubwa sana katika siasa na sera mbalimbali kimataifa. Nataka kufahamishwa kama heshima na hadhi ya Tanzania kuhusu msimamo, siasa na sera mbalimbali kimataifa imepanda chati au imeshuka chati. Kama imepanda chati, ni kwa vigezo vipi? Kama imeshuka chati, ni kwanini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuhoji juu ya suala hili, kwa nini Bara la Afrika halina kura ya *VETO* katika Baraza kuu la Umoja wa Mataifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ninalopenda kuongelea ni juu ya Balozi zetu katika nchi za nje. Binafsi, naomba nifahamishwe ni nchi ngapi ambazo Tanzania ina Balozi katika nchi hizo? Nchi ngapi ambazo Tanzania ina Balozi katika hizo? Nchi hizo ni zippi? Pia ni kwanini baadhi ya nchi hatuna Balozi hizo anayetuwalishi? Pia ni nchi ngapi na zippi zilizo na Balozi hapa nchini? Kwa nini baadhi ya nchi kama zile *Thailand* hazina uwakilishi wowote hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo vibaya vile vile nikitaka kufahamishwa juu ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika. Katika kuusemea umoja huu wa nchi za kiafrika, nataka kufahamishwa juu ya msimamo wa umoja huu kuhusu vita vinavyoendelea huko Libya. Je, kwa nini umoja huu umeshindwa kuwa huru? Je, Tanzania ina msimamo gani juu ya uvamizi wa majeshi ya *NATO* dhidi ya Gaddafi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri zaidi tukapata ufanuzi zaidi, ni kwa jinsi gani Tanzania inapoamua kuijunga na ushirikiano wowote ule wa kikanda, ni vigezo vipi tunatumia. Pia ni vigezo vipi tunatumia kujitoa katika ushirikiano huo wa kikanda? Je, Tanzania imepata faida zippi katika ushirikiano wa kikanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba pia kufahamishwa hadhi ya lugha ya Kiswahili kimataifa. Je, Kiswahili ni lugha rasmi katika Umoja wa Mataifa? Kama hapana, ni kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema inayoniwezesha kupata fursa ya kuchangia hotuba hii kimaandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Waheshimiwa Mabalozi wote na Watendaji wote wa Wizara kwa mafanikio yaliyopatikana katika kutekekeza mpango wa kazi wa mwaka 2011/2012 na kuzidi kuimarika kwa mahusiano ya baina yetu na nchi za nje ambao umeleta manufaa katika nyanja mbalimbali za uchumi, kisiasa, kielimu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajielekeza katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya maduhuli yanayotokana na *visa* kutoka kwenye Balozi zetu zinabakia kwa asilimia 100 kwenye Balozi hizo kwa ajili ya kutumia. Hii ni kinyume cha matakwa ya *article 135* ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1997 na kifungu cha II cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2001 (*as revised in 2004*) vifungu tajwa hapo juu inataka makusanyo yote ya mapato yapelekwe Mfuko Mkuu (*consolidated fund*) ndipo zipangiwe matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba Wizara ya Fedha na Uchumi iachiwe mamlaka ya kusimamia na kudhibiti makusanyo hayo yanayotokana na *visa* na pia kubadilisha kiwango cha kubakiza maduhuli katika Balozi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubakiza maduhuli kwa asilimia 100 kwenye Balozi zetu zinasababisha matumizi ya ziada ambayo hayakuidhishwa na Bunge. Kwa mujibu wa ripoti ya *CAG* ya mwaka 2009/2010, Balozi zifuatazo zilifanya matumizi ya zaidi ya kiwango kilichoinidhishwa na Bunge kama ifuatavyo:-

JINA LA UBALOZI	KIASI
(i) <i>Tanzania Embassy – Kinshansa</i>	Sh. 177,079,048/=
(ii) <i>Tanzania High Commission – London</i>	“ 832,815,497/=
(iii) <i>Tanzania Embassy – Moscow</i>	“ 533,129,381/=
(iv) <i>Tanzania Embassy Stockloim</i>	“ 177,891,747/=
(v) <i>Tanzania Embassy – Beijing</i>	“ 209,611,023/=
(vi) <i>Tanzania Embassy – Tokyo</i>	“ 282,738,520/=
(vii) <i>Tanzania Embassy – Abu Dhabi</i>	“ 865,057,652/=

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kwamba utaratibu wa kubakiza maduhuli unavunja Katiba na Sheria za Fedha na unachangia matumizi mabaya ya mapato ya Serikali. Naomba Wizara kwenye majumuisho yake, itoe maelezo yanayojitosheleza na izielekeze mara moja Balozi zake kutoendelea kuvunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1997 *article 135*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kuwa la Wizara wakati inapeleka pesa za matumizi (*exchequer issues*) kutozingatia *exchange rate* kwenye nchi ambazo tumefungua Balozi. Pesa hizo zinapelekewa kwa kutumia Tanzania shilingi, lakini kwa mfano pesa zinapelekwa Ubalozi wa Tanzania, *Washington* kwa kutumia Shilingi ya Kitanzania, lakini wakati Taasisi za Fedha (mabenki) zinapeleka pesa hizo itazibadilisha kwa pesa ya kigeni ya nchi husika (*US Dollar*) madhara yake kutockana na kuporomoka kwa thamani ya shilingi, pesa zinazopatikana zinakuwa kidogo sana na hazikidhi mahitaji ya Balozi zetu. Hatima yake Balozi zetu zinakuwa na madeni, hivyo kuzivunjia hadhi ya kidiplomasia. Naiomba Serikali kupitia Wizara hii kuzingatia thamani ya shilingi wakati wa kutuma pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mahusiano ya Mataifa ya nje na msimamo wa Tanzania juu ya vita kati ya Serikali na waasi nchini Libya, nasononeshwa sana na namna nchi za Magharibi zinavyoingilia masuala ya ndani ya Libya kwa kigezo cha kulinda raia. Huu ni uonevu, kwani imethibitika kuwa ni waasi ndio wanaopambana na Serikali ya Libya. Mataifa ya nje hasa ya *NATO* Uingereza, Marekani haipaswi kuwachagulia kiongozi Taifa la Libya. Naomba Serikali itoe tamko kali la kulaani mapigano yanayoendelea nchini Libya na kukemea mataifa ya nje yaache kutumia nguvu ya ziada kuishambulia Libya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. SULEIMAN NASSIB OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, kashfa ya rada imetia aibu sana nchi yetu, ndani na nje ya nchi. Inafaa watuhumiwa wote washtakiwe kwa kupelekwa Mahakamani. Pia Serikali ichukue hatua thabiti ili dola za kimarekani milioni 29.5 zilizoko *BAE* zirejeshwe nchini kwa haraka kama inavyowezekana. Pesa hizi zisipelekwe kwa *NGO* lakini ziende Hazina ya Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna malalamiko ya muda mrefu kuwa Wanzanzibar hawapati nafasi ya kuajiriwa katika Wizara. Kuna Wazanzibar kidogo sana waliomo katika Wizara. Hivyo, tunaitaka Wizara iwe wazi zaidi katika uajiri. Kadhalika lazima Zanzibar ipewe nafasi maalum katika ajira. Hili litangazwe rasmi katika vyombo vyote vya habari. Mfano mzuri ni Wizara ya Ulinzi ambayo huajiri idadi maalum ya Wazanzibar katika kila ajira inayofanyika.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata majibu ya Kampuni ya *M/S General Business and Equipment Supplies* ya mjini Itigi waliodhulumiwa *Trucks* mbili na *trailer* na wanajeshi wa Serikali ya Rwanda, walipora magari hayo. Mahakama zote mbili ya Rwanda na Tanzania ziliwapa haki kampuni hii wafidiwe. Mpaka leo Wizara hii imeshindwa kutoa ufumbuzi wa tatizo hili ambalo ni la kidiplomasia kwa mujibu wa barua Kumb. Na. J/A.130/43/117 ya tarehe 3/1/2007 ya Wizara ya Sheria na Katiba. Rejea barua yangu Kumb.Na. OJMM/IT/JAS/2 ya tarehe 6/3/2010 kwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni diplomasia gani ya uchumi Wizara hii inaendesha wakati inadharau wawekezaji wa ndani kama *General Business and Equipments Co. Ltd.*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona wakulima wetu wanashindwa kupata masoko ya biadhaa zao nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Balozi wa Rwanda ni kwanini hashughulikii tatizo la kampuni ya *General Bussiness and Supplies* kama Waziri yuko *too busy*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue* ya Libya ni *fiasco* kwa AU na Tanzania. Gaddafi anasulubiwa tu kwa sababu ya mafuta, ndege ya *Lockerbe* na advocacy yake ya *African Unity*. Mataifa makubwa hayapendi kuona Afrika moja, yanapenda viraka vya nchi, Afrika ili iendelee kupata maslahi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza chombo cha usalama na ulinzi cha AU kipeleke kikosi kitakachoundwa na askari wachache kutoka kila nchi wanachama wa AU kiende kuisadia Serikali halali ya Libya. *NATO* haitaweza kuadhibu nchi zote za Afrika.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu unajikita katika Afrika Mashariki. Kumekuwa na kudhalilishwa sana Watanzania hasa Kenya, ukiwa na gari na kuanzia mpakani unasumbuliwa na kukamatiwa gari hata kama imeingia kihalali, lazima wahitaji rushwa. Mtanzania ukiwa Kenya, unakamatwa na kuombwa kitambulisho na hata kama una *passport*, lazima wahitaji rushwa. Je, haya matatizo ya kusumbuliwa wananchi yatakwisha lini? Je, watu wengine wanaokuja Tanzania, mkifanya kama wao, kutakuwa na Afrika Mashariki? Nataka majibu. Kumekuwepo na unyanyasaji wa wafungwa, watu wanafungwa na kusumbuliwa sana Magereza. Wafanya biashara wanaokwenda Nairobi, wanasumbuliwa sana kwa kunyanyaswa na Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

MHE. ANNE K. MALECELÀ: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kusema kwamba naunga mkono hoja. Nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake na Katibu Mkuu kwa jinsi wanavyojitahidi kulijengea Taifa letu heshima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyojitahidi kuwa na mahusiano mazuri na Mataifa mengine bila ya kujali udogo na ukubwa wa Taifa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nionyeshe masikitiko yangu ya dhati kwa Mataifa makubwa ambayo yanaingilia mambo na utawala wa ndani wa nchi ndogo na hata kusogea zaidi na kujaribu kushiriki kuwaondoa viongozi wa nchi hizo au Mataifa hayo madogo. Naseme kwa dhati kwamba Tanzania tusiunge mkono tabia hii ya Mataifa makubwa, tuonyeshe wazi hata kama tutanyimwa misaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utafiti wangu wa uhakika, nimegundua kwanza wafanyakazi wetu wa Balozi zetu wanapata matatizo sana, mishahara yao inachelewa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuishi nchi za njie kama huna pesa ni sawa na kutafuta kifo, kwani kule nje hakuna cha mjomba wala shangazi. Naomba Serikali ijitahidi kujali mishahara ya wafanyakazi wetu wa Tanzania, waipate kwa wakati, kwani wanadhalilika sana na wanapata shida sana. Serikali itoe kauli kuhusu suala la mishahara kwenye Balozi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kumpongeza Waziri kwa jinsi alivyo imara kuwadhibiti watu wowote wanaowakilisha nchi nyingine hapa nchini kwetu, pale anapoona wanaingilia mambo ya ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema wenzetu wanapopata matatizo (nchi za Kiafrika) tukatumia matatizo yao kama funzo kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia kwenye maeneo matatu. Diplomasia ya uchumi, uraia wa nchi mbili na hali mbovu ya Balozi za Tanzania katika nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishi katika dunia ya utandawazi. Wengine wanaiita dunia ya “Utandawizi” kusisitiza kutamalaki kwa ubeberu mamboleo ambao unaendelea kutawala uchumi wa dunia kwa kunufaika zaidi kutokana na shughuli zote za kibiashara zinazoendelea hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hali hii, Tanzania na nchi nyingine za Afrika zinapaswa kutumia kila njia ili kunufaika kiuchumi na utandawazi mamboleo. Kwa kuwa dunia ya leo ni ya ushindani mkubwa, Balozi zetu katika nchi za njie lazima zijipange upya katika juhudhi za kutafuta masoko kwa ajili ya bidhaa za Tanzania, kuitangaza Tanzania kiatalii na kutafuta wawekezaji katika maeneo mbalimbali ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Balozi zetu zinapaswa kusaidiana na Usalama Taifa ili kufanya Ujasusi wa kiuchumi. Ujasusi huu uhusu makampuni yapi yanafaa kuwekeza nchini kwetu, yapi hayafai, na kadhalika. Balozi zetu zisaidie pia kuishauri Serikali mikataba ipi ya kibiashara inafaa na ipi haifai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na jukumu hili, tunahitaji wanadiplomasia weledi, mahiri na Wazalendo ili kuhakikisha nchi yetu haipotezi fursa za kibiashara na aina nyingine za ushirikiano. Tunahitaji wanadiplomasia wenye upeo wa kutosha kuhusu utandawazi, ni nini na fursa zilizopo na wenye uelekevu, ujasiri na uthubutu katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nini kifanyike? Napendekeza kwamba Serikali iteue Mabalozi na Maafisa wao kwa misingi ya ujuzi na sifa zao, na siyo kwa sababu za kisiasa au urafiki; Mabalozi na Maafisa wa Balozi wapewe mafunzo maalum ya diplomasia ya uchumi na hasa ujasusi wa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uraia wa nchi mbili ni muhimu, siyo kwa kutoa haki kwa wahusika tu, bali pia kwa sababu za kuvutia uwekezaji nchini. Mimi binafsi naunga mkono uraia wa nchi mbili, hasa kwa watoto (waliozaliwa nchi za nje) wake/waume (ambao ni raia wa nchi nyingine) wa Watanzania. Kuwapa uraia watu hawa kutawapunguzia wahusika gharama za kuwepo hapa nchini usumbufu unaoambatana na kutokuwa raia, na kutoa fursa kwa wahusika washiriki katika shughuli za kiraia. Serikali isisite kuhusu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, lazima tuchukue hadhari za kiusalama kwa kutotoa uraia kiholela kwa yeoyote anayetaka. Lazima kuwe na vigezo na katika nchi nyingine ni pamoja na kuweza kusema lugha ya Taifa kwa ufasaha, ambayo kwetu ni Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majengo ya Balozi nyingi ni mabovu na yanaonyesha uchakavu wa kutisha. Serikali ichukue hatua haraka ili kutatua tatizo hili ili aibu hii iondoke. Kama fedha haitoshi, Serikali itafute fedha na kila mwaka ihakikishe inakarabati Balozi zisizopungua 10 ili hatimaye Balozi zetu ziwe na hadhi inayostahiki. Naomba Waziri aeleze, jambo hili litaanza kushughulikiwa lini?

MHE. AMOS G. MAKALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pamoja na jitihada za Wizara na Taasisi nyingine kuwashirikisha Watanzania walioko ughaibuni, bado kuna malalamiko ya Watanzania hao kuhusu mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna urasimu wa mamlaka za Mapato na Bandari katika kushughulikia mzigo wanaoleta Tanzania kama misaada na zana za kilimo, elimu na vifaa vya afya kiasi kwamba urasimu huo unasababisha misaada hiyo kutokufika kwa wakati na wakati mwininge kushindwa kuzikomboa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ucheleweshaji wa leseni, usajili wa kampuni kwa Watanzania waishio nje wanaotaka kufungua au kufanya biashara kupitia fursa mbalimbali zilizopo katika nchi wanazoishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo Watanzania ambao wameshamaliza masomo katika nchi mbalimbali na wanapotuma maombi, kigezo cha kuwa nje ya nchi kinawafanya wasifikiriwe katika ajira za hapa nchini.

MHE. WARIDE BAKARI JABU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kuwasilisha hotuba yake vizuri. Pia napenda kumpongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa ufanyaji kazi wao mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru nchi yangu ya Tanzania kwa kushiriki kikamilifu katika shughuli za Jumuiya ya Afrika, Jumuiya ya Madola pamoja na ushirikiano mzuri wa diplomasia duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja kwanza kwenye suala la Ofisi za Balozi nje ya Tanzania. Pamoja na kuwa na Balozi nyingi za Tanzania nje ya nchi mbalimbali, lakini kuna tatizo kubwa kwamba Balozi hizo hazipo katika hali nzuri ya hadhi za kimataifa na ofisi hizi ndizo uso wetu wa kutangaza diplomasia ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la misafara ya viongozi wa nchi wanapotembelea nje ziwe zinazingatia uwiano na upande wa pili wa Muungano. Kwani misafara hii haiwashirikishi Wajumbe kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar na pia Wabunge wanaoshiriki ni wachache, lakini aghalabu Wabunge wa kutoka Zanzibar huwa hawamo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Wizara iangalie uwezekano wa kuongeza Maafisa kutoka Zanzibar katika Wizara na hata Ofisi zake za kibalozi kwani utakuta Balozi nyingi hazina vijana kutoka Zanzibar. Hivyo, naiomba Wizara ifikirie kuajiri vijana kutoka Zanzibar ili nao wapate kushiriki katika shughuli za kidiplomasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara ifikirie uwiano wa uteuzi wa nafasi za Mabalozi kutoka Zanzibar na Tanzania Bara. Hivi sasa nafasi tatu za Mabalozi wamestaafu. Hivyo, nashauri Balozi hizi zirejeshwe Zanzibar na pia ziongeze nafasi nyingine. Ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuipongeza Wizara kuanzia Waziri mpaka Watendaji wake kwa hotuba nzuri ya Bajeti ya mwaka 2011/2012. Naomba niwapongeze tena kwa kazi nzuri mnazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri suala la uraia wa nchi mbili linangojewa kwa hamu. Je, kwanini limekawia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa ushindi wa kupata fedha za rada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Libya inaonewa, utaratibu wa *OAU* kuisaidia umefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutafuta masoko nje kwa bidhaa zetu za Tanzania ni kazi muhimu sana. Tunaomba muongeze msisitizo na kasi. Huu ndiyo ukombozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni moja kati ya nchi ambazo zimedhamiria kushiriki katika kuleta amani Afrika na duniani kwa ujumla. Moja kati ya maeneo ambayo wanajeshi wetu wamepelekwa kwa madhumuni ya kulinda amani ni Lebanon na Darfur, Sudan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko toka kwa vijana wetu wanaipa heshima nchi yetu na kuhatarisha maisha yao. Vijana hawa wanalamika kwamba yapata miezi sita hawajalipwa mishahara, wakiulizwa wakuu wao waliokuwa nao kwenye *operation* wanawaambia kwamba *UN* hakuna pesa. Wakati huo huo kuna wanajeshi wa JWTZ wanafanya kazi ya *Observers* nchini Lebanon na Darfur wanalipwa kila mwisho wa mwezi dola 2000. Wanachohoji kama *UN* haina pesa, hizo zinapatikana wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanalamika pia wamelazimishwa kufunguliwa *account CRDB* ambapo pesa zao zinafanyiwa biashara na kwamba kila askari anatakiwa kulipwa na *UN* dola 5000 kwa mwezi lakini cha ajabu wanalipwa dola 800 tu kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, askari hao pia wamekuwa wakilalamika makato mbalimbali wanayokatwa kwa kisingizio kwamba wanaandaa askari kwenda kulinda amani Darfur na kwamba waliamua kuwa dola 257 zikatwe kwa muda wa mwaka mmoja kisha waendelee kulipwa. Walengwa ambao ni walinzi wa amani Lebanon, cha ajabu hazijarejeshwa na hazijulikani zinakwenda kwenye akaunti gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walinzi wa amani Darfur wapo chini ya Umoja wa Afrika (*AU*) na walinzi wa amani Lebanon wapo chini ya Umoja wa Mataifa (*UN*). Sasa iweje pesa hizo ziendelee kukatwa kutoka kwenye mishahara ya walinzi wa Lebanon?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo wanajeshi wetu wanaona hawatendewi haki ni kuhusu pesa ya chakula. Pesa hizo hulipwa kwa kila mwajeshi akiwa kwenye mafunzo, masomo, *operation* za nje au ndani ya nchi. Cha kushangaza pesa hizo walinzi wa amani hawazipati. Wakiuliza kwa nini wakatwe pesa zao wakati Serikali imeshatoa pesa hizo, wanaambiwa kwamba pesa hizo zinaingia kwenye mfuko wa *Chief of Stuff*. Wakihoji zaidi wanaambiwa kwamba watasitishwa kuendelea na zoezi la kulinda amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate majibu ya kina kuhusiana na malalamiko ya vijana wetu hasa ikizingatiwa kwamba mpaka sasa vijana wetu hali zao ni mbaya sana! Malalamiko yameshapelekwa Makao Makuu ya Jeshi, kwa Waziri wa Ulinzi na kwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, lakini hakuna hatua yoyote iliyo chukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda mrefu sasa Watanzania tunasubiri kuona nchi yetu inajiunga na *OIC*, Jumuiya ambayo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iliwahi kujiunga na ikatakiwa ijitoe kwa sababu hilo lilipaswa kufanywa na Tanzania. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilijitoa kwa kupisha Tanzania kujiunga. Mpaka leo bado nchi yetu hajijiunga na kupoteza misaada ya kiuchumi ambapo Jumuiya inatoa. Nchi ya Msumbiji na Uganda ni wanachama wa *OIC* na wao wanapata misaada mingi ya kiuchumi kutoka Jumuiya hii, je, Serikali yetu itajiunga lini na *OIC*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi zetu za Ubalozi zilizoko nchi za nje ukiangalia kitabu cha pili kinachohusiana na Matumizi ya Serikali zote isipokuwa Ubalozi ulioko Addis Ababa, Cairo, Washington, Harare na Lilongwe wamepewa fedha za ziada kwa mwaka 2011/2012 ukilinganisha na mwaka 2010/2011. Balozi hizo tano zimepewa fedha pungufu mwaka 2011/2012 ukilinganisha na mwaka 2010/2011. Limefanyika hilo wakati maisha yanaendelea kupanda. Kwa nini limetokea hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Ukanda wa Bahari ya Hindi wa Afrika ya Mashariki unakabiliwa na uharamia wa wananchi wa Somalia. Nadhani *AU* na *UNO* kwa pamoja wakae ili waangalie uwezekano wa kuanzishwa jeshi la wanamaji (*NAVY*) ili walinde ukanda huo, imani yangu kama jeshi hilo litakuwa na vifaa vya kutosha vya baharini basi uharamia utapungua au utamalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa hotuba ya Waziri ukurasa wa 37 aya ya 73(b) Wizara hii pia hutangaza utajiri mkubwa wa vivutio vya utalii. Ninachopenda kufahamu jukumu hili Wizara inalitekeleza vipi? Kwani tatizo moja la ukuaji wa utalii katika nchi yetu ni kuwa utangazaji huko nje ni mdogo kuliko nchi moja jirani hapa Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jukumu hili ninataka kujua Wizara imetangaza vipi utalii kwa mwaka 2010/2011 na imejipanga vipi kutangaza utalii kwa mwaka 2011/2012. Ahsante.

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kutoa shukrani za dhati kutohana na mashirikiano ya uongozi ulioandaa hotuba hii ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kujua katika Wizara yako idadi ya Mabalensi katika nchi za nje, pia kati ya mabalensi hao ni wangapi wanatoka sehemu moja ya Muungano yaani Zanzibar?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ushirikiano wa Kimataifa, mimi naingia Bunge hili swalii la Ushirikiano wa Kimataifa halijajitokeza. Lakini kwa suala hili lilijitokeza kwa njia ambayo haieleweki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zetu zinaenda na Katiba, leo tunaenda na kusema suala la Ushirikiano wa Kimataifa halimo katika Katiba. Kwa nini suala la ushirikiano

liingizwe kwenye Muungano wakati chombo kikuu ambacho Katiba hamna katika Muungano. Kuna haja gani ya kulazimisha suala hili kwamba lazima liwe la Muungano. Kuliingiza suala hili bila ya kuwa ndani ya Katiba hatuoni ni kukiuka taratibu husika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Libya. Umoja wa Afrika umefikia wakati Afrika kuungana kwa kijeshi ili kuhakikisha tatizo linalojitokeza katika nchi yoyote ya Afrika ni tatizo la Afrika nzima. Hakuna sababu vita hivi vya Libya vinaenda mwezi wa nne na hakuna ufumbuzi uliopatikana ila kufariki kwa ndugu zetu huko Libya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu Nyerere alisema kujitawala Tanzania haimaanishi imejitawala, ila Afrika nzima iwe imejitawala. Umoja wa Afrika haujawa na imani ya dhati kuhusu suala la Libya. Nchi za Afrika kila moja inalinda maslahi yake ili nchi za Ulaya wasijehasimiana na kukosa misaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wa Libya alitaka nchi za Afrika ziungane na nchi kama mbili zilikuwa tayari nchi zilizosalia hazikuwa tayari ili kila mmoja kulinda maslahi binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Afrika haikuungana zikiwa pamoja nchi za Magharibi siku zote zitazichezea nchi za Afrika kwa kila nchi ya Afrika ambayo inaonyesha nia ya kufanikiwa kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uraia wa nchi mbili si suala la maslahi kwa Tanzania, leo unasema upige kura wakati sehemu huishi ilhali una uraia tu mwananchi awe na uraia wa nchi moja tu.

MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kwa maandishi katika Wizara hii ya Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikupongeze kwa mchango mkubwa sana unaoutoa katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 17 katika kitabu chako ulieleza kwamba kuna askari wetu katika nchi ya Darfur ambao wameungana na wanajeshi wengine kwa kulinda amani wa Umoja wa Mataifa. Je, ni askari wangapi ambao wanatumikia Umoja wa Mataifa ambao ni Watanzania na ni muda gani watakuwa huko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 29 kipengele cha 55 kuwa Watanzania wanaoishi katika nchi hizo hawapatwi na madhara yoyote na ukasema Watanzania 83 kutoka Misri na nane kutoka Libya. Watanzania wangapi ambao wamebakia nchini Libya? Kwa Watanzania hasa Wazanzibar wengi wao wanaishi Libya.

Kuhusu Balozi zetu za nje, katika ukurasa wa 32 kifungu 61 umeeleza kuwa Wizara ina jumla ya watumishi 440 kati ya watumishi hao 240 wapo Makao Makuu. Watumishi 19 wapo ofisi ya Mambo ya Nje Zanzibar na 172 wako katika Balozi zetu za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, katika Balozi za nje hukusema Bara wangapi na Zanzibar wapo wangapi na kifungu 62. Mafunzo kwa watumishi ni wangapi watumishi kutoka Zanzibar ambao nao wamepelekwa mafunzoni iwe ya muda mrefu au muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho katika fursa ya uwekezaji na vivutio vya utalii wetu Tanzania, nikisema Tanzania nina maana na Zanzibar. Mheshimiwa Waziri je, unaitangazaje Zanzibar na vivutio vya utalii na uwekezaji? Ahsante, naomba kuwasilisha.

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa makini na kuwashirikisha Watanzania waliopo ughaibuni tunaweza kukusanya mapato makubwa kutokana na kundi hili muhimu. Leo Kenya kwa miezi hii ya mwanzo yaani Januari – Mei, 2011 Kenya wamefanya makusanyo ya karibuni dola milioni 334.7; je, kwa miezi saba iliyobaki inawezekana Wakenya wakarudisha karibuni dola milioni 700.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nigeria kwa mwaka 2004 peke yake wanatarajija kurudisha fedha kwao na kutoa mchango kwa Taifa hilo karibuni dola za Marekani bilioni 6 - 8. Je, Tanzania tumejipanga vipi kwa hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakenya wanaoishi nje ya Kenya walipeleka *open petition* kwa viongozi wao akiwamo Rais Mwai Kibaki, Waziri Mkuu Raila Odinga na Spika wa Bunge pamoja na Mawaziri. Walichoomba kutoka kwao Kenya ni pamoja kutambuliwa kwao katika mchango wa teknolojia, kiuchumi na kiutamaduni, hivyo Tanzania tumejipangaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha lingine ni kuona baadhi ya nyumba za Mabalozi wetu walioko nje ya nchi zikiwa na madeni kwa kutowalipa kwa wakati wapangishaji mfano mzuri wa Malaysia. Tunaomba Serikali iwe makini kulipia pango ili tusichafue heshima ya Mabalozi wetu waliopo nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabalozi wote wapangwe kiuchumi ili waisaidie nchi yetu mfano mzuri kwamba Balozi zetu zote zaidi huwa zina *consider* utalii. Nashauri Balozi zetu zifanye kazi za kiuchumi na kimaendeleo kulingana na maeneo yao mfano Malaysia awe anashughulikia Kilimo, *IT*, biashara na wawekezaji walio imara na makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu iwe na *co-ordination* baina ya *chamber of commerce, foreign office* na Mabalozi. Tukifanya hivyo tutasaidia kupata wawekezaji walio wazuri na sio *bogus investors* tupime maeneo yetu ya ardhi yenye madini na tuwape wamiliki wa ardhi au maeneo hayo elimu kuitia ma-*geologist* na kujua ni aina gani ya madini yaliyomo ardhini, hapo tutaweza kuwapa fursa wawekezaji wasio wajanja wanaokuja na kupora rasilimali zetu. *Information is power, but what is more powerful is the use of information.* Hivyo tuwape taarifa kamili wamiliki wa ardhi zenye madini ili wawe na elimu Walau *preliminary report* itakayowasaidia katika mfumo wa *win-win situation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu Zanzibar katika nafasi yake ya Muungano kwenye hii Wizara. Ni lini Wazanzibar watapata nafasi zaidi katika Balozi zetu pamoja na maofisa mbalimbali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuepukane na kundi la wazamiaji hatuna budi kuwapatia kazi vijana mbalimbali wanaosomea ubaharia kwa kushirikiana na makampuni ya meli duniani. Mfano mzuri ni nchi ya Phillipines na vijana wake wengi hupata ajira katika meli mbalimbali duniani. Hivyo tukajifunze ili kupunguza wazamiaji na wakati huo huo tutatoa ajira halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Mabalozi wa USA Balozi Sefue, wa UK Balozi Kalaghe na Balozi Sisco wa Malaysia. Sitowasahau Mabalozi wa Kenya na Zambia, nao ni wachapakazi kama hao niliowataja kabla yao. Mabalozi hawa wana sifa zote na ni wachapakazi mahodari wanaokumbana na changamoto mbalimbali za kuendesha ofisi zao kutokana na Bajeti ndogo wanazopangiwa tuisahau *Diaspora*, tuendelee kuchachamaa na kuwatumia Mabalozi wetu kwa mambo yote mawili yaani kisiasa na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza shukrani, kwa nini fedha za Maendeleo za Bajeti ya mwaka 2010/2011 ni sawa na ya mwaka 2011/2012 mbona *OC* na nyingine wameongezewa. Ahsante.

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Bernard Kamilius Membe, Waziri wa Mambo ya Nje na Uhusiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Mahadhi Juma Maalim, Naibu Waziri, Bwana John Michael Haule, Katibu Mkuu kwa kuteuliwa kuongoza Wizara hii muhimu sana.

Pia nawapongeza Wakurugenzi na Mabalozi wetu wakiwemo Mabalozi wadogo kwa kazi nzuri wanayofanya kuliwakilisha Taifa letu kikamilifu. Zaidi sana napenda nikiri kuwa kuongezeka kwa idadi ya wawekezaji toka nje imetokana na kazi nzuri inayofanywa na wawakilishi, wakishirikiana na viongozi na watendaji wa sekta husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia Bajeti ya Wizara nimeona kuwa zipo kasma zilizopunguziwa gawio hivyo kuhitaji maelezo kwani huweza kuathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Maeneo husika ni yafuatayo:-

(a) Kifungu 1001- Kasma 210100 - mishahara imepungua kutoka shilingi 611,689,500 hadi shilingi 556,171,000. Je, kilichosababisha kupungua ni nini?

(b) Kifungu 1007 – Kasma 210100 – mishahara imepungua kutoka shilingi 117,370,000 hadi shilingi 96,138,000. Naomba maelezo tafadhali.

(c) Kifungu 1009 - Kasama 210300 – posho imeongezeka kutoka shilingi 9,000,000 mwaka 2010/2011 hadi shilingi 57,250,000. Ongezeko hili ni kubwa sana hivyo naomba maelezo juu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya majengo ya Ofisi za Ubalozi, mapema mwaka 2010 nilitembelea Ofisi ya Ubalozi wa Tanzania Geneva Uswisi. Hali ya jengo na samani za ofisi hiyo hairidhishi na haiwakilishi hadhi ya Taifa letu ipasavyo. Nashauri kuwa Serikali ikarabati ofisi hiyo pamoja na nyingine na kuweka samani bora zaidi.

Vilevile mwezi Aprili mwaka huu nilikwenda Nairobi kuhudhuria Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Makazi. Nashukuru kuwa ofisi yetu ya Ubalozi ilitoa Afisa aliyetupokea na kutuhudumia mimi na ujumbe wangu hadi siku ya mwisho. Hata hivyo nilisikitika kuona ofisi hiyo haina magari, yaliyopo yamechakaa hivyo nashauri kuwa ofisi hiyo ipewe fedha za kununua magari.

Kuhusu hadhi ya Balozi zetu, mwezi Machi 2011 nilikwenda Istanbul, Uturuki kushiriki Mkutano wa Kimataifa wa Maendelo ya Makazi. Mimi na ujumbe wangu tulipata mapokezi mazuri sana toka kwa wenyeji wetu pamoja na Balozi mdogo wa Tanzania nchini Uturuki. Naomba kukiri kuwa ofisi hiyo imejizatiti viliyo kuliwakilisha Taifa letu na kulinda maslahi yake. Naomba Waziri wa Mambo ya Nje ampongeze Balozi mdogo wa Tanzania nchini Istanbul kwa kazi nzuri anayofanya ya kushawishi wawekezaji na wafanyabiashara kuja kuwekeza Tanzania.

Kwa kuzingatia kasi ya ukuaji wa biashara baina ya Tanzania na Uturuki nashauri kuwa hadhi ya Ubalozi mdogo ulioko Istanbul ipandishwe kuwa Balozi kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano Mkuu wa *UN Habitat 2016*; Mkutano mkuu wa Pili wa *Habitat* utafanyika mwaka 2016. Tunashauri kuwa Serikali ya Tanzania kuititia Ubalozi wetu New York na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi iombe mkutano huo ufanyike nchini Tanzania. Mkutano huo utafungua fursa nyingi za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uteuzi wa Mabalozni nilipotembelea Nairobi mwezi Aprili 2011 nilibaini kuwa nafasi ya Balozi wa Tanzania nchini Kenya imekuwa wazi muda mrefu. Hali hiyo huathiri utekelezaji wa majukumu muhimu ya ofisi hiyo kwani yapo maamuzi ambayo Kaimu Balozi hawezi kuyafanya. Nashauri kuwa hatua zichukuliwe kujaza nafasi zote za mabalozni zilizo wazi ili kufanya ofisi hizo zitekeleze majukumu yao kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uraia wa nchi mbili, naipongeza sana Wizara na wadau wengine kwa kutambua umuhimu wa uraia wa nchi mbili kwa maendeleo ya Taifa letu na kuchukua hatua zifaazo. Nashauri suala hili liharakishwe isipokuwa kwamba hatuna budi kuwa makini tusije tukafungua milango ya uraia wa Taifa letu kwa maharamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuzuia uharamia Bahari ya Hindi, napongeza juhudzi zinazochukuliwa na Serikali kushirikiana na wanachama wa *Inter-Governmental Committee on Shipping (ISCOS)* kutafuta utatuzi wa kero ya maharamia wa Kisomali

kwa njia ya amani. Naamini kuwa kitendo cha kualika Puntland na Serikali ya muda ya Somalia kushiriki shughuli za kamati hiyo (*ISCOS*) kutasaidia kupata utatuzi wa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha na naunga mkono hoja.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Maafisa wote wa Wizara walioshiriki katika maandalizi ya hotuba ya Bajeti ya Wizara hii kwa kuandaa hotuba hii vizuri na kuiwasilisha vizuri hapa Bungeni. Pamoja na pongozi hizo napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya uraia wa nchi mbili (*dual citizenship*). Suala hili limekuwa likzungumzwa sana siku za nyuma na hata katika Bajeti ya mwisho (2010/2011) ya Bunge la Tisa lilizungumzwa sana. Nakumbuka Mheshimiwa Membe Waziri wa Mambo ya Nje aliahidi kuendelea kulifanyia kazi suala hili. Mbali ya kuzungumzia namna ya kuwashirikisha Watanzania wanaoishi ughaibuni (*Diaspora*) katika masuala mbalimbali hususani masuala ya kiuchumi, nashauri mchakato wa uraia wa nchi mbili uharakishwe. Nasema hivyo, kwa sababu suala hili limechukuwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *African Peer Review Mechanism (APRM)* au mchakato wa kujitathmini kwa utawala bora Barani Afrika ni chombo muhimu katika kuendeleza na kudumisha utawala bora Barani Afrika. Ili chombo hicho kiwe na nguvu zaidi ni bora kijengewe uwezo wa rasilimali watu na rasilimali fedha. Aidha, kwa sababu chombo hiki kinahusika na utawala bora nashauri watu wanaokuwa katika chombo hicho wawe na uadilifu wa kutosha. Nashauri pia kwamba nchi zote ambazo zitapatikana kuwa na utawala mbaya basi zikaripiwe au zipewe onyo na Umoja wa Afrika (AU) ili ziheshimu na kufuata misingi ya utawala bora.

Kuhusu vurugu zinazoendelea katika nchi mbalimbali, vurugu za kisiasa zinazoendelea katika maeneo mbalimbali Barani Afrika na katika baadhi ya nchi za Kiarabu ni kielelezo tosha cha ukosefu wa utawala bora. Ukiufatilia sana utaona kwamba vurugu zinatokea katika nchi ambazo viongozi wake wamehodhi madaraka au katika nchi za Kifalme. Kwa mfano Rais wa Misri alikaa madarakani karibu miaka 30, Gadaffi wa Libya amekaa miaka 42, Tunisia zaidi ya miaka 25. Katika hali kama hiyo tunategemea nini. Viongozi wa nchi hizo wanapoanza kukataliwa wanaona kama wananchi wanafanya fujo, jambo ambalo si kweli. Gadaffi, Al Asadi wa Syria na kadhalika wanatumia nguvu kubwa sana kukabiliana na nguvu ya umma.

Kwa maoni yangu, viongozi kama hao wamepoteza uhalali wa kutawala, hawana aibu tena mbele ya wananchi wao wanaowaongoza.

Naomba nishauri kama ifuatavyo, kwa nchi ya Libya pamoja na ukweli kwamba *NATO* imefanya makosa kuishambulia Libya kutoka angani, lakini pia Gadaffi nae amepoteza haiba ya kuongoza, maana anatumia nguvu kubwa kukabiliana na waasi. Katika kufanya hivyo wananchi wengi wasio na hatia wameendelea kuuawa (kufa).

Gadafi anastahili kutengwa na Umoja wa Afrika (*AU*). Aidha, Wizara hii imshauri Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa ili viongozi wote wa nchi ambazo ni wanachama wa Umoja huo na wanaendelea kung'ang'ania madaraka hali wanakataliwa na wananchi, basi watengwe. Demokrasia kama msingi muhimu sana wa utawala bora ipewe nafasi ni vizuri watawala wanaong'ang'ania madaraka pasipo ridhaa ya wananchi waelewe na wafahamishwe kwamba sauti ya watu ni sauti ya Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu diplomasia ya kiuchumi, nchi yetu itafaidikia zaidi kama tutaimarisha zaidi Balozi zetu nje ya nchi. Balozi zetu lazima zitafute wawekezaji wenye tija katika nchi yetu, watangaze kwa nguvu sana fursa za utalii ambazo zinapatikana katika nchi yetu. Aidha, Balozi zetu katika nchi ambako tuna ofisi za Ubalozi. Nashauri pia tukafanya ujasusi wa kiuchumi, kuiba teknolojia nzuri ambayo inaweza kusaidia kuinua uchumi wetu siyo jambo baya, nashauri tuliwekee mkakati mzuri. Nashauri pia tufungue ofisi zaidi za Ubalozi katika maeneo/nchi mbalimbali duniani zenye uchumi mzuri, zenye fursa za kibiashara na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuona kwamba nchi ya Somalia haina Serikali kwa karibu miaka 22 sasa. Katika kipindi chote hicho nchi hiyo imetawaliwa na mapigano ya koo ambayo yamesababisha wananchi wengi kupoteza maisha na wengine kuikimbia nchi yao. Kwa ujumla maisha nchini Somalia ni mabaya pengine kuliko hata maisha ya gerezani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua hivi *AU* pamoja na Umoja wa Mataifa wameshindwa kurejesha amani nchini humo? Hawa Al-Shabaab wana nguvu gani za kushinda *AV* na *UN* kwa maoni yangu naona kama hakuna nia ya dhati! Hivi nchi karibu 54 za Afrika zikiungana zitashindwa kuwaangamiza Al-Shabaab kweli? Naomba nia ya dhati iwepo. Mungu awaangalie raia wa Somalia wanaoendelea kuteseka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha na naunga mkono.

MHE. HAMAD ALI HAMAD: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nchi ya Libya ni mwanachama wa Umoja wa Afrika na kwa kuwa ilivamiwa na nchi za Magharibi na *NATO* na kwa kuwa tangu uvamizi huo kwa Libya, Umoja wa Afrika ulikaa kimya na haukusema chochote kama vile haukuathirika wala kuhuzunishwa kwa uvamizi huo uliofanywa dhidi ya mwanachama wao. Je, ni kwa nini umoja huu ulikaa kimya? Na haioni kwamba ukimya huu wa Umoja wa Afrika anaweza kuwa chanzo cha kujiiondoa kwa baadhi ya nchi wanachama kwa kukosekana kwa mapenzi na mashirikiano mema baina ya nchi wanachama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasemekana kwamba majeshi yetu yanaposhiriki katika vita vyta kusaidia kuzikomboa nchi nyingine zenye vita baina yao, hulipwa kwa fedha za Tanzania ilhali wenzao wanalipwa fedha za kigeni, naomba mtuambie je, ni kwa nini na je, huku si kuwadhalilisha wanajeshi wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina Mabalozi wangapi nchi za nje na kati ya hao ni wangapi ambao wametoka Zanzibar?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Balozi yetu nchini Malaysia inadaiza deni la nyumba kwa kipindi cha miezi sita sasa, jambo hili ni aibu kwa Tanzania, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze ni kwa nini tunafikia kuingia katika aibu hii kudaiwa kwa Balozi zetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia Waziri alieleze Bunge lako ni kwa nini hadi leo hii, Tanzania katika suala la kupiga kura bado haijaona umuhimu kwa Watanzania walioko nje ya nchi, kutengenezewa utaratibu wao nao kuchagua Rais wao katika chaguzi za hapa nchini, wakati Serikali yetu ni shahidi kwamba raia wa nchi nyingine waliopo hapa Tanzania, wakati wa chaguzi za nchi zao na wao huandaliwa mazingira mazuri ya kupiga kura za kuchagua viongozi wao hapa hapa walipo Tanzania. Je, ni lini Tanzania nasi tutafanya hivyo ili kuonesha kulinda haki za kidemokrasia kwa kila raia wetu bila kujali yuko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara kwa kazi nzuri wanazofanya na kwa hotuba nzuri ya Bajeti ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kuendelea kuwa mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*) na pia *SADC*. Licha ya *EAC* kuendelea kukua kwa kuongezeka kwa nchi za Rwanda na Burundi na uwezekano wa kuendelea kuongezeka kwa Sudan ya Kusini na Somalia, kuna mkakati gani wa kisheria unaoendelea kuiruhusu nchi yetu kuwa mwanachama ndani ya Jumuiya zaidi ya moja. Watanzania wanaendelea kusubiri ushauri na mwelekeo wetu na hatma ya suala hilo. Hivyo tunaomba kusikia kauli ya Serikali kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nchi ya Kenya kuendelea kuwa wagumu kuachia Watanzania na Waganda kufanya biashara ndani ya Kenya kwa uhuru, wakati tunaendelea kupiga hatua chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*) kuwa masoko huria kwa nchi wanachama bado Kenya inaonekana na kuendelea kulalamikiwa na wafanyabiashara wa Tanzania na hata Uganda (*Business Times* la tarehe 20/7/2011) kuwa wagumu kuwapa nafasi huru kwa wafanyabiashara wa nchi jirani kuingia na kufanya biashara kwa uhuru. Mara nyingi hufanyiwa vitisho na au kuachia Wakenya kusimamia biashara zao nchini Kenya. Pamoja na kwamba hali hii inatakiwa kuratibiwa na Wizara ya Viwanda na Biashara bado uwakilishi wa nchi katika nchi za nje unapaswa kuratibiwa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwekezaji wa shamba la Mpira Kihuhwi - Muheza aliywatoroka wafanyakazi, Wizara ya Viwanda na Biashara iliwasilisha katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa maombi ya kusaidia kumtafuta mwekezaji *Menchentile Rubber*, iliyokuwa inaendesha kwa mkataba shamba la Mpira (*Kihuhwi Rubber Plantation – Muheza*) ambayo ni kampuni iliyotoka Kenya kwa kutoroka kabla kutekeleza amri halali ya Mahakama ya Tanzania kumtaka kulipa mafao ya wafanyakazi wa shamba aliloingia mkataba wa kuliendesha. Wananchi wanaendelea

kusubiri kauli wananchi msaada wa Wizara hii baada ya kushirikishwa na Wizara ya Viwanda na Biashara mwaka uliopita 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kusaidia kutafuta mwekezaji kujenga kiwanda cha kusindika Matunda Wilayani Muheza, kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitoa ahadi ya kusaidia Muheza kupata mwekezaji katika sekta ya usindikaji pamoja na jitihada zinazoendelea kufanyika naomba rasmi Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa sasa kusaidia kutafuta mwekezaji. Tufuatilie pia jitihada zifuatazo;

(i) Kauli ya Mheshimiwa Rita Mlaki, Bungeni alipokuwa akichangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu 2011/2012, kuwa yupo mwekezaji nchini Kenya na angependa kuwekeza Tanzania kwa ujenzi wa Kiwanda cha Juisi.

(ii) Jitihada nilizofanya nilipotembelea Italy mwaka 2009/2010 eneo lenye mashamba makubwa ya machungwa Cecilia ambapo Kiongozi Mkuu wa Taasisi ya Casa Famiglia Rosetta Association (*NGO*) Father Vicenzo Source alionyesha nia ya kuwekeza Tanzania basi Wizara na Ubalozi wetu unaosimamia uwakilishi wetu Italy usaidie kuendelea kufuatilia *NGO* hivyo kuwashawishi kuwekeza Tanzania. Simu zake ni *mobile* (+39) 335 7208936 na *phone* (+39) (0) 934 508326.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio yangu kwamba tutashirikiana kuisaidia nchi yetu Tanzania. Naunga mkono hoja.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Nje inapaswa kutueleza ni nani aliandaanu mkataba wa kununua rada pamoja na nani aliyesaini mkataba wa ununuzi wa rada kwa niaba ya Tanzania, ili tujue ni nani aliyeiliingiza Taifa katika hasara na kujidhalilisha mbele ya Taifa la Uingereza ambako ndiyo nchi rada iliponunuliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali kupitia Wizara yake ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa itueleze imejifunza nini kutokana na migogoro inayoendelea katika nchi za Libya, Yemen, Syria, Misri, Tunisia na Malawi kwa sasa. Je, Serikali imojiandaaje kukabiliana na hali hiyo ili isitokee nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hati isiyoridhisha toka kwa baadhi ya Balozi zetu toka kwa CAG kwa mwaka wa fedha 2008/2009 na 2009/2010, katika ripoti za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) imoonyesha kuwa kuna baadhi ya Balozi zetu zilipata Hati Zisizoridhisha (*Qualified Report*) kutokana na matumizi mabovu ya fedha za Serikali ilizopewa. Je, Wizara sasa inaweza kutueleza ni hatua gani wamechukua kwa Balozi hizo zinazoiwakilisha nchi maana hiyo inatafsiri mbaya kwa wananchi kuwa na wawakilishi wenyewe matumizi mabovu ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu (*SW*) kwa neema na rehema zake nyingi anazonijalia ikiwa ni pamoja na kunipa afya na uwezo wa kuandika machache ambayo ni mchango wangu kwa wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii kueleza kuwa nchi yetu imepata heshima kubwa machoni mwa Mataifa ya nje na hata kwenye Umoja wa Mataifa. Heshima hiyo bado hajawafikia wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana heshima ya mtu na zaidi ya Taifa iendane na kujinasua kiuchumi. Wizara hii bado hajafanya juhudzi zozote za kufanya utafiti wa kiuchumi kwa ajili ya Watanzania. Nchi yetu ina vitu vingi (bidhaa) na vizuri vinavyohitajika katika nchi mbalimbali duniani, lakini Wizara hii imekaa kimya muda wote toka nchi ipate Uhuru bila kuifanyia kazi changamoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii imeshindwa kutangaza vivutio vyatagalii vilivyoko nchini ikiwa ni pamoja na Mlima Kilimanjaro, mbuga za wanyamapori, viota mbalimbali vyatagalii, magofu ya kale, fukwe za bahari, maziwa, mito na vivutio vyatagalii ya hewa nzuri na zaidi hali ya utulivu na amani ili yoko nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivutio vyote hivyo vizuri tulivyonavyo Wizara imeshindwa kuvitangaza ili kuvutia watalii na kukuza vipato vyatagalii wetu na Taifa kwa ujumla. Badala yake Wizara imekuwa ikifanya utalii yenye kwa kuzunguka nchi mbalimbali duniani kwa ziara zisizo na tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la aibu baada ya miaka 50 ya Uhuru, Waziri kulieleza Bunge katika hotuba yake ya mwaka wa fedha 2011/2012 kuwa imepanga kuitangaza nchi yetu kama moja ya nchi zenyet giza mazingira muafaka ya uwekezaji duniani, kutangaza vivutio vyatagalii, kuzitafutia masoko bidhaa zetu katika nchi za nje na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inathibitisha kuwa Wizara hii yenye kwa watalii lakini hawafanyi kazi kwa maslahi ya Watanzania wengi walio maskini sana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni wakati muafaka kabisa wa kuwatambua Watanzania waishio nje na kumaliza haraka mchakato wa kuruhusu uraia wa nchi mbili hasa kuanzia kwa Watanzania wenye uraia wa nchi nyingine ili waweze kurudi na kushiriki katika michakato mbalimbali ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nina wasiwasi mkubwa na uwezo wa nchi yetu kuhimili shinikizo kutoka nje. Nina wasiwasi huu kuto kana na hali ya ulegevu wa Serikali hata katika kukusanya kodi kwa makampuni makubwa ya kigeni yanayochimba madini na yanayofanya biashara hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi umenizidi pale Mheshimiwa Rais wetu hivi karibuni tu alifanya ziara nchini Malaysia na alitamka akiwa huko kuwa wana hofu ya

kuyabana makampuni hayo kutokana na hofu walijonayo ya kunyimwa misaada na nchi yanakotoka makampuni hayo. Upo wapi hapo uwezo wa nchi kuhimili shinikizo kutoka nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hii Serikali haina budi kuimarisha Umoja wa Kitaifa, kuondoa mifarakano kati ya wananchi na Serikali ili tujenge umoja wa kweli na wa dhati bila kujali tofauti za kisiasa ili tujenge uwezo wa kweli wa kutoza kodi inayostahili kwa makampuni ya kigeni na kuhimili kikweli shinikizo kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tushikamane, Afrika tushikamane tuinusuru Libya isimalizwe. Tukilegea na kuiacha Libya iteketee, basi tusisahau msemo wa wahenga usemao ukiona mwenzio anyolewa, wewe tia maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumaliza kupigwa nchi zenyenye mafuta, zamu yetu wenye dhahabu, almasi, *ruby*, *Tanzanite* inafuatia!

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwasilisha. Ahsante sana.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema kuhudhuria mikutano mbalimbali na ni muhimu pia kuwapa Watanzania taarifa mbalimbali za fursa za kibiashara zilizoko nje. Pengine tuwe na fursa ya maongezi (*discussion*) kati ya Mabalozi na Wabunge, Mabalozi na Halmashauri za Wilaya na Mabalozi na Wafanyabiashara kwa Sekta mbalimbali nchi nzima kama vile Wafanyabiashara na Halmashauri zinazoshughulika na mazao kama Kahawa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yafanyike mapema kabla ya msimu wa kilimo kuanza ili wakulima wajialdha vizuri, lakini pia tuwe na vitengo au watu maalum kwa ajili ya kufanya *economic intelligence* (iwe *industrial, engineering et cetera*) na kufikisha habari hizi hapa nyumbani na tuwe na utaratibu wa kutekeleza yale yanayoletwa ama sivyo hata waleta habari watakata tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maendeleo yalivyo, kwanza, ninaipongeza Serikali kwa kufungua Ubalozi pale Brazil na Malaysia. Ninapendekeza Serikali ifufue Ubalozi pale Soul – South Korea, kwani wameonesha nia thabiti ya kushirikiana na Tanzania. Tufungue Ubalozi pale Tel Aviv Nchini Israel; hawa wanashikilia kwa kiwango kikubwa teknolojia ya kilimo, lakini pia Watanzania wengi sasa wanasadari kuelekea huko kwa sababu za kiuchumi na kidini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitakia Wizara utekelezaji wa mafanikio wa majukumu yao kwa mwaka 2011/12.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza sana Wizara kwa kuanzisha Diplomasia ya Uchumi mwaka 2008 na kuiendeleza. Huu ni mwelekeo mzuri wa kuongeza na kukuza uwekezaji nchini mwetu.

Ninaiomba Wizara isilegeze uzi katika hili, maana nchi yetu ina rasilimali nyingi sana, kilicho kidogo ni uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila bajeti inaporuhusu, ninaiomba Wizara iendelee kujenga majengo ya Balozi ili kupunguza gharama kubwa sana za kupanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Uraia wa Nchi Mbili inachelewa sana. Kwa maoni yangu, maana mchakato wa Katiba Mpya utachukua muda sana, inawezekana ikawa tayari mwaka 2014; kwa nini Muswada wa Sheria ya Uraia wa Nchi Mbili usitangulie Katiba Mpya ilimradi tu matakwa ya Katiba Mpya yazingatiwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ubalozi wa Uingereza umeanzisha mtindo wa kutoa viza za usafiri nchini Kenya kwa Afrika ya Mashariki yote. Hii inaleta usumbufu kwa Watanzania, hasa pale wanapotaka kusafiri kwa dharura. Ninaiomba Wizara ianze mazungumzo na Ubalozi huo ili urejeshe utoaji viza nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja

MHE. PROF. PETER M. MSOLLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninapenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara, kwa hotuba nzuri, ambayo pamoja na mambo mengine, imeonesha dhahiri namna Tanzania inavyoonekana na Mataifa mengine Duniani. Ninaipongeza Wizara kwa kutekeleza majukumu yake vizuri licha ya ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninapenda kuchukua nafasi hii, kuipongeza Serikali yetu kwa ushiriki wake katika kuleta usuluhisho wa mgogoro kati ya Serikali ya Sudan na Sudan ya Kusini, ikiwa ni pamoja na kupeleka Majeshi ya Ulinzi wa Amani. Sasa Sudan Kusini ni Taifa jipya na lenye fursa nyingi za ushirikiano ikiwa ni pamoja na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hayo, ninashauri Serikali yetu iwe mstari wa mbele katika kufungua Ubalozi Nchini Sudan ya Kusini.

MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ninachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa kazi yao njema. Ninaomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna malalamiko mengi kwamba, Ofisi zetu za Ubalozi zilizoko nchi za nje ni hohehahe (*no maintenance*). Tafadhalilichunguze hili kwani linatia walakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sudan ya Kusini, ninatoa pongezi sana kwa kutuwakilisha kwenye sherehe hizo. Nina maswali mawili kuhusiana na tukio la Uhuru wa Sudan ya Kusini:-

(a) Je, sababu zipi za msingi zimeifanya Sudan ya Kusini ijitenge na sasa kuwa nchi mbili na sababu hizo ni suluhisho na uhalali wa kuruhusu nchi igawanyike?

(b) Je, kilichotokea Sudan (mgawanyiko wa nchi moja kuwa nchi mbili) kinaweza kuashiria kutoa fundisho lipi (*potential risk or opportunities*) kwa nchi nyineza za Afrika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sasa Tanzania iliripoti kwamba, inafanya tathmini ya hoja ya mahitaji ya kuwa na *dual citizenship*; je, mchakato huu utakwisha lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuthibitisha kwamba, Tanzania ni mionganii mwa nchi yenye utajiri wa madini muhimu ya *uranium* duniani; je, nchi imejipanga vipi ili kwanza kujihami na Mataifa makubwa yanayoweza kusababisha mitafaruku ya kisiasa nchini ili wao wapenye kuchukua *uranium*? Kumbuka haya yalitokea Jamhuri ya Congo (Zaire).

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa kujitathmini kwa Utawala Bora (*APRM*), umechukua muda mrefu kwa kuwa Wizara haioni umuhimu huo ambao kama nchi tuliridhia na tayari tumetumia pesa nyingi na taarifa ambayo tayari ilikwishaandaliwa na kukamilika, imepitwa na wakati na yapo mambo mengi ama yamebadilika, kuondoka au kuongezeka hata kama timu ya wataalam itakuja hivi karibuni (Agosti, 2011), ninayo mashaka kama Ripoti hiyo inaweza kutusaidia sana kama hakuna pesa zilizotolewa za kuboresha taarifa ambayo imeandaliwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni muhimu kwa ustawi na maendeleo ya Taifa letu. Nitapenda kupata ufanuzi na hali halisi ya *APRM* na fedha iliyotengwa itolewe kwa wakati ili kufanikisha kusudio la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushuru sana.

MHE. AGGREY D. J. MWANRI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo langu la Siha, ninaomba kuchukua fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Bernard Kamilius Membe (Mb), Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa hotuba yake nzuri, ambayo ameitoa katika Kikao cha Bunge kinachoendelea asubuhi hii. Ninaamini wengi tumeelimika kutokana na hotuba hii, hususan kuhusu mambo mengi yanayotokea duniani na pia katika Bara la Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nimpongeze Mheshimiwa Mahadhi Juma Maalim (Mb), Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ambaye kama Waziri Membe mwenyewe, amekiri amekuwa wa msaada mkubwa na hivyo kuleta ufanisi wa hali ya juu katika Wizara. Ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali iendelee kutoa elimu zaidi kuhusu uwepo wa mfumo wa Utandawazi Duniani ili Wananchi waweze kujuwa umuhimu wa mfumo huo na madhara yake kwa jamii. Ipo haja ya kuonesha jinsi utandawazi

unavyoweza kukuza uchumi wa nchi yetu kwa njia ya mawasiliano, biashara na uwekezaji na wakati huo huo kuonesha jinsi maadili ya nchi yetu yanavyoweza kumomonyoka kutokana na kuingizwa kwa picha za ajabu ajabu ambazo ni hatari hasa kwa watoto wadogo wenye umri nchini ya miaka 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua fursa hii kuchangia kwa maandishi Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza la mchango wangu ni haja ya Wizara hii kutakiwa kuwa kifua mbele katika shughuli zozote halali, ambazo Mtanzania anashiriki nje ya nchi. Umekuwepo ukiwa na hali ya unyonge kwa Watanzania wawapo nje ya nchi wanapotafuta riziki kwa ajili yao au hata kwa manufaa ya Taifa. Mfano rahisi ni wafanyabiashara wanaokwenda Nchi za DRC na Sudan kufaidi fursa zilizoko huko. Masimulizi ya madereva wa mizigo katika mipaka ya Tunduma na Kasumbalasa ni kuwa, wafanyabiashara wa nchi nyingine na hasa Afrika Kusini wanapata huduma nzuri mipakani ukilinganisha na wale wa Tanzania. Pendelezo hapa ni kuwa, Wizara hii inapaswa kuwakingia kifua Watanzania ili wapate huduma na hata Mikataba ya Biashara. Nchi hizi tunazisaidia kwa gharama kubwa, majibu yake ni kuwa tupate nafasi ya kwanza ya kufanya nao biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nchi zilizotuzunguka, Mabalozi wetu popote walipo, wanapaswa kutafuta fursa za uchumi na kudokezea wajasiriamali wetu. Hii ni kuanzia biashara ndogo mpaka biashara/fursa kubwa. Balozi wa Kenya nchini Tanzania ni mfano mzuri wa kuigwa. Anajua wapi zabibu inalimwa na ni mkulima gani anaweza kuwa na zabibu za kutosha kuuza nchini Kenya. Zaidi ya hiyo, ameonekana akidadisi kuwa ni wapi inaweza kupatikana ardhi kwa Wakenya kulima zabibu, kwani zabibu ilimwayo hapa inatoa mvinyo wenye ubora mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hapa ni Ubalozi utakaoweza kutambua fursa kwa kuanzia zile ndogo. Fursa ndogo kwa nchi za jirani au hata za mbali, utawahusisha watu walio wengi na kuchangamsha uchumi. Tumepata nini kwenye hii Sudan mpya? Zipo habari kuwa mahindi yapelekwayo Kenya, yanapita tu kuelekea Juba. Je, kwa nini Wizara isiweeleze wajasiriamali au hata Wakulima wa Tanzania; faida ya bei inayoweza kupatikana ili tulenge masoko hayo kimkakati? Utaratibu huu siyo mpya India, Japani na sasa China. Utaratibu huu wa kuwalinda na kuwaongoza watu wake wanaposhambulia fursa za nje ya nchi wameutumia/wanautumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni hoja ya Wizara hii kupitia Balozi za majirani zetu, kuzidisha mahusiano mema. Mkoa wa Kagera, Wananchi wake wamekuwa wakionewa na Wananchi wa Nchi za Burundi, Rwanda na Uganda. Imani yangu ni kuwa, hali hii inaweza kukoma iwapo Wizara yetu itaonesha kujali na kukemea kwa ukali, pindi tatizo linapotokea. Hii haijalishi kama Wizara za Ulinzi na Mambo ya Ndani zinachukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia taarifa za Wavuvi wa Ziwa Tanganyika kuvamiwa na watu toka DRC, hali ni hiyo hiyo Ziwa Victoria. Kwa mpango maalum, makundi ya mifugo inaingizwa Mkoani Kagera kuchungwa na kuharibu mashamba na mazingira. Vitendo hivi vinafanyika wakati Nchi za Rwanda na Uganda, mifugo hiyo itokayo ikifahamu. Kwa hiyo, ni busara Wizara ikahusika mapema kuzuia tabia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii, kazi ya kupenda taswira ya taifa letu. Ahsante.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninapenda kuchangia kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninampongeza Waziri kwa kutoa hotuba nzuri, lakini ningependa kujua kwa nini Mkoa wa Kigoma una Balozi Ndogo za Congo na Burundi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nchi tunaweza kuwa na Uanachama wa SADC na EAC kwa pamoja; na je, suala hili haliwezi kusababisha mgongano wa Kisera baina ya Jamhuri hizi mbili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko ya Watanzania kuuawa huko South Africa; je, Waziri anaweza kutuambia ni Watanzania wangapi wameuawa; na je, kuna Watanzania wangapi South Africa? Jitihada gani zimebekwa na Serikali kuzuia au kuwalinda Watanzania hao waishio nchini humo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Waziri amesema Tanzania ni nchi ambayo inaheshimika; je, Wizara ina takwimu kuwa ni Watanzania wangapi wanaishi nchi za nje na ni shughuli gani wanazifanya?

Kwa kuwa kumekuwa na wimbi la wahamiaji kujishughulisha na ajira mbovu kama ushoga, ukahaba, ujambazi na biashara ya madawa ya kulevyta, kutokana na maisha ya Ulaya kuwa *expensive*; je, Serikali ina mpango gani wa kuwarudisha Watanzania hawa nyumbani ili kuinusuru nchi hii kupata aibu kwa kuwa kwa nchi za wenzetu baadhi ya biashara hizo haramu zinaruhusiwa na zinalipiwa kodi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, ninaomba kuwasilisha.

MHE. PEREIRA A. SILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie Hotoba hii. Ninampongeza Waziri na Watendaji, kwa utendaji mzuri na pia kwa Hotuba maridhawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuipongeza Wizara, ninaomba nichangie katika vipengere vifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana kuona kwamba, Libya imevurugwa, Wananchi wengi kuuawa chini ya Azimio la UN. Ninashangaa kwamba, UN bado

haijasoma kutokana na kutumika vibaya kwa Maazimio yake inayotoa mara kwa mara. Lazima *UN* iwe na njia bora *ya utatuzi* wa migogoro kuliko kutegemea Maazimio ambayo mara nyingi hupendekezwa na wakubwa, ambao mara zote wanakuwa na ajenda za siri. *UN* iongeze jitihada zake kwani ni dhahiri kwamba, Libya katika kipindi kidogo kijacho, itakuwa Somalia ya Mwaka 2011 na gharama zake kifedha na kimaisha tunazielewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, iliamua kujiunga na *OIC*, kwa lengo la kuinua uchumi wake. Kwa wakati huu na kufuatia ukumbusho wa mara kwa mara, Serikali ya Muungano iliahidi kutoa jibu la suala hili na hadi leo jibu hili halijatolewa; ni vyema tukajenga utamaduni wa kutoa majibu ya masuala kama haya; vinginevyo, tunasababisha watu ambao hawapendi Muungano kupata mwanya kuvuruga umoja wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na uchelewaji wa kujaza nafasi za Mabalozi kwenye nchi mbalimbali, ambako Mabalozi wetu wanaondoka hasa baada ya kufikia umri wa kustaaifu. Jambo hili hupunguza tija kwenye Balozi zetu, kwani ni dhahiri kwamba, Makaimu huwa wamepewa vikomo vya maamuzi yao. Katika kujaza nafasi hizi, ni busara kuangalia haja ya kuwa na wawakilishi na uwiano mzuri wa pande mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa namba 26 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amezungumzia suala la ushirikishwaji wa Watanzania walio nje ya nchi katika uwekezaji na ukuzaji wa uchumi. Ninafuraha kuliunga mkono jambo hili, kwani ninalelewa faida zake kama tutalipa nafasi yake. Watanzania wakiwekeza ni rahisi kuelewa Sera zilizopo na kusaidia zaidi kirasilimali ambazo tunazihitaji. Kwa vile Serikali imekamilisha maandalizi ya mazingira wezeshi ya ubia wa kiuwekezaji kati ya Serikali na Sekta Binafsi, Watanzania walioko nje ndiyo wabia bora kuliko wengine wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio na kuongezeka kwa tija ya uamuzi wetu wa kutumia rasilimali za Watanzania walio nje, ni vyema Serikali ikakamilisha mchakato wa Sheria itakayoruhusu Watanzania kuwa na uraia wa nchi mbili. Hili litakuwa ni chachu tosha ya kufanikisha azma yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua fursa hii kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Bernard Membe, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara, kwa Hotuba nzuri na yenye kutoa matumaini. Tuna imani na kazi mnazozifanya na tunaomba mwendelee hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *visa* za kuingia baadhi ya nchi hususan Canada, Uingereza na nyingine, zilipoamua kuhamishia huduma zao za kutoa *visa* na kuzipeleka Nairobi; hatua hii imetusababishia adha kubwa kwa Wananchi wetu na Viongozi wake katika kupata *visa*. Zoezi la kupata *visa* linachukua muda mrefu na

gharama ni kubwa, kwa vile Wananchi wanalazimika kufuatilia maombi yao Nairobi wakati mwingine Wananchi wamelazimika kubadili taratibu zao za kusafiri kwa sababu ya kukosa *visa* kwa wakati. Binafsi, nilishawahi kuahirisha safari baada ya kucheleweshewa *visa* kwa muda mrefu. Mbona Wananchi wa nchi hizo wanapata *Visa* za Tanzania kutoka Balozi zetu nchini mwao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ichukue hatua zitakazolenga kurudisha huduma ya *visa* nchini mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inatumia fedha nyingi sana kulipa pango kwa Ofisi za Balozi pamoja na nyumba za Watumishi katika Balozi zetu. Serikali sasa iweke mkakati/mpango maalumu wa kununua au kujenga majengo yake katika Balozi zetu nje. Katika nchi nyingine kama Msumbiji na Uingereza, tuna viwanja tulivyopewa na nchi husika na katika baadhi ya nchi tumetishiwa kunyang'anywa viwanja hivyo. Kujenga Balozi zetu ni uwekezaji. Kutohitajika kulipa pango na kutoza pango katika majengo yetu ya Balozi, kutasaida kupunguza gharama za uendeshaji wa Balozi zetu. Serikali itafute namna mbalimbali za kupata fedha kwa ajili ya kujenga majengo ya Balozi zetu nje. Mbinu hizo zijumuise mikopo kutoka taasisi za fedha ndani ya nchi na nje ya nchi. Pia kutafiti uwezekano wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kushiriki katika zoezi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongea Hotuba ya Waziri. Pia ninampongeza Waziri kwa kazi nzuri anazozifanya kutuwakilisha huko nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Tanzania uchumi wake umedoroa; na kwa kuwa kudorora huku kunatokana hasa na kuzisaidia nchi karibu zote Kusini mwa Jangwa la Sahara katika kuzikomboa Nchi kama Zimbabwe, Mozambique, Angola, Namibia, South Africa, Seychelles, Congo, Uganda, Guines Bissau na kadhalika; na kwa kuwa baadhi ya nchi hizo zimeimarika kiuchumi; kwa nini basi nchi hizo zisirudishe fadhila kwa Tanzania na hivyo kuchangia maendeleo ya watu wake? Kuna mikataba gani ambayo inatakiwa ifuatwe ili Tanzania isaidiwe na nchi hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka kati ya Tanzania na Malawi bado una utata. Sisi tunadai mpaka ni katikati ya Ziwa Nyasa; Malawi wanadai mpaka ni kandokando ya Ziwa Nyasa upande wa Tanzania; utata huu utakwisha lini? Leo Malawi kuna fujo; je, fujo hizi haziwezi kutuathiri sisi tunaokaa Mwambao wa Ziwa Nyasa upande wa Tanzania? Naomba kujibiwa maswali haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninaomba nimpongeze Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayofanya kuiweka nchi yetu katika ramani nzuri duniani na kwa kuleta uhusiano mwema na nchi mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya siasa katika Nchi zote za Kiarabu siyo shwari na kama tunavyoona, kuna wimbi kubwa la mageuzi. Sisi Watanzania tunaguswa zaidi kiuchumi kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta, ambayo yanazalishwa zaidi katika Nchi za Mashariki ya Kati. Ukiiondoa suala la uchumi; uhusiano wetu na Nchi za Mashariki ya Kati zenyet matatizo ya kisiasa ukoje? Je, Tanzania inaunga mkono mageuzi katika maeneo hayo au inaunga mkono tawala zilizopo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wengi wako nje ya nchi yao, siyo kwa mapenzi lakini wengi wao wanatafuta maisha bora. Wengi wao wangetamani kurudi nyumbani kama Watanzania na siyo kama wageni. Ninajua Serikali ina nia ya kuanzisha uraia wa nchi mbili, lakini utekelezaji wake unakwenda polepole sana. Ninaomba Serikali iharakishe kuleta Muswada huu Bungeni ili Watanzania waliopoteza uraia wao, kwa sababu ya kuhamia huko, waweze kurejea. Maslahi ya raia wa nchi mbili ni ya uchumi vile vile. Watanzania wengi wamekua kiuchumi; hivyo, wataweza kuwekeza Nchini Tanzania na hivyo kuinua uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia sasa imebadili mwelekeo kutoka siasa kwenda kwenye uchumi. Mabalozi wetu wana nafasi nzuri ya kuanzisha Miradi ya Kiuchumi kwa kushawishi wawekezaji kutoka nchi hizo kuja kuwekeza Tanzania. Siyo vibaya, moja katika vigezo ambavyo Mabalozi wetu wanaweza kupimwa, iwe pamoja na umahiri wao katika kutafuta wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo Watanzania wachache wanashikilia nafasi za juu katika Taasisi za Kimataifa, ikiwemo Umoja wa Mataifa wenyewe. Tunaiomba Wizara ya Mambo ya Nje na Uhustiano wa Kimataifa, ifichue nafasi zaidi ili Watanzania wengi zaidi wafanye kazi huko. Hayo yakifanyika, kuna ulazima wa kutoa nafasi sawa kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na idadi kubwa ya vijana wazamiaji kutoka nchini kwetu, chanzo kikubwa kwa vijana wetu ni kutafuta ajira. Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kukabiliana na wimbi hili, lakini mambo mawili hayajafanyiwa kazi; hivyo, ninashauri ufanywe ufafiti ili kujua vijana wanaokwenda kuzamia wana ujuzi wa aina gani ili tuangalie upungufu tulionao katika kukidhi shida yao. Pili, tuimarishe Taasisi za Mabaharia ili ziweze kuratibu vizuri upatikanaji wa kazi katika nchi za kigeni. Tatu, tulimarishe Shirika letu la Meli ya Ubia na Wachina ili vijana wetu pia waajiriwe katika meli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejitahidi kuboresha Balozi zetu, lakini kuna haja ya kuimarishe Balozi zetu ili ziweze kuhimili ushindani wa wawekezaji na kupanua masoko ya bidhaa zetu. Pia ni vyema Serikali ikawa na Kitengo cha Kushughulikia Ukusanyaji na Utawanyaji wa Taarifa za Wawekezaji na Masoko yaliyoko nje na ndani ya nchi. Aidha, Serikali kwa kupatia Taasisi za Wafanyabiashara (*STAMICO* na *NDC*), ipate takwimu za kina ili wanaokuja kuwekeza wasiwadhulumu Watanzania kwa kukosa takwimu za rasilimali zilizopo hasa katika Sekta za Madini na Maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iharakishe kuwapatia Watanzania ambao kwa dhati yao, wana nia ya kutumia ama rasilimali walizonazo au elimu na uzoefu kuja kuutumia hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya Afrika kutumia umoja wao kwa kupinga au kuridhia Maazimio kwa pamoja (*Block Voting*), hasa yale ambayo yataingilia Uhuru wa Ustawi wa Nchi.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninaunga mkono hoja wa Wizara kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nielezwe kwa nini Watoto wa Wabunge hawapatiwi *Passport za Kibalozi* (*Diplomatic Passport*) wakati wake zetu wanapata. Ninaomba nipatiwe maelezo au ikiwezekana Mheshimiwa Waziri aruhusu na watoto wetu wanne wapate *Diplomatic Passport*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Wabunge tunaposafiri kwa safari za kibinafsí tunawajibika kulipia *visa* wakati Wabunge wote tuna *Diplomatic Passport*? Vilevile kwa nini sisi tunatoza fedha kidogo katika *visa* kuliko wenzetu wa nchi za nje hasa Uingereza na USA?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Kidiplomasia ni kioo cha jamii, ninaomba bajeti yake iongezwe ili kiweze kuwa na heshima yake kama zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa shukrani za dhati kwa Ofisi za Ubalozi wa Cairo, Misri, Kinshasa na DRC, kwa ushirikiano mkubwa walioutoa kwa Timu yangu ya *Simba Sports Club* ilipokwenda kuwakilisha nchi. Ninaamini ya kuwa, Wizara yako itafikisha salamu hizo za pongezi katika Ofisi hizo za Ubalozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninaunga mkono hoja ya Wizara.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Membe (Mb), Naibu wake, Katibu Mkuu wa Wizara na Timu nzima, kwa maandalizi na mawasilisho ya Hotuba ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninachangia jambo moja tu, nalo ni *APRM*, ambayo ni *Mechanism* iliyoridhiwa na Bunge letu Tukufu, lakini utekelezaji wake hapa nchini unasuasua kutokana na kukabiliwa na changamoto nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimechaguliwa kuliwakilisha Bunge letu kwenye Baraza la *APRM* na hivyo kwa kuhudhuria mikutano michache, nimejifunza kuwa ni chombo muhimu sana kwa utawala bora wa nchi yetu. Hiki ni chombo kitakachotoa picha nzuri ya nchi yetu Kimataifa kuititia taarifa zake za tathmini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachosikitisha ni jinsi Wizara inapochelewa kushughulikia changamoto hizo ikiwepo yafuatayo:-

(i) Pengo kubwa la bajeti (bajeti finyu), inayotengwa na Wizara kila mwaka kwa ajili ya shughuli hizo.

(ii) Chombo kimegubikwa na madeni ambayo hayana ufumbuzi wa haraka.

(iii) Kutopatiwa *Legal Entity* rasmi ili iweze kukamilisha utekelezaji wa maswala mbalimbali kisheria. Hii ni hali inayozua maswali mengi kiutendaji na hii itawawezesha kupata *own-vote* - fungu la fedha.

(iv) Upatikanaji wa fedha ili kuhakiki ripoti yetu ya nchi, inayotarajiwa kufanyika haraka – TSh. 533 milioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuona nchi za Wanachama wenzetu ikiwepo Kenya, Uganda, Rwanda, Burkina Faso, Ghana, South Africa, Nigeria na Zambia, wameshakamilisha tathmini zao za awamu ya kwanza, wako kwenye mchakato wa awamu ya pili na ya tatu. Tanzania haijakamilisha CSAR kwa miaka miwili iliyopita. Hakuna mwanga mbele kuona mwelekeo ni vipi bila kuondoa changamoto nilizozitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge hili kuhusu kukabiliana na kuondoa changamoto zote ili Ripoti ya Tanzania, inayosubiriwa kwa hamu na nchi zingine kutokana na amani yetu, iweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwa kuweza (*ku-maintain*) uhusiano mwema na nchi nyingi duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itaanzisha *Dual Citizenship?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa mchango wangu, ninaomba nitangulize pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa Hotuba waliyowasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia kuhusu Wananchi wanaopata tabu sana kupewa *visa* za kwenda nchi nyingine hata kama watatimiza vigezo vyote. Ninaomba hili liangaliwe, maana tumekuwa na wageni wengi sana hapa Tanzania. Ningeshauri pia Balozi zetu ziwe makini kutoa *visa* kwa wageni wanaotaka kuingia ndani mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu vijana wetu/raia wa nchi yetu, waliopata makosa ya jinai na kufungwa nje. Je, Serikali

yetu huwa inatoa mchango gani wa kuwasaidia? Je, tunazo takwimu zao? Je, upo uwezekano wa kubadilishana wafungwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikihamasisha sana raia wetu walio nje ya nchi yetu kuja kuwekeza katika nchi yao. Je, kuna vivutio gani inawapatia ili kweli waone umuhimu wa kurudi kuja kuwekeza katika nchi yao? Ninaishauri Serikali sasa iwe na makakati wa kuweka vivutio kwa ajili ya kurudi nyumbani na kutumia ujuzi wao na kuona umuhimu wa kuwekeza na kuleta faida kwa nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumekuwepo na usumbufu mkubwa kwa Wananchi wetu, waliokaa nje ya nchi muda mrefu, wanaporudi na mali zao kama magari, fanicha na kadhalika, hulipishwa ushuru mkubwa vifaa hivyo. Hilo pia Serikali ilipe kipaumbele. Tumeshuhudia makontena ya raia hao wakiuzwa mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache, ninaomba kuunga mkono hoja.

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuunga mkono hoja, ninaomba kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa baadhi ya Ofisi za Balozi zetu zilizoko nchi za nje haziko katika hali nzuri; ninashauri Ofisi hizo ziboreshweli ziendane na hadhi ya nchi yetu ya Tanzania, kwa sababu Tanzania ni nchi yenye sifa nyingi ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuishauri Serikali iwashauri Watanzania walioko nje ya nchi, ambao ni wataalam wa fani mbalimbali, waweze kurejea nchini hapa kwa ajili ya kufanya kazi na kuijenga nchi yao, kwa sababu Serikali hii ndiyo iliyowasomesha na kuwafikisha hapo walipo sasa. Ninashauri Serikali baada ya kukubaliana na Watanzania hao ambao ni wataalam, waweze kuwapatia ajira na kuwalipa vizuri ili waendane na ujuzi wao na siyo kuwadharau. Serikali ikifanya hivyo, wataalam hawa watabakia Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. BENEDICT N. OLE NANGARO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa pongezi nyingi kwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa kuandaa Hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania iwe *player* mkubwa katika kusukuma *African Union*, ishughulikie amani katika eneo la Somalia na Sudan ili kuzuia hali kuchafuka zaidi *East African*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania itafute jinsi ya kuunda timu ya *SADC* itakayotafuta suluhu nchini Malawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ijipange vizuri zaidi na kila mwaka pesa ya maendeleo itengwe ili kununua ama kujenga Balozi mbili ama tatu katika nchi zile *strategic*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Balozi wetu wa Kudumu nchini Roma, anayetuwalisha *FAO*, *WFP* na *IFAD*, apewe pia jukumu la kusimamia na kuwakilisha katika Shirika la Afya ya Wanyama Duniani, yaani *OIE*. Japo Makao Makuu ya *OIE* yapo Paris – Ufaransa, *nature* ya shughuli zake inafanana sana na zile za *FAO*, *WFP* na *IFAD* na kuna shughuli nyingi wanazofanya na mashirika hayo *UN* yaliyopo Rome.

MHE. JASSON S. RWEIKAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. Jukumu mojawapo la Wizara hii ni uwakilishaji wa nchi hii huko nje na kuimarisha ushirikiano na Mataifa mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni nilikuwa katika Nchi ya Malaysia. Ubalozi wetu huko una hali mbaya sana kifedha. Hawana fedha kabisa, Balozi alitueleza kuwa hata nyumba anayokaa, ambayo ni ya kupanga (*rented*), karibu anafukuzwa. Tayari kapelekewa notisi ya kuhama, wapangaji wengine wanakwenda kukagua wakati yeeye na familia yake wakiwemo. Hali hii ni aibu kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri na kusisitiza, tufanye hima kuondoa aibu hii. Hawa watu wetu wataishije huko nje? Tuwapelekee fedha haraka. Ninaunga mkono hoja.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na afya njema kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa imani aliyoionyesha kwangu kwa kunitua kuwa Naibu Waziri katika Wizara hii. Pia nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete na Mheshimiwa Makamu wa Rais, Dkt. Mohamed Ghalib Bilal kwa ushindi wao na ushindi wa CCM katika uchaguzi Mkuu wa 2010. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumshukuru kipekee Mheshimiwa Bernard K. Membe, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa msaada wake mkubwa na wa dhati kwangu kwa kuniongoza vema na kunielekeza ili kufanya kazi zangu kwa ufanisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa uongozi wake mahiri ndani ya Bunge hili. Aidha, napenda kuwapongeza sana Mheshimiwa Spika na Naibu Spika, kwa kuchaguliwa kwao katika nafasi hizo na kwa namna wanavyoliongoza Bunge hili. Pia napenda kuwapongeza

Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, wewe mwenyewe Mheshimiwa George B. Simbachawene na Mheshimiwa Sylvester Maselle Mabumba kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti na kwa namna mnavyoonyesha uwezo mkubwa wa kuliongoza Bunge katika kipindi hiki kifupi. Pia nawashukuru sana Wabunge wenzangu wote kwa ushirikiano wao wanaoendelea kunipa. Nawaombea kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yao hapa Bungeni na kwenye Majimbo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa namna ya pekee, kuwashukuru wananchi wenzangu na wapigakura wangu wa Jimbo la Muyuni. Nawashukuru kwa imani kubwa waliyoionyesha kwangu kwa kunichagua kuwa Mbunge wao. Nitaendelea kuwa nao karibu na kushirikiana nao kuliletea Jimbo letu maendeleo. Kwa pamoja tutapiga hatua kubwa ya maendeleo katika Jimbo letu la Muyuni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kuishukuru sana familia yangu kwa uvumilivu wao kwangu na kwa namna inavyonisaidia na kuniunga mkono katika majukumu yangu. Aidha, shukrani za dhati ziende kwa Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Mabalozi, Viongozi na wafanyakazi wakiwemo wasaidizi wangu katika Wizara ya Mambo ya Nje, kwa ushirikiano, ushauri na msaada wao katika utekelezaji wa majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, sasa nianze kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kwanza, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, wote waliochangia hoja hii ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Ni dhahiri kwamba michango yao itatusaidia sana katika kufanikisha shughuli za Wizara na kuimarisha ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la ufinyu wa bajeti. Kuna michango mingi iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge ya aidha kugusia moja kwa moja suala la ufinyu wa bajeti katika Wizara hii au kutoa michango mingine ambayo jibu lake ni tatizo la ufinyu wa bajeti katika Wizara. Naomba nikubali, kwa mfano hoja ambazo zilitolewa na Mheshimiwa Dkt. Augustino Mrema na Mheshimiwa Sanya ambazo moja kwa moja waligusia tatizo la ufinyu wa bajeti. Ni kweli Wizara yetu kutokana na majukumu yake fedha inazopipata hazitoshii kutekeleza majukumu hayo. Kuna matatizo mengine ambayo yameelezwa na Waheshimiwa Wabunge, yanathibitisha tatizo hilo la fedha katika utekelezaji wa majukumu yetu. Hata hivyo, napenda kuwashukuru Wizara ya Fedha kwa sababu kuna mambo ambayo licha ya tatizo hilo la ufinyu wa bajeti lakini mara zote matatizo ya Balozi zetu yamekuwa yakishughulikiwa hata mara nyingine kunakuwa na uchelewaji kidogo kwa mfano suala la mishahara tofauti na ilivyoelezwa hapa na baadhi ya wachangiaji, pango la nyumba, ofisi katika zile sehemu ambazo Wizara haina nyumba zake za ofisi na pia huduma muhimu za maji au umeme. Fedha hizi zimekuwa zikitolewa kila baada ya miezi mitatu na mara moja inaweza kuchelewa lakini hazikosekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kwa zile shughuli nyingine muhimu nazo wakati mwengine ni kweli kumekuwa kuna tatizo kubwa la fedha na hili linaonekana hata katika kiwango ambacho tumekipata licha ya kwamba bajeti yetu ilikuwa kwa mwaka

uliopita ni bilioni 112 ambazo hazitoshi lakini katika upatikanaji pia tulipata bilioni 94 ambazo ni sawa na asilimia 83. Hiyo bila shaka inaathiri utendaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilihusishe suala hili la ufinyu wa bajeti pia na michango mingi iliyotolewa kwa mfano, ya kufungua Balozi ndogo katika sehemu mbalimbali au ya kufungua Balozi katika nchi mbalimbali. Wizara inapenda na bado inashughulikia kuhakikisha kwamba tunakuwa na Balozi au Balozi ndogo katika sehemu ambazo ni muhimu katika kuimarisha mahusiano na nchi hizo na pia kwa maslahi yetu ya kiuchumi. Lakini tumekuwa tukikwama katika kutekeleza azma hiyo kutokana na saa nyingine tatizo la kuwa na bajeti ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo limechangiwa na wajumbe wengi kidogo na ambalo napenda kuligusia ni suala la mahusiano yetu na Israel pamoja na Palestina. Ni kweli Tanzania tulivunja uhusiano wa Kibalozi na Israel mwaka 1967 kufuatia vita vya siku sita baina ya Israel na Misri na Rais wa Misri wa wakati huo Anwar El-Sadat kuziomba nchi za Kiafrika kumuunga mkono kwa kuvunja mahusiano na Israel. Kwa hiyo, nchi nyingi za Kiafrika ikiwemo Tanzania tulivunja mahusiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jitihada za Misri na Israel wenye kuleta amani ambazo zilizaa makubaliano ya *Camp David* au *Camp David Accords* baina ya Waziri Mkuu wa wakati huo wa Israel Begin pamoja na Anwar El-Sadat na kwa hiyo, wenye Israel na Misri kurejesha uhusiano na sisi pia zikiwemo nchi nyingi pia za Kiafrika tulirejesha tena na Israel na kwa hiyo, tuna uhusiano wa Kibalozi baina ya Tanzania na Israel. Ubalozi wetu ambao uko Misri ndio ambao unatuwakilisha nchini Israel na Ubalozi wa Israel ulioko Nairobi ndio unawakilisha Israel nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wale ambao walikuwa wakisema tufungue ubalozi nchini Israel, ni kwamba, tayari Ubalozi upo hata kama haupo ndani ya Israel lakini upo Misri na unafanya kazi hizo. Lakini uhusiano wetu na Palestine tangu miaka ya 1960 umeendelea kuwa imara na unaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nigosie suala la *Diaspora* ambalo limegeswa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamesisitiza umuhimu wa Watanzania ambao wanaishi nje katika maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kadhalika. Wapo ambao pia wamegesia kwamba hatua za kuhakikisha kuwa Watanzania hawa wanachangia vizuri katika maendeleo ya nchi yetu imekuwa ni taratibu mno hasa likiwemo suala la uraia wa nchi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyoelezwa katika Bajeti ya Mheshimiwa Waziri, tayari hatua zimechukuliwa na kuna kitengo cha *Diaspora* ambacho kinaratibu masuala ya Watanzania hawa ambao wanaishi nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uraia wa nchi mbili tusilione kama limechelewa kwa kiasi kikubwa hatua zilizochukuliwa na Wizara zimeweza kuamsha mwamko kwa suala hili kwa Watanzania walio wengi. Miaka michache iliyopita tusingepata Wabunge wengi ambao wangeliunga mkono na kulishabikia kama ambavyo

wamefanya safari hii. Kwa hiyo, hatua hizo zimewezesha sasa kuweza kujipanga vizuri na suala hili kuweza kukubalika kwa Watanzania walio wengi na kwa Waheshimiwa Wabunge kama mlivyoonyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda nigosie suala ambalo limegusiwa katika suala la *diasporas* ambalo linahusu Watanzania wanaume wanapooa wao wana uwezo wa kutoa uraia kwa wake zao pamoja na watoto. Lakini wanawake wa Kitanzania wanapoolewa na wageni wao hawana fursa hiyo. Hii ni kweli kwamba sheria hii inaonyesha kupitwa kidogo na wakati na kwa wale wanafatilia masuala ya haki za binadamu na hasa haki za jinsia watatambua kesi ambayo ni maarufu ya *Unit DAU* dhidi ya *Attorney General* ya Botswana ambayo tangu miaka 1990 Mahakama ilitoa uamuzi kwamba Sheria kama hiyo haiwezi kusimama na kwamba ni lazima ili kuleta usawa wa kijinsia haki hiyo ipatikane kwa wote. Kwa hiyo, tunaamini katika kushughulikia suala la *Diaspora* pia tutaweza kulishughulikia suala hilo kwa pamoja ili kweli tuweze kuwa na usawa wa jinsia kama ilivyo katika Katiba yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa mchango wako. Sasa nitamwita mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Bernard Membe.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, wote ambao tangu asubuhi wamefanya kazi kubwa ya kuonyesha umahiri wa kuuliza maswali mazito, yanayostahili kujibiwa. Maswali ni mengi sana, tutajitahidi kuyajibu yale ambayo muda utaturuhusu lakini naahidi pia kuwapatia majibu wakati wa vifungu kwa wale ambao watapenda kuweka *intervention* au kuingilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote naomba kwanza niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi. Ni orodha ya watu 75 yupo Mheshimiwa Anne Kilango, Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi, Mheshimiwa Amos Makalla, Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mheshimiwa Mchungaji Dokta Getrude Rwakatare, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Mwanamrisho Abama, Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Goodluck J. Madeye, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa David E. Silinde, Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis, Mheshimiwa Dokta Lucy Nkya, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Dokta Hamis Kigwangalla, Mheshimiwa Ignas A. Malocha, Mheshimiwa Gaudence K. Kayombo, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Aggrey Mwanri na Mheshimiwa Charles Mwijage. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Mussa Silima, Mheshimiwa Dokta Shukuru Kawambwa, Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Ismail A. Rage, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Betty Machangu, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mheshimiwa Christowaja G. Mtinda, Mheshimiwa Eng. Athumani Mfutakamba, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu, Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine, Mheshimiwa Subira Mgatu, Mheshimiwa Moses J. Machali, Mheshimiwa Dokta Augustino L. Mrema, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Dokta Charles Tizeba, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Selemani Zedi, Mheshimiwa Esther N. Matiko, Mheshimiwa Regia Mtema, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Mheshimiwa Juma S. Juma na Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile wapo Mheshimiwa Chiku A. Abwao, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Naomi Kaihula, Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mheshimiwa Dokta William Mgimwa, Mheshimiwa Maryam Msabaha, Mheshimiwa Sylvester Mabumba, Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa, Mheshimiwa Desderius Mipata, Mheshimiwa Augustino A. Masele, Mheshimiwa Saleh Pamba, Mheshimiwa Modestus D. Kilufi, Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mheshimiwa Mahadhi Juma Mahadhi, Mheshimiwa Kebwe S. Kebwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kutajitokeza wengine naomba wasisite kunipa orodha ya waliochangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza, Mheshimiwa Augustino Maselle, Msemaji wa taarifa ya Kamati; Mheshimiwa Ezekiel Wenje, Msemaji wa Kambi ya Upinzani na Waziri mwenzangu Kivuli, Mheshimiwa John Magalle Shibuda, Mheshimiwa Dokta Mary Mwanjelwa, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Paul Lwanji, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa Moses Machali, Mheshimiwa Regia Mtema na Mheshimiwa Mwenyewe Mwenyekiti ambaye alichangia kwa muda wa nusu dakika Mheshimiwa Simbachawene. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna orodha nyingine hapa Mheshimiwa Steven Ngonyani nadhani amechangia kwa upande wa maandishi. Mheshimiwa Dokta Khamis Kigwangalla naye amechangia kwa maandishi, nilimsahau, samahani sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Bunge lako Tukufu kabla sijakwenda kwenye maswali binafsi.....

MWENYEKITI: Ndio dakika zako 15 zinaanza.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:

Kabla sijakwenda kujibu maswali ambayo tumeshatayarisha majibu hapa kwa muhtasari yako maeneo nane ambayo ningependa kuyatolea majibu kwa ujumla. Kwanza kabisa niungane mkono na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, katika kufafanua matatizo ya ufinyu wa bajeti yetu. Ni kweli kabisa pigo la Wizara ya Mambo ya Nje na siyo ya Tanzania peke yake, Wizara nyingi za mambo ya Nje zinazotegemea bajeti ya Serikali peke yake huwa zinashindwa kukidhi mahitaji ya maafisa wake nje na ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo tatizo kubwa la ufinyu na kama alivyoeleza mwenzangu katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Wizara ilipata asilimia 84 tu ya kiwango kilichopangwa kutoka bilioni 112 hadi bilioni 93 tu. Upungufu wa karibu bilioni 21 si haba, unaleta matatizo makubwa. Ni ufinyu wa bajeti, fedha hazitoshi na watu wetu wanaumia sana. Napenda kuungana na Wabunge wote mliotembea kwenye Balozi zetu kujionea wenyewe. Ukweli unauma lakini lazima utamkwe. Kama tungekuwa na uwezo wa fedha hali ya Mabalozi wetu na Maafisa wake isingekuwa ile mliyowakuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuwasifu sana Mabalozi pamoja na Maafisa wao kwa uvumilivu na uzalendo wa kuipenda nchi yao. Pamoja na matatizo yote lakini wanaelewa nia nzuri ya Wizara ya Mambo ya Nje wanaelewa nia nzuri ya Bunge lako Tukufu kwamba mngependa kiwango kinachotolewa kwenye Wizara kitolewe chote na kile kinachoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kipatikane chote. Nasema kwa wote mlionchangia kuhusu uchache wa bajeti kuanzia Mheshimiwa Kaka yangu Augustino L. Mrema pamoja na kaka yangu Sanya na Wabunge wenzangu wa CCM na wengine wote, nasema ahsanteni sana kwa kuliona tunaloliona. Watu wetu wanapata matatizo makubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuangalia tufanye nini mbele ya safari kuhusu tatizo hili, nasema kwanza ni jukumu la Bunge lako Tukufu, kuendelea kuiunga mkono Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, tupewe hela zaidi. Lakini pia tumeponga mkakati wa kutafuta fedha nje ya bajeti lakini zinazothibishwa na *exchequer* na Wizara ya Fedha pamoja na Serikali yenyewe kwa kuiga wenzetu wanachokifanya duniani. Wizara nyingi za Mambo za Nje zina vitega uchumi vya majengo yao duniani. Unapojenga kwa kutumia *development* bajeti au fedha za maendeleo au za mikopo kutoka benki wanapangisha nyumba zile na nyumba hizi zinasaidia kuleta fedha kwa ajili ya kulipia gharama za kwenye Balozi pamoja na kuchunga na kuhakikisha kwamba maafisa wake wanaishi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumenunua jengo *Washington DC* miaka miwili iliyopita la ghorofa nane, sasa hivi tuko mbioni kupata wapangaji katika nyumba. Tuna mpango wa kununua jengo *New York* kwa gharama ya dola milioni 25, Bunge lilikwishaidhinisha fedha za maendeleo na sasa hivi tuna dola milioni 13 pale tupo katika hatua za mwisho za kununua jengo la Kitega Uchumi *New York*. Ni matumaini yetu kwamba jengo lile likipatikana pamoja na jengo lililoko *Washington* nina hakika kabisa katika kipindi cha miaka miwili ijayo tutakuwa tunazungumza hadithi nyingine. *Inshallah* Mungu atatusadia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada hizo zinaendelea kuja Nairobi na kiwanja chetu cha London, tuna viwanja Nairobi na London na sasa hivi tunazungumza na Benki Kuu (BoT) tunazungumza pia na NSSF ili kuwezesha kwa njia ya uwazi (*transparency*) na ukweli unaoeleweka wa maridhiano kati ya pande hizo tatu Benki, NSSF na Wizara ya Mambo ya Nje kujenga majengo ya Kitega Uchumi mali ya *Foreign Affairs* ili tuweze kuwekeza ili tuweze kupata fedha kunusuru mamia ya maafisa wetu wanaopata tabu nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ambalo ningependa kulizungumza ni suala la Zanzibar na Wizara ya Mambo ya Nje. Limeulizwa na wengi na limeandikwa na wengi. Ningependa kujibu kama ifuatavyo, kwamba ni kweli kabisa Wizara yetu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ni Wizara ya Mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sahihi pia kwa wenzetu wa upande wa Zanzibar kuhoji tunafanya nini kuhakikisha pia tunawahusisha Maafisa wa Zanzibar kwenye Wizara yetu? Ningependa kusema kwamba tangu uhuru hadi sasa Serikali na Wizara imekuwa inashirikisha Maafisa Makao Makuu na kwenye Balozi zetu kutoka Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka yote hii ingawa siyo hamsini kwa hamsini tunahakikisha kwamba wenzetu wa Zanzibar wanashirikishwa kikamilifu katika nafasi za juu za Wizara pamoja na kuwaweka maafisa wake kwenye sehemu nyeti. Ningependa kutoa taarifa kwa wenzetu Wazanzibari kama ifuatavyo, kwamba katika kipindi cha mwaka 2011/2012 kwa kuzingatia haya na vilio hivi Wizara katika nafasi zake zinazoombwa safari hii kujaza nafasi tisa za Mabalozi zipo nafasi za wenzetu kutoka Zanzibar ndani mle.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nimeongea na Rais wa Zanzibar miezi mitatu iliyopita na katika mazungumzo aliniomba hilo hilo kwamba tuwe na vijana kutoka Serikali ya Zanzibar wa kuwasambaza kote katika Balozi zetu. Napenda nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba mwezi Septemba, mwaka huu wakati muhula wa kwanza kwenye Chuo cha Diplomasia utakapoanza tutakuwa na kundi la kwanza la vijana wasomi wazuri kutoka Zanzibar kujiunga na Chuo cha Diplomasia na baada ya hapo watasambazwa kwenye ofisi zetu za Balozi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia niseme tutapeleka Mzanzibari kwenye nafasi *New York* ya kusaidia Balozi, tutapeleka Mzanzibar kwenye ofisi ya Jiddah ambayo ni *General Consular* yote hayo katika kuhangaini na wenzetu wa Zanzibar na kuliha kikishia Taifa na dunia kwamba tunajali na tukisema tunafanya. Tunaomba uvumilivu na Wazanzibari wenzetu mtuelewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kulizungumza ni suala la *APRM* ambalo limechezewa vizuri sana na Mheshimiwa Arfi na baadaye ndugu yangu Shibuda. Sasa ndugu Shibuda simwoni hapa nilitaka nimueleze kwamba pole kwa yote yanayompata huko akishindwa atume *application* CCM itampokea kwa mikono miwili lakini nashukuru pamoja na matatizo yote hayo ameweza kuuliza swali la msingi na

analozungumzia uasilia wa Chama cha *TANU*. Nimevutiwa na msimamo wake, tutajitahidi kufanya kila linalowezekana arudi alikotoka ili tujadili. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa hakuna bwana mwache Waziri ajibu hoja yake.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunilinda.

Sasa Mheshimiwa Shibuda pamoja na wengine *APRM* safari hii inapokea bilioni mbili na arobaini na tisa milioni, zote hizi ni jitihada za Wabunge za kuhakikisha kwamba tunapata hela za kutosha. Lakini si hilo tu, kuanzia mwezi Agosti mwishoni na Septemba mwanzoni tutapokea timu ya watu waliokuja kuhakiki suala la *APRM*, wiki mbili zilizopita nilipokuwa *Marlabo Equatorial Guinea* nilizungumzia na niliwaambia Wabunge wa *APRM*. Wamenihakikisha kuwa timu ile inakuja, sasa inakuja kufanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, inakuja kuiripoti *APRM* ambayo mle ndani mna masuala ya siasa na demokrasia, mle ndani mna masuala mazima ya namna Serikali yetu inavyopambana na migogoro na kusuluhiha migogoro ya ndani na nje ya nchi yetu. Yako masuala ya elimu, yako masuala ya *gender* namna tunavyoshirikisha wanawake katika kuwapatia nafasi kwenye madaraka katika nchi hii. Yapo masuala ya kiuchumi yanayojitokeza mle ndani. Yako masuala ya Tume zetu za Uchaguzi kama zipo huru au laa. Yako masuala ya jamii ambayo yanajitokeza kwenye taarifa hii. Ni taarifa ya kujirudi na kuijangalia sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti hii ikishakuwa imehaririwa hatua itakayofuata, Serikali yetu italetewa ili kutoa majibu ya maswali yatayojitokeza na wataalam wanaokuja. Baada ya Serikali yetu kutoa majibu Bunge hili lako Tukufu litapata nafasi ya pili mara yake ya kwanza ilikuwa ya kuhamasisha Wabunge. Lakini ya pili, itakuwa ni kujadili *substance* kujadili masuala yatakayojitokeza kwenye *APRM* kabla hatujalipeleka ama mwezi Januari au mwezi Julai Addis Ababa au kwingine kokote ambako *AU* itafanyika ili sasa Tanzania ikatathminiwe na kuijipima yenewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningependa kuwaambia Watanzania kwamba mfumo huu wa kujitazama na kujikosoa wenyewe maana yake ndiyo maana ya *APRM* kwa kweli. Mtindo huu si mtindo mpya kwa utamaduni wa Mtazania na kwa hasa uasilia wa *TANU* ambao ndugu yangu Shibuda aliusema. Siasa ya kujikosoa, ndiyo ipo humu ndani. Sasa siasa hii ya kujikosoa ina lengo la kuifanya nchi iwe safi tu na ni lengo zuri sana. Hatuna lengo la kupata pesa zaidi kutoka nje kwa sababu *European Union* pamoja na Marekani wamesema sasa hivi suala la kutoa hela kwa watu waliofanya vizuri wa *APRM* halipo tena. Isipokuwa sisi wenyewe litusaidie kwa kitu kinaitwa *best practice*. Yaani Tanzania inafanya nini ukilinganisha na Kenya. Kenya inafanya nini ukilinganisha na Afrika Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunakwenda vizuri. Ningependa kuchukua nafasi hii kuwapongeza Wabunge ambao wanashabikia vizuri sana *APRM* na ni matumaini yangu kwamba inapofika mwaka 2012, suala hili litakuwa limefika kikomo. Sasa lipo suala la *behaviour* ya baadhi ya Mabalozi wa nchi za nje nchini. Waziri mwenzangu Kivuli aliposoma taarifa yake ilinigusa vizuri kidogo, lakini ningependa nifafanue mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, *paper* iliyonukuliwa kwamba tulitoa kwenye Baraza la Mawaziri. Nilitaka nirekebishe vitu viwili. Moja, *paper* ile ilitolewa kwenye semina elekezi. Baraza la Mawaziri lilikuwa moja tu, kati ya msururu wa watu waliokuwepo, halikuwa limetolewa kwenye Baraza la Mawaziri, kama lingekuwa limetolewa kwenye Baraza la Mawaziri *Paper* ile isingeonekana.

Lakini la pili ambalo ningependa niliseme kwamba *paper* hii imezungumza mambo muhimu sana. Lakini mengine yameachwa. Ningependa kabla ya kuomba radhi, *paper* hii itolewe kwenye vyombo vya habari ili nihukumiwe na Watanzania. Yamezungumzwa mambo mazito na manene yenye ukweli. Nasema wala sioni tatizo kuomba radhi, lakini nitaomba radhi baada ya Watanzania kuisoma taarifa yote. Wasipate *extracts* za kuonyesha kwamba kuna kosa, sisi ni wanasayansi na tumesoma, tutoe *document* yote, tuwaache wananchi watupime kabla ya kuomba radhi. Nasema wananchi wakiisoma hakuna cha kuomba radhi, isipokuwa makofi ya kupigiwa na kusitisizwa kwamba ulichokifanya Membe endelea nacho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, taarifa tulizozitoa kuhusu Mabalozi. Ningependa Waziri mwenzangu na rafiki yangu sana apate muda wa kusoma *Vienna Convention*. Si vizuri Wabunge wote wakasoma ni *document* kubwa. Tujitahidi kusoma tunapopata madaraka ya aina hii, tunasikilizwa mno, tusome *Vienna Convention*. Tukisoma mle kwenye *best practice* ya Vienna, tutagundua kwamba yapo mambo ambayo siwezi kuyasema kwenye Bunge lako Tukufu, ni ya jikoni. Uhusiano kati ya *sending state* na *receiving state* nchi inayotuma Balozi na inayopokea Balozi mambo yote tunayoshughulikia Wizara ya Mambo ya Nje ni *embargo* hayatakiwi kusema hadharani. Nawea kutoa tu pitcha ifuatayo kwa faida ya Bunge lako Tukufu lakini siwezi kuzama kwenye jiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo tabia za Mabalozi ambazo lazima zirekebishwe. Toka nimekuwa Waziri wa Mambo ya Nje hadi hivi sasa tume simamisha *Consul* wa Balozi na kumwondo nchini. Sasa ni hiari yake aseme, asiposema mimi sitasema. Katika kipindi changu cha miaka mitano tumeonya Mabalozi wanne kwa vitendo wanavyovifanya na wamekiri makosa. Wanaweza wakayasema, wanaweza wasiyaseme.

Lakini nikuchekeshe Mheshimiwa Mwenyekiti balozi mmoja na amekwenda kwenye nchi yake. Alipofika kule amechaguliwa kuwa Profesa wa *University*. Ametoa makala ya kazi yake nchini Tanzania, nini alichokifanya, shughuli gani alizozifanya na changamoto alizozifanya na Kambi la Wapinzani. Ameeleza kwa undani jitihada alizozifanya kila kukicha, kuunganisha wapinzani. Kwa sababu ni Profesa hajali. Maana msije mkadhani kila anayekuwa Balozi hapa akirudi kwao anaendelea kuwa balozi.

Ametoa kwenye *brochure ambayo* niko tayari kwa faida ya Bunge lako Tukufu baadaye kuikabidhi muone tunachodhani kwamba ni siri sana si lazima kiwe siri. Nitafurahi sana *agenda* hii siku moja mkinia tuizungumze, lakini siyo kwa kusema majina. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee *Vienna Convention*. *Vienna Convention* ni kitu cha hatari sana. Mnachokisema nyinyi tusikifanye, dunia nzima inakifanya. Ni *Vienna Convention* ya 1961. Unachojaribu wewe kusema tusikifanye, dunia nzima inakifanya, *we can not be an exception*. Tunaposema kwamba kwenye Ofisi ya Balozi, watu hawaruhusiwi kwenda mpaka upate kibali maalum, ni *universal principal* siyo Tanzania. Tunaposema tusiende kwenye nyumba zao kwa shughuli za kawaida, au kwenye ofisi zao kwa shughuli za kawaida, wako pale juu wanajua na wanazingatia na wanakubali. Si jambo tunalitunga tunga, sisi ni sehemu ya Umoja wa Mataifa. Ndiyo maana nasema hivi tukipata muda tusome *Vienna Convention*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uelewa wenu Wabunge ni mkubwa mno. Tusome basi ili tusipoteze muda kubishana kwa vitu ambavyo hatuwezi kuvizungumza. Kwa hiyo, nasema tena radhi haipo hapa. Shughuli tunazozifanya ndiyo wajibu wangu. Nilitumwa na Waziri Mkuu na Waziri Mkuu nimekufanyia kazi yako na bado nadhibiti hawa watu na tutaendelea kuwadhibiti. Hata kwa kusema hivyo, lakini tutaendelea kuwadhibiti tu. Nimewadhibiti, sasa wakiamua kusema, wawaambie, lakini siwezi kusema kitu na hii ningependa Bunge lielewe, dunia nzima inafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa nakala kwa ruhusa baadaye ya watu kupitia *The Convention of Vienna* ingawa ipo kwenye *internet*, tuisome tu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *dual citizenship* na *diaspora*. Vita hii imepamba moto. Nashukuru kwa mwamko mpya ninaouona ndani ya Bunge hili la kutuhimiza *Foreign* kwamba kwa kweli suala la *diaspora* ya kuunganisha nguvu ya wananchi wetu wa Tanzania walioko nje pamoja na wenzetu amba wako ndani kuunganisha nguvu ili kuleta *remittance* za mapato makubwa, ni jambo jema sana. Lakini pia hili la *dual citizenship* ambalo nilikuwa nalihutubia vizuri sana naona linapata moto mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwamba, nashukuru sana. Kilichokuwa kinatuchelewesha ni nini? Kilichokuwa kinatuchelewesha ni kwamba, suala la *dual citizenship* na Mheshimiwa Leticia ananisikiliza, suala hili kumbe ni la Muungano. Tunahitaji kupata ridhaa ya upande wa pili. Mheshimiwa Dokta Shein alipoingia kwenye madaraka na kuunda Idara ya *Diaspora* akawa ametusaidia sana. Kwa sababu kule elimu inaendelea na karibuni itakwenda kwenye Baraza la Wawakilishi kwenda kulielimisha jambo hili. Halafu pia litarudi hapa ili kulielimisha hili jambo ili twende kazini. Watanzania wanaokaa nje ambao sasa ni zaidi ya milioni tatu, ni nguvu moja kubwa ya maendeleo ya nchi yetu na hatuwezi kuwaacha wakae hivi hivi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuwajengee mazingira mazuri yatakayowafanya washiriki katika mipango ya kuleta fedha nchini kwao na wenye hawakuisaliti Tanzania. Hii dhana ya kufikiria kwamba wananchi wanaokaa nje ya Tanzania ni

wasaliti, ni dhana potofu. Wale si wasaliti kwa Kiingereza *they are not traitors, they are just smart*. Wamekwenda kupalilia na kulimia nje, wamekwenda kuhemea kule nje ili walie kivulini. Nina hakika mtaniunga mkono na mtatuunga mkono *Foreign* kwamba wakati umefika wa kuwa na *smart citizenship*. Nyinyi mnaita *dual citizenship*, lakini mimi naita *smart citizenship*. Wananchi amba ni *smart* wako nje ya nchi, wanahemea kwa ajili ya nchi yao, kwa ajili ya kusomesha ndugu zao, kwa ajili ya kusomesha shangazi zao, kwa ajili ya kusomesha watoto wao, kwa ajili ya kutibu watu wao, wapate mikopo kwenye benki wanazokaa, wapate kazi nzuri kule wanakoishi ili walete pesa zinazolingana na zile zinazopatikana Ghana, hela zinazolingana na Kenya, mabilioni ya dola kuleta kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Nawashukuruni Waheshimiwa Wabunge kwa kazi ya kuunga mkono hili na vita hii tunaendelea nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la Nairobi-London-Maputo. Hati za majengo na *status* yake. Ningependa tu nithibitishe kwamba ni kweli tunayo matatizo ya hati na hili ningeweza kulisema hata la Uganda ulivyosema katika mchango wako. Tatizo la jengo letu la Uganda ambalo tulilipata wakati wa vita mwaka 1980 baada ya majeshi yetu kuingia Kampala, hakuna *document*. Kwa hiyo, tunashindwa, na tunazungumza na Serikali ya Uganda, wamefanya *search*, tusije tukachukua nyumba ya mtu na tukafanya shughuli tukawa *embarrassed* na inawezekana wengine wamekufa. Kwa hiyo tumepata tabu sana kupata nyaraka za kuthibitisha na kulichukua lile jengo ili kulifanya tunachotaka kukifanya. Lakini jitihada zinaendelea na hivyo hivyo kwa majengo mengine tulipoteza nyaraka. Nyaraka hazikuwepo siyo kwamba tulipata tukazipoteza, nyaraka hazikuwepo. Kwa hiyo nchi mbalimbali zinajaribu kufanya kila linalowezekana tuweze kupata nyaraka ili tuweze kumiliki vizuri majengo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa London nafurahi kutangaza kwamba, kwa majengo yetu ya London sasa tunayo hati. Nairobi na Maputo tutapata lakini pia mtakumbuka wenzetu kwa upande wa Maputo tunapata tabu sana. Jengo lilijengwa na Waren, walipoondoka hawakuacha nyaraka zozote, hata tulipowafuata wakasema ni siri yao. Kwa hiyo, sasa tuna mpango wa kutengeneza tu nyaraka mpya kwa kushirikiana na Serikali ya Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Rada BAE. Niyaseme mambo matatu. La kwanza, nitumie nafasi hii kushukuru sana Kamati ya Bunge lako Tukufu iliyongozwa na Mheshimiwa Job Ndugai, yupo Mheshimiwa Zungu, yuko Mheshimiwa Cheyo na yupo Mheshimiwa Kairuki. Viumbe hawa na Waheshimiwa hawa wamefanya kazi nzuri sana kule London. Lakini wamefanya kazi nzuri London kwa sababu ya umoja wa Bunge hili. Kwa sababu ya msimamo wa Bunge hili. Nilifarijika sana kwamba tulipotoa *statement* yetu ya Serikali, kuna wale walioshangilia wazi wazi na wale walionikonyeza kwa *body language*, Bunge lote liliunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nawaangalia sana na wenzangu wengine nikawa napata kope kope tu na watu wanashangilia kidogo. Anagonga na mguu, niliwasoma. Baada ya msimamo wa nchi yetu kujulikana na hasa baada ya Bunge lako Tukufu kuonesha msimamo, Bunge la Uingereza limeunga msimamo wa Bunge la Tanzania kwamba pesa milioni 29.5 lazima ziende kwenye Serikali yetu, Serikali ya

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini siyo hilo tu Serikali ya *Conservative* narudia, naweka neno *Conservative* makusudi. Serikali ya *Conservative* ambayo kama wangekuwa wanachukua *ideological positions* wangeweza kabisa kutupinga. Lakini walikwenda *beyond politics* wakaenda kwenye *principles*. Serikali ya *Conservatives* ya Uingereza imeacha *ideological positions* zetu na kwenda kwenye *principles* na napenda kulitangazia Bunge hili kwako kwamba Serikali yote ya Uingereza kwa pamoja imeiambia *BAE* ipeleke fedha milioni 29.5 kwenye Serikali yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnapoungana na kushikana katika masuala ya maslahi ya Taifa mnafanikiwa na hii ndiyo Tanzania aliyoiacha Mwalimu Nyerere. Lazima tuungane na napenda tena kusema nawashukuruni wote. Lakini hata kama kuna wachache walitupinga, walifanya hivyo kutekeleza hatima ya demokrasia, sasa nini kilichotokea. Kilichotokea sasa *BAE* imepewa *ultimatum* ya kutuma pesa zile kwenye Serikali yetu na nimemwomba kaka yangu Mkulo awapatie *account number, route number, bank number* na awape *deadline* na watoe na *interest* mle ndani kwa kutukalisha miezi sita na fedha zile. Narudia kwenu hakuna muujiza wa kwenda popote mbali ya kuja Serikalini, tusipoteze wakati, hili jambo limekwisha, *read my lips*. (*Makofi*)

Hakuna *account* ya ajabu ajabu inayokwenda *BoT, read my lips*. Hela zetu, za wafanyakazi wetu, za walipa kodi wetu, lazima zije kwenye Serikali na ningependa kwa faida ya Taifa waelewe sababu iliyotolewa ya kwa nini fedha hizi lazima zije Serikalini. Sababu za msingi ni mbili. Moja toka tumepata uhuru Serikali zote zinazopita Uingereza zinatoa pesa zake za *ODA* na hizi za *GBS* pamoja na *bilateral assistance* kupitia *DFD, DFDA* kupitia kwenye Serikali yetu kwenda kwa wananchi na hata mwaka mmoja haujatokea Waingereza wameishutumu Serikali kwamba imechachukua, wamejenga hoja pale, 29.5 za *BAE*. Lakini hoja ya pili ni hii. Wewe *BAE* ni nani? Wewe ni mwanasiasa? Wewe ni muuzaji wa silaha, ni muuzaji wa rada, wewe mambo ya siasa haya, mambo ya siasa na huduma kwenye Bunge, kwenye Serikali umejifunza wapi? Waachie watu wa siasa masuala ya siasa. (*Makofi*)

Leo *BAE* anajifunza kuwa mwana siasa, aongee na wanasiisa wa Tanzania kuamua wema wa bandia kwamba ana hela za kutupa sisi, hata kidogo. Sasa huko waliko *BAE* tunawaambia *that money must come, and come it must*. Wasubiri *route number* na *account number* ili wazilet pesa zetu. *On short of that, tutapeleka kesi yetu sasa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili awaburuze Mahakamani na nawaambieni hawapo tayari kwenda Mahakamani. Zitakuja tu.* (*Makofi*)

Lakini lipo jambo la pili la kulisema. Sasa Mheshimiwa Machali anasema pale, nina imani sana na wewe. Mpaka akavizungumza vitu vingine nisivyovitaka. Sikiliza bwana, samahani Mheshimiwa Mwenyekiti. Asikilize Mheshimiwa, wala sizungumzi hapa kutohana na imani ya Waheshimiwa Wabunge, najua tuna imani ya wananchi. Tunafanya kazi hizi kwa imani ya wote. Tulichokifanya na tunachoendelea kukifanya ni kwamba suala la *BAE* limegawanyika makundi mawili na hili naliweka *clear* kwa nia nzuri sana.

Kundi la kwanza *BAE* ni kazi ya *Foreign* na kazi yetu ya *Foreign Affairs* pamoja na *Foreign Affairs* ya Uingereza ambayo ni ya *International Cooperation*, tulikuwa tunafanya kazi ya kuhakikisha kwamba baada ya kumalizika kesi siku ya tarehe 21 Desemba mwaka 2010 sisi Wizara hizi mbili tulikuwa tunahakikisha kwamba tunafuatilia fedha ili zirudi. Jukumu hili ndilo lililopewa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kufuatilia fedha ambazo ilikuwa kwenye *jurisdiction* au mamlaka yangu ili zirudi nchini na sitalala usingizi mpaka zirudi hizi hela zote *and to the point*, wale waliokuwa wanataka hela hizi zipitie kwenye *account* zingine zingeliwa, zisingefika zote, sasa tunataka zije zote. Sasa hiyo ndiyo *the first function* na ndiyo *responsibility* ya kwanza ya *BAE*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi la pili la *BAE* ndio linalo-*deal* na watuhumiwa, hilo ndio linakwenda kwenye *Good Governance, TAKUKURU* na Katiba na Sheria. Hili halipo kwangu na wala sioni haya kulisema halipo kwangu; lakini itoshe tu kusema, watuhumiwa wapo na tutawapata mbele ya safari. Watuhumiwa wapo, asije mtu kusema kwamba kesi hii tunarudishiwa hela zetu hakuna watuhumiwa! Hapana! Hapana! Watuhumiwa wapo. Vyombo vinavyohusika watabaini, lakini...

WABUNGE FULANI: Wataje, wataje!

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshasema sio kazi yangu!

MWENYEKITI: Waheshimiwa tusikilizane. Hamfuatilia vizuri. Kwa hiyo, kama mme fuatilia vizuri, sio kazi ya Wizara yake kutaja watuhumiwa, viro vyombo vinavyofanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Waziri, endelea. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na hilo limeshakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala sasa la kigezo kinachotumika kuteua Mabalozi na kwamba, Mabalozi wengine ni wazee. Sasa nijibu kwa (a) na (b).

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kigezo kinachotumika kuteua Mabalozi kote Duniani ni *discretionary*, kwa Kiswahili chake ni pale inapompendeza Kiongozi wa nchi, nani amteue; kama anavyoteua Waziri wa Mambo ya Nje, ukiuliza vigezo vyenyewe ni nani anayevijua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikikupendeza, inasema vile! Ikimpendeza Mkuu wa Nchi, anachagua Mawaziri, anachagua Wakuu wa Mikoa, anachagua Mabalozi. Kwa hiyo, imempendeza ndio maana watu wanachaguliwa na sasa hivi wako watu wanashubiri na Rais imempendeza. (*Kicheko*)

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini tuna wazee *over 60 years?*

(i) Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee dawa! Hivi ni nani huyo anapita kusema kwamba leo Dokta Mrema, ubavu wa mzee ukilala vizuri akawa Balozi London, ni nani atamlaumu Dokta Mrema! (*Makof/Kicheko*)

(ii) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba kwa bahati mbaya, tulipitia kipindi cha miaka 90 ambacho Serikali ilahirisha ajira.

Katika kipindi kile kwa vyovyothe vile tulikosa *generation* ya vijana kuingizwa katika nafasi hizi. Matokeo yake sehemu kama *Foreign* ukakuta watu kwa ile *gape* ya miaka 10 mpaka 15, basi wale waliokuwa miaka 45 wakati ule ndio hao mnaowakuta mnasema ni wazee. Lakini nikiwapigia simu wanasema Mheshimiwa Membe, bado sisi ni vijana na tuna nguvu, utuache tuendelee. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la Mkataba wa *Mwalimu Julius Nyerere Convention*. Mheshimiwa Mtema, amezungumza jambo kubwa na mimi mwenyewe nikastuka, nikasema ni lazima nilifuatilie kwa haraka sana lisije likaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jibu nililonalo ni kwamba Balozi Mombo, ambaye alikuwa Katibu Mkuu wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, alisaini Mkataba huo pamoja na Kampuni hiyo ya Wachina. Sasa Mkataba huo Mama, ambao ni *Parent Agreement*, ulisainiwa kabisa na Katibu Mkuu, Balozi Patrick Mombo. Halafu Mikataba midogomidogo iliyotokana na Mkataba Mama, ilisainiwa na *Acting DAP*, kwa maelekezo ya Katibu Mkuu, ambaye alikuwa safarini wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naweza nikatamka tena kwa sababu siwezi kusema jambo lisilo la kweli humu ndani; Mikataba ile sasa imebainika kwamba, ilisainiwa. Ningeshangaa kama Taifa kubwa kama la Wachina, wangekubali kufanya mambo chini ya uvungu na hasa nikiwepo mimi mwenyewe, hatuwezi kukubali kusainisha mikataba hii chini ya uvungu uvungu, Awamu ya Nne haifanyi hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la kaka yangu Lwanji! Sasa hapa pana shilingi, shilingi ya kwanza hii nadhani imeshawezekana; sasa iko shilingi ya pili ya Kaka yangu Lwanji! Kaka yangu Lwanji, amezungumza kwa hasira kidogo mpaka alifika mahali anahojo ni kwa nini Wizara inatembea na magari meusi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Kanuni ya Magari ya Wizara za Mambo ya Nje. Kanuni hii ni pekee kwa Wizara za Mambo ya Nje kwa sababu, magari yake ndio yanayotumika kupokea wageni wa Kimataifa na rangi nyeusi sio mbwembwe, ndio rangi iliyoteuliwa na Wizara karibu zote za Mambo ya Nje duniani. Jamani, tupo tu kwenye huo mstari na sio mbwembwe za Membe, kuleta magari meusi Wizara ya Mambo ya Nje, hata kidogo! Lakini pia kwa ukali huo huo akasema unaona sasa, hata picha ukienda pale mlangoni unakuta!

Mheshimiwa Mwenyekiti, picha anayoisema Mheshimiwa Lwanji, ni bango linaloleaza diplomasia ya urchumi. Wala haina dhambi, bango la Wizara kubeba jina au

picha ya bosi wao na nimependeza sana pale, hakuna anayeikasirikia na inapendeza vizuri. Lakini Mheshimiwa Lwanji, kama unanishauri nikaitoe, nipo tayari kuitoa kesho. Wala sio mbwembwe, tulikuwa tunauza tu diplomasia ya uchumi kwa mtu anayekuja kututembelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme tena, kama kuna Wizara inapata wageni wa nje na wa ndani, ni *Foreign Affairs*. Katika siku zangu zote ninazokaa na mashahidi ni Watanzania, wanapojaa kwenye kumbi zote kupokea wageni hawa! Leo ninapokuja kuambiwa na mwenzetu kwamba tuna mbwembwe! Ofisi yetu ipo sawa na *State Department*, kwamba hatutaki kuwaona watu na kama Mbunge haendi, je, wenzetu wengine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wangu wa Jimbo la Mtama, wanajaa pale! Sio Wabunge na wala hawana vyeo vyovyote. Waheshimiwa Wabunge, ninyi ni mashahidi, watoto wenu, wana wenu na wajukuu na watu wengine wote wanakuja Wizara ya Mambo ya Nje. Kama hilo lilimtokea kaka yangu Lwanji, wala hakuwa na sababu ya kuzungumza maneno makali ya aina hiyo! Najua ana akili! Najua anaipenda nchi yetu, lakini wala hakuhitaji kuzungumza maneno makali kuonesha hoja yake hiyo! Angezungumza kwa lugha ya kawaida tu, ningemwelewa vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna haja ya kwenda mbali zaidi *ku-capture* kitu unachotaka kukifanya, tunakielewa vizuri! Lakini nimjibu basi, suala lake la *MS General Service*, ambalo limeshughulikiwa kwa kikamilifu sana ni suala la miaka 17 iliyopita! Leo nahukumiwa kwa kushughulikia suala hili kwa muda wa mwaka mmoja na nusu! Tena mwaka wenyewe ni wa uchaguzi wa mwaka 2010! Hukumu hii sio nzuri hata kidogo! Lakini nimweleweshe tu kwamba, ajenda ya *MS General Service*, tumeiweka kwenye mkutano wa pamoja ambao utafanyika tarehe 8 mwezi ujao, mjini Arusha kati ya Tanzania pamoja na nchi ya Burundi, hiyo itakuwa miongoni mwa ajenda. Naomba shilingi yangu ili niende zangu Arusha, nikakufanyie kazi hiyo pamoja na shughuli nyingine za Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijue sasa dakika zilizobaki ili nigonge mawili matatu, kabla sijaomba fedha!

MWENYEKITI: Mheshimiwa, bado una dakika 10. Wewe gonga tu.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nashukuru. Sasa liko suala hapa kutoka kwa Victor Mwambalaswa, Ubalozi wa Uingereza, kwa kweli na Canada pia, kwa sababu Balozi hizi mbili ndiyo zimesemwa, kutolea *Visa* yake nchini Kenya!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, mwezi Mei, 2011, nilipokuwa Uingereza kwa mwaliko wa mwenzangu Waziri wa Uingereza, ajenda ya kwanza niliyoizungumza kwa niaba ya Watanzania, ni lalamiko linalohusu matatizo ya upatikanaji wa *Visa* inayowalazimu Watanzania kuzipeleka *Visa* hizi Nairobi! Mbele ya Balozi wa Uingereza nchini Tanzania, Waziri wa Uingereza wa

Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, aliahidi kulishughulikia suala hili mwaka huu na kumwagiza Balozi kwamba, wafanye kila linalowezekana wapate *scanners*, wapate watu, ili athari ya Watanzania kuomba *Visa* kupitia Nairobi, linalotudhalilisha wote likome. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba uvumilivu wa Waheshimiwa Wabunge na nitaahidi kuja kulitolea maelezo suala hili pindi tutakapopata majibu. Lakini tutalipa nguvu mpya ya kuhakikisha kwamba hili tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine, kutoka Tarime anasema ni nchi ngapi ambazo Tanzania ina Balozi katika nchi hizo na ni nchi zipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni swali kubwa kidogo, lakini nataka niseme nchi zenyе Ubalozi Tanzania ni Algeria, Angola, Belgium, Brazil, United Kingdom, Burundi, Canada, *DRC*, Cuba, Denmark, *Egypt*, Finland, *France*, Ujeruman, Holysea, India, Indonesia, Iran, Ireland, Italia, Japan, Kenya, Korea, Libya, Malawi, Mozambique, Namibia, Netherlands, Nigeria, Norway, Oman, Palestina, Rwanda, Urusi, Saharawi, Saudi Arabia, Somalia, South Africa, Spain, Zimbabwe, Zambia, Yemen, Vietnam, Marekani, Uganda, U.A.E., Uturuki, Syria, Switzerland, Sweden na Sudan. Jumla ya Balozi 52 zipo hapa. Achilia mbali zile ambazo ziko nje ya Tanzania, lakini masuala yote ya Ubalozi yanapotakiwa zinakuwepo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi wenyewe Watanzania ndio tuna Balozi 32. Tuna Balozi Malawi, Zambia, Rwanda, Burundi, *DRC*, Nigeria, Kenya, Uganda, Ethiopia, Brazil, Afrika Kusini, Marekani, Uingereza, Canada, Malaysia, Umoja wa Mataifa Newyork, Ujeruman, Zimbabwe, Ubelgiji, Italia, Sweden, Ufaransa, Japan, India, Misri, Saudi Arabia, Mozambique, China, Oman, Urusi, *Emirates*, Geneva. Ningependa hapa niongeze tena kwamba, tumechukua *very seriously*, angalizo lililotolewa na Kambi ya Upinzani pamoja na wenzetu, kwamba ni vizuri tukawa na *Trade Offices* lakini pia sehemu kama Gwanzuu, ambayo ina Watanzania wengi ambao wanakwenda kufanya biashara pale, tukaipa hadhi ya kuwa na Ofisi Ndogo. Mheshimiwa Wenje, hapo umenigusa vizuri sana na hilo ni lazima mimi na wewe tushirikiane kulitekeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Wenje, aliuliza tena swali kwamba labda huu Waraka Namba 64 umepitwa na wakati? Nilishajibu haujapitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dokta Shukuru Kawambwa, Balozi za Uingereza na Canada, kuhamisha utoaji wa *Visa*? Hili nalo nimeshalijibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imechukua hatua gani kwa Balozi zilizopata hati za hesabu zisizoridhisha? Sasa kinachofanyika ni kwamba pale ambapo imebainika kwamba, kwenye Ubalozi fulani kuna matatizo ya uhasibu ya makusudi na ya uzembe wa makusudi, wanakuwa wanaitwa na wanakuwa *reprimanded* na kuonywa! Akishaonywa zaidi ya mara mbili na harekebishiki, basi hatua za kinidhamu, za kiutumishi

zinachukuliwa. Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita tulirudisha Wahasibu nane Makao Makuu. Wahasibu hao walitoka bada ya kupata hati chafu na baada ya kubaini kwamba matatizo hayo yalitokana na wao, tuliwarejesha nyumbani na kuwapeleka wapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa John Mnyika, Kifungu Namba 1002, ni sababu zipi zilizosababisha, ni kwa nini pesa hizi zimekuwa nyingi huku tofauti na mwaka 2011?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kasma hii imekuwa na fedha nyingi za bajeti kwa mwaka 2011/2012 kwa kuwa ukomo wa bajeti kwa mwaka 2010/2011 ulikuwa kidogo zaidi. Aidha, baadhi ya fedha za mafunzo kwa mwaka wa fedha 2010/2011 zilikuwa katika Idara ya Utawala na Rasilimali. Lakini kwa mwaka wa fedha huu, bajeti yote ya fedha za mafunzo zimepangwa katika kifungu hicho cha 1002.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Kasma Namba 210500, Kifungu Namba 1005, kinahusu Stahiki za Mkurugenzi na Wakurugenzi Wasaidizi wa Idara. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, kasma hii ilipangiwa bajeti ndogo kutokana na ufinyu wa fedha za bajeti. Lakini kutokana na ongezeko la bajeti kwa mwaka huu wa fedha, kasma hiyo imeweza kupangiwa fedha za bajeti za nyongeza. Ni matumaini yangu kwamba, hapa shilingi nayo ya ndugu yangu John, nimeinasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Magdalena Sakaya alizungumzia safari za nje za Viongozi Waandamizi. Sasa ningependa niseme hivi kwamba, mwaka jana katika hotuba yangu nilizungumzia suala la safari za Viongozi nje ya nchi. Nikasema kwamba Rais, ametuagiza tufanye *study*, *comperative study* na tuone namna ya kupunguza safari zile. Kwa muda wa kipindi cha mwaka mzima tumefanya *research* ya nchi zote za Afrika na tukaona mambo kadhaa. Lakini itoshe tu niseme kwamba, Mheshimiwa Rais, ameridhia kwamba idadi ya Maafisa au idadi ya Wajumbe katika misafara ipungue. Katika kipindi cha mwezi sasa kwa safari ya *Seychelles* kwa mfano, tulituma wajumbe 30 na katika safari ya Afrika ya Kusini, tulijaribu kwa majaribio kabisa kutuma wajumbe 34.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuliomba Bunge lako Tukufu, kwamba zipo sababu za kiusalama zinazosababisha wakati mwingine tuwe na wajumbe wengi kidogo. Niseme kwa waziwazi kabisa kwamba, kwa mfano, unapompeleka Mheshimiwa Rais, kwenye nchi ambayo usalama wake uko mashakani, kutokana na taarifa za wenyeji kwamba, mnapofika huku mje na ulinzi wa kutosha. Kwa hiyo, ulinzi kwa Mheshimiwa Rais, unaimarishwa zaidi. Lakini sio hilo tu, hata ulinzi kwenye ndege, haupaki tu pale kiwanjani na kuiacha kama inavyokuwa *commercial flights*, ndege ya Kiongozi wenu inabidi ni lazima ilindwe pale. Kwa hiyo, haya ndio maeneo mengine ambayo yanasaababisha watu kuwa wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu wakati mwingine idadi inategemea unakwenda nchi gani. Wakati mwingine kiongozi anakwenda kwa shughuli za uwekezaji kwa shughuli za biashara, kwa mfano, kama safari ya juzi. Kwa hiyo, safari za aina ile

mnaweza mkaona wajumbe wanakwenda kwa wingi zaidi, kutegemea na madhumuni ya safari ambayo Mheshimiwa Rais, anaifanya. Lakini naomba niwaahidi Waheshimiwa Wabunge, tuvute subira, tutakapotoa orodha kamili ya *categorisation*, kwamba kiongozi fulani atatembea na watu kadhaa, kiongozi fulani atatembea na watu kadhaa na kutakuwa na *flexibility*, tutakuja kuitoa taarifa hiyo kupitia kwenye Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, ndugu yangu Machali, aliniulizia suala la Ngara, majibu tafadhali! Sasa Mheshimiwa Machali, naomba nilijibu swali hili wakati wa shughuli hizi. Kwa sababu, jibu lake sina hapa na sitaki kujibu kutoka kichwani, lakini wataalam wangu watakuwa wamenisaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa.

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 34 - Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa

Kif. 1001 - *Administration and General* Tshs.4,729,578,000

MWENYEKITI: Sasa kila atakayekuwa anatajwa basi atakaa.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Fungu hilo la Mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Mimi sito hata thumni ila nitaongeza shilingi. Ninataka anisaidie kitu kimoja; kuna Watanzania wengi amba wanishi nje ya nchi hasa Kenya, wakishafika mpakani wanakuwa hawasumbuliwi, lakini wakiwa ndani ya Kenya wanakuwa kila siku wanasumbuliwa sana; mara kitambulisho, mara *passport* na mwisho wananyanyaswa kwa kiasi kikubwa sana. Sasa kwa kuwa hizi nchi ni moja ya Nchi za Afrika Mashariki; Waziri ananiambia nini kuhusiana na Watanzania wanaoishi Kenya? (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Ngonyani, kwa swali lake nzuri. Wiki moja iliyopita, Waziri mwenzangu wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Vuai, alituma ujumbe Kenya wa kufanya uchunguzi wa madai yanayolingana na haya na ujumbe ule ulirudi na tulipata majibu ya kuridhisha. Ninaomba Mheshimiwa Ngonyani, utuachie sisi swali hilo ili kwa kushirikiana na Ubalozi wetu, pamoja na Vyombo vingine vya Serikali, tufanye kama tulivyofanya wiki mbili zilizopita, tulijaribu kuangalia kero za Watanzania waliopo Kenya na pia kero za Watanzania waliopo Doha, amba wametuandikia na wameeleza hali hiyo na tutafutilia tutakupa majibu ya kuridhisha.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Mimi ninataka ufanuzi kidogo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri; Waziri alipokuwa anajibu suala la *Dual Citizenship*, nilipata picha ambayo sikuilewa kidogo; maana Waziri alisema kwamba, tunaendelea na vita hii. Sasa kama Kiongozi wa Serikali, akitoa kauli hiyo ninashindwa kuelewa kwamba inapokelewaje na Watanzania! Kwa hiyo, nilitaka tu anifafanulie kwamba; kuna ugomvi gani au kuna matatizo gani katika suala hili mpaka Waziri aseme kwamba tunaendelea na vita hii; ni vizuri Watanzania wakaelewa? Ninashukuru sana.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, vita hii nilikuwa na maana ya kusema mjadala huu; samahani sana kama nilikwenda nje kumaanisha vita ya kwetu, ni mjadala unaoendelea kati ya Wanazuoni na Wataalam mbalimbali.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, nilitaka kujuu kwa miaka yangu yote mitano nimekuwa ninazungumzia habari ya mpaka wa Ziwa Nyasa kati ya Malawi na Tanzania na jibu limekuwa ni hilo hilo tutafanya, tutafanya; tunashindwa kuwekeza na wawekezaji wanakuja; je, suala la mpaka litakwisha lini?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la shemeji yangu, Mheshimiwa Komba, kama ifuatavyo:-

Marais wawili walipokutana mapema mwaka huu; Rais Kikwete na Rais Bingu Wa Mutharika, waliagiza kwamba, Wizara mbili; Wizara ya Mambo ya Nje ya kwetu pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje ya Malawi, waifanye kazi hiyo. Wataalam wameanza kazi hiyo na tunakusudia katika kipindi cha mwaka huu, mimi na mwenzangu, tutakutana kuititia Taarifa ya kina ya Wataalam wa pande zote mbili, zinazohusu mgogoro wa mpaka kwenye Ziwa Nyasa na kote kule kati ya Malawi na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hilo tu, Kamati ile pia inaangalia uwezekano wa kuimarisha ulinzi na kuona uwezekano wa kurudisha Majeshi yetu ya Ulinzi kwenye vituo vya mpakani kwenye eneo ambalo Mheshimiwa Komba anatoka. Ninamwomba Mheshimiwa Komba, avute subira na hili ninalisimamia mwenyewe.

MHE. REGIA E. MTEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninaelezea kuhusu *Julius Nyerere Convention*, nilikuwa nime-refer kwenye Taarifa ya CAG iliyotoka tarehe 26 Machi, 2011. Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, Katibu Mkuu alisaini Mkataba huu. Kwa hiyo, maana yake Ripoti hii ya CAG haina uhalali. Swali langu; ninapenda kujuu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilipitia Mkataba huu ama laah; kama ambavyo CAG ameeleza?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijibu hivi; pale tumezungumza neno la Mikataba

Mama; *Mwalimu Julius Nyerere Convention Centre* inajengwa na *Concession Law* ya China. Mkataba Mama kwa vyovyote vile utakuwa mikononi mwa China. Ninaomba nipate muda, tuone kama *CAG* alikuwa na *access* ya Mikataba Mama. Taarifa ya ofisi inajieleza kwamba, Mkataba Mama ulisanowi na Balozi Patrick na ndiyo wakati ule tulivyokuwa tunafanya jambo hili.

Mimi ningeomba nikirudi Wizarani, tuulize wenzetu wa China, ambao ndiyo wenye Mradi, maana wanatujengea ili tupate nakala itakayothibitisha hilo. Inawezekana wakati Timu ya *CAG* ilipokwenda Wizarani ilikutana tu na Mikataba Midogo Midogo na siyo ule Mkataba Mama, ambao nimeusema mbele ya Bunge lako Tukufu. Ninaomba tupate muda ili baadaye tulitoe.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kupitia kifungu hiki cha Mshahara wa Waziri, ningeomba kupata ufanuzi kuhusu jambo moja la Kisera. Ninaelewa kwamba, jukumu mojawapo la Kisera la Wizara hii ni kujenga taswira pana ya nchi yetu Kimataifa. Sasa kuna suala mahususi ambalo nililiuliza kuhusiana na tuhuma juu ya Watanzania kushiriki kwenye masuala ya uuzaji wa silaha haramu ambazo zinachafua taswira ya nchi yetu.

Ninaelewa kwamba, Mheshimiwa Membe, analifahamu jambo hili, kwa sababu mwaka 2000 lilijadiliwa kwenye Baraza la Usalama wa Umoja wa Mataifa na mwaka wa 2006 lilijadiliwa vilevile Umoja wa Mataifa. Sasa ningependa kupata kauli ili tusichafuke kama Watanzania, kwa sababu ya matendo ya watu binafsi kuhusiana na tuhuma hizi hususan tuhuma zinazoihusu Kampuni ya Meremeta, kwa sababu wengi wamezoea kufikiria kwamba, ilikuwa ni kashfa sijui ya utoroshaji wa madini peke yake na ufisadi wa pesa za Watanzania shilingi bilioni 100, lakini kuna tuhuma nzito vilevile za kuhusiana na utoroshaji wa silaha. Kwa hiyo, ninaomba ufanuzi kuhusu hilo.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sahihi kabisa kusema kwamba, Watanzania na hasa Wizara yetu, wanayo haja ya kujua nini kinachoendelea na kuthibitisha madai mbalimbali yanayotolewa kama hili ambalo limetolewa na Mheshimiwa Mnyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala alilolisema Mheshimiwa John Mnyika ni zito, linastahili kutoa majibu ya uhakika na nilivyojiandaa leo katika shughuli hizi, suala la silaha na suala la Meremeta, halikuwepo kwenye *vocabulary* yangu. Tunaomba suala hili tulitafutie muda ili tuweze pengine kulitolea majibu, sitaweza kutoa majibu ya haraka haraka kwa swali zito.

MWENYEKITI: Ahsante. Hata hivyo, huo ni ufanuzi; ni masuala yanayohusu ulinzi na usalama; ni masuala yanayohitaji mazingira maalum; kwa hiyo, Mheshimiwa Mnyika, ninaomba uridhike. Sasa nitamwita Mheshimiwa Hamad Ally.

MHE. HAMAD ALLY HAMAD: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami katika mchango wangu wa maandishi, nilitaka kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri; kwa kuwa Tanzania tumekuwa tukishuhudia raia au wakazi wa nchi nyininge katika vipindi

vya uchaguzi katika nchi zao wanakuwa na maandalizi ya kupiga kura wakiwa hapa Tanzania. Sasa nilitaka kujua kwa Watanzania walioko nje ya nchi ambayo inasemekana ni zaidi ya milioni tatu; tuna mpango gani wa wao kuweza kupiga kura wakati wa Uchaguzi katika nchi yetu?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema sasa tunajikita katika kuimarisha *Diaspora* na suala la *Dual Citizenship*; moja ya faida, tukishapata idadi ya Watanzania, tukishawashirikisha katika masuala ya maendeleo yetu, tukishaondoa kero zao hasa suala la *Dual Citizenship*, tutakuwa na takwimu za Watanzania walioko nje, tutakuwa na takwimu za viongozi walioko nje hata sehemu zile ambazo ubalozi haupo na itakuwa rahisi kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzisha sasa Sera ya kuwataka Watanzania wanaoishi nje, kushiriki kwenye Demokrasia ya Uchaguzi. Twende na suala la *Diaspora* na *Dual Citizenship* halafu tutafika kunakotakiwa.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninapenda nipate ufanuzi kutoka kwa Waziri katika kifungu cha *Hospitality and Supply Service*. Ukiangalia kwa Wizara nzima, hiki kifungu kimepangwa tofauti tofauti; kuna baadhi ya Balozi wamepewa fedha hizi, lakini kuna Balozi zingine hawajapewa. Halafu Idara ya *Communications and Education* wamepangiwa shilingi 1,202,000,000 na Idara ya *Protocol* milioni 517, wakati Idara zingine wamenyimwa.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninadhani tunaangalia kifungu namba 1001; sivioni hivyo kama visto mbele angenisubiri halafu nijibu vizuri.

MWENYEKITI: *Okay, sawa sawa, upo sahihi Mheshimiwa Waziri; ninadhani hiki unachozungumzia Mheshimiwa Mbunge kipo mbele, ukifika wakati wake basi utaauliza fungu hilo. Sasa nimwite Mheshimiwa Dkt. Kigwangala.*

MHE. DKT. HAMIS A. KIGWANGALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii. Mimi ningependa tu nipate ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwamba; katika zama hizi za uchumi wa pamoja kwa maana ya *globalization*, kumekuwa kuna ushindani mkali sana, ambao unaelekezwa kwa washindani wa upande wa pili. Sijui Tanzania sisi tumejipanga vipi ili kuweza kuukabili ushindani wa Makampuni makubwa ya Kimataifa ambayo siku zote yamekuwa yakiingia nchini kwetu yakikomba *resource* zetu, yakiiba *resource* zetu kuitia njia haramu, mikataba ya ovyo na isiyo na tija; na mwisho wa siku tunajikuta sisi tunapoteza.

Mheshimiwa Waziri anatueleza nini kuhusu uwezo wetu wa kushindana katika *ku-negotiate* na makampuni ya nje? (*Makofii*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa suala hili lisingekuwa langu sana, lakini ipo sehemu inanihu kama Mwanadiplomasia wa Kiuchumi. Sehemu ambayo Wizara yangu

inahusika katika masuala ya biashara (*investment*) na Mataifa Makubwa, ni pale Balozi zetu zinapoagizwa ku-*cross check*, yaani kuangalia uhalali, kuwepo na ukweli wa hasa makampuni yanayokuja kwenye *briefcase* hapa nchini na kujaribu kutapeli au kuchakachua shughuli hizo na Watanzania wanaowakuta hapa. Nitumie nafasi hii kutoa wito kwa Watanzania, Viongozi wa Mashirika, Viongozi wa *NGOs*, Viongozi wa *Investments* na Biashara mbalimbali, unapopata mtu kutoka nje kwenye Mataifa hayo, anayedai kwamba, yeze ni mwekezaji au ana biashara nzuri, tafadhal sana wasiliana na Ubalozi wetu au Ofisi yetu ili tufanye *cross checking*, ndiyo hii ambayo wenzetu wa Upinzani leo asubuhi waliita *economic intelligence*.

Sisi tunatakiwa tuchunguze kwanza uhalali au uzuri wa hiyo kampuni kabla hatujaingizwa kwenye mkenge au kabla hatujaingia kwenye shughuli hizo. Kwa hiyo, hiyo ndiyo sehemu ambayo mimi ninaona tunahusika zaidi. Nina hakika kabisa, kwa hali ya mazingira ya sasa ya kiuchumi, nchi yetu ipo tayari kabisa kupambana na wenzetu, kwa sababu tunazo Sheria na Kanuni za *Investment* na *Business* kutoka *Tanzania Investment Centre*, ambazo zinaifanya kabisa nchi yetu iwe *competitive*. Kwa upande wa Wizara yangu, ombi langu ni hilo kwa wawekezaji wa nyumbani.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ufanuzi ni mzuri sana na pengine ni vizuri Wananchi wakaandaliwa *Desk Maalum*, kwa sababu ushirikiano katika biashara, mambo mengi ni makubwa sana kati ya Watanzania na Wageni. Kwa hiyo ni vizuri kukawa kuna *Desk Maalum*, kwa ajili ya kazi hiyo. Tunaendelea Mheshimiwa Mwanjelwa.

MHE. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Nilipokuwa ninachangia asubuhi, nilielezea suala la *economic diplomacy* na hii ni katika nchi za nje na ushirikiano wetu wa Kimataifa. Vilevile tukumbuke kwamba, *economic diplomacy* ipo hata hapa nchini. Katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 34, amezungumzia kuhusu Kituo cha Kimataifa cha Mikutano pale Arusha; sasa nilikuwa ninataka kujua kwa nini iwe Arusha tu kwa sababu tuna mikoa mingine hapa nchini mfano, Mbeya, Mwanza na kwingineko?

Pamoja na kwamba, hiki Kituo kinaweza kikawa na *quantity* na *capacity* zake na *asset* zikawa ni nyingi na pengine kinaweza kikawa kinapanua uwigo wa Kituo cha *AICC* pale Arusha; lakini yawezekana hata Menejimenti yake ikawa siyo nzuri. Ningombaa Mheshimiwa Waziri atufafanulie. Ninashukuru.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazo zuri kabisa, lakini majibu yenyewe ndiyo haya kwamba, *Arusha International Conference Center* ilijengwa zamani, miaka ya 70 na kwa kweli ule siyo Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano ambao unawenza uka-*compete* na Kenya, unawenza uka-*compete* sasa na Uganda na nchi nchi ambazo zimetuzunguka.

Kwa hiyo, wazo la *AICC* pamoja na Wachina ambao walifanya *feasibility study*, wakasema ni vizuri pale Arusha tukawa na kitu kinachoitwa *Convention Centre*, ambayo

ni babukubwa ya hii *Conference Centre*, ambapo hata sisi tunapokutana kwenye Afrika Mashariki hatutoshi.

Sio hilo tu, Ukumbi ule wa *AICC* sasa umevamiwa na vikundi vingi sana; kuna *East African Legislative Assembly*, Bunge lao limo mle ndani, kuna suala la *ICTR* Mahakama yao ipo kule ndani, halafu Wafanyakazi wamejaa sana. Kwa hiyo, ilikuwa ni wazo letu, pamoja na *AICC* na kwa sababu wana ardhi ya kutosha ni kwamba, ili *tu-compete* na Kenya na ili tupate *conferences* katika Ukanda huu wa Afrika Mashariki na *COMESA*, pamoja na kila kitu, ni vyema tukawaweka palepale kwenye Geneva ya *Africa Convention Centre*, ambayo itavunja *record* ili tuweze kupata pesa zaidi na nyingine ndiyo zitasaidia kuiendesha Wizara ya Mambo ya Nje.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Mabumba.

MHE. SYLVESTER MASSELLE MABUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

Katika mchango wangu wa maandishi, nilimwuliza Mheshimiwa Waziri kuhusu utekelezaji wa Sera ya Diplomasia ya Kiuchumi. Balozi zetu zimeweza kutekeleza kwa kiasi gani; kwa maana ya kuvutia uwekezaji kutoka katika nchi ambazo zinawakilisha?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Economic Diplomacy* au Diplomasia ya Kiuchumi katika Balozi zetu, kwa kweli wamejitahidi pamoja na kwamba, bajeti ilikuwa finyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka mitatu iliyopita, kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii, Balozi zetu ziliwezeshewa kiasi cha dola 10,000 katika kila Ubalozi ili kuweza kutengeneza matangazo na vijitabu kuweza kutoa *CDs* za kuvutia utalii nchini kwetu. Zoezi hili lilifanikiwa kwa kiasi kikubwa sana, hasa katika kutoa mabango ya kueneza utalii na matokeo yake ni kwamba, idadi ya Watalii ingawa ilishuka mwaka 2009 na 2010 kutohana na m dororo wa kiuchumi duniani, hali ya utalii ilipanda zaidi baada ya mwaka 2009 na 2010 hadi kufikia watalii wasiopungua milioni 800. Hii yote inatokana na kasi ambayo Mabalozi wetu nje wanajitahidi sana kuleta wawekezaji. Hilo la kwanza.

La pili, ni kwamba, hata katika masuala ya uwekezaji na biashara, kinachofanyika sasa hivi katika Balozi zetu ni utengenezaji wa vitabu vya mahitaji. Hivi karibuni mtaona mahitaji ya biashara zinazohitajika London, kwa mfano, Mabalozi sasa watazitengeneza na kuzileta kwa Watanzania na sisi tutazitoa kwa Watanzania ili kuwaeleza *opportunities* zilizopo kwenye nchi ambazo tuna Ubalozi ili wazihangaikie. Watanzania watapata pia sehemu ambazo zina uwekezaji huko duniani kama Afrika Kusini, Brazil na kadhalika. Mipango yote inaendelea ili kuwaambia Watanzania wenye uwezo wa kuwekeza nje, tutatoa taarifa zote. Kazi hii inafanyiwa *research* na maandishi pamoja na Balozi zetu. Hivo ndiyo *Economic Diplomacy*.

Kutokana na mawazo tulyopeana na Wizara ya Fedha, tunategemea kuunda *Unit* au Idara ndogo ya *Diplomacy*, ambayo itashirikiana na Wizara ya Fedha, pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Kilimo, Wizara yangu pamoja na Wizara nyingine za Kiuchumi ili kuweza kuratibu biashara gani na nafasi zipi zilizopo ndani ili kuwawezesha Watanzania kuwa na taarifa za uchumi, taarifa za mazao ya biashara na kuwa na taarifa za uwekezaji waweze kuhangaikia kwa sababu sisi sasa ni Taifa kubwa.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, kwa ufanuzi. Mheshimiwa Martha Umbulla.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Mimi pia sina tatizo na mshahara wa Waziri, lakini nilitaka ufanuzi mdogo tu kwenye mchango wangu wa maandishi.

Kwanza, nimpongeze sana Meshimiwa Waziri, kwa *support* kubwa aliyoonesha kwa shughuli za *APRM* Tanzania. Kuna jambo dogo ambalo pengine amelisahau ama sikumsikia vizuri, nalo ni la *Autonomacy Legal Entity* kwa *APRM* Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuundwa kisheria kwa chombo hiki ni jambo muhimu sana, kwa sababu siyo tu itapunguza mzigo wa Wizara kutenga fedha kila mara, kwa sababu ikiwa imeundwa kisheria itakuwa na *Vote* yake yenye na wataweza kutafuta *sources* za fedha mahali pengine. Ninajua hilo lipo ndani kabisa ya uwezo wa Mheshimiwa Waziri na umakini alionao ninaoujua; naomba maelezo ili na *APRM* Tanzania iweze kuundwa kisheria kama ambavyo nchi Wanachama wamekuwa nayo ambayo imeundwa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba maelezo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ufanuzi.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Martha Umbulla, yuko sahihi na kwa Watanzania wasiomwelewa vizuri ni kwamba; anachosema ni vizuri *APRM*, yaani huu mchakato wa kujitathmini wenye au kujikosoa wenye, hiki chombo kiundwe kisheria ili kiwe na uwezo wa kuajiri na kufukuza ili kiwe na uwezo pengine hata wa kukosoa ili kuweza kufanya kazi zake.

Tulipokwenda Malabo, Equatorial Guinea, wiki mbili zilizopita, tumeanza kulifanya kazi suala hili katika kuziangalia zile nchi 12 ambazo tayari zina *APRM*; ni utaratibu gani wa kuhalalisha *APRM* kisheria wameufuata. Pindi tutakapopata tathmini ya nchi za wenzetu 12 na sisi hatutasita kuiga, ikiwemo uwezekano wa kuanzisha chombo hiki kisheria.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Manyanya.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu nilikuwa nimezungumzia pia kuhusu umuhimu wa kuharakisha kuundwa kwa Bunge la SADC, lakini katika majumuisho ya Waziri, ninadhani kwa ajili ya muda, sijamsikia kabisa akilisemea hilo, nikiamini kwamba Tanzania ni kiungo muhimu katika kufanikisha suala hilo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ufanuzi.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa rahisi kuunda kwa Bunge la Afrika Mashariki, kwa sababu sasa tuko kwenye *Common Market*, tunaelekea kwenye *Monetary Union* halafu tunakwenda kwenye *Federation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatakiwa nchi hizi ziwe zimeshafikia *level* fulani ya kuweza kujadili mambo kwa pamoja ya kiuchumi, kisiasa na kidiplomasia. Kwa upande wa SADC, hatujafikia sehemu ya *Common Market*, ambayo inawaruhusu watu, bidhaa, fedha na utaalamu wote, ku-exchange kati ya hizo nchi; tumepishanapishana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumaini yangu ni kwamba, baada ya kutoka kwenye *Customs Union*, ikishafika kwenye *Common Market*, nina hakika tutakapokuwa tunaelekea kwenye *Monetary Union*, wazo la kuwa na Bunge *fully-fledged*, yaani Bunge kamili la SADC litakuwepo. Kwa hivi sasa kwa sababu ya mpishano wa nguvu za kiuchumi na kwa kuwa hatujafikia kwenye ile *level* ya *Common Market*, inakuwa ni vigumu kuanzisha Bunge kamili linalojitosheleza upande wa SADC.

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa kufanuzi. Mheshimiwa Dkt. Mrema.

MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kuhusu diplomasia ya uchumi na hasa suala la chakula. Sasa hivi tunaambiwa Sudan ya Kusini kuna njaa kubwa sana, pia Somalia na Kenya. Mwanzoni mwa mwezi Julai, Serikali ilizua mahindi yasiende nchi za jirani, kwa sababu ya upungufu wa chakula. Nimesoma gazeti la juzi wanasema kwamba, kama nchi za jirani zinataka chakula, basi zizungumze na Serikali. Sasa kwa nini Serikali isitumie nafasi hii ya matatizo ya wenzetu ambao hawana chakula ili lile soko lililopo pale Himo katika Jimbo la Vunjo, badala ya kuzuia chakula kisiende na hatuna uwezo wa kuzuia chakula kisiende kwani kinakwenda, badala ya kuhamasisha Jimbo langu pale Himo, Watu wa Sudan wenye njaa wakaja pale Himo, Watu wa Somalia wakaja pale Himo, Watu wa Kenya wakaja na sisi Halmashauri tukapata ushuru na vijana wetu wakapata kazi.

Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, atusaidie katika suala hili la Diplomasia ya Uchumi ili tuweze kupata manufaa ya hizi biashara zinazojitokeza katika nchi yetu.

MWENYEKITI: Ingawa swali lenyewe limetawanyika kidogo, lakini kwa niaba ya Serikali Mheshimiwa Waziri ufanuzi!

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, swali hili ni kubwa lakini urahisi wa kwangu uko hapa; kama Himo ingekuwa na Soko linalojulikana na kufahamika, ningekuwa mstari wa mbele kuliwa Soko la Himo duniani, kwa maana ya Southern Sudan pamoja na Somalia. Sasa sina hakika wakija Himo wanamwona nani; ni mkulima mmoja mmoja au pana soko ambalo watu wana uhakika wa kupata bidhaa zile; kuna soko?

MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA: Lipo.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Basi nitaomba nilipeleke suala hili kwa mwenzangu Waziri wa Kilimo ili alifanyie kazi na kazi hiyo niache niifuatilie.

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa ufanuzi. Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pale Kigoma tuna Ubalozi Mdogo wa Burundi na Kongo, ambao walifanya makubaliano maalum, yaani waliingia Mkataba na Hospitali Binafsi ya Mtanzania inayoitwa *Kigoma International Health Centre*. Kwa miaka 11 sasa, mwenye Hospitali hiyo anaudai Ubalozi Mdogo wa Kongo, sasa hivi kulingana na muda unavyokwenda deni pamoja na riba limekuwa shilingi milioni mia moja ishirini na saba, laki sita na themanini na tatu na shilingi arobaini na nne. Kidiplomasia kwa kweli hawezi kuishaktaki Ubalozi.

Sasa ninapenda kujua Serikali itasaidiaje ili deni hilo liweze kulipwa kwa sababu ni muda mrefu sasa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri sijui umemwelewa? Kama umemwelewa basi unawenza kutoa ufanuzi.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, ameuliza swali ambalo Wizara ina habari nalo na ni suala ambalo Wizara tulikuwa tunalishughulikia na Ubalozi wa Kongo. Ninashukuru *Dean wa Diplomatic Community*, Mheshimiwa Juma Mpango, yupo hapa na anasikia kwamba, Ubalozi Mdogo wa Kongo unadaiwa kwenye Hospitali ile. Hili ni jambo ambalo tunalfahamu na Balozi wa Kongo nchini Tanzania, analifanya kazi. Kwa kuwa leo yupo, nitakapokuwa naye kwenye chakula cha usiku huu, nitamkumbusha vizuri suala hili vizuri na zile takwimu na Mheshimiwa Mhonga unipatie hizo takwimu ili niweze kumkumbusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningeomba kwa nafasi hii nitoe tamko kwamba, uhusiano wetu na Congo DRC ni mzuri sana na ni wa kihistoria. Hivi karibuni kulizuka maneno kwenye baadhi ya vyombo vya habari vikileta mashaka kwamba, Rais Joseph

Kabila, hakuzaliwa Kongo, lakini mambo hayo yalikuwa ni ya kiuadui na *critics*, lakini habari zilienea na zikafika hadi huku kwetu.

Ninapenda kujibu swal la Mheshimiwa Mhonga la kudumisha uhusiano wa kidiplomasia kati ya Kongo na Tanzania, kuwahakikishia Watanzania na kuihakikishia Serikali ya Kongo kwamba, tuna imani na Serikali iliyopo ya Jamhuri ya Kongo, tuna imani na Uongozi wa Rais Joseph Kabila na tuna uhakika kwamba, Rais Joseph Kabila ni mzaliwa wa Kongo, ni Rais wa Kongo, anastahili kuheshimiwa na tujiepushe na mambo yoyote yale yanayoweza kuleta uhasama kati yetu na Kongo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa tamko hili.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Halima Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Nchi yetu imekuwa ikishiriki katika ulinzi wa amani Afrika na Duniani kwa ujumla na hivi karibuni tulipeleka Wanajeshi wetu Lebanon na Darfur. Sasa kumekuwa na malalamiko sana kutoka kwa vijana wetu, ambao wanapeperusha bendera yetu huko nchi za watu kwamba, wanasahaulika sana kulipwa stahiki zao.

Ninataka Mheshimiwa Waziri anisaidie, kwa sababu nilileta kwa maandishi ninajua inahusisha Wizara zaidi ya moja, lakini Wizara yako haiwezi kulikwepa hili; ninaomba unipe Kauli ya Serikali kuhusiana na hili na hatua gani mnatarajia kuzichukua ili tuisiwakatishe tamaa vijana wetu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ufanuzi.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, swal la Mheshimiwa Mdee ni zuri na sahihi. Kwa sababu ni kweli kabisa kwamba, sasa hivi Tanzania inashiriki kwenye ulinzi wa Majeshi ya Amani nchini Darfur na Lebanon.

Pia ni ukweli kwamba, kumekuwa na matatizo ya malipo kwa Askari hawa, siyo yanayotokana na matatizo ya kiutawala lakini yaliyokuwa yanatokana na kiwango kidogo sana cha *allowance*, ambazo Umoja wa Mataifa ulikuwa unatoa.

Leo ninafurahi kutangaza kwamba, mwezi uliopita, yaani Juni, 2011, Kamati inayoshughulikia *Peace Keepers* ya Umoja wa Mataifa, kufuatia ombi la Mabalozi wa Afrika kuhusu Askari wanaofanya kazi kwenye Vituo vigumu kama Lebanon pamoja na Darfur na sehemu nyingine kama DRC, kuwaongezea posho zao ili waweze kufanya kazi zao vizuri. Ninafurahi kutangaza kwamba, sasa posho za Askari hawa zimepandishwa rasmi na ni matumani yangu kuwa, posho za Askari wote wanaotumikia Umoja wa Mataifa, zimepanda kwa karibu mara mbili ya kile walichokuwa wanakipata. Matumaini yangu ni kwamba, Askari wa kulinda amani wa Umoja wa Mataifa kutoka Tanzania waliopo Lebanon na waliopo Darfur, watafanya kazi zao vizuri bila malalamiko.

Tutafuatilia zaidi kujua tatizo lipo wapi hasa; ni udogo wa posho walizokuwa wanazipokea au utawala mbaya ambao ulikuwa unawakumba. Hili ni swali zito na tutalifanya kazi.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa ufanuzi. Kwa mujibu wa Kanuni ya 104(1), kwa sababu wanaotaka ufanuzi ni wengi na ili Kamati ya Matumizi iweze kumaliza muda wake, nitaongeza dakika 30 hadi saa 2.15.

Sasa nitamwita Mheshimiwa John Lwanji.

MHE. JOHN. P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nilichangia kwa kuzungumza na kwa maandishi pia, labda ingewekwa kwenye *record* kwa sababu sikusikia jina langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nimechangia kwa hisia kali kuhusu ...

MWENYEKITI: Mheshimiwa, *microphone* yako hiyo naomba uisogeze karibu.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichangia kuhusu Kampuni yetu ya *Itigi General Business and Equipment Supplies*, ambayo inachimba *gypsum*. Kwa sababu ni suala la muda mrefu na kama ulivyoosikia, Mheshimiwa Waziri amekiri ni miaka 17 sasa na hao watu wana haki.

Mimi ninalilia ajira za watu wangu kwani walikuwa wanaajiriwa pale, lakini wengi wakaondoka kwenda kutafuta ajira kwenye maeneo mengine na kwa sababu hii, sehemu kubwa ya mali za hao watu ilikuwa *impounded*. Kwa hiyo, kwa kuwa nimepata jibu na anasema kwamba, atalipeleka kwenye *Summit* watakapokutana kati yake, yaani Serikali ya Tanzania na Rwanda, basi nitasubiri jibu hilo na hivyo ninaunga mkono hoja maana ni uungwana.

Ila tu nipate ufanuzi kidogo tu pale ...

(*Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lwanji, muda wako umekwisha.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Imetosha, kwani Mheshimiwa Waziri hoja yako ataishughulikia na wala hana sababu ya kueleza tena maana majibu ni yale yale. Sasa ninamwita Mheshimiwa Mbilinyi.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wakati Mheshimiwa Waziri anajibu alisema kwamba, Rais anateua Viongozi wakiwemo Mabalозi ikimpendeza. Sasa mimi ninaona ni ukweli lakini siyo kitu cha kukiongea kwa

mbwembwe kama alivyoongea Mheshimiwa Waziri kwamba, ikimpendeza, kwa sababu haya ndiyo matokeo tunakuwa na upungufu kwa Viongozi wetu kutokana na kwamba, sifa zinazomfanya ateuliwe hakuna zaidi ya kumpendeza Rais.

Mimi ninashauri kwamba, sasa umefika wakati wateuliwa wote wa Rais, yaani *Presidential Appointments* zote za Rais zipitie Bungeni ili Bunge liwahoji na kuwathibitisha au vinginevyo, zaidi ya kumpendeza Rais; sijui Rais huwa anatumia sifa gani nyingine kuteua Watendaji?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ufanuzi.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Mbilinyi.

Suala la kumpendeza mtu ili apate kiongozi liko hata Majimboni kwetu, Wabunge wote wanateuliwa na Wananchi ikiwapendeza wala hakuna vigezo vinavyoweza kutolewa kwenye Bunge lako Tukufu kwamba, tunachaguliwa kwa sababu hii. Upendezaji ule ule wa Wananchi ndiyo unaokwenda kwa *Head of State*, lakini siyo vibaya mbele ya safari na Dunia inafanya, kwenye maeneo ambayo Bunge litapenda na wao waungane katika mtindo ikiwapendeza waweze kuungana na Rais kuteua Mabalozi, ujaribu kufanya hivyo. (*Makofit*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa ufanuzi. Ninamwita Mheshimiwa Haroub Mohamed Shamis.

MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi, niligusia suala la *Diaspora* na *Dual Citizenship*, ambalo nilitaka Serikali iliangalie. Mheshimiwa Waziri wakati anafanya majumuisho, ameitaja hii kama ni *Smart Citizenship* na mimi kwa kweli nimependa *terminology* hii. Kweli hawa watu ni *smart* na mionganini mwao, wapo ambao walitoka nje ku-toil kutafuta elimu, wamepata elimu na wamerudi nchini wanatumikia Taifa hili, lakini wanafanya kazi kama *expatriates*. Sasa Mheshimiwa Waziri amesema hapa kuwa, mchakato huu wa *Smart Citizenship* utakuwa tayari sambamba na uzindulijiwa wa Katiba Mpya. Ninaona kama ni kipindi cha miaka mitatu inayokuja na hawa watu tayari wanalitumikia Taifa na wanakosa zile *incentives* zao za kwamba, wao ni Watanzania.

Je, Serikali haiwezi kuwapa *priority* hawa ikawaweka katika *waiting list* ya *Smart Citizenship* wakawa ni wa mwanzo na wakaanza kupewa vipaumbele, wakaajiriwa kama ni Watanzania sasa pamoja na kwamba, hawajakuwa na uraia ambao tayari uliishaanzishwa?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, yote mawili yanawezekana, pale Wizara mbili zitakapoainisha maeneo ambayo hayapungui kumi na moja. Katika maeneo hayo kumi na moja ya uraia, kumi ni ya Waziri mwenzangu wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Masuala ya haki ya raia, kuzaliwa, kuoa na kuolewa, haki za kupiga kura, watu ambao ni *adopted*, Mtanzania

mmemwokota mahala, *adoption* yake, anapata *status* gani. Masuala ya *resident permits* na mengine kama kumi hivi, hayo yanamhusu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na linalonihusu mimi ni moja tu la *Diaspora*. Sasa tukishakamilisha mipango hii na Waziri mwenye dhamana akaleta hapa baada ya kutoka kwenye Baraza la Mawaziri, hatutajali kama kipindi hicho tumeshakuwa karibu na Katiba au kimetangulia, tukiwahi si haba tutaendelea na utaratibu huu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwa muda mrefu kimekuwepo kilio mionganoni mwa watu ambao wana asili ya Tanzania, lakini hawana Uraia wa Tanzania, pamoja na wageni ambao wangetamani sana kuwepo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa kilio chao ni kwamba, wanataka kuiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ifikirie kuwa na utaratibu wa kuwa na hati za muda mrefu ili waweze kutoa mchango wao wa kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, baada ya kulitafakari jambo hili la msingi, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, sasa imepewa agizo la kuandaa Waraka Maalum kwa ajili ya Baraza la Mawaziri, ambao utajenga hoja juu ya utaratibu wa kuwa na hati za muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Waraka huu utakuwa tayari mapema mwezi ujao kwa ajili ya kuwasilishwa katika vikao vinavyostahiki. Mimi ninaamini kwamba, jambo hili limekuja katika wakati mwafaka, ambapo kuna kilio kikubwa sana cha baadhi ya Watanzania kutaka kuwa na utaratibu wa kuwa na uraia wa nchi mbili. Kwa maana hiyo basi, suala la utaratibu wa kuwa na uraia wa nchi mbili linaweza kusubiri mpaka pale Katiba itakapokuwa imefanyiwa mabadiliko, pengine jambo hilo linaweza kuchukua muda kati ya miaka mitatu mpaka minne, lakini hili la utaratibu wa kuwa na hati ya muda mrefu ni hakika pengine ifikapo mapema mwezi Januari au Februari mwakani, linaweza likawa tayari. (*Makofit*)

MWENYEKITI: Ninakushukuru Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa ufanuzi mzuri. Ninafikiri kilio cha wengi sasa kimepata majibu. Sasa nimwite Mheshimiwa Jasson Rweikiza.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Katika mchango wangu wa maandishi, nimesema kwamba, Nchi za Afrika Mashariki tumepiga hatua na moja ya mambo ambayo tumeyafanya ni kufungua milango kwa Wananchi wa nchi hizi kwenda nchi yoyote mionganoni mwa nchi hizi kutafuta kazi na kuajiriwa. Kufuatia hatua hiyo, vijana wengi wa Kenya wako Dar es Salaam, tunawaona kwenye hoteli na sehemu nyingine wanafanya kazi. Kule Bukoba wapo Walimu na watu wengine ambao hawana kazi.

Sasa nikamwuliza Mheshimiwa Waziri, Wizara imechukua hatua gani kusaidia vijana wetu wa Tanzania kwenda katika nchi hizo nyingine kuchukua fursa hizo hasa ukizingatia pale Bukoba tunapakana na Rwanda, Burundi, Uganda na hata Kenya siyo mbali. Kwa hiyo, kama kungekuwa na uwezo wa vijana hao kusaidiwa, wangechukua nafasi hiyo haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, anijibu kama ni Wizara yake pekee au na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki; wana mkakati gani kusaidia vijana wetu hawa?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nimemwelewa vizuri, sasa hivi Jumuiya ya Afrika Mashariki tuko kwenye Soko la Pamoja (*Common Market*), baada ya muda tutakwenda kwenye *Monetary Union* na baadaye *Political Federation*. Katika kipindi hiki cha *Common Market* kama nilivyosema awali, Wananchi, Wataalam, wanaruhusiwa kwenda katika nchi zote. Wafanyabiashara, Wawekezaji, wanaruhusiwa kwenda katika nchi zote. Bidhaa na mitaji inaruhusiwa pia kutembea katika nchi zote. Hiyo ndiyo sifa ya *Common Market*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaloliona kwenye Wizara yetu ni kwamba, Serikali yetu inapaswa ijiandae katika kuwawezesha vijana; wawekezaji na wafanyabiashara kwenda kwenye masoko ya wenzetu nje. Lazima ziwepo benki zenyne urafiki au zinazoweza kuwawezesha vijana hawa kukopesheka pale wanapopata Miradi katika nchi jirani. Isiwe mtu unakwenda Kenya, unapata Mradi, unarudi Tanzania, unakaa mwezi mmoja na nusu au miezi miwili ukitafuta benki ya kukopa ili uweze kupeleka huduma kule kunakohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tujipange, tuwe na benki zilizotengwa maalum kwa ajili ya kuwawezesha Wafanyabiashara, Wawekezaji na Watanzania machachari, waweze kukopa na wakopesheke ili kulifika Soko la Afrika Mashariki ya Kati ikiwepo Sudan ya Kusini, ambayo itajiunga hivi karibuni.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwenye mchango wangu wa maandishi, niligusia suala zima la watu waliouawa *South Africa* na ninafikiri kuna baadhi ya Watanzania walipatwa na majanga haya, kama si ndugu zao basi jamaa zao. Nilitaka Mheshimiwa Waziri awaeleze Watanzania kwamba; ni Watanzania wangapi walikumbwa na maafa hayo huko *South Africa*; na ni hatua zipi Serikali ilizichukua kuwanusuru Watanzania wenzetu wanaoishi huko?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka nitakapopata taarifa vinginevyo, wakati wa *Xenophobia* kilichokuwa kimejitokeza ni kwamba, Watanzania wote waliokuwa kwenye maeneo ya hatari kwenye Miji ya Afrika Kusini, walijiorodhesha kwenye Ubalozi wetu na baadaye yakakodiwa mabasi mawili na kuwarejesha Watanzania wale kuja nyumbani. Hatukuwa na taarifa ya vifo, lakini ninahitaji kusahihishwa. Nitapenda kupata muda tu ninong'one na wenzangu kwa dakika moja ili nione kama kulikuwa na kifo kilichokuwa involved.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, tuliwachukua wote wale ambao waliomba kurudi nyumbani na kazi kubwa ilifanywa na Ubalozi wetu. Ningependa kuwashukuru sana Maafisa ambao waliwasindikiza Watanzania hao na wakati ule ninakumbuka Mheshimiwa Halima Mdee, alikuwa Afrika Kusini na alitusaidia sana

kupata takwimu na taarifa zilizokuwa zinahusu Watanzania ambao walikuwa wamenasa katika jambo hili. Sikuwa na taarifa ya kifo, hilo ninaomba nisiji- *commit*, lakini ninachojua ni kwamba, karibu Watanzania wengi tuliwarejesha kwa mabasi.

MHE. JOHN M. SHIBUDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajielekeza kwenye hoja yangu ya swali, ninaomba nisaidie Bunge hili liendelee kutumia maneno fasaha ya Kiswahili. Mheshimiwa Waziri, alipokuwa akijibu suala la malipo ya askari wetu walioko Lebanon, amesema posho; hapa haziitwi posho, jina stahiki zinaitwa ujira wa mwia. Kwa nini ninalisema suala hili? Kwa sababu posho wanalipwa Manamba, vijana wetu hawakwenda Lebanon kufanya kazi ya umanamba. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba dakika zangu niende kwenye swali. Kuhusu juhudhi na maarifa nilizozungumza naomba kusema kwamba, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa juhudhi walizotumia kufuata malipo ya Rada hatimaye Bunge la Uingereza likaweza kukubali na kuunga mkono Bunge la kwetu. Je, dhulumati zinazofanywa kupitia mikataba mibovu, Wabunge wa Mabunge hayo wana kauli gani hasa kuhusu dhulumati zinazofanyika Tanzania?

Je, Mheshimiwa Waziri umejituma vipi kuibua hoja iende kwenye Mabunge hayo? Unakumbuka nilisema kwamba, utashtakiwa katika Mahakama, wapi ushtakiwe kwa kutumia madaraka vibaya? Je, kwa nini usishtakiwe kwa kutojituma? (*Kicheko*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru kengele iligongwa wakati mUafaka. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa John Shibuda, kwa kunifunza msamati; ‘ujira wa mwia’. Hoja yake ni nzito, pale anapohoji kwamba tunafanya nini basi kwa Mikataba mingine katika kudai haki kote duniani? Kama anavyosema suala hili tulilolishughulikia la *BAE*, ndilo hasa lilikuja *officially* kwenye Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Mimi nina hakika kabisa, hizi bilioni ishirini na tisa zikishaingia, sisi Mawaziri tutajipanga kujaribu kuona ni sehemu gani tena ambazo pengine zitastahili nguvu za pamoja kudai pesa za aina hii. Hili ni wazo zuri na siyo vibaya tukalifuatilia mbele ya safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwamba, wenzetu wa Lebanon pamoja na Darfur, watapata ujira wa mwia hivi karibuni na hatutakuwa na matatizo.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Nilikuwa ninaomba kumwuliza swali Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Tarehe 23 Machi, 2011, aliandikiwa barua na Waziri Mkuu ya kutaka kudhibiti mienendo isiyoridhisha ya Balozi na Waraka wake kwa Baraza la Mawaziri akabainisha baadhi ya mienendo isiyoridhisha ya Mabalozi walioko hapa nchini. Baadhi ya mambo katika ukurasa wa tatu wa Waraka huo inasemwa; baadhi ya Mabalozi kuruhusu ofisi na kumbi zao za mikutano kutumika na Vyama vya Upinzani kupanga mikakati dhidi ya

Serikali; na baadhi ya Mabalozi kutumia nyumba zao kama kumbi za mikutano na kukutana na Viongozi wa Vyama vya Upinzani kufanya mikakati ya namna ya kuunganisha nguvu ya pamoja na kufanikisha azma ya kukiondoa Chama Tawala kutoka madarakani kwa kuwa kimekaa muda mrefu: Kama wapo Mabalozi wanaofanya hivyo; *conclusion* ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ilikuwa tumewaandikia barua za onyo, lakini hapa inaonekana ni uhaini na katika Waraka huu inasemwa kwamba, Mabalozi kwenda kwenye Majimbo ya Wabunge wa Upinzani; je, ni kosa Mabalozi wa nchi hii kwenda kwenye Majimbo yanayotawaliwa na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

Pili, ...

MWENYEKITI: Ahsante ni swali moja tu.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kungekuwa na muda ningeyajibu yote, lakini ninaomba nijibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina hakika kama alikuwepo nilipokuwa ninajibu swali hili. Kwa faida ya Mheshimiwa Godbless Lema, nilisema hivi; *document* tulioitoa ya Semina Elekezi ni ya ukweli wa kila *paragraph*; na ningeomba wanaofikia magazeti, inaruhusiwa itoke kwenye magazeti, tupate maoni ya Wananchi kwa sababu ni *document* nzuri sana. Ninadhani Mheshimiwa Mbunge alipokuwa nje, nilieleza kwamba, niliambiwa pale omnia radhi, nikasema siombi, itoke kwanza kwenye Vyombo vya Habari nihukumiwe na Wananchi. Ninaomba nisisitiza; tulichokisema pale tumeficha mengi sana, tungeamua kusema mengi tusingekuwa hapa, tunazingatia miiko ya Vienna Convention ambayo inanitaka pamoja na mambo yote hayo, kuhakikisha kwamba, tunadumisha Uhusiano wa Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tumefukuza mtu, tumeonya watu na humu ndani yetu tumeonya mtu tayari katika suala hili, lakini ni mambo ya jikoni, wakiamua kusema wenyewe watakuja kusema. Kama alivyosema Balozi wa nchi fulani, miaka mitatu iliyopita, ambayo nimeahidi kuipa Kamati ya NUU taarifa ya utendaji wake wa kazi nchini Tanzania, kwa muda wa miaka mine; alichokifanya, aliokutana nao, mikakati aliyokuwa anaifanya kwa sababu sasa ni Profesa wa Chuo Kikuu nje ya nchi. Nitatoa *document* hiyo, Watanzania mwone baadhi ya vitendo vya watu tunaojaribu kuwatetea hapa, hatuwezi kuwatetea. Watu hawa wako pale, *deans* na hawa nimepewa mimi dhamana ya kuwadhibiti, tuacheni tufanye kazi. (*Makofi*)

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

(*Hapa kipaza sauti kilikuwa kinasumbua*)

MWENYEKITI: Unaweza ukahamia *microphone* nyingine.

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sina haja ya kukamata mshahara wa jirani yangu, lakini ninataka ufanuzi kidogo. Katika Bunge lililopita, ilikuja hoja hapa, *hot cake* kabisa, juu ya suala zima la *OIC* na sikupata maelezo yoyote katika hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri wakati ule alisema kwamba, kuna Taratibu, Kanuni na Sheria, ambazo zinafanyiwa marekebisho huko *OIC*, lakini pia akaeleza kwamba, suala zima la kujiunga na *OIC* siyo la kidini bali ni la kiuchumi zaidi. Je, mpaka sasa hivi Serikali ina kauli gani juu ya hoja ya Tanzania kujiunga na *OIC*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Serikali haina kauli kwa sababu jambo hili wakati wake haujafika. Tulisema mwaka 2012, lisiletwe sasa. Ninakushukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuuliza swalii.

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni mengi sana ya nje yanayokuja kuwekeza katika nchi yetu yakiwemo mabenki, makampuni yanayokuja kuwekeza kwenye migodi ya madini na hata kwenye mawasiliano, *yakifika* kuna kazi nyingine wanakuja na *expatriates* kutoka kwao. Mimi ninaamini alivyosema Mheshimiwa Mbunge mwenzangu wa Upinzani kutoka *CUF* kwamba, Watanzania walioko nje pia wapo wengi sana ambao ni Wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuiuliza Serikali; haioni kwamba wakati umefika wa kutengeneza *pool* ya *expatriates* ya Watanzania ambao wako nje na tukai-*cluster* kwamba *engineers* ni wangapi, *accountants* ni wangapi, tukawa nayo; na yale makampuni yanapokuja tuweke sheria ya ku-regulate kwamba, kabla hawajaleta *expatriates* wao kwanza tuangalie kwenye ile *pool* kuna Watanzania wangapi wanaoweza kuja kuchukua nafasi za kazi hiyo? Mheshimiwa Waziri, ninaomba ufanuzi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi maana ninataka niwatendee haki, nimebakiwa na wawili tu.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana mia kwa mia na ndugu yangu Mheshimiwa Ezekia Wenje.

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri kuhusu nafasi za Wazanzibari katika Diplomasia hii ya Mabalozi wa Nje, ametwambia kwamba, amekutana na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, wakaandaa mikakati ya kuanzia mwezi wa

Septemba, kuwachukua wanafunzi na kuwapeleka katika Chuo cha Diplomasia na vilevile kuteua Mabalozi wawili ambao wanategemewa kuwa New York na Jeddah. Mimi ninasisitiza zaidi kwamba, hata ukiangalia Mabalozi wetu wa Nchi za Kiafrika, huwakuti Wazanzibari wakiwa huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, hamshauri Rais wa Jamhuri ya Muungano ashirikiane na mwenzake Rais wa Zanzibar ili na yeye impendeze zaidi kuwachagua Wazanzibari kuchukua hizo nafasi kama inavyompendeza kuwachagua watu wa Bara? (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Sanya, tuone itakavyompendeza Mheshimiwa Waziri naye.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo lake litachukuliwa.

MHE. JOSEPH M. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Katika kuchangia hoja kwa maandishi na kwa kuzungumza, nimeuliza suala la mpaka wa Tanzania kusogezwa na kumegwa na Warundi. Ninaomba ufanuzi; nini kauli ya Serikali juu ya ni lini eneo lile litarejeshwa sehemu ya Tanzania na lisibaki Burundi?

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa umeelewaka. Mheshimiwa Waziri ufanuzi.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala zito sana, linalohusu Kamati ya Ulinzi na Usalama na Wizara ya Mambo ya Nje. Ninaomba shilingi asiiondoe niipate ili tulifanyie kazi ya kina kwa maslahi ya Taifa letu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, kwa kushirikiana na Waziri muweze kufanya kazi kwa maslahi ya Taifa. Wote mmeweza kupata fursa.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1002 - <i>Finance and Accounts</i>	Shs. 538,787,000
Kif. 1003 - <i>Foreign Affairs Office Zanzibar</i> ...	Shs. 332,644,000
Kif. 1004 - <i>Policy and Planning</i> ...	Shs. 486,515,000
Kif. 1005 - <i>International Cooperation</i> ...	Shs. 2,434,111,000
Kif. 1006 - <i>Europe and America</i> ...	Shs. 326,128,000
Kif. 1007 - <i>Asia and Australia</i> ...	Shs. 317,361,000
Kif. 1008 - <i>Africa</i>	Shs. 5,541,031,000
Kif. 1009 - <i>Regional Cooperation</i>	Shs. 4,881,299,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya*

Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1010 - *Protocol* Shs. 15,117,595,000

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kupitia Mafungu yote ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa katika *Subvote 1010, item number 220700 - Rental Expenses*, zimetengwa shilingi 2,317,210,490. Hoja yangu hapa; nilipopitia vifungu vyote nikajaribu kujumlisha kwenye Fungu hilo, ninapata karibu shilingi 11,000,000,000 kwa Mafungu yote.

Hoja yangu hapa ni kwamba; hizi ni fedha nyingi ambazo tunalipa kama pango ninavyoolewa. Sasa nilitaka Mheshimiwa Waziri anieleze tunakuja na mpango mkakati gani wa kuhakikisha kwamba, tunapata majengo yetu wenyewe kwenye Ofisi zetu za Ubalozi ili tuondokane na kupanga majengo na kuendelea kulipa pesa nyingi namna hii? Pamoja na kwamba, alishaanza kueleza kuwa, tunanunua majengo katika baadhi ya maeneo, lakini nini mpango mkakati sasa wa kuhakikisha kwamba tunaondokana na hali hii kabisa?

Ahsante Mwenyekiti.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokisema Mheshimiwa Zambi ni sahihi kabisa; ukiachilia mbali London, India, New York na Washington ambako tuna majengo yetu wenyewe; tunayo kazi ya ziada ya kuhakikisha kwamba, tunapata nyumba zetu wenyewe.

Waheshimiwa Wabunge na wewe Mwenyekiti, mtakumbuka kwamba, hela zinazotuwezesha kupata na kununua nyumba hii ni *Development Budget*, ambayo ilianza kupatikana mwaka 2007/2008, 2008/2009, 2009/2010 na tunakwenda vizuri. Kipindi cha mwaka 2010/2011, tumeptata shilingi bilioni 44.5. Safari hii mkiidhinisha uwezo wetu wa kujenga nyumba zaidi, kununua nyumba zaidi ili tutokane na tatizo hili, tutafanikiwa. Kwa hiyo, jibu hapa ni *Development Budget*.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni nilivyosimama nilikuwa ninahoji *item number 221400 - Hospitality Supplies and Services*. Nimejaribu kupitia Wizara kwa ujumla, nikaona kwamba, *allocation* ya hizi fedha zinatofautiana; kuna baadhi ya maeneo wamepangiwa fedha nyingi, ikiwemo Idara ya *Protocol* na nikaona kwamba, maeneo mengine hawajaweza kupangiwa hizi fedha. Nilikuwa ninaomba ufanuzi kutoka kwa Waziri; kwa nini hapa wamepanga jumla ya shilingi 517,334,494 wakati maeneo mengine hawajapewa fedha hizi?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi hiki kilichotengwa ambacho kinaonekana ni kikubwa ni kwa ajili ya Sherehe za Miaka 50. Wizara ndiyo inayopokea wageni wote, kwa hiyo, makabrasha, vipeperushi, vitabu, vitakavyokuwa pamoja na wageni

watakaokuja kutoka nje, akiwemo *Princess Charles*; ni pesa ambazo zinatumika kwa *hospitality* na Sherehe ya Miaka 50.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Subvote* hiyo hiyo, *item number 230400 - Routine Maintenance and Repair of Vehicles and Transport Equipment*, hapa zipo shilingi 10,000,000. Vilevile *item 410800 - Rehabilitation of Vehicles and Transport Equipment*, ina shilingi 177,000,000. Ninataka Waziri anipe tafsiri ya neno “*Rehabilitation*” na hili neno “*Repair*”; yote kwa ajili ya magari. Sasa sijui ku-*rehabilitate* gari anakusudia nini?

MWENYEKITI: Ahsante, muda wako umekwisha na Waziri amekuelewa.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Ninaomba nijiridhishe tu; ana maana ya 410800; na kwamba anauliza maana ya *Rehabilitation of Vehicles and Transport Equipment*; si ndio?

MWENYEKITI: Ndiyo maana yake.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Ni matengenezo ya magari.

MWENYEKITI: Ahsante. Siyo gari moja ni magari mengi. Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 104(2), sasa tunakwenda kwenye *guillotine* ili Kamati ya Matumizi iweze kukamilisha kazi yake.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1011 - <i>Legal Services</i>	Shs. 1,671,164,000
Kif. 1012 - <i>Information, Education & Communication</i>	Shs. 1,302,311,000
Kif. 1013 - <i>Middle East Division</i>	Shs. 258,526,000
Kif. 1014 - <i>Internal Audit Unit</i>	Shs. 141,657,000
Kif. 1015 - <i>Procurement Unit</i>	Shs. 208,156,000
Kif. 1016 - <i>Information and Communication Technology</i>	Shs. 67,403,000
Kif. 1017 - <i>Diaspora Engagement & Opportunity</i>	Shs. 131,998,000
Kif. 2001- <i>Embassy of Tanzania – Addis Ababa</i> ... Shs.	892,277,000
Kif. 2002 - <i>Embassy of Tanzania – Berlin</i>	Shs. 1,776,946,000
Kif. 2003 - <i>Embassy of Tanzania – Cairo</i>	Shs. 595,191,000
Kif. 2004 - <i>Embassy of Tanzania – Kinshasa</i>	Shs. 797,422,000
Kif. 2005 - <i>Embassy of Tanzania – Abuja</i>	Shs. 778,726,000
Kif. 2006 - <i>High Commission of Tanzania – London</i> ..Shs.	2,009,942,000

Kif. 2007 - *High Commission of Tanzania – Lusaka* ...Shs. 692,592,000
 Kif. 2008 - *High Commission of Tanzania – Maputo* ..Shs. 873,151,000
 Kif. 2009 - *Embassy of Tanzania – Moscow* Shs. 1,907,166,000
 Kif. 2010 - *High Commission of Tanzania – New Delhi* Shs .1,215,144,000
 Kif. 2011- *Permanent Mission To The UN- New York* Shs. 2,882,502,000
 Kif. 2012- *High Commission of Tanzania – Ottawa* ... Shs. 1,367,032,000
 Kif. 2013 - *Embassy of Tanzania – Paris* Shs. 2,133,493,000
 Kif. 2014 - *Embassy of Tanzania – Beijing* Shs. 1,352,422,000
 Kif. 2015 - *Embassy of Tanzania – Rome* Shs. 1,891,547,000
 Kif. 2016 - *Embassy of Tanzania – Stockholm* Shs. 1,297,466,000
 Kif. 2017 - *Embassy of Tanzania – Tokyo* Shs. 1,662,626,000
 Kif. 2018 - *Embassy of Tanzania – Washington* ... Shs. 1,714,958,000
 Kif. 2019 - *Embassy of Tanzania – Brussels* ... Shs. 1,465,353,000
 Kif. 2020 - *Permanent Mission to The UN-Geneva* Shs. 2,168,757,000
 Kif. 2021 - *High Commission of Tanzania Kampala* Shs. 822,513,000
 Kif. 2022 - *High Commission of Tanzania – Harare* Shs. 722,034,000
 Kif. 2023 - *High Commission of Tanzania – Nairobi* Shs 1,625,277,000
 Kif. 2024 - *Embassy of Tanzania – Riyadh* ... Shs. 1,156,879,000
 Kif. 2025 – *High Commission of Tanzania – Pretoria* Shs. 269,178,000
 Kif. 2026 - *Embassy of Tanzania – Kigali* ... Shs. 639,908,000
 Kif. 2027 - *Embassy of Tanzania – Abu Dhabi* Shs. 1,710,597,000
 Kif. 2028 - *Embassy of Tanzania – Bujumbura* Shs. 659,258,000
 Kif. 2029 - *Embassy of Tanzania – Muscat* Shs. 765,066,000
 Kif. 2030 - *High Commission of Tanzania – Lilongwe* Shs. 577,568,000
 Kif. 2031 - *Embassy of Tanzania – Brasilia* Shs.1,532,748,000
 Kif. 2032 - *High Commission of Tanzania Kuala Lumpur* Shs. 1,160,872,000

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa

Kif. 1004 - *Policy and Planning* Shs.44,500,000,000

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

T A A R I F A

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, kifungu hadi kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko yoyote. Hivyo basi, ninaomba kutoa hoja kwamba, Makadirio hayo sasa yakubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa
kwa Mwaka 2011/2012 yalipitishwa na Bunge*)

MWENYEKITI: Kwa sababu hiyo basi, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge, kwa mjadala mzuri wa siku ya leo. Kipekee, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa kazi kubwa mliyoifanya leo. Pia niwatakie kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yenu. Bila ya kumsahau Katibu Mkuu na Watendaji wote, maana shughuli hii ya leo mpaka imekwisha, ninajua kazi kubwa sana imefanyika na kwa hiyo niwapongeze sana na niwatakie kila la kheri katika shughuli yetu.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. DKT. HAMIS A. KIGWANGALLA: Mwongozo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, bado sijamaliza. Basi Mheshimiwa ili nikutendee haki omba huo mwongozo wako.

MHE. DKT. HAMIS A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa fursa hii. Mapema leo hii baada ya Kipindi cha Maswali na Majibu, kwa mujibu wa Kanuni ya 47(1 - 4) na Kanuni ya 48(1- 4), niliomba kuwasilisha hoja ya dharura ili tuweze kujadili upunguzwaji wa bei ya kununulia pamba, unaofanyika kwenye sehemu ambazo zinalima na kuuza pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninasikitika sijapewa fursa ya kufanya hivyo mpaka sasa hivi na kule wakulima wanakosa mahali pa kwenda kuuza pamba yao. Pamba kwa wale wasiofahamu ni zao ambalo linalimwa na linaendesha uchumi na maisha ya watu ya kila siku kwa takriban asilimia 40 ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba mwongozo wako.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, kwanza, suala la bei ya pamba ni jana tu Mheshimiwa Waziri Mkuu, ametoka kuulizwa swali na alijibu na kama kulikuwa kuna maoni zaidi, Serikali ipo na pengine mngeweza kuwasiliana.

Kwa mujibu wa Kanuni hiyo hiyo ya 48(1)(a), hoja yako haipati mshiko kwa sababu ingeweza tu kuruhusiwa kama ingekuwa hajatolewa taarifa inayohusiana na jambo hilo. Tayari Serikali ilikwishatoa taarifa ya jambo hilo na kwa hiyo Serikali inafanya jitihada ya kushughulikia suala hilo.

Ukienda ile ya 48 hiyo hiyo 3(b) ili hoja hiyo iwe ya dharura, lazima iwe imetokea siku hiyo hiyo na karibuni na imeletwa bila kuchelewa. Kwa kuwa jana ulikwishatolewa baadhi ya ufanuzi kwa taarifa yake, ninaamini unaweza ukaendelea kutafuta majibu zaidi au mashauriano zaidi, maana yake ni tatizo kwa namna nyingine yoyote na siyo lazima ukapitia hoja ya dharura. Huo ndiyo mwongozo wangu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo, ninayo matangazo hapa. Kwamba, Wabunge wote, kesho tarehe 23 Julai, 2011, Jumamosi, mnatangaziwa kuwa kutakuwa na Mechi ya Mpira wa Miguu (Bonanza) pamoja na Mpira wa Pete kati ya Timu ya Waheshimiwa Wabunge na Timu ya *NMB* pamoja na Timu ya Mpira wa Miguu ya *Tanzania All Stars Veteran*.

Mechi hiyo itachezwa katika Uwanja wa Jamhuri, Mjini Dodoma, kuanzia saa 9.00 alasiri. Mgeni rasmi atakuwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda.

Waheshimiwa Wabunge wote, mnaombwa kufika uwanjani kuishangilia Timu yenu. Pia kesho hiyo hiyo kuanzia saa 4.00 kutakuwa na *Pool Table pale Tiger Motel, Area C*, ambapo Timu ya Bunge itakuwa inacheza na Timu ya Viongozi wa Mchezo wa *Pool Table Taifa*.

Kwa hiyo, tunawakaribisha Waheshimiwa Wabunge, mfike kwa ajili ya kuishangalia Timu yenu ya *Pool Table* na mgeni rasmi atakuwa Mheshimiwa Mathias Chikawe, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora. Wote mnakaribishwa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa siku ya leo shughuli zetu tumekamilisha na hivyo nichukue nafasi hii, kuahirisha Bunge hadi Jumatatu, tarehe 25 Julai, 2011, Saa Tatu Asubuhi.

(*Saa 2.15 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu,
Tarehe 25 Julai, 2011 Saa Tatu Asubuhi*)